# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 3 Mei, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatayo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Randama ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa mwaka wa Fedha 2013/2014.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria, kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Katiba na Sheria Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunapowasilisha Mezani lazima vitu vile viwepo. Hapa nina kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria, kitabu cha Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, lakini ya kwenu Upinzani haipo. Iko wapi? Zilizowasilishwa hizi hapa, ya kwenu iko wapi?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, hili ni jambo geni kidogo. Sijawahi kuona katika Bunge lako Tukufu ukitoa matamshi kama haya. Naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba, kama Kanuni zinavyosema, maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni yatawasilishwa kwenye Bunge lako na Wabunge watapata nakala zao kama ilivyo kawaida siku zote.

**SPIKA:** Si mnasema tufuate Kanuni, ninachokisema ni kwamba mnaponiwasilishia mezani zipo hizi, sasa hizo zenu ziko wapi? Siyo kwamba ni kitu kigeni, nauliza iko wapi? Kanuni ya 99(5). Sasa nyie mnang'aka, mimi nauliza iko wapi? Kwanini hamjibu? Iko wapi?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, hotuba yetu inapelekwa kwenye Idara ya Uchapaji sasa hivi, shida iko wapi?

**SPIKA:** Sasa hivi haipo! Kwa hiyo, naomba ku- *withdraw* ile, haijawasilishwa. *(Makofi)*

Tunaendelea, Katibu.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 135

### Ujenzi wa Barabara za Lami Kawe

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA (K.n.y. MHE. RITA L. MLAKI)** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara kwa kiwango cha lami katika Jimbo la Kawe hususan barabara za Mikocheni, *Mbezi Beach* na Tegeta ambako kuna mali za thamani kubwa.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga na kupanua barabara ya *Old Bagamoyo* kutoka makutano ya barabara ya Kawawa hadi *round about* ya Kawe ambako hutokea mafuriko eneo la *Mayfair* na kuna msongamano mkubwa wa magari.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara za Mikocheni, *Mbezi Beach* na Tegeta zipo katika Jimbo la Uchaguzi la Kawe. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inaendelea kujenga barabara za lami ikiwa ni pamoja na barabara ya *Journalism* iliyopo Mikocheni yenye urefu wa kilomita 1.1 pamoja na daraja la Mto Feza kwa gharama ya shilingi milioni 840. Vilevile ujenzi wa barabara ya Tegeta Soko la Nyuki iliyopo Tegeta yenye urefu wa kilomita 1.0 kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi milioni 512.7.

Aidha, daraja la Ndumbwi lililoko *Mbezi Beach* nalo linajengwa ili kupunguza foleni katika eneo hilo ambalo linagharimu kiasi cha shilingi milioni 325.9. Pamoja na kazi hizo, Serikali imetenga shilingi milioni 700.0 katika mwaka 2012/2013 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya *ITV* hadi kwa Warioba yenye urefu wa kilomita 1.6 kwa kiwango cha lami. Mkandarasi ameishapatikana na ujenzi utaanza Mei, 2013.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mipango hiyo, Serikali imeandaa mpango muda mrefu wa kujenga barabara za Jiji la Dar es Salaam unaojulikana kama *Dar es Salaam Metropolitan Development Project* ambao utahusisha pia ujenzi wa barabara za Jimbo la Kawe ikiwemo barabara ya *TANESCO* – Msasani – Msasani Soko la Samaki yenye urefu wa kilomita 1.5. jumla ya kilomita 25.25 zitajengwa kupitia mpango huu katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* iliajiri kampuni ya *NORPLAN (T) Ltd.,* kufanya usanifu wa barabara ya *Old Bagamoyo (Mwai Kibaki Road)* yenye urefu wa kilomita 5.3 na barabara ya *Garden* yenye urefu wa kilomita 1.2 kwa ajili ya kupanuliwa kwa kiwango cha njia mbili ili kupunguza msongamano wa magari katika barabara hiyo.

Hata hivyo, kabla ya kuanza upanuzi wa barabara hiyo, Serikali imepanga kuanza na ujenzi wa mfereji wa maji ambao utapeleka maji ya mvua baharini ili kuepuka mafuriko

ambayo yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara katika eneo la *Mayfair* hadi *TMJ.* Katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 zimetengwa jumla ya shilingi bilioni 6.0 kwa ajili ya kazi hiyo. Serikali inaendelea na tathmini ya malipo ya fidia kwa wakazi wa eneo hilo ambao nyumba zao zitaathiriwa na zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa mfereji huo, Serikali itaweka katika mpango kuhusu upanuzi wa barabara hiyo kuwa njia mbili ili kuondoa msongamano wa magari uliopo. *(Makofi)*

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii. Naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, tayari Serikali ina mpango wa kupanua barabara ya *Old Bagamoyo* na kwa kuwa tayari kuna mpango pia wa kujenga mifereji ambao utawezesha maji kuelekea baharini ili kuweza kuepusha mafuriko pamoja na msongamano wa magari.

Je, Serikali iko tayari sasa kuwaambia wananchi wa Kawe ni lini zoezi hilo litaanza?

(b) Kwa kuwa, asilimia kubwa sana ya barabara za Jiji la Dar es Salaam ni za changarawe na kwa kuwa Serikali kwa kipindi kirefu imekuwa inatumia fedha nyingi sana kukarabati barabara hizi mara kwa mara zikiwemo za jimbo la Ukonga ambazo asilimia 98 ni za changarawe?

Je, Serikali iko tayari sasa kuanza mpango wa kujenga barabara za lami katika jiji la Dar er Salaam ili kuepusha gharama nyingi pamoja na changamoto wanazozipata wananchi kwa barabara hizi kuwa mbovu mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Eugine Mwaiposa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza hili analolisema Mheshimiwa Mwaiposa la kuweka mkondo wa kutolea maji kwa maana ya *drainage system* ndiyo tatizo la msingi lililoko katika eneo lile.

Ujenzi mwingi umefanyika pale, jana nilikuwa nazungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa eneo lile, nikamwambia nataka pia kujua ni nini kilichotokea mpaka watu wamejijengea kiasi hicho. Hili ni tatizo ambalo tunalo nchi nzima. Maji yakiishajaa pale basi ndiyo unaona kelele zinakuwa nyingi hapo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka niseme kwamba hii kazi itafanyika. Lini itaanza, nimesema hapa kwamba, kuna hawa wenzetu wa *NORPLAN* halafu kuna *feasibility study* ambayo inafanyika sasa hivi. Barabara haijengwi tu hivi hivi, ni lazima uwe na watu ambao wanakwenda pale kucheki ili kujua kinachohitajika, mahitaji yaliyoko pale na nini.

Kwa hiyo, nilitaka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Mwaiposa kwamba, kazi hii tunapozungumza sasa hivi inaendelea kwa sababu ni kero kubwa sana. Hili tatizo linalotokea Dar es Salaam sasa hivi limesababishwa na hili jambo ambalo anali- *address* Mheshimiwa Mbunge.

Sasa kuhusu barabara za chanagarawe ni kweli kabisa kwamba, ukijenga barabara za changarawe, kesho asubuhi mvua inaweza ikanyesha ukakuta imesomba yote ikaenda. Sasa tunachofanya hapa ni kwamba, hii *Dar es Salaam Metropolitan Development Project* ambayo tumeweka pale inakwenda pia Manispaa ya Ilala, hiyo *plan* iko kule.

Hizi ni fedha ambazo mnaona tunajenga miji mbalimbali kama Arusha, Dodoma hapa, kule Kigoma, tukaitengea Dar es Salaam utaratibu wake kwa sababu ilionekana inakomba fedha zote zile, ndiyo maana tukaweka huu mpango. Huo mpango tunao, sasa ni suala la kipaumbele kwamba, wanapopelekewa fedha wao wapange na kusema hizi fedha ziende katika eneo gani.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mwaiposa kwamba tuko tayari kukaa nae tumsaidie kwa sababu mpango huu tayari upo huko.

**MHE. ZARINA Z. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Manispaa ya Dar es Salaam hususan wilaya ya Kinondoni imebadilisha barabara zake nyingi sana ambazo zilikuwa za changarawe na kuzifanya lami nyepesi. Lakini kwa sababu ya huu msongamano malori makubwa yanayotoka mikoani yanapita na kuziharibu hizi barabara katika kipindi kifupi sana.

Je, Waziri anasemaje, yuko tayari tukitoka hapa twende Dar es Salaam tukapite kwenye zile barabara na atwambie atatusaidiaje kuzirudisha hizi barabara zetu ambazo tumezijenga kwa kiwango cha changarawe na kuharibika haraka sana?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zarina Madabida kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nilipata shida kidogo alipoanza alisema lami nyepesi baadaye alipomalizia akasema barabara za changarawe, lakini nahani pia...

**MHE. ZARINA Z. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, ni lami nyepesi.

**SPIKA:** Unasema pale unapoitwa, siyo unasema tu unavyotaka.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, sawa.

Ni kweli kwamba tunachofanya sasa hivi, kwanza kabisa hizo lami nyepesi ukipitisha haya malori makubwa, mizigo haibebwi na malori. Ukienda nchi hizi kubwa kubwa kama Marekani, Uingereza, mizigo inabebwa kwa treni. Ndiyo maana atakapokuja Waziri anayehusika na eneo hili la usafirishaji, mtaona mpango wake mkubwa pale ni kuimarisha njia ya treni. Ukiishaona mizigo inabebwa na treni basi umeondokana na tatizo la msingi katika maeneo haya.

Hata hivyo, kwa vile bado tunatumia barabara hapa, ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Madabida kama barabara zetu zitaendelea kutumika hivyo na magari makubwa yanapita, maana yake ni kwamba tatizo hili litaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, sisi tunashirikiana na *TANROADS,* tunaweka mizani barabarani ili kupima mizigo ili kujua ina uzito kiasi gani. Sasa yeye ametaka tufuatane twende Dar es Salaam. Waziri wangu yuko hapa anasikia wala hana tatizo, mimi nitaondoka akihitaji tutakwenda kule tukaziangalie hizo barabara.

Lakini kubwa ambalo tunalifanya sasa hivi katika barabara hizi zote zinazozungumzwa hapa ni pamoja na kuhakikisha kwamba, tunazielekeza katika ile *Dar es Salaam Rapid Transport.* Ndiko tunakokimbilia ili watu wetu waweze ku-*access* kuingia katika hii barabara ambayo sasa watakuwa wanakwenda kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, tuko tayari kufuatana naye.

**SPIKA:** Namwona Mheshimiwa Halima anasimama mara elfu kumi. Haya swali la nyongeza Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza Mheshimiwa Madabida awe anakuja kwenye vikao vya halmashauri, hayo mambo huwa haji, halafu anauliza hapa.

**SPIKA:** Aah, uliza swali, hizo habari. Naomba uondoe maneno yako ya mwanzo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, sawa sawa.

Wakati Naibu Waziri anajibu swali amezungumzia suala la mfereji wa *six billion*. Vilevile ikumbukwe Serikali inagharamia six billion kwa sababu iliuza maeneo ambayo yalikuwa mkondo wa maji kwa wale Warabu. Swali langu ni hivi, eneo ambalo linaathirika sana ambalo haliko katika huu mpango wa six billion ni barabara ya Mandazi *(Mandazi Road)* ambayo inaunganisha *Old Bagamoyo Road* na Kimweri.

Hii ni barabara muhimu sana kwa watu ambao wanakaa bonde la Mpunga. Sasa nilitaka Serikali iniambie kwa sababu tokea mwezi wa Pili Manispaa ya Kinondoni imeandika barua kwa TAMISEMI kuwaomba hii barabara iingizwe katika huu mpango wa *Dar es Salaam Metropolitan Project,* mpaka sasa hakuna jibu. Nilitaka Serikali iniambie ina mkakati gani kuhusiana na barabara muhimu sana ya *Mandazi Road* ambayo kwa miaka mitatu mfululizo kumekuwa kuna ahadi ambazo hazitekelezeki. Kwa hiyo, nataka nipate jibu makini kutoka kwenye Serikali.

**SPIKA:** Swali la nyongeza, kama ungekuwa makini ungeleta. Haya naomba Waziri ujibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima Mdee.

Mheshimiwa Spika, barabara ambazo ziko katika mradi huu zilichaguliwa na Halmashauri husika. Sisi tulichofanya tuliwapa *menu* tu, wao wenyewe ndiyo walichagua. Sasa baada ya kuwa wamepanga, haiwezekani tena wakawa wanachomekea chomekea njiani. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Aliko Kibona anapaswa kuuliza swali hilo. Kwa niaba yake Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale.

Na. 136

**Posho kwa Wenyeviti wa Vijiji**

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE (K.n.y. MHE. ALIKO N. KIBONA)** aliuliza :-

Kwa muda mrefu Serikali iliishaahidi kuangalia uwezekano wa kuwalipa posho Wenyeviti wa Vijiji kutokana na kazi kubwa wanayofanya ya kusimamia shughuli za maendeleo ya Taifa:-

Je, viongozi hao wataanza kulipwa lini posho hiyo muhimu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kazi kubwa zinazofanywa na Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa katika kusimamia shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao. Majukumu hayo yameongezeka kutokana na utekelezaji wa

Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi ambapo Serikali inapeleka raslimali fedha, vifaa na raslimali watu kwa wingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Uamuzi huu wa Serikali umesaidia kuwapa fursa wananchi kujiwekea vipaumbele vya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia fursa na vikwazo vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, viongozi wa ngazi za msingi za Serikali za Mitaa wanayo majukumu mengi ambayo ni kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika uchangiaji wa mirad ya maendeleo na kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo kupitia Kamati za Maendeleo za Vijiji.

Kwa kutambua hilo Serikali kupitia kila Halmashauri imeweka utaratibu wa kuwalipa posho Wenyeviti wa vijiji na mitaa kutokana na vyanzo vya mapato ya ndani ambavyo ni asilimia 20. Mgawanyo wa fedha hizi ni kwamba asilimia 3 hutumika kwa ajili ya maendeleo na asilimia 17 hutumika kwa ajili ya utawala ikiwemo kulipa posho hizi za Wenyeviti wa Vijiji. Hata hivyo, viwango ambavyo hulipwa vinatofautiana kati ya Halmashauri moja na nyingine kulingana na makusanyo ya mapato ya ndani katika vyanzo vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa inayoikabili Serikali, ni ufinyu wa Bajeti pamoja na makusanyo kidogo katika Halmashauri. Aidha, mkazo umekuwa ukitolewa kwa Halmashauri zote chini kuhakikisha kuwa asilimia 20 hiyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri zinapelekwa katika vijiji, kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kubuni vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kulipa posho hiyo, Serikal imeweka utaratibu wa kuwajengea uwezo Wenyeviti wa vijiji na Mitaa ambapo kila Halmashauri hutenga na kuidhinishiwa fedha za kujenga uwezo katika Bajeti ya kila mwaka.

Kati ya fedha hizo, asilimia 40 hupelekwa katika ngazi ya kijiji/mtaa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ofisi na mafunzo kwa viongozi hao. Lengo ni kuwajengea uwezo wa kusimamia majukumu yao kwa ufanisi. Napenda kutumia fursa hii kuzielekeza Halmashauri zote kuhakikisha fedha ambazo ni asilimia 20 ya mapato ya ndani ya Halmashauri zinapelekwa katika vijiji ili sehemu ya fedha hizo zitumike kulipa posho ya viongozi hao lakini pia kuhakikisha asilimia 40 ya fedha za kujenga uwezo zinazotengwa kila mwaka zinapelekwa katika ngazi ya Kata na Vijiji/Mtaa ili kuwajengea uwezo viongozi hao kupitia katika Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo. *(Makofi)*

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, asilimia 20 ya pesa ambazo zinapelekwa katika vijiji hazibainishwi wazi kwamba zinalipa posho za Wenyeviti isipokuwa mikutano ndiyo inaendeshwa.

La kwanza, Sasa naiuliza Serikali ni lini itabainisha wazi kwamba labda asilimia 10 au 15 itakuwa ni posho kwa ajili ya Wenyeviti?

La pili, kwa kuwa, Wenyeviti ndiyo vinara kabisa wa maendeleo vijijini ni lini Serikali sasa itatoa fedha kwa ajili ya Wenyeviti kutoka katika Serikali Kuu na siyo Serikali za Mitaa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hili ainisho nililolitoa hapa ni ainisho linalotokana na ushuru ambao ungekusanywa kule katika Halmashauri.

Kuna kitu kinaitwa *nuisance taxes* yaani *tax* ambayo inaleta kero vitumbua, samaki wa kukaanga, mandazi, mchicha mchicha, vile vitu vinavyopita wanasema haya dagaa, haya dagaa tena, haya dagaa, wanasema dagaa.

Hiyo Serikali ikafuta, Serikali ilipofuta ikasema hivi sisi tutaleta kitu kinachoitwa fidia na ndiyo maana Bunge lako hapa kujibu swali la pili, ikaja na kitu kinachoitwa *general purpose grant* na katika hii Bajeti tunayokwenda nayo bilioni 63 zikatengwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Manjale alikuwepo hapa na sisi wote tulikuwepo hapa ikarudishwa tena ilikuwa bilioni 10 ikarudishwa ikaja bilioni 63. Kwa hiyo msuli wa Serikali Kuu unauona pale. Tunachosema hapa tunatoa maagizo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo ni kweli anavyosema Mchungaji hapa wapo watu wengine wanakusanya pale kwenye Halmashauri zinakaa pale.

Waheshimiwa Wabunge kama mnaijua Halmashauri ambayo haipeleki hii posho kwa Wenyeviti wa vijiji na Vitongoji tuleteni majina yao, tuleteni sisi hapa halafu sisi tushuke nao jumla jumla hizi fedha zinatengwa. (*Makofi/ Kicheko*)

**SPIKA:** Naona tuendelee sasa. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Betty Machangu. Watu mpaka wameuza dagaa. Naibu Waziri mpaka ameuza dagaa hapa.

Na. 137

**Ulinzi wa Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro**

**MHE. BETTY E. MACHANGU** aliuliza:-

Miti iliyoko katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro ni mirefu zaidi ya mita 30 na kufanya doria zinazofanywa *KINAPA* kubaini uharibifu wa vyanzo vya maji na wakatao miti kuelekea kugonga mwamba:-

(a) Katika mazingira ya miti mirefu kiasi hicho kwa nini doria za Helikopta zisitumike ili kuleta ufanisi wa kuwakamata waharibifu wa hifadhi hiyo?

(b) Kwa sababu Jeshi la Wananchi wa Tanzania hufanya mazoezi ya kijeshi/kivita mara kwa mara kwenye maeneo mbalimbali nchini, na ili kuleta ufanisi katika kulinda hifadhi zetu za Taifa nchini. Je, ni kwa nini Serikali I isiliagize Jeshi kufanya mazoezi yao ya kawaida katika maeneo ya hifadhi nchini ili liweze kupambana na kuwakamata waharibifu wa hifadhi zetu?

(c) Kwa kutumia "*water gauges*" ni rahisi kufahamu kiasi cha mtiririko wa maji kutoka vyanzo vya maji hasa katika vyanzo vya mito itokayo mlimani, kwamba "*rate of flow*" ikipungua ni dhahiri vyanzo vya maji vimeharibiwa hivyo doria itiliwe mkazo. Je, Serikali inatumia "*water gauges*" katika vyanzo vya mito inayoanzia Msitu wa Hifadhi ya Kilimanjaro ili kudhibiti kwa ufanisi uharibifu wa vyanzo vya hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Doria za anga kwa kutumia helikopta hufanyika katika maeneo ya Mlima Kilimanjaro katika kipindi ambacho hali ya hewa inaruhusu. Mafanikio ya doria kama hizi siyo makubwa kutokana na msitu mnene uliofunga kuzunguka Mlima Kilimanjaro na miteremko, makorongo na mito, na hivyo kusababisha ugumu wa kuwaona wahalifu wa chini. Hali ambayo husababisha helikopta kushindwa kutua katika sehemu nyingi za msitu.

Mheshimiwa Spika, doria nyingi zinazofanyika katika Mlima Kilimanjaro ni zile za miguu ambapo magari huwapeleka askari jirani na maeneo tarajiwa ya doria. Hii imekuwa na ufanisi na mafanikio makubwa na imesaidia sana kudhibiti uhalifu katika hifadhi.

Pamoja na doria za miguu na magari, Shirika la Hifadhi za Taifa litaendelea kutumia helikopta katika kudhibiti uhalifu kwenye maeneo ya wazi katika hifadhi ya Mlima Kilimanjaro na kwenye Hifadhi zingine nchini.

(b) Serikali haina mpango wa kuliagiza Jeshi la Wananchi Tanzania kufanya mazoezi yao ya kawaida katika maeneo ya Hifadhi nchini kwa sababu zifuatazo:-

(i) Mafunzo wanayofanya ni ya utumiaji wa silaha za kivita;

(ii) Mazoezi ya kijeshi kwa kawaida hayafanyiki katika maeneo ya Hifadhi za wanyamapori; na

(iii) Mazoezi haya yakifanyika hifadhini yataathiri utalii.

Aidha, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wengine katika kukomesha ujangili.

(c) Shirika la Hifadhi za Taifa lina Idara ya ikolojia ambayo pamoja na mambo mengine hufuatilia na kukusanya takwimu za hali ya hewa na kupima ubora wa wingi wa maji katika hifadhi ili kushauri na kupendekeza njia za kitaalum za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Kilimanjaro imekuwa ikishirikiana na wataalam wa Bonde la Pangani kupima wingi wa ubora wa maji katika maeneo kumi na tano (15) yaliyopo ndani ya Hifadhi kwa kutumia vifaa vya kisasa kama vile *Advanced Stream Flow Meter* na *Multi-parameter Expech water Quality Mete*r wakati wa kiangazi na masika na kushauri hatua za kuchukua. *(Makofi)*

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu utaratibu wa kutumia Polisi katika *check points* katika hifadhi zetu na hususani

Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro hazijazaa matunda kwa sababu ya uchache wa Polisi. Je, Serikali ipo tayari sasa kutumia wanafunzi wa Chuo cha Polisi yaani *CCP* angalau kwenye mazoezi yao yaani *field attachment* ili kunusuru tatizo hili?

La pili, ili kuendeleza utalii, utafiti na uhai wa ndege na wanyama katika hifadhi zetu kuna haja ya kutunza na kila mara kurejesha bionwai yaani *bio- diversity* iliyopo.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kugawia wananchi wa vijiji jirani na hifadhi zetu miti yote ya asili ili wapande kwenye maeneo yao na hivyo kuwaondoa tamaa kuingia msituni kukataa miti, lakini hasa hasa kurudisha bionwai katika yale maeneo ambayo yameharibika sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, moja, tunamshukuru sana Mheshimiwa Betty kwa kuendelea kuwa na Serikali katika jitihada zake za kuhakikisha kwamba Mlima Kilimanjaro na *integrity* yake inaendelea kulindwa. Na nimjibu tu kwamba Serikali inalishukuru sana Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Wizara yetu katika kuendelea kulinda maliasili na katika kuendelea kudhibiti wahalifu ambao wanatusumbua nchi nzima.

Katika kuwatumia na kushirikiana na Jeshi la Polisi litakuwa ni Jeshi la Polisi lenyewe kuamua kuwatumia wanafunzi wake kama vile ambavyo sisi tunawatumia wanafunzi wa Mweka katika mazoezi mbalimbali yanayoendelea na kufundisha kazi.

Mheshimiwa Spika, la pili, tunaendelea na kufanya ufatifi kwanza, TAWIRI kama Shirika letu muhimu katika utafiti wa wanyamapori, lakini vilevile utafiti ambao unafanywa kwa kusimamiwa na Taasisi yetu ya Misitu *TSF* na tunamhakikishia Mheshimiwa Betty Machangu na wananchi

wa Kilimanjaro na wananchi wote wanaozunguka Mlima Kilimanjaro tutaendelea kupanda miti, tutaendelea kutoa miche ya miti tukishirikiana na Halmashauri zinazozunguka Mlima Kilimanjaro.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, Misitu wa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro unavunwa na wahalifu wakishirikiana na baadhi ya viongozi pamoja na wafanyakazi wa *TANAPA* na taarifa hii tulipewa katika *RCC* na Mkuu wa Mkoa katika utafiti ambao Taasisi moja isiyo ya Kiserikali ilifanya na kuikabidhi kwa Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, naiuliza Serikali lini tutaacha kufanya siasa katika mambo mazito kama haya na kuchukulia hatua wahalifu ambao wanaharibu maliasili zetu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu kwa kifupi pia uzizungumze sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kupambana na wahalifu wa aina yoyote na endapo atagundulika mhalifu yoyote ambaye ni mtumishi katika hifadhi zetu za Taifa hatutasita kabisa kumchukulia hatua na wahifadhi wa Mlima Kilimanjaro wanaendelea sana kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Rombo na mimi mwenyewe nilifika na kuzungumza na Madiwani wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo

Tulizungumza na Mheshimiwa Selasini na katika tatizo lao moja lililojitokeza la tembo kutoka Kenya kuvamia, kuua na kuathiri mazao na wananchi wa Rombo Serikali ilifanya uamuzi haraka tuka-*de-employ* kikosi ambacho kimeendelea kuzuia na wana *technique* za kuweza kuwazuia tembo na kuwafukuza badala ya kulazimika kuwaua. Nafikiri ushirikiano huo tunahitaji na sisi tutazingatia alichokisema Mheshimiwa Selasini. *(Makofi)*

Na. 138

**Kuendeleza Kitalu cha Kigosi North**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Kitalu cha Kigosi North kwenye Pori la Akiba Kigosi kwa muda mrefu kimeachwa bila mwekezaji wa kukiendeleza hivyo kutoa mwanya kwa ujangili na uharibifu wa mazingira:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukiendeleza kitalu hicho ili kiweze kufikia kiwango cha kuweza kuvutia wawekezaji?

(b) Huduma za utalii ni pamoja na kuwepo kwa huduma za hoteli za kitalii.

Je, Serikali itatoa kipaumbele cha mwekezaji wa hoteli kwenye pori hilo la Kigosi *North*?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kwamba kitalu cha Kigosi *North* hakijapata mwekezaji. Hata hivyo, ili kuimarisha ulinzi wa wanyamapori katika kitalu hicho, Serikali ilianzisha kituo cha Lwahika ambapo askari wasiopungua watano wafanya doria za kudhibiti ujangili na uharibifu wa mzingira katika eneo hilo.

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha ulinzi wa eneo hilo ikiwa ni pamoja na kuidadi wanyamapori ili kutambua mwenendo, aina na idadi yao katika eneo hilo. Aidha, miundombinu ya eneo hilo imeendelea kuimarishwa ili kitalu hicho kiweze kufikia kiwango cha kuwavutia mwekezaji.

(b) Wizara inahamasisha wadau wa utalii kuwekeza katika ujenzi wa Loji na Hoteli katika maeneo ya hifadhi na mapori ya akiba na ikiwemo Pori la Akiba la Kigosi.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza, Sheria Namba 5 ya Hifadhi ya Wanyamapori kifungu 23 kinazuia utafiti wa madini mengine yoyote isipokuwa madini ya Urani, mafuta na gesi.

Je, utafiti unaofanywa wa madini ya dhahabu katika kitalu hicho unafanyika kwa sheria namba ngapi? (*Makofi*)

La pili, kwa kuwa, shughuli zinazofanyika katika kitalu hiki hazifahamiki vyema na Madiwani wa Halmashauri ya Bukombe na Mbogwe.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kufanya ziara katika Wilaya yetu ya Bukombe na Mbogwe ili kufafanua jambo hili?

**SPIKA**: Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu wa kifupi sana muda unakwenda.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Maselle kwanza nitafanya ziara hiyo mapema iwezekanavyo baada ya shughuli hizi za Bunge hili la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, swali lake la mwisho ambalo lilikuwa kwanza ni kweli kitalu hicho ni eneo ambalo linafanyiwa utafiti na Kampuni ya Tanzania *American International Corporation* 2000 *Limited* tangu tarehe 26 Septemba, 2005 na Kampuni hii inazo leseni tatu za utafiti ambazo ningeweza kumpa baadaye.

Lakini niseme tu kwamba kuna sheria ambayo imepitishwa na Bunge lako Tukufu kuruhusu utafiti wa aina kadhaa ya madini ikiwemo hiyo ambayo wanafanya Kampuni hii katika maeneo haya ya hifadhi za mapori ya akiba.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, pori hili la Akiba la Kigosi Muyowosi kwa upande wa Mashariki linapakana na Wilaya za Bukombe, Mbogwe na Kahama na kwa kuwa, eneo hili limekuwa ni kichakaa cha majambazi na majangili. Ni lini Serikali sasa inafikiria kuipandisha hadhi eneo hili la Mashariki kuwa Hifadhi ya Taifa ili liweze kuleta tija kwa Taifa badala ya lilivyo hivi sasa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna changamoto kubwa sana ya ujangili na matukio mbalimbali katika maeneo haya aliyoyataja ikiwa ni pamoja na hili pori Kigosi ikiwa ni pamoja na wahamiaji haramu ambao wamekuwa wakitoka nchi za jirani na kujificha hapo. Serikali inalitambua hilo na juhudi za makusudi moja zinafanywa kuendelea kuhakikisha kwamba pori hili linadhibitiwa dhidi ya majangili.

Lakini la pili, utaratibu ambao tunautumia ili kupanda hadhi pori kuwa sehemu ya Hifadhi za Taifa *TANAPA* unazingatia mambo mengi ya kisayansi na sisi tupo tayari kuendelea kufanya utafiti huo na endapo maeneo haya yatakidhi mahitaji au masharti ambayo yanakubaliwa na sheria ya Hifadhi za Taifa hatutasita kufanya hivyo.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kugawa vitalu baada ya marekebisho ya Sheria Namba 5 ya Mwaka 2009. Nilitaka kujua kwa kuwa, vitalu vingi vilivyogawiwa havizingatia uhifadhi yaani ikoloji na inaleta usumbufu sana hasa kwa wanyama na usumbufu kwa baadhi ya wawindaji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia upya ili vitalu hivyo vizingatie uhifadhi.

**SPIKA:**Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna maelezo mengi tofauti ambapo tunaendelea kuyapata kutoka wadau ikiwa ni pamoja na hoja hii aliyoisema Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kwamba baadhi ya vitalu ilikuwa ni kitalu kimoja vikagawiwa vikawa vitalu vitatu, na kwa mantiki hiyo kama kitalu kilikuwa kimoja na kinaruhusiwa kuvuna wanyama 30 kikigawiwa vikawa vitalu vitatu kwa maana hiyo utavuna wanyama 90.

Ni suala ambalo Mheshimiwa Waziri analo tunaendelea kuliangalia na hatutasita kabisa kuchukua hatua ambazo ni za makusudi kuweza kurekebisha dosari ambazo zinaweza kujitokeza kutokana na ushauri ambao tunaupata na majadiliano ambayo yanaendelea katika Wizara na sehemu zingine.

Na. 139

**Kuchimba Mabwawa ya Maji Nanyumbu**

**MHE. DUSTAN D. MKAPA** aliuliza:-

Vijiji vingi vya Wilaya ya Nanyumbu havina maji safi na salama:-

Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuchimba mabwawa ili kuondoa tatizo hilo hasa katika maeneo yaliyoathirika zaidi katika Kata za Sengenya, Chipuputa, Mnanje, Likokona, Mikangaula na Nandete?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dustan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu, Serikali imeanza utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa kuchimba visima virefu vyenye mtandao wa mabomba, kuvuna maji ya mvua kwa kuchimba mabwawa na kuweka mifumo ya uvunaji wa maji ya mvua kwenye mapaa ya nyumba.

Kupitia programu ya Sekta ya Maji, mwaka huu wa 2012/2013, Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu imepanga kutekeleza miradi ya maji katika vijiji vya Ndwika Kata ya Mangaka, Nandembo Kata ya Lumesule, Chivirikiti Kata ya Nandete, Holola Kata ya Mnanje na Chipuputa Kata ya Chipuputa. Ujenzi wa mradi kwenye kijiji cha Ndwika umeanza na vijiji vya Nandembo, Chivirikiti, Chipuputa na Holola viko katika hatua mbalimbali za manunuzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali itajenga bwawa kubwa na kulaza mtandao wa mabomba katika Kata ya Sengenya litakalohudumia vijiji viwili (2) vya Sengenya na Mara kwa gharama ya shilingi bilioni 1.

Serikali pia inaendelea na uhamasishaji wa uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia mapaa ya nyumba. Kwa sasa, Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu inaendelea kujenga mifumo ya uvunaji maji ya mvua katika nyumba za watumishi na jengo la Halmashauri ya Wilaya ili wananchi waweze kuiga teknolojia hiyo.

**MHE. DUSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali la msingi niliomba kujengewa mabwawa ya maji. Nashukuru kupata hilo moja katika Kata ya Sengenya.

Kwa kuwa hivi juzi Wizara ya Maji imeongezewa shilingi bilioni 185. Je, inaweza kunihakikishia kujengewa mabwawa angalau mawili katika Wilaya yangu ya Nanyumbu?

Swali la pili, Serikali itayatumiaje maji ya mto Ruvuma kuwasaidia wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu kupata maji safi na salama?

**SPIKA:** Ahsante kwa kuuliza maswali kwa kifupi na Mheshimiwa Naibu Waziri na wewe ujibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongezewa fedha katika Wilaya ya Nanyumbu kutokana na ongezeko ambalo tumepata juzi nataka kumhakikishia kwamba kama alivyotamka Mheshimiwa Waziri kwamba kila Halmashauri itapata vijiji viwili hii inamaanisha kwamba na Nanyumbu itakuwepo na tutawashirikisha wao sasa waweze kuainisha ni mradi gani uweze kutekelezwa katika hivyo vijiji viwili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya mto Ruvuma naweza nikasema kwamba ni wazo zuri na namshukuru, lakini kwa sasa vyanzo vilivyopo vinatosha kabisa kuweza kuwapatia maji wananchi wa Nanyumbu. Lakini vilevile tujue kwamba hii rasilimali ya maji ya Ruvuma ni rasilimali ya kutumia sisi leo, kesho na baadaye.

Kwa hiyo itakapofikia muda wake tutaweza kufanya utafiti na kuona kama tutatumie yale maji ya mto Ruvuma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilufi swali la nyongeza, sasa usiende kuuliza swali la Mbarali, lazima liwe swali la kisera kwako.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Tatizo la wananchi wa Nanyumbu halitofautiani sana na tatizo la wananchi wa Mbarali.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji kutoka mto Mpeng'o kuelekea Wilayani Mbarali ni tumaini kubwa sana kwa kuhudumia Kata za Mawindi na Ipuani na baadaye Igava, Rujewa, Ubaruku na Songwe Malilo.

Je, ni lini utekelezaji wa mradi huu utaanza kwa sababu upembuzi yakinifu ulishafanyika?

**SPIKA:** Sijui kama Waziri anakumbuka, kama hukumbuki ni swali geni kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze amekuwa akifuatilia sana mradi huu. Nimhakikishie kwamba katika miradi iliyoombewa fedha na Kamati ya Kudumu ya Bunge inahusisha mradi huu pia wa kutoa maji kutoka Njombe kwenda Mbarali ambao utafaidisha vijiji vya Wanging'ombe na vijiji vya Wilaya ya Mbarali. *(Makofi)*

Na. 140

**Tatizo la Maji – Kata ya Mbokomu**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO** aliuliza:-

Tatizo la Maji katika Kata ya Mbokumu hususan Vijiji vya Korini Kusini, Juu na Tema pamoja na Vitongoji vyake limekuwa la muda mrefu sana hivyo kuathiri Wakazi hao:-

(a) Je, ni lini tatizo hili litakuwa historia?

(b) Kwa kuwa, vyanzo vya maji havikidhi mahitaji ya wakazi wa maeneo hayo; Je, Serikali haioni uwezekano wa kuwa na vyanzo mbadala vikiwemo vile vya maji ardhini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, vijiji vya Korini Kusini na Korini Juu ni miongoni mwa vijiji vilivyowekwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maji chini ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Ujenzi wa miundombinu ya maji katika vijiji hivyo umeanza tarehe 14 Januari, 2013 na umepangwa kukamilika mwezi Septemba, 2013 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.027.

Aidha, hivi sasa kijiji cha Tema kinapata huduma ya maji kwa asilimia 75. Huduma ya maji kwa kijiji hicho itaongezeka baada ya mradi wa maji wa Korini Kusini na Korini Juu kukamilika ambapo maji yote yaliyokuwa yakitumika kwa vijiji vya Korini Kusini na Korin Juu yatatumika kwenye kijiji cha Tema.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na jiografia ya Kata ya Mbokumu pamoja na aina ya miamba iliyopo, uwezekano wa kupata maji chini ya ardhi ni mdogo sana.

Hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini imetafuta chanzo mbadala cha chemchem ya Mrusunga chenye uwezo wa kutoa maji kiasi cha lita za ujazo 859,200 kwa siku. Kiwango hicho cha maji kinakidhi mahitaji ya maji kwa wakazi wa Korini Kusini na Korini Juu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake na nakubaliana naye kwa sababu nimetoka huko juzi na nimekuta tayari wananchi wanachimba mitaro.

Mheshimiwa Spika, lakini ni kweli pia kwamba miamba ya Kata ya Mbokumu ni migumu sana kwa ajili ya kutoa maji. Lakini tuna chanzo kingine kizuri sana cha maji katika chemchem ya Mangi pale Rau ambapo tayari wananchi

wamechangishana zaidi ya shilingi milioni 20 na ilikuwa imebakia shilingi kama milioni 100 ili waweze kumaliza lakini uwezo wao ndio huo.

Nilikuwa naomba Serikali itoe tamko kama inaweza kuwasaidia wananchi wale shilingi hizo milioni 100 ili waweze kukamilisha mradi huo hasa ikizingatiwa kwamba idadi ya watu katika vijiji hivyo au Kata hiyo inazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Kata ya Makongo Dar es Salaam vilevile kuna tatizo kubwa sana la maji na Serikali iliahidi mwaka jana kununua pampu kubwa ili kuweza kusukuma maji katika mitaa ya Mbuyuni pamoja na mtaa wa Makongo.

Nilikuwa naomba kujua ni lini Serikali itakamilisha ahadi yake hiyo ili wananchi waweze kupata maji safi na salama? (*Makofi)*

**SPIKA:** Sasa na Makongo imeingiaje haya.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze na nimshukuru kwa kutupa shukrani kwamba mradi ule umeanza. Lakini nimhakikishie kwamba Serikali hii ipo tayari kushirikiana na wananchi kwenye mradi ule ambao wao wameuanzisha. Kwa hiyo, tutalichukua, tutalifanyia kazi na ni moja ya miradi ambayo inaweza ikaingizwa kwenye hivi vijiji viwili ambavyo tumetangaza kama mtapewa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu mradi wa Makongo hili ni swali jipya naomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane ili kufuatilia vizuri na kumpa jibu sahihi kuhusu kinachoendelea Makongo.

Na. 141

**Athari za Vituo Vingi Vya Mizani Kwa Wafanyabiashara**

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH (K.n.y. MHE. MKIWA A. KIMWANGA)** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sana wadau wa usafirishaji na wafanyabiashara wa nchi jirani wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam wamekuwa wakilalamikia urasimu uliopo barabarani unaotokana na vituo vingi vya Mizani, TRA, na kusimamishwa mara kadhaa na Askari wa Usalama Barabarani jambo linalowafanya kuchelewa Bandarini na ama kuharibika kwa bidhaa walizobeba:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kuondoa adha hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sheria ya Usalama Barabarani "*The Road Traffic Act. 1973" (No. 30 of 1973)* na "*The Road Traffic Maximum Weight of Vehicles Regulations*" ya mwaka 2001 magari yote yenye uzito kuanzia tani 3.5 na kuendelea yanatakiwa kuingia kwenye vituo vya mizani na kupima uzito wakati wa safari zao, hivyo Wizara inatekeleza sheria katika kupima magari hayo.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la kupima magari ni kulinda barabara na madaraja ambayo ujenzi wake unaligharimu Taifa fedha nyingi sana.

Hata hivyo uzoefu unaonyesha kuwa pamoja na wasafirishaji kufahamu tunayo mizani, zaidi ya asilimia 25 ya magari yanayopima kwenye mizani hubainika kuzidisha uzito na hivyo kuchangia katika kuharibu barabara. Bila shaka hali ingekuwa mbaya zaidi endapo wasingekuwa na mizani ili waweze kupima.

Mheshimiwa Spika, vituo vilivyopo vimewekwa kwa kuangalia uwezekano wa kupima magari mengi kwa wakati mmoja. Vituo hivyo ni *Central Corridor* yenye kilometa 1297 na vituo 7, *Dar es Salaam Corridor (Tanzam Corridor)* yenye kilometa 915 na vituo 5, *South Coast Corridor* yenye kilometa 556 na vituo 3, Kaskazini Mashariki (*Northern East*) yenye kilometa 786 na vituo 3.

Hatua mbalimbali zimechukuliwa ili kuongeza ufanisi na kupunguza msongamano kwenye vituo vya mizani. Hii ni pamoja na kuweka mizani pande zote mbili za barabara kwenye vituo ambavyo vilikuwa na mzani upande mmoja; kuajiri wafanyakazi wapya wa vituo vyote vya mizani walio na sifa zaidi na pia mpango wa kujenga mizani za kisasa (*multi deck and weigh in motion*) kwa kuanzia na eneo la Vigwaza.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwaelimisha wasafirishaji mujibu wa kufuata sheria ili wajiepushe na uzidishaji wa mizigo katika magari yao ili kuepuka usumbufu. Aidha, Wizara itaanzisha mfumo wa kisasa zaidi wa kupima magari hayo tukianzia na mizani itakaojengwa eneo la Vigwaza.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswala mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya nchi za Afrika Mashariki, Tanzania ni nchi ya kwanza inayoongoza kwa urasimu na rushwa barabarani. Hii inatokana kwa kuwa Tanzania ina vituo vingi sana vya ukaguzi wa magari. Kwa mfano kutoka Dar es Salaam hadi Lusumo ina vituo 30. Je, Mheshimiwa Waziri ni lini ataondoa usumbufu huu.

Swali la pili, wafanyabiashara wengi wamekuwa wanalalamika kwa kuchelewa mizigo yao kufika mahali inapokwenda, kwa sababu ya vituo hivi vingi. Je, Mheshimiwa Waziri haoni itasababisha wafanyabiashara wahamie nchi nyingine na kuikosea mapato Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa sikubaliani naye kwamba kuna utafiti unaonyesha kwamba Tanzania tunaongoza kwa urasimu na rushwa. Suala la rushwa ni tabia ya watu na hiyo huwezi kusema Tanzania tunaongozwa, kwa hiyo hiyo naikataa. Pia si kweli kwamba tuna vituo vya mizani 30 kwenda Rusumo, tuna vituo 7 kwenye *Central Corridor* na tumeshaeleza.

Kwa hiyo vituo ambavyo katika suala la msingi tunazungumzia vituo vya mizani, sasa hivyo vituo vingine 30 mimi sivifahamu. Ndio najua kwamba kweli kuna haja ya kuangalia muda ambao msafirishaji anatoka Bandarini kwenda kwa mfano Rusumo labda badala ya kuchukua siku 3 iweze kuchukua siku 2.

Suala hili tunaliangalia na ndiyo maana nimesema kwamba tunajenga vituo na mizani ya kisasa zaidi ambayo gari litakuwa halisimami linapita linapima huku linakwenda. Kwa hiyo kwa namna hiyo muda wa kusafiri utakuwa ni mfupi zaidi na tutaweza kusafirisha mizigo kwa muda mfupi na kuongeza uchumi kwa haraka zaidi.

Na. 142

**Kukabiliana na Tatizo la Usafiri Dar es Salaam**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU( K.n.y. MHE. FATUMA A. MIKIDADI**) aliuliza:-

Pamoja na jitihada za Serikali za kuongeza barabara katika bajeti hii kwa kuweka barabara za juu *flyover* katika Jiji la Dar es Salaam lakini bado msongamano wa magari na watu katika Jiji hilo bado ni mkubwa:-

Je, wakati Serikali ikiendelea na mpango wake wa kuweka *"flyover"* haiwezekani kuweka mpango wa dharura wa usafirishaji wa abiria kutumia Reli kwenye maeneo ya Ubungo, Tabata, Mabibo, Buguruni, Yombo Vituka na Tabata Relini japo kwa asubuhi na jioni tu kama zinavyofanya nchi za Harare na Afrika Kusini?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ushauri wake ambao hata hivyo Serikali ilikwishaliona jambo hilo na katika mwaka huu wa fedha 2012/2013 imeanzisha huduma za usafiri wa abiria kwa njia ya reli katika Jiji la Dar es Salaam kwa lengo la kupunguza msongamano barabarani na msongamano wa abiria ndani ya mabasi.

Katika kutekeleza mpango huo, Taasisi zinazohusika, yaani *RAHCO, TRL* na *TAZARA* ziliboresha miundombinu ya reli iliyopo katika Jiji la Dar es Salaam kwa kuifanyia ukarabati pamoja na kuvifanyia matengenezo vichwa vya treni na mabehewa ambavyo vinatumika katika kutoa huduma hiyo. Huduma za usafiri wa treni kwa reli zote mbili *(TAZARA* na *TRL)* katika Jiji la Dar es Salaam zilianza tarehe 29 Oktoba, 2012.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Reli ya Kati *(TRL)* huduma hiyo ni ya kuanzia Stesheni ya Ubungo Maziwa hadi Stesheni ya Dar es Salaam. Usafiri huo una vituo vingine vya abiria sita (6) katika sehemu za Kamata, Buguruni kwa Mnyamani, Tabata Reli, Tabata Mwananchi, Makuburi na Mabibo. Huduma zinatolewa kwanzia saa 12.20 hadi saa 5.14 asubuhi na kutoka saa 10.00 jioni hadi saa 3.46 usiku.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *TAZARA,* huduma hiyo ni ya kuanzia Stesheni ya Mwakanga hadi Kurasini na Mwakanga hadi *TAZARA* Stesheni. Vituo vya kati vipo sehemu ya Kwa Fundi Umeme, Yombo kwa Limboa, Lumo Kigilagila, barabara ya Kitunda, Kipunguni B, *Moshi Bar,* Majohe, Shule

ya Sekondari Magnus, Mwakanga, Chimwaga, Maputo, Mtoni Relini, Kwa Azizi Ali na Kurasini. Huduma zinatolewa kuanzia saa 10.45 alfajiri hadi saa 5.04 asubuhi na kutoka saa 10.00 jioni hadi saa 4.00 usiku.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningependa nimwulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza kwamba huduma ya Reli ya Kati yaani *(TRL)* hakuna kutoka Pugu kwenda Jijini ambapo ingeweza kuwasaidia wakazi wa Gongo la Mboto, Pugu pamoja na wakazi wa maeneo ya Ukonga. Nini mpango wa Serikali wa kuanzisha huduma hii kutoka Pugu kwenda Jijini?

La pili, nini mpango wa Serikali kuboresha huduma ya reli ambayo itasaidia sana kupunguza *traffic volume* kutoka Bandarini kwenda katika maeneo mengine ya ndani na nje ya nchi hii ikiwa ni pamoja na mradi ule wa ujenzi wa *Truck Port* pale Kisarawe ambao utasaidia sana kupunguza mizigo ambayo inatoka Bandarini na kuweza kuunganishwa kwenye *access* ya barabara kuu kwenda katika nchi za jirani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi nina dakika 5 tu kwa maswali matatu yaliyobaki.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kuweka usafiri wa treni pia katika hiyo njia ya Reli ya Kati kuanzia stesheni kuelekea Pugu na ikiwezekana hadi Morogoro. Ziko treni maalum kwa ajili hiyo ambazo tuko katika mchakato wa kutafuta fedha na tukizipata hizo tutanunua *diesel multiply units* ambazo zinaweza kutoa huduma hizo za kati ya Pugu Stesheni au Morogoro kwa urahisi zaidi, kwa hivyo huo mpango upo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uimarishaji wa Reli ya Kati kwa ujumla naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira tarehe 16 Mei, 2013 tutatoa kwa urefu sana mkakati uliopo wa Serikali wa kuboresha Reli ya Kati kwa ujumla hapa nchini.

Na. 143

**Ukarabati wa Viwanda Vya Nguo Nchini**

**MHE. HUSEIN N. AMAR** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua jukumu gani la kuvikarabati vya nguo kama vile Mwatex ili mkulima aweze kuuza pamba yake kwa bei yenye faida?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'wale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwea Spika, Serikali imekuwa ikitoa unafuu wa kodi *(Tax Remmision)* kwa wawekezaji wanaoingiza mashine na mitambo kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa viwanda vyote vikiwemo viwanda vya nguo kama vile *MWATEX (Mwanza) MUTEX (Musoma), 21 Century (Morogoro) Sunflag (Arusha)* na kadhalika. Unafuu huo wa kodi unatoa fursa kwa wawekezaji wenyewe kuweza kutumia teknolojia ya kisasa, kuzalisha kwa ubora kwa ajili ya mauzo ya ndani na nje ya nchi na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa viwanda vya nguo nchini, Serikali kwa kupitia Mamlaka ya kutenga maeneo huru ya uzalishaji kwa mauzo ya nje *(EPZA),*imetenga maeneo ya kipaumbele ambapo hadi hivi sasa jumla ya viwanda 13 vya kutengeneza nguo *(Textiles)* vimejengwa.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa viwanda hivyo, viwanda vitakuwa na uwezo wa kusindika na kuongeza thamani ya pamba inayolimwa na wakulima wa hapa nchini na hivyo kuwawezesha kuuza pamba yao kwa bei yenye faida.

**MHE. HUSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanatia matumaini kwa wakulima wa pamba. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani wa viwanda hivi kuvibaini ni viwanda vingapi mpaka sasa hivi vinafanya kazi.

(b) Viwanda hivi vikiwa vinafanyakazi ina maana vitaongeza ajira kwa Watanzania. Je, ni viwanda vingapi mpaka sasa hivi vinafanya kazi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza kuwa ni viwanda vingapi vinavyofanya kazi. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kuwa *MUTEX* ya Musoma, *MWATEX* ya Mwanza viwanda hivi vyote vinafanya kazi ingawa hapo mwanzo vilikuwa vina suasua lakini kwa sasa hivi vinafanya kazi kwa ukamilifu na wawekezaji wameonyesha nia kubwa sana na uwezo mkubwa sana wa kuviendeleza viwanda hivi ili viweze kufanya kazi.

Kwa takwimu kidogo ni kwamba MWATEX sasa hivi wanaweza kuajiri wafanyakazi baada ya kuwa umeme kuwa ume - *stabilize* hadi kufikia 1000. *MUTEX* Wanaweza kuajiri hadi 200, URAFIKI wanaweza kuajiri wafanyakazi 760 na hii inaendana na teknolojia ya kisasa kama kiwanda kinatumia teknolojia ya zamani bado wale wafanyakazi wa zamani wataendelea kuwepo lakini sehemu kubwa ya viwanda hivi kwa kushirikiana na kilimo vinaendeshwa na vijana.

Mheshimiwa Spika, MWATEX sasa hivi ninapoongea wameanzisha training wing ambayo inayofundisha kwa ajili ya teknolojia ya kisasa katika viwanda hivi. Ajira kwa vijana kwa sasa hivi imeshika kasi hasa kwasababu ya teknolojia ya kisasa na kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kuwa viwanda hivi vinafanya kazi.

Serikali kwa sasa inavifuatilia kwa karibu sana kuhakikisha kuwa viwanda hivi vinafanya kazi vikiwemo na viwanda vingine mbali na *MWATEX,* kuna URAFIKI kinafanya kazi, kuna *TWENTY FIRST CENTURY* cha Morogoro kinafanya kazi, AFRITEX cha Tanga kinafanyakazi pamoja na *Tabora Mills* nayo inafanyakazi kwa kutumia pamba.

Na. 144

**Ukarabati wa Bwawa la Ikowa**

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE** aliuliza:-

Ukarabati wa skimu ya umwagiliaji ya Chalinze unaoendelea hivi sasa umeshaanza kuwalea manufaa baadhi ya wakulima kwa kuwapatia mazao ya chakula na biashara kwa kipindi kifupi cha msimu wa mwaka:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kulikarabati Bwawa la Ikowa linalotoa maji ya kutosheleza shughuli za kilimo cha umwagiliaji kwa mwaka mzima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje Mbunge wa Chilonwa, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika,Bwawa la Ikowa lilijengwa kati ya mwaka 1957 na 1958 kupitia Idara ya Maji na Umwagiliaji *(WD&ID)* kwa madhumuni ya kilimo cha umwagiliaji kwa eneo la hekta 40 na kwa matumizi ya Mifugo na Binadamu. Baada ya bwawa hilo kutumika kwa takribani miaka 32, lilijaa tope kutokana na uharibifu wa mazingira ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za kibinadamu na mifugo na hivyo kupunguza uwezo wake wa kuhifadhi maji.

Aidha, katika kipindi hicho bwawa hilo lilikumbwa na tatizo la kumomonyoka kwa tuta upande wa juu *(Upstream)*kutokana na kujaa na kupwa kwa maji *(water wave action)*ambapo kujaa tope na kumomonyoka kwa udongo wa tuta kuendelea hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya upembuzi gharama inayohitjika kurejesha uhai wa bwawa hilo ni takribani shilingi bilioni 2.5. Kwa ajili ya kuongeza kimo cha la bwawa kwa meta moja(1), wa tuta kwa km1, na kukarabati sehemu ya juu *(upstream)* ya tuta.

Mheshimiwa spika, baada maelezo hayo, naomba kujibu swali la mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mfuko wa kuendeleza kilimo cha umwagiliji ngazi ya Wilaya *(DIDF)*ilitenga shilingi milioni 300 kwa mwaka wa fedha 2010/ 2011, na shilingi milioni 300 mwaka 2011/2012. Hata hivyo, kutokana na gharama kubwa za kukarabati bwawa hilo fedha hizo hazikutosha kukamilisha ukarabati huo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa skim ya Chalinze kwa wananchi wa Chilonwa fedha hizo zilielekezwa kwenye ukarabati wa skim ya Chalinze ambayo maji yake yanatokana na bwawa la Ikowa ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na kusakafia mfereji mkuu wenye urefu wa kilomita 4 na kuboresha barabara yenye urefu wa km 2.5, kujenga vigawa maji 11 na kukarabati sehemu tuta inayokinga maji ya mvua yasiharibu tuta la bwawa lililobomoka urefu wa meta 64.

Mheshimiwa Spika, kutokana na gharama kubwa ya ukarabati wa bawawa hilo, Serikali inaendelea kutafura fedha kwa ajili ya kukarabati bwawa hilo ikiwa ni pamoja na kutenga fedha za kutosha katika bajeti ya Serikali na kuandaa maandiko ya kuombea fedha kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha kama vile mfuko wa pamoja wa Msaada wa Chakula unaosimamiawa na Serikali ya Tanzania

na Japan *(Food Aid Counterpart Fund (FACF)* ili kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kumalisha ukarabati wa bwawa hilo kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Chilonwa na Mkoa wa Dodoma.

**MHE.HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, ninakusuhukuru sana kwa nafasi hii, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimkwa Waziri, nina maswali mawili:-

(a) Mheshimiwa Waziri amesema kuwa Serikali inaendelea kutafuta fedha kupitia Bajeti ya Serikali ningependa kujua mpaka sasa ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa Bwawa hili?

(b) La pili, amesema kuwa kuna utaratibu wa kupelela maandiko katika vyombo mbalimbali ili kuombea fedha, ninapenda pia kujua maandiko haya yamepelekwa katika vyombo vipi na mchakato wake umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, tumesema Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya mradi huu wa Chalinze na gharama zake tumesema kwa kupata ukamilifu ili turudishe katika hali ya zamani zinatakiwa bilioni 2.5 hizo ni hela nyingi sana.

Kwa hiyo, tunachofanya tunakadiria kuangalia kama tunaweza kufanya marekebisho kwa awamu ili wananchi wanaotumia skim ile wapate matumizi ambayo yanaweza kusaidia katika kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, maandiko yanayofanyika, yanafanyika na kanda ya Umwagiliaji kwa maana ya *Zonal Department* kwa Kanda hii ya Katikati ambayo Makao Makuu yake yako Dodoma, maandiko haya yanajumuisha miradi ambayo iko Wilaya ya Bahi, Kondoa, Chilonwa, Kongwa na maeneo yote haya. Jana tulikuwa Wilaya ya Bahi tumeanz kupitia miradi ya Wilaya ya Bahi tutafika mpaka miradi hiyo ya Chilonwa Kondoa na kadhalika ili tupate tathimini ya miradi ya Umwagiliaji kwa Kanda hii ya kati kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa chakula katika Kanda hii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Muda umekwisha na tumechukua muda wa dakika zingine huko. Kwa namna ya pekee sana, ninapenda kutambua uwepo wa Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Tanzania Mheshimiwa Mohammed Chande Othman. *(Makofi)*

Pia Jaji Kiongozi Mahalama Kuu ya Tanzania Mheshimiwa Faki Jundu ninaomba usimame wapo na Majaji wengine lakini pia kwa namna ya pekee nitambue uwepo wa Maaskofu kumi wa Kanisa la Sabato Tanzania wako hapa Dodoma kwa shughuli zao. Ninaomba wasimame Maaskofu pale walipo asanteni sana na ninaomba muombee nchi hii iendelee kuwa ni nchi ya Amani, nchi ya utulivu na nchi ya upendo kama inavyostahili na sisi humu mtuombee tu si mnatujua mambo yetu? Ahsanteni sana na karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, nitangaze shughuli za kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria na Utawala Mheshimiwa Pindi Chana anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa leo watakuwa na Kikao cha Kamati saa saba mchana, kukutana na Tume ya Mipango na Kikao hicho kitafanyika katika Hoteli ya *VETA.* Kwa hiyo, wanakwenda *VETA* hawa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake watakuwa na Kikao saa saba mchana leo, katika ukumbi namba 227. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Mheshimiwa James Lembeli anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa leo saa saba na robo watakuwa na Kikao katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati kuwa leo saa saba mchana watakuwa na Kikao cha Kamati katika ukumbi namba 231. Kwa hiyo, hizo ndizo kazi zitakazofanyika mchana. *(Makofi)*

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne 2012

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu ninapenda kutoa Kauli ya Serikali Bungeni kuhusu taarifa ya awali ya Tume ya Taifa ya Kuchunguza Matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha nne mwaka, 2012.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 49 (1)ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la mwaka 2007 ninaomba kuwasilisha taarifa ya awali ya Tume ya Taifa ya Kuchunguza matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha 2012. Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2012, yalionyesha kuwa kiwango cha ufaulu kimeshuka kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na miaka ya hivi karibuni.

Matokeo yaliyotangazwa mwezi Februari, 2012 yalionyesha kuwa kati ya wanafunzi laki tatu na sitini na saba, mia saba hamsini na sita waliofanya mtihani huo, watahiniwa laki moja na ishirini na sita elfu, mia nane na arobaini na saba ndiyo waliofaulu.

Katika idadi hii wanafunzi waliofaulu katika daraja la kwanza hadi la tatu ni ishirini na tatu elfu mia tano na ishirini sawa na 6.4% na daraja la nne ni laki moja na tatu, mia tatu ishirini na saba sawa na 28.1%.

Mheshimiwa Spika, watahiniwa laki mbili na arobaini, mia tisa na tisa sawa na 65.5% ya wanafunzi wote waliofanya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2012, walipata daraja la sifuri. Kushuka kwa kiwango cha ufaulu kulihusu shule za aina zote yaani sekondari za Serikali ikijumulisha zilizojengwa kwa nguvu za wananchi, shule binafsi na Seminari na takwimu zinaonyesha kuwa ukilinganisha na matokeo ya kidato cha nne mwaka 2011 na mwaka 2012 shule za wananchi matokeo yao yameshuka kwa 1.82%, shule za umma zile za zamani zile kongwe yameshuka kwa 6.43%, shule binafsi yameshuka

kwa 6.39%,na kwa shule za Seminari yameshuka kwa 7.29% hali hii inaonyesha kuwa matokeo katika shule za wananchi yameshuka kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na yale ya shule za umma za zamani yaani zile kongwe.

Mheshimiwa Spika, shule binafsi na shule za Seminari ambazo zilitegemewa kufanya vizuri zaidi ya zile za wananchi ambazo matokeo yake yameshuka zaidi kwa 6.4% na 7.3%. Kutokana na matokeo hayo yasiyoridhisha na ambayo yako nje kabisa ya mwenendo wa ufaulu kwa miaka ya karibuni Serikali iliamua kuunda Tume ya kuchunguza kushuka kwa kiwango cha ufaulu wa mtihani wa Taifa wa Kidatocha nne mwaka 2012, kwa madhumuni ya kupata ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, Hadidu za Rejea. Tumeya Uchunguzi ilipewa hadidu za Rejea zifuatazo:-

(1) Kubainisha sababu za matokeo mabaya ya mitihani wa kidato cha nne mwaka 2012.

(2) Kubaini sababu za kushuka sababu za kushuka kwa ufaulu wa Mtihani wa Taifa wa Kidato cha nne mwaka 2011/ 2012.

(3) Kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua kukabiliana na tatizo la mwenendo wa kushuka kwa kiwango cha elimu mara moja, kipindi cha muda mfupi, kati na kipindi cha muda mrefu.

(4) kutathimini nafasi ya Halmashauri katika kusimamia Elimu ya Sekondari katika Halmashauri zake.

(5) Kuainisha sababu nyingine zinazoweza kuwa zimechangia hali hii ya matokeo.

Mheshimiwa Spika, katika kutafakari Hadidu za Rejea hizo Tume imejikita katika kujibu maswali makuu matatu:-

(1)Kwa nini matokeo ya kidato cha nne kuanzia mwaka 2008 yamekuwa na mserereko wa kushuka kuliko miaka iliyotangulia?

(2) Kwa nini wanafunzi wa Kidato cha nne wa mwaka 2012, matokeo yao yalikuwa mabaya kuliko ya wenzao ya mwaka 2011, pamoja na kuwa ufaulu ulishuka tangu mwaka 2008?

( 3) Nini kifanyike?

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Tume ya Uchunguzi; Tume ya Uchunguzi iliongozwa na Professor Sifuni Mchome kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania na ndiye alikuwa Mwenyekiti, Wajumbe wengine walioteuliwa waliteuliwa kutoka Baraza la Wawakilishi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Madhehebu ya Dini, Chama cha Walimu, Muungano wa wenye shule binafsi na Muungano wa Walimu wa Sekondari. Orodha ya Wajumbe wa Tume hii ni kama ifuatavyo:-

(1) Professor Sifuni Mchome – Tume ya Vyuo Vikuu Mwenyekiti.

(2) Mheshimiwa Bernadetha Mshashu- Bunge la Jamhuri ya Muungano – Makamu Mwenyekiti.

(3) Mheshimiwa Abdul Marombwa – Mbunge na Mjumbe

(4) Mheshimiwa Suleiman Hamis - Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

(5) Mwalimu Honorata Chitanda – Chama cha Walimu Tanzania.

(6) Ndugu Rakesh Rajan- Twaweza.

(7) Mwalimu Daina wa Temu- Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari.

(8) Mwalimu Kizito Innocent Lawa – Taasisi ya Elimu Tanzania.

(9) Mwalimu Mbarouk J. Makame- Baraza la Elimu Zanzibar.

(10) Professor Mwajabu Posi- Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

(11) Mwalimu Nurdin Mohammed – Chuo cha Ualimu cha Halmain.

(12) Ndugu Peter Maduki- Baraza la Kikristo Huduma za Kijamii.

(13) Ndugu Mahmoud Mringo- Chama cha Wamiliki na Mameneja shule na vyuo visivyo vya Kiserikali.

(14) Ndugu Abdalah Mohammed – Chuo Kikuu Taifa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Tume ya Uchunguzi. tarehe 28 Aprili, 2013, Tume ya Uchunguzi wa Matokeo ya Kidato cha nne mwaka 2012, ilikamisha kazi yake katika awamu ya kwanza na kutoa taarifa ya awali. Uchambuzi wa taarifa hiyo ya awali unaonyesha kuwa kutokana na Uchunguzi uliofanyika kwa muhtasari Tume imebaini mambo muhimu yafuatayo:-

Matokeo ya kidato cha nne kuanzia mwaka 2008, yamekuwa na mserereko wa kushuka kuliko miaka iliyotanguliwa kwasababu mbalimbali ikiwemo changamoto zinazotokana ya mafanikio yaliyopo sana ya kuongozeka sana kwa idadi ya shule za msingi na sekondari hususani katika mwaka 2001 na sasa 2013, na hivyo kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi walioko shuleni kwa mfano; katika kipindi cha mwaka 1961 hadi 2001 idadi ya wanafunzi wa shule ya msingi imeongezeka kutoka laki nne na themanini na sita elfu, mia nne sabini mwaka 1961hadi milioni nne, laki nane sabini na tano elfu, mia saba sitini na nne mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, sawa na ongezeko la milioni nne, mia tatu, themanini na tatu themanini na tisa elfu, mia mbili tisini na nne katika kipindi hicho cha takribani miaka arobaini,hata hivyo, kati ya mwaka 2001 hadi 2012 wanafunzi wameongezeka kutoka milioni nne, laki nane na sabini na tano elfu, mia saba sitini na nne mwaka 2001 hadi milioni nane mia mbili arobaini na saba elfu mia nne sabini na mbili mwaka 2012, sawa na ongezeko la wanafunzi milioni tatu laki tatu na sabini na moja elfu mia saba na nane katika kipindi cha takribani miaka 11 na hivyo kufanya jumla ya wanafunzi wote wa shule za msingi kuwa milioni nane, laki mbili na arobaini na saba elfu mia nne sabini na mbili mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka elfu kumi na moja, mia nane thelathini na mbili mwaka 1961, hadi laki mbili themanini na tisa elfu mia sita tisini na tisa mwaka 2001, ambayo ni sawa na ongezeko la wanafunzi laki mbili sabini na nne elfu, mia nane sitini na saba katika kipindi hicho cha miaka arobaini. Lakini kati ya mwaka 2001 hadi 2012 idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka laki mbili themanini na tisa elfu, mia sita tisini na tisa mwaka 2001, hadi milioni moja laki nane na themanini na nne elfu mia mbili sabini, mwaka 2012, sawa na ongezeko la wanafunzi milioni moja laki tano tisini na nne elfu mia tano sabini na moja katika kipindi cha miaka kumi na moja tu.

Mheshimiwa Spika, juhudi hizi zimetokana na mpango ulioandaliwa chini ya mpango wa maendeleo ya Sekta ya Elimu wa Mwaka 1999, mipango hii ni pamoja na:-

(i) Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi MMEM wa mwaka 2000 ambapo MMEM I ambayo ililenga katika kufungua shule zaidi ili wanafunzi wengi wa rika lengwa waweze kujiunga na elimu ya msingi. MMEM II ambayo ililenga katika kuboresha ubora wa elimu iliyotolewa katika shule za elimu za msingi na MMEM III ambayo ililenga katika kuendelea kuimarisha ubora wa elimu ya msingi baada ya mafanikio ya MMEM ya I na II.

(ii) Mpango wa elimu ya sekondari MMES kwa mwaka 2004 ambapo MMES I ambayo ililenga katika kufungua shule zaidi za sekondari katika ngazi za Kata ili wanafunzi wengi zaidi wanaomaliza elimu ya msingi waweze kujiunga na elimu ya sekondari kidato cha kwanza. MMES II ambayo ililenga katika kuendelea kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari kadri idadi ya wanafunzi wa elimu ya sekondari wanavyoendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoambatana na mafanikio haya ni pamoja na mazingira yasiyoridhisha ya kufundishia na kujifunzia ikiwemo upungufu wa miundombinu muhimu ya shule kama vile madarasa, maabara, madawati, maktaba, nyumba za walimu, hosteli na majengo mengine muhimu ya shule. Vilevile kuna tatizo la uhaba wa walimu, vitabu, zana za kufundishia na matatizo ya ukaguzi wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Tume imebaini kuwa, mfumo wa elimu ya msingi na sekondari unakabiliwa na changamoto nyingine mbalimbali ambazo Taifa linapitia kwa sasa ikiwemo masuala ya kisera, kisheria, kimfumo, kimuundo pamoja na changamoto za uhaba wa rasilimali fedha na rasilimali watu. Tume inaendelea kufanyia kazi maeneo haya kwa kushirikiana na watalaam na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matokeo ya kidato cha Nne ya mwaka 2012, Tume imebaini kwamba pamoja na wanafunzi hawa kuwa katika mazingira yanayofanana na yale ya wenzao wa miaka iliyopita na kwamba ufanisi katika shule kwa ujumla umekuwa unashuka kwa sababu mbalimbali, ufaulu wao umeshuka zaidi kwa sababu ya mabadiliko ya mchakato wa kuandaa na kutoa matokeo ya mtihani wa mwaka 2012. Mfumo uliotumika mwaka 2012 katika kupanga matokeo ya madaraja ni tofauti na ule uliotumika mwaka 2011 na miaka iliyotangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchunguzi unaonesha kuwa, mwaka 2011 Baraza la Taifa la Mitihani lilikuwa linachakata alama za mwisho kwa kutumia mfumo ambao ulikuwa unabadilika kutegemea hali ya ufaulu wa wanafunzi ambao

ni National Min *Difference (NMD).* Utaratibu huu ulitokana na tofauti ya wastani wa Kitaifa wa alama za maendeleo kutoka alama za maendeleo endelevu *Continuity Assessment (CA)* na watahiniwa wote na wastani wa Kitaifa wa ufaulu wa mitihani ya mwisho kwa somo husika. Kila mtahiniwa aliongezewa *National Min Difference* iliyokokotolewa katika alama za mtihani wa mwisho ili kupata alama itakayotumika katika daraja la ufaulu. Kimsingi kila somo lilikuwa na *NMD* yake kulingana na *continuity assessment* zilivyo katika mwaka husika. Lakini mwaka 2012 ilitumia mfumo mpya wa kuwa na viwango maalum vya kutunuku *fix grade range*. Tume imebaini kwamba pamoja na kwamba mfumo huo uliandaliwa kwa nia nzuri utaratibu huo mpya haukufanyiwa utafiti na maandalizi ya kutosha kabla ya kutumika.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya awali ya Tume, kwa kuzingatia masuala mbalimbali yaliyojitokeza wakati wa uchunguzi, Tume katika taarifa yake ya awali imetoa mapendekezo mbalimbali yakiwemo yale yanayohitaji kutekelezwa kwa haraka na kutokana na kuwepo na mapendekezo hayo ambayo inabidi yafanyike kwa haraka tarehe 29 Aprili, Baraza la Mawaziri lilipokea taarifa ya awali ya Tume na kuijadili ambapo liliridhia Mapendekezo hayo yaanze kutekelezwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, maamuzi ya Baraza la Mawaziri yanalenga kutenda haki kwa Walimu na Wanafunzi ambao juhudi zao za kufundisha na kujifunza zimepimwa kwa kutumia mfumo mpya ambao hawakupata fursa ya kushirikishwa na kuandaliwa. Mapendekezo hayo ni kama yafuatayo:

(i) Matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne 2012 yafutwe na yaandaliwe upya kwa kutumia utaratibu uliotumika mwaka 2011. (*Makofi*)

*(ii)* *Standardization* ifanyike ili matokeo ya wanafunzi yalingane na juhudi walizoziweka katika kusoma kwa mazingira na hali halisi ya Tanzania na uamuzi wa Taifa kuongeza Idadi ya shule na wanafunzi wakati wa uwekezaji katika ubora unaendelea.

(iii) Baraza la Taifa la Mitihani limeelekezwa kuzingatia kuwa pamoja na kwamba sheria ya kuanzishwa kwake inawaruhusu kufanya marekebisho ya mchachato wa mtihani lakini marekebisho yeyote ya kubadilisha utaratibu wa kupanga viwango vya ufaulu na madaraja ya matokeo ya mtihani lazima yahusishe wadau wote wanaohusika na mitaala, ufundishaji na mitihani.(*Makofi*)

(iv) Wakati Tume imeendelea kukamilisha kazi yake uamuzi wa Baraza la Taifa la Mitihani la kutumia utaratibu mpya wa kupanga viwango vya ufaulu madaraja ya matokeo ya mitihani uliotumika mwaka 2012 usitishwe na badala yake Baraza la Mitihani litumie utaratibu wa mwaka 2011 kwa kidato cha Nne na cha Sita kwa mitihani yote ukiwemo utaratibu wa *standardization* na kutoa matokeo mapya kwa kuzingatia maelekezo haya.

(v) Aidha, mchakato wa mfumo wa Tuzo wa Taifa *National Qualification Framework* na mfumo wa kutahiniwa, kutathmini maendeleo ya mwanafunzi katika masomo yake *National Assessment Framework* ukamilishwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume, kutokana na umuhimu wa mapendekezo haya Baraza la Mawaziri limeamua kwamba utekelezaji wa mapendekezo hayo uanze mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tume ya Uchunguzi itaendelea kukamilisha taarifa yake vizuri kwa kuhusisha wadau mbalimbali ili kupata maoni zaidi na ushauri wao juu ya mambo mbalimbali yaliyobainika wakati wa uchunguzi kabla ya kuikamilisha na kuitoa kwa matumizi ya Umma na vyombo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, Serikali inaipongeza sana Tume kwa kutoa mapendekezo ya awali ambayo Serikali imeyaridhia. Aidha, Serikali inawashukuru wananchi wote na wadau mbalimbali wa sekta ya elimu wanaoendelea kutoa maoni na ushauri wao kwa Tume.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawahakikishia wananchi kuwa itaendelea kuboresha elimu nchini ili kuwezesha watoto wetu wapate mafanikio katika maisha na maendeleo yao, kwani wahenga wanasema: *Elimu ni Ufunguo wa Maisha.*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kuwasilisha taarifa ya awali.(*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunategemea wakati wowote kupewa nakala ya rasimu ya elimu na tumeshauri kwa nguvu sana Serikali ikae na Kamati yetu ya Huduma za Jamii lakini tutakuwa na semina kwa Wabunge wote lakini baada ya kupewa hiyo nakala muwe mnasoma siyo tuende pale ukumbini tusikilize tu.

Kwa hiyo, tunaomba waandae nakala za kutosha kwa ajili ya Wabunge wote, lakini kazi kubwa itafanyika katika ngazi ya Kamati, maana yake wenzetu wana utalaam na wana muda na wanaweza kudadisi na kufuatilia kwa nguvu zaidi. Kwa hiyo, tunashukuru kwa taarifa hiyo. Katibu tuendelee.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali Mwaka 2013/2014
### Wizara ya Katiba na Sheria

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, Utangulizi; Kutokana na taarifa yangu niliyoiwasilisha kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala tulipokutana kwa lengo la kujadili na hatimaye kupitisha maombi ya Mpango na Bajeti ya Wizara yangu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara Katiba na Sheria, uliopitishwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa Mwaka wa fedha 2013/2014.

**SPIKA:** Wale wanaoamua kutoka wawe wanatoka kwa utulivu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati na kwa kazi kubwa waliyoifanya na kwa ushauri wao walioutoa wakati wa kupitia Makadirio ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Wizara na Majukumu yake; kulingana na Muundo wa Wizara yangu, majukumu yanayotekelezwa yanajumuisha: kuratibu mfumo wa utoaji haki nchini, kusimamia mambo ya katiba na utawala wa sheria, kuendesha mashtaka na kuitetea Serikali mahakamani, na kusimamia utaratibu wa kutoa huduma ya msaada wa sheria kwa jamii. Majukumu hayo yanatekelezwa na Taasisi zifuatazo:-

(i) Mahakama ya Tanzania;

(ii) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(iii) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;

(iv) Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania;

(v) Tume ya Utumishi wa Mahakama;

(vi) Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA);

(vii) Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (*Law School of Tanzania); na*

(viii) Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, (*Institute of Judicial Admnistraion).*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hebu msianze kuzungumza tunasikiliza hotuba.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Malengo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Malengo ya Mwaka 2012/2013.

Katika mwaka 2012/2013, Wizara ilipanga kutekeleza malengo ya Muda wa Kati kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele kama ifuatavyo:-

(i) Uratibu wa Mchakato wa Mabadiliko ya Katiba;

(ii). Usimamizi wa Usikilizaji na Uendeshaji wa Mashauri;

(iii) Uimarishaji wa Shughuli za Usajili, Ufilisi na Udhamini;

(iv) Uimarishaji na Uboreshaji wa Vyuo vya Mafunzo ya Sheria;

(v) Uimarishaji wa Utoaji wa Ushauri wa Kisheria Nchini;

(vi) Kufanya tafiti, mapitio, uandishi wa Sheria, Kanuni na Hati Mbalimbali; na

(vii) Usimamizi wa Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Uratibu wa Mchakato wa Mabadiliko ya Katiba; katika Mwaka wa Fedha 2012/2013 Wizara yangu imeendelea kuratibu Mchakato wa Mabadiliko ya Katiba. Tume ya Mabadiliko ya Katiba imeanza kazi rasmi tarehe 1 Mei, 2012. Madhumuni ya kuanzishwa kwa Tume ni kuratibu, kukusanya, kuchambua na kutathmini maoni ya wananchi kuhusu mabadiliko ya Katiba. Kwa kuzingatia muda ambao Sheria imeelekeza, Tume imeweka malengo ya kuwezesha kupatikana kwa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ifikapo Aprili 26, 2014.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2012/2013, Tume ilitekeleza shughuli zake kama ifuatavyo:-

(i) Kutoa elimu kwa umma na kuhamasisha wananchi kushiriki katika hatua zote za mchakato wa mabadiliko ya Katiba kupitia vyombo vya habari (Redio, Luninga, Magazeti, Tovuti) machapisho mbalimbali na katika mikutano;

(ii) Kuandaa na kusambaza nakala 1,700,000 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, nakala 400,000 za Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Sura ya 83, Katiba ya Zanzibar nakala 19,000, Vipeperushi 800,000 vinavyoeleza majukumu ya Tume, Vipeperushi 670,000 vyenye maswali yanayoulizwa mara kwa mara na majibu yake nakala 588,600 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba sura ya 83 kwa lugha nyepesi;

(iii) Kuandaa mifumo/njia mbalimbali ya ukusanyaji wa maoni ya wananchi kama vile mikutano ya hadhara katika Wilaya zote nchini, mikutano ya Makundi Maalum, tovuti na mitandao ya kijamii, barua kwa njia ya posta, barua pepe, nukushi, ujumbe wa simu, makala, kujaza fomu maalum za Tume pamoja na magazeti;

(iv) Kukusanya maoni ya wananchi kuhusu Mabadiliko ya Katiba katika Wilaya zote nchini na kuyachambua maoni hayo;

(v) Kuandaa, kuchapisha na kusambaza nakala 50,000 za Mwongozo kuhusu Muundo na Utaratibu wa kuwapata Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya (Mamlaka ya Serikali za Mitaa);

(vi) Kutoa elimu kwa umma kuhusu utaratibu wa uundwaji wa Mabaraza ya Katiba, majukumu ya Mabaraza hayo na kuandaa ratiba ya uchaguzi wa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba (Mamlaka ya Serikali za Mitaa);

(vii) Kuunda Mabaraza ya Katiba ya Wilaya (Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(viii) Kusimamia uchaguzi wa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya (Mamlaka ya Serikali za Mtaa);

(ix) Kuandaa Mwongozo wa Mabaraza ya Katiba ya Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu; na

(x) Kuandaa Ripoti ya Awali na Rasimu ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Tume hii pia, inalo jukumu kubwa la kusimamia Mabaraza ya Katiba. Tume imeyagawa Mabaraza ya Katiba katika Makundi mawili; kundi la kwanza ni Mabaraza yatakayosimamiwa na Tume (Mabaraza ya Katiba ya Wilaya – Ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa) na kundi la pili ni Mabaraza ya Katiba ya Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana.

Hadi sasa Tume imeweza kuwapata Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba katika Ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kupitia chaguzi na taratibu mbalimbali ambapo jumla ya Wajumbe 10,932 wamepatikana katika Mikoa 17. Katika kufanikisha kupatikana kwa Wajumbe, Tume ilitumia Mfumo wa Serikali za Mitaa na taratibu za Mikutano katika ngazi za Serikali za Mitaa zilizopo sasa (Vijiji, Mitaa na Kata).

Utaratibu huu ndio ulioainishwa kwenye Sheria zinazosimamia Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Aidha, kwa mujibu wa Ratiba ya shughuli za Tume, mikutano ya Mabaraza ya Katiba itaanza mwezi Juni, 2013 na itaendelea hadi mwezi Agosti, 2013.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 10 cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83, Tume ya Mabadiliko ya Katiba inayo mamlaka na uhuru katika utekelezaji wa majukumu yake.

Aidha, Tume imekuwa na utaratibu wa kutoa taarifa kuhusu jambo lolote linalopangwa kutekelezwa na kutoa taarifa baada ya utekelezaji wake kupitia mikutano na vyombo vya habari, magazeti, majadiliano katika redio, luninga na majarida ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, Usikilizaji wa Mashauri nchini katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 Mahakama ya Tanzania imesikiliza mashauri katika ngazi mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Mahakama ya Rufani ilianza Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ikiwa na idadi ya mashauri 1,743 yaliyosalia kutoka miaka ya nyuma.

Aidha, Mahakama ya Rufani ilipokea mashauri mapya 450 na hivyo kuwa na jumla ya mashauri 2,193. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2012 hadi Machi, 2013 Mahakama imesikiliza na kuyatolea maamuzi jumla ya mashauri 275 sawa na asilimia 13 ya jumla ya mashauri yote na hivyo kubaki na jumla ya mashauri 1,918.

Aidha, uwezo wa wastani wa uondoaji wa mashauri *(Clearance Rate)* katika Mahakama ya Rufani kwa tathmini ya kipindi cha miezi sita iliyopita ni asilimia 61

(ii) Mahakama Kuu ilianza Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ikiwa na idadi ya mashauri 9,737 yaliyosalia kutoka miaka ya nyuma. Aidha, Mahakama Kuu ilipokea mashauri mapya 7,547 na hivyo kuwa na jumla ya mashauri 17,284. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2012 hadi Machi 2013 Mahakama Kuu imesikiliza na kuyatolea maamuzi jumla ya mashauri 5,191 sawa na asilimia 30 ya jumla ya mashauri yote na hivyo kubaki na jumla ya mashauri 12,093. Aidha, uwezo wa wastani wa uondoaji wa mashauri *(Clearance Rate)* katika Mahakama ya Kuu kwa tathmini ya kipindi cha miezi sita iliyopita ni asilimia 70.

(iii) Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara, ilianza Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ikiwa na idadi ya mashauri 285 yaliyosalia kutoka miaka ya nyuma. Aidha, Mahakama ilipokea mashauri mapya 118 na hivyo kuwa na jumla ya mashauri 403. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2012 hadi Machi 2013 Mahakama ya Biashara imesikiliza na kuyatolea maamuzi jumla ya mashauri 74 sawa na asilimia 18 ya jumla ya mashauri yote na hivyo kubaki na jumla ya mashauri 329. *(Makofi)*

Aidha, uwezo wa wastani wa uondoaji wa mashauri *(Clearance Rate)* katika Mahakama ya Biashara kwa tathmini ya kipindi cha miezi sita iliyopita ni asilimia 64.

(iv) Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, ilianza Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ikiwa na idadi ya mashauri 1,597 yaliyosalia kutoka miaka ya nyuma. Aidha, Mahakama ilipokea mashauri mapya 674 na hivyo kuwa na jumla ya mashauri 2,271. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2012 hadi Machi 2013 Mahakama ya Kazi imesikiliza na kuyatolea maamuzi jumla ya mashauri 491 sawa na asilimia 22 ya jumla ya mashauri yote na hivyo kubaki na jumla ya mashauri 1,780. Aidha, uwezo wastani wa uondoaji wa mashauri *(Clearance Rate)* katika Mahakama ya Kazi kwa tathmini ya kipindi cha miezi sita iliyopita ni asilimia 73.

(v) Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi, ilianza Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ikiwa na idadi ya mashauri 5,393 yaliyosalia kutoka miaka ya nyuma. Aidha, Mahakama ya Ardhi ilipokea mashauri mapya 427 na hivyo kuwa na jumla ya mashauri 5,820. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2012 hadi Machi, 2013 Mahakama ya Ardhi imesikiliza na kuyatolea maamuzi jumla ya mashauri 427 sawa na asilimia 7 ya jumla ya mashauri yote na hivyo kubaki na jumla ya mashauri 5,393. Aidha, uwezo wa wastani uondoaji wa mashauri *(Clearance Rate)* katika Mahakama ya Ardhi kwa tathmini ya kipindi cha miezi sita iliyopita ni asilimia 100.

(vi) Mahakama za Hakimu Mkazi, ilianza Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ikiwa na idadi ya mashauri 25,002 yaliyosalia kutoka miaka ya nyuma. Aidha, Mahakama ilipokea mashauri mapya 980 na hivyo kuwa na jumla ya mashauri 25,982. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2012 hadi Machi 2013 Mahakama imesikiliza na kuyatolea maamuzi jumla ya mashauri 612 sawa na asilimia 2 ya jumla ya mashauri yote na hivyo kubaki na jumla ya mashauri 25,370. Aidha, uwezo wa wastani wa uondoaji wa mashauri (Clearance Rate) katika Mahakama ya Hakimu Mkazi kwa tathmini ya kipindi cha miezi sita iliyopita ni asilimia 73.

(vii) Mahakama za Wilaya, zilianza Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ikiwa na idadi ya mashauri 31,025 yaliyosalia kutoka miaka ya nyuma. Aidha, Mahakama za Wilaya ilipokea mashauri mapya 94,872 na hivyo kuwa na jumla ya mashauri 125,897. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2012 hadi Machi 2013 Mahakama za Wilaya imesikiliza na kuyatolea maamuzi jumla ya mashauri 104,359 sawa na asilimia 83 ya jumla ya mashauri yote na hivyo kubaki na jumla ya mashauri 21,538. Aidha, uwezo wa wastani wa uondoaji wa mashauri *(Clearance Rate)* katika Mahakama za Wilaya kwa tathmini ya kipindi cha miezi sita iliyopita ni asilimia 110.

(viii) Mahakama za Mwanzo, zilianza Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 zikiwa na idadi ya mashauri 124,959 yaliyosalia kutoka miaka ya nyuma. Aidha, Mahakama za Mwanzo zilipokea mashauri mapya 650,181 na hivyo kuwa na jumla ya mashauri 775,140. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2012 hadi Machi 2013 Mahakama imesikiliza na kuyatolea maamuzi jumla ya mashauri 577,425 sawa na asilimia 74 ya jumla ya mashauri yote na hivyo kubaki na jumla ya mashauri 197,715. Aidha, uwezo wa wastani wa uondoaji wa mashauri *(Clearance Rate)* katika Mahakama za Mwanzo kwa tathmini ya kipindi cha miezi sita iliyopita ni asilimia 89.

Mheshimiwa Spika, Uendeshaji wa Mashauri nchini; katika kutekeleza jukumu la kuiwakilisha Serikali katika mashauri mbalimbali ndani na nje ya nchi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeendesha mashauri ya Jinai, Madai na Katiba katika Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu na Mahakama zilizo chini ya Mahakama Kuu isipokuwa Mahakama za Mwanzo. Aidha, Ofisi pia imeendelea kuratibu mashauri ya usuluhishi (*arbitration*) ambapo manne (4) ya Mahakama Kuu na 11 ya Tume ya Usuluhushi *(CMA).* Hadi Machi, 2013 kulikuwa na jumla ya mashauri ya madai 682 yakijumuisha mashauri mapya 132. Mashauri haya yote yalifunguliwa dhidi ya Serikali na Kesi moja (1) ya Madai ilifunguliwa na Serikali. Mashauri hayo yako katika hatua mbalimbali za kusikilizwa na kutolewa maamuzi na Mahakama Mashauri ya madai yaliyohitimishwa hadi mwezi Machi, 2013 ni 40 na kubaki mashauri 642.

Mheshimiwa Spika, aidha, kulikuwa na jumla ya Maombi ya madai 285 yaliyofunguliwa yakiwemo mapya 89 yaliyopokelewa katika kipindi cha Julai 2012 hadi Machi 2013. Maombi haya ya madai yalifunguliwa dhidi ya Serikali. Hadi Machi, 2013 maombi ya madai 63 yalihitimishwa na maombi 222 yanaendelea kusikilizwa. Vilevile, palikuwepo na Rufani za madai 46 zikijumuisha mpya saba (7). Kati ya hizi rufani mbili (2) zilihitimishwa na kubaki na rufani 44 ambazo zinazoendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuhusu masuala ya upatanishi (arbitration) mgogoro mmoja (1) unaohusu Serikali ulishughulikiwa kati ya Mashauri yaliyobakia. Hali kadhalika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kuendesha mashauri ya rufani za uchaguzi yatokanayo na uchaguzi Mkuu wa 2010 ambayo ni kutoka Kigoma (3), Tabora (2), Mara (1), Sumbawanga (1), Dar es Salaam (1), Mtwara (3), Kagera (1) na Arusha (2). Kati ya mashauri hayo, mashauri matano (5) yamehitimishwa na mashauri tisa (9) yanaendelea kusikilizwa katika Mahakama ya Rufani.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Kurugenzi ya Mashtaka iliendelea kutekeleza jukumu lake la kuendesha mashauri ya jinai katika Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu na Mahakama zilizo chini ya Mahakama Kuu na pia iliendelea kuratibu kazi za upelelezi unaofanywa na vyombo vya upelelezi isipokuwa Mahakama za Mwanzo. Jumla ya mashauri 14,453 yaliyokuwepo na mengine mapya 13,487 ya Mwaka 2012/2013 yaliendelea kuendeshwa Mahakamani.

Mashauri haya yanahusu kesi mbalimbali ikiwa ni pamoja na mashauri yaliyohusisha mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi, udanganyifu na utakatishaji wa fedha haramu. Hadi mwezi Machi 2013 mashauri 5,257 yalihitimishwa na kubaki mashauri 22,683 yatakayoendelea kuendeshwa katika ngazi mbalimbali za Mahakama pamoja na Mashauri mapya yatakayopokelewa.

Mheshimiwa Spika, katika uendeshaji wa mashauri yanayohusu watu wenye ulemavu wa ngozi, jumla ya matukio 60 yaliripotiwa na polisi nchi nzima. Mashauri 12 yanaendelea kusikilizwa, mashauri 14 yameondolewa mahakamani na mashauri 10 yameamuliwa ambapo Jamhuri imeshinda mashauri yote. Mashauri 24 yanaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na vyombo vya upelelezi vya TAKUKURU na Jeshi la Polisi ni mshiriki mkubwa katika mapambano dhidi ya rushwa. Hadi kufikia Mwaka 2012/2013 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imepokea jumla ya majalada 317 yaliyohusu rushwa kubwa na ubadhirifu kutoka vyombo vya upelelezi vya TAKUKURU na Jeshi la Polisi.

Kati ya Majalada hayo, 95 yaliandaliwa hati za Mashtaka na kupewa kibali cha kushtaki, jalada moja (1) lilifungwa na majalada 65 yalirudishwa kwa vyombo husika kwa ajili ya kufanyiwa upelelezi zaidi na majalada 156 yanaendelea kufanyiwa kazi na Divisheni ya Mashtaka.

Mheshimiwa Spika, Vilevile, katika kuhakikisha kwamba mali zilizopatikana kwa njia zisizo halali zinarejeshwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inasimamia urejeshwaji wa mali na fedha *(Asset Recovery and Forfeiture)* katika mashauri mbalimbali.

Katika kipindi hiki mali zilizotaifishwa ni pamoja na magari manne (4) katika mikoa ya Morogoro (1), Dar es Salaam (1) na Tanga (2) na nyumba tatu (3) pamoja na fedha Shilingi bilioni saba (7) zinazotakiwa kurejeshwa baada ya watuhumiwa watano kutiwa hatiani katika shauri la madawa ya kulevya. Watuhumiwa hao wamekata rufaa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/ 2013 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kuendesha mashauri 14 yanayohusu makosa ya wizi, kugushi na kutakatisha fedha ambayo yaliyobaki katika kipindi cha mwaka 2011/2012 katika Mahakama mbalimbali nchini zikiwemo Mahakama ya Hakimu Mkazi Dar es Salaam, Arusha na Nzega. Mashauri haya yanahusu takribani kiasi cha Shilingi Bilioni 48.

Hadi Machi, 2013 kulikuwa na jumla ya kesi tatu (3) zilizotolewa hukumu. Kesi moja (1) yenye kuhusisha kiasi cha takriban Shilingi Bilioni moja washtakiwa waliachiwa huru lakini Jamhuri imekata rufaa na kesi mbili (2) washtakiwa wametiwa hatiani na wanatakiwa kurudisha fedha zipatazo Shilingi Milioni 960. Vilevile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendesha mashauri yanayohusu madawa ya kulevya ambapo katika kipindi cha Julai 2012 hadi Machi 2013 kesi moja (1) ya madawa ya kulevya ilihitimishwa kwa Mahakama kuwatia hatiani watu watano kwa kila mmoja kuhukumiwa kifungo cha miaka 25.

Mheshimiwa Spika, Utenganishaji wa jukumu la Upelelezi na Mashtaka *(Civilianisation of Prosecutions Service);* katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kutenganisha Jukumu la Upelelezi na Mashtaka *(Civilianisation of Prosecutions Service)* ili kuondoa tatizo la haki kuchelewa kutendeka, kesi kuchukua muda mrefu Mahakamani kwa sababu ya muda mrefu unaotumika katika upelelezi.

Hatua mbalimbali ziliendelea kuchukuliwa ikiwa ni sehemu ya utekelezaji, uelimishaji na uenezaji wa utaratibu huu katika Mikoa na Wilaya zote za Tanzania Bara. Hatua hizi ni pamoja na kuajiri Mawakili wa Serikali na kufungua ofisi katika Mikoa mitano (5) ya Morogoro, Manyara, Kigoma, Njombe na Pwani pamoja na Wilaya za Monduli na Temeke. Hadi sasa zipo Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mikoa 22 ya Tanzania Bara.

Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Iringa, Singida, Dodoma, Mtwara, Lindi, Mara, Kagera, Ruvuma, Rukwa, Mwanza, Kilimanjaro, Tanga, Tabora, Shinyanga, Morogoro, Pwani, Kigoma, Manyara na Njombe. Aidha, lengo la kuwa na Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mikoa mitatu iliyosalia ya Geita, Simiyu na Katavi litakamilishwa katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Hadi Machi, 2013, Divisheni ya Mashtaka ilikuwa inaendesha kesi katika Mahakama za Wilaya 22 za Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya zilizotajwa hapo juu. Lengo ni kufikisha huduma za mashtaka karibu zaidi na wananchi. Aidha, Mpango huu wa kutenganishwa kwa shughuli za upelelezi na mashtaka umesaidia sana kupunguza idadi ya kesi zinazofunguliwa Mahakamani na msongamano wa mahabusu na wafungwa magerezani. Idadi ya Mahabusu imepungua kutoka 17,932 kwa mwezi Julai, 2012 hadi kufikia mahabusu 16,973 mwezi Machi 2013. Vilevile, idadi ya wafungwa imepungua kutoka 17,868 kwa mwezi Julai 2012 hadi kufikia wafungwa 17,497 mwezi Machi, 2013.

Mheshimiwa Spika, lakini la msingi zaidi ni kuwa, utenganishaji huu unafanywa kwa misingi ya utawala bora. Si vyema kukipa chombo kimoja cha dola madaraka ya kuhisia, kutuhumu, kukamata, kupeleleza na kushitaki bila udhibiti wa chombo kingine.

Wataalam wa utawala wanasema *"Regulation is the hallmark of Government"* ndiyo maana kuna EWURA, TICRA, SSRA na kadhalika. Na ndani ya Serikali nako ni muhimu kuwa na utaratibu huu wa *"checks and balances".* Nchi nyingi ambazo mifumo yao ya Sheria na Utawala inafanana na sisi wana utaratibu huu. Marekani mashtaka huendeshwa na Mwanasheria Mkuu kupitia *"District Attorneys".* Uingereza kuna *"Crown Prosecution Agency"* na kadhalika. Na hapa kwetu ndiyo tuna Mwanasheria Mkuu kupitia Ofisi ya *DPP.*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na Asasi zisizo za Kiserikali, iliunda kikosi kazi kwa ajili ya kufanya utafiti na kuwasilisha mapendekezo yatakayoisaidia Serikali kubuni utaratibu wa utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa watu wasio na uwezo wa kulipia gharama za kisheria. Kikosi kazi hicho kimefanya utafiti na tayari mapendekezo ya kutunga sheria itakayoratibu utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa umma na kuwatambua watoa huduma za msaada wa kisheria kwa umma, ikiwa ni pamoja na Wasaidizi wa Kisheria *(Paralegals)* yameshawasilishwa Serikalini. Taratibu za kupata Sheria hiyo zinaendelea vizuri na ni matumaini yetu kwamba, Rasimu ya Sheria hii itawasilishwa katika Bunge hili Tukufu katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Wizara yangu ilianzisha Kamati ya Kitaifa ya Kuzuia Mauaji ya Kimbari. Kamati hii imeanzishwa kutokana na makubaliano yaliyofikiwa kati ya Nchi Zinazozunguka au za Ukanda wa Maziwa Makuu *(The International Conference on the Great Lakes Region - ICGLR).* Nchi husika zilifikia makubaliano katika Mkataba uliosainiwa na nchi zote wanachama ya kuweka utaratibu wa kubaini viashiria vya uvunjifu wa amani na kusababisha vita katika eneo la Maziwa Makuu. Tanzania imesaini *Protocol for the Prevention and Punishment of the Crimes of Genocide, War Crimes, Crimes Against Humanity and all Forms of Discrimination,* ambayo pia yanaitaka Nchi Wanachama kuanzisha Kamati za Kitaifa za Kuzuia Mauaji ya Kimbari.

Nchini Tanzania, Kamati hiyo ilianzishwa mwezi Februari, 2012 na Kamati hii ina jukumu la kubaini dalili au viashiria vya uvunjifu wa amani ya nchi yetu, kuishauri Serikali pamoja na kujenga uelewa wa Wananchi kuhusu umuhimu wa kuzuia uvunjifu wa amani na mauaji na uhalifu dhidi ya binadamu nchini. Kamati hii ya Kitaifa ina Wajumbe wafuatao: Ofisi ya Rais - Ikulu; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ofisi ya Waziri Mkuu; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; Wizara ya

Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Wizara ya Vijana, Habari, Utamaduni na Michezo; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Chuo Kikuu cha Dar es salaam; na Taasisi ya Wakfu ya Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, mapema mwezi Disemba, 2012, Wizara kupitia Kamati hii imefanya Mkutano na Viongozi wa Dini zote ambapo Viongozi wa Kidini walijadili nafasi yao katika kulinda na kudumisha amani nchini. Mikutano ya Kamati hii ni endelevu na ili iwe na tija, hutumika kuishauri Serikali na pia kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuzuia mauaji na uhalifu dhidi ya binadamu nchini.

Katika utekelezaji wa Mpango huu, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mshauri wa Umoja wa Mataifa kuhusu kuzuia Mauaji ya Kimbari, imeandaa Mkutano wa Kimataifa utakaofanyika nchini Tanzania mwishoni mwa mwezi Mei, 2013. Mada kuu ya mkutano huu itakuwa ni njia bora na fursa mpya katika kuzuia Mauaji ya Kimbari, Hatua za Kiserikali na Matumizi ya Kiteknolojia Kikanda *(Best Practices in New Opportunities in Genocide Prevention, Governmental Action, Technology in Regional Contexts).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Wizara yangu imeratibu na kuandaa Mkutano wa Kimataifa wa Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Kupambana na Ugaidi uliofanyika Dar es Salaam kuanzia tarehe 26 - 28 Februari, 2013 na kuhudhuriwa na Wajumbe kutoka Nchi 36 Duniani. Ujumbe au mada kuu katika Mkutano huo ulikuwa ni *"Bringing Terrorists to Justice; Policy Challenges in the Prosecution and Prevention of Terrorism".*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara yangu imekamilisha tafiti kuhusu hali ya watoto wanaokinzana na Sheria na pia kuhusu upatikanaji wa haki sheria kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka 18 kwa kushirikiana na *UNICEF*. Kutokana na utafiti huo, Wizara imeandaa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Haki Sheria kwa watoto. Mpango Mkakati huu utaboresha

mfumo mzima wa upatikanaji wa ulinzi na haki kwa watoto nchini. Vilevile, Mpango Mkakati huu utasaidia kuweka pamoja mikakati ya namna bora ya kushughulikia masuala ya haki sheria kwa watoto nchini. Mpango Mkakati huu unaandaliwa Waraka wa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kujadili na kupitisha Mpango Mkakati huu ili uweze kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara yangu imeendelea kupokea malalamiko ya aina mbalimbali toka kwa Wananchi na yameshughulikiwa. Malalamiko mengi yalielekezwa kwenye Taasisi na Vyombo vya Serikali vinavyojishughulisha na utoaji haki na usimamizi wa Sheria. Malalamiko hayo yalishughulikiwa kwa kuwasiliana na Vyombo au Taasisi husika kama njia ya kuyatafutia utatuzi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeendelea kutekeleza jukumu la kuimarisha utoaji wa ushauri wa kisheria kuhusu masuala ya Mikataba ya Kibiashara, Kimataifa, Katiba na Haki za Binadamu. Aidha, Ofisi pia imeshiriki katika mikutano mbalimbali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Umoja wa Mataifa, Nchi Wanachama wa Kusini mwa Afrika *(SADC)* na Nchi za Umoja wa Afrika, kwa ajili ya kufanya majadiliano na kutoa ushauri wa kisheria. Majadiliano ambayo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeshiriki ni ubia wa kibiashara kati ya Umoja wa Nchi za Ulaya na Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EPA)*; kuanzishwa kwa Itifaki ya Umoja wa Fedha; Itifaki ya Mahakama ya Nchi Wanachama wa Kusini mwa Afrika; kuanzisha Soko Huru baina ya Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki, *SADC* na *COMESA*; kurekebisha Mkataba wa kuanzisha Mahakama ya Umoja wa Afrika; kurekebisha Mkataba ulioanzisha Bunge la Afrika; Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kuzuia kusambaa kwa silaha ndogo; kurekebisha Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; na majadiliano ya mgogoro wa mpaka baina ya Tanzania na Malawi. Vilevile, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeshughulikia na kutoa ushauri wa kisheria katika mikataba (*Contracts)* 330. Kati ya Mikataba hii, mikataba 295 ilihusu manunuzi ya umma na Mikataba 35 ilihusu masuala ya

uwekezaji. Vilevile, Mikataba ya Makubaliano *(MoU)* 58 ilishughulikiwa na makubaliano baina ya Nchi na Nchi *(Bilateral Agreement)* 21; mahudhurio ya vikao 185 vilivyohusu Majadiliano ya Mikataba na Mahusiano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza mwaka jana katika Bunge lako Tukufu, Serikali imeendelea kutelekeza Mpango wa Uendeshaji Shughuli za Serikali kwa Uwazi *(Open Government Partnership - OGP),* ambao ulianzishwa tarehe 21 Septemba, 2011. Mpango huu unasimamiwa na Wizara yangu na kuratibiwa na Kamati ya Kitaifa chini ya Uenyekiti wa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mpango huu umeendelea kutekelezwa na Sekta tatu za kipaumbele za huduma za jamii ambazo ni Afya, Maji na Elimu. Mpango wa Serikali wazi unajikita katika maeneo ya kuweka uwazi zaidi katika uendeshaji wa shughuli za Serikali, ushirikishwaji wa Wananchi katika mpango wa utekelezaji, uwajibikaji na uadilifu, Utawala Bora, kupambana na rushwa na matumizi ya teknolojia na ubunifu. Malengo ya Mpango huu ni kuimarisha usimamizi wa matumizi ya rasilimali za umma, kuboresha utoaji wa huduma, kuongeza usalama wa nchi na kuongezeka kwa uwajibikaji wa kitaasisi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango huu, yafuatayo yamefanyika:-

(i) Mpango Kamili wa *OGP Tanzania* umeandaliwa na kuwasilishwa Makao Makuu ya *OGP* katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Viongozi wa Nchi Wanachama wa *OGP* uliofanyika Brasilia Brazili tarehe 17 - 18 Aprili, 2012.

(ii) *Road Map* na Bango kitita ya *Commitments* ya shughuli zitakazotekelezwa hadi kufikia Juni, 2013 imeandaliwa na kusambazwa kwenye sekta husika.

(iii) Wizara nane zimeandaa Mipango Kazi yao na kuiwasilisha kwenye Kamati. Wizara hizi ni Ofisi ya Rais - Ikulu, Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Maji, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

na Wizara ya Fedha. Aidha, kwa hivi sasa Kamati imeandaa Mkakati wa Mawasiliano kuhusu utekelezaji wa Mpango wa *OGP Tanzania (Open Government Partnership Communication Strategy)* na vilevile Kamati inashirikiana kwa karibu na Wakala wa Serikali Mtandao *(e-Government Agency)* kuhakikisha Tovuti ya Wananchi *(Citizen Portal)* inaanza kazi mapema iwezekanavyo ili iweze kuhudumia Wananchi. Aidha, Waraka wa Mapendekezo ya Kutunga Sheria ya Uhuru wa Habari *(Freedom of Information Law)* unaandaliwa na Wizara husika ambayo ndiyo yenye dhamana ya masuala ya habari nchini, na utawasilishwa kwenye ngazi za maamuzi na hatimaye sheria kutungwa na kuletwa katika Bunge lako Tukufu.

(iv) Kuhudhuria Kikao cha Mawaziri wa Nchi zinazotekeleza Mpango wa Serikali Wazi *(OGP)* kilichofanyika Mjini London kuanzia tarehe 22 – 25 Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara yangu itaendelea kusimamia Mipango Kazi ya Sekta za kipaumbele na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazoendelea kujitokeza katika utekelezaji wa Mpango wa Serikali Wazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, imekamilisha Taarifa ya Mfumo wa Haki za Madai *(Civil Justice System Review)* na Taarifa ya Mapitio ya Tamko la Sheria za Mila zinazofuata mkondo wa ukoo wa mama *(Matrilineal Societies)*. Taarifa hizi zimewasilishwa kwangu ili ziweze kufanyiwa kazi zaidi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kutolewa kauli Bungeni ya hatua zitazochukuliwa. Tume iko katika hatua za mwisho za kukamilisha Taarifa ya Mapitio ya Sheria zinazosimamia Usuluhishi na Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi. Aidha, Rasimu ya Awali ya Mapitio ya Mfumo wa Sheria zinazosimamia Huduma za Jamii kwa Wazee imeandaliwa ili kuwezesha kufanya utafiti katika Mikoa 12 ya Tanzania ambayo ni Kagera, Shinyanga, Mara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Dodoma, Mbeya, Rukwa Ruvuma na Pwani. Kwa upande wa Mapitio ya Mfumo wa Sheria unaosimamia Haki za Walaji *(Consumer*

*Protection)*, taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi zimeanza.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013 Tume imefanya uchambuzi wa hukumu za kesi za Mahakama ya Rufani ya Tanzania zipatazo 100 ili kuainisha misingi ya Kisheria *(Legal Principles)* na kuweka misingi hiyo katika tovuti yake ili kuwarahisishia wadau kuelewa tafsiri ya maamuzi ya Mahakama ya Rufani kuhusu vipengele vya kisheria vilivyotumika. Vilevile Tume imewasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Rasimu tano za tafsiri za Sheria katika Lugha ya Kiswahili. Pia Tume imeendelea kutoa elimu ya Sheria kwa umma kupitia vipindi vya redio na runinga kwa lengo la kuelimisha jamii kuhusu haki, wajibu na masuala mbalimbali ya Kisheria.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliendelea kutekeleza jukumu la kuandaa Miswada ya Sheria na kuiwasilisha mbele ya Bunge kwa ajili ya kujadiliwa na hatimaye kupitishwa na kuwa Sheria za Nchi. Hadi mwezi Machi, 2013 jumla ya Miswada sita iliandaliwa; kati ya hiyo, Miswada minne ilipitishwa na kuwa Sheria, Miswada miwili bado haijapitishwa. Aidha, kazi ya kuzifanyia urekebu Sheria zilizopitishwa na Bunge iliendelea kufanyika ambapo Sheria 14 zilifanyiwa urekebu, jumla ya Sheria Ndogo 260 zilitayarishwa na kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali na Maazimio 11 yaliwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitekeleza jukumu la kutafsiri Sheria kwa Lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Ofisi imetafsiri jumla ya Sheria saba katika Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamiaji wa Haki za Binadamu, Utawala Bora na Masuala ya Katiba. Kwa upande wa masuala ya Katiba na Haki za Binadamu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipokea maombi ya mashauri ya Kikatiba na Haki za Binadamu 73 na kuhitimishwa 17; hivyo, kubaki mashauri 56 yanayoendelea kusikilizwa. Aidha, Ofisi

ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliweza kushiriki vikao mbalimbali kuhusiana na masuala ya haki za binadamu kama vile Kikao cha Kamati ya Haki za Binadamu inayosimamia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni ambapo Taarifa ya Nchi ya Mkataba huo ilijadiliwa Novemba, 2012 huko Geneva, Uswisi; Kikao cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Marekani; na Kikao cha Tume ya Haki za Binadamu na Watu (*African Commission on Human and People's Rights)* kilichofanyika Gambia Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeshiriki kwenye wiki ya Maadhimisho ya Kitaifa ya Haki za Binadamu ambayo hufikia kilele chake tarehe 10 Desemba kila mwaka kwa kushirikiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Wizara ya Katiba na Sheria. Katika maadhimisho hayo, taarifa mbalimbali za nchi kuhusu Haki za Binadamu na mapendekezo yanayotolewa na Kamati au Tume zinazosimamia Mikataba husika ya Kimataifa ya Haki za Binadamu kuhusu Tanzania zilitolewa kwa Wananchi. Madhumuni ya maadhimisho hayo yalikuwa ni kuwawezesha Wananchi kufahamu hali halisi ya Kitaifa katika masuala ya Haki za Binadamu na jinsi Tanzania inavyotekeleza shughuli za kulinda na kukuza Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara ya Katiba na Sheria kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ilipanga kudumisha Utawala Bora nchini kwa kusimamia Utekelezaji wa Haki za Binadamu kama zilivyoelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Tamko la Umoja wa Mataifa na Tamko la Afrika la Haki za Binadamu. Katika kutekeleza hili, Tume imekamilisha kuandaa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu ambao umewasilishwa Serikalini kwa ajili ya Kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri. Aidha, Tume iliendelea kushughulikia malalamiko ya Wananchi kwa kupokea na kufuatilia malalamiko, kutoa ushauri wa kisheria, kufanya uchunguzi na utafiti juu ya masuala yanayohusu haki za binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Tume iliendelea kupokea na kushughulikia malalamiko mapya na ya zamani kulingana na uwezo uliokuwepo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2013 Tume ilikuwa imeshughulikia jumla ya malalamiko 8,350. Kati ya malalamiko hayo, 7,165 ni ya miaka ya nyuma na 1,185 ni mapya. Kati ya Malalamiko hayo 688 yalihitimishwa baada ya kupatiwa ufumbuzi na kubakia na malalamiko 7,662 yanayoendelea kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, Tume iliongeza juhudi za kuleta ufumbuzi wa malalamiko ya Wananchi na migogoro ya ardhi. Vilevile, Tume ilikamilisha uchunguzi na kutoa mapendekezo kwa mamlaka husika kuhusu ukiukwaji wa haki za Watumishi wa Mamlaka ya Maji Safi na Taka *(DAWASCO)*, Mgogoro kati ya Wafugaji na Wakulima wa Wilaya ya Rufiji na Mgogoro wa Ardhi Mabwepande, Wilaya ya Kinondoni. Aidha, Tume iliitisha na kuendesha vikao vya kujadili taarifa za uchunguzi wa hadharani kuhusu migogoro ya ardhi na uhamishwaji wa watu katika ardhi yao ulioshirikisha wadau mbalimbali kutoka Taasisi za Serikali na Binafsi. Vilevile Tume ilifanya kaguzi katika vituo 100 vya vizuizi *(detention facilities)* katika Wilaya 21 ili kupima na kutathmini hali na haki za watoto waliozuiwa katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, imetoa elimu kwa umma kuhusu Haki za binadamu na Utawala Bora kupitia vipindi vya redio, runinga na machapisho mbalimbali. Jumla ya machapisho 38,250 yalisambazwa na Wananchi 1,594 walipatiwa ushauri wa kisheria. Aidha, Tume ilitoa mafunzo kwa waandishi wa habari 112 katika Mikoa sita ya Tanzania Bara ya Iringa, Dodoma, Lindi, Morogoro, Mwanza, Tanga na Mjini Magharibi kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini umeanza mazungumzo na wadau wa usajili wa watoto ambao ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), juu ya namna ya kuboresha shughuli za usajili wa watoto. Rasimu ya Mkataba wa Makubaliano kati ya *RITA*, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu namna ya kusogeza huduma za usajili wa vizazi na vifo kufikia ngazi ya kata imekamilika na rasimu hiyo inatarajiwa kujadiliwa katika Kikao cha Wadau kitakachofanyika tarehe 3 Mei, 2013.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango wa kusajili watoto chini ya umri wa miaka mitano unaojulikana kama *"U5BRI – Under 5 Birth Registration Initiative"* ulianza kwa majaribio kwa kipindi cha wiki sita yaliyofanyika kuanzia tarehe 4 Juni, 2012 katika Manispaa ya Temeke. Jumla ya watoto 15,513 walio na umri wa chini ya miaka mitano walisajiliwa na kupewa vyeti vya kuzaliwa. Wakala unaendelea kutekeleza Mpango huo ambao ni mkakati wa kupunguza mlundikano wa vizazi ambavyo havijasajiliwa. Maandalizi ya kueneza mpango au mkakati huu yamefanyika katika Wilaya zote za Mkoa wa Mbeya kwa kufanya utafiti wa awali *(Baseline Survey)* na kutoa hamasa kwa makundi mbalimbali ya Viongozi kama vile Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa *(RCC)*, Wakurugenzi wa Halmashauri zote za Mkoa wa Mbeya, Vikao vya Madiwani na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya. Utekelezaji wa Mkakati huu unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, sanjari na Mkakati huo wa kusajili watoto walio na umri chini ya miaka mitano, Wakala pia unatekeleza mkakati wa kusajili watoto wa umri kati ya miaka 6 hadi 18 *(6 - 18 Birth Registration Initiative)* waliopo mashuleni ambao umefanyiwa majaribio katika Wilaya ya Igunga. Katika majaribio hayo, jumla ya watoto 1,499 walisajiliwa katika kipindi cha miezi miwili kuanzia tarehe 18 Februari, 2013 na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa *RITA* umeendelea kusogeza huduma za usajili kwa Wananchi, kwa kuendesha kampeni za uhamasishaji ambazo zilipelekea kusajili vizazi 331,272, vifo 59,099, ndoa 6,094, talaka 42, uasili wa watoto 23 na kufunga mirathi moja, kuandika na kuhifadhi wosia 37.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ya ufilisi, Wakala pia uliteuliwa na Mahakama kuwa mfilisi wa

muda ili kusimamia mali za Kampuni ya Mitambo ya Kufua Umeme ya *IPTL*. Katika shauri namba 49 la mwaka 2003 lillilohusu IPTL, Mahakama ya Rufani ilitoa maamuzi ya kufuta amri ya kuifilisi *IPTL* iliyotolewa tarehe 17 Disemba, 2012, hivyo Wakala kubaki na jukumu la kuwa Mfilisi wa muda *(Provisional Liquidator)* wa Kampuni hiyo hadi shauri hilo litakapomalizika.

Mheshimiwa Spika, katika masuala ya udhamini, Wakala una jukumu la kusimamia mali zisizokuwa na uangalizi maalumu, mali zisizokuwa na mwenyewe na zile zinazopaswa kumilikiwa na watoto walio chini ya umri wa miaka 18 ambao hawana waangalizi maalum *(Guardians),* kwa mujibu wa Sheria ya Mdhamini wa Serikali ambapo Wakala *(Administrator General),* huteuliwa na Mahakama kama Mdhamini wa Serikali *(Public Trustee)*.

Mheshimiwa Spika, pia, Wakala husimamia mirathi baada ya kuombwa na ndugu wa marehemu au kuteuliwa na Mahakama. Shughuli nyingine inayofanyika ni kusajili Miunganisho ya Wadhamini ili kuwapatia nguvu ya kisheria ya kumiliki mali kwa niaba ya Taasisi zao. Wadhamini wa Taasisi za Kijamii, Kidini, Mifuko ya Maendeleo ya Kijamii, Vilabu vya Michezo pamoja na Vyama vya Siasa husajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini, Sura ya 318, Toleo la 2002. Hadi kufikia Machi, 2013, Wakala umesajili Miunganisho ya Udhamini 204 na kutoa elimu kwa madhehebu ya dini mbalimbali na kutoa hati za usajili kwa Wadhamini wa Vyama vya Siasa, Vikundi, Makanisa, Misikiti na Mali zipatazo151. Pia, Wakala imetembelea Vikundi vya Udhamini katika Wilaya ya Morogoro, Iringa na Arusha.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuboresha mazingira ya kazi, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, unaendelea na ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Ofisi za Wakala lililopo katika Mtaa wa Makunganya Mjini Dar es Salaam ambao unatarajiwa kukamilika katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, katika kuiimarisha Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania *(Law School*

*of Tanzania),* Wizara yangu kupitia Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria *(Legal Sector Reform Programme),* imekamilisha ujenzi wa majengo ya kudumu ya Taasisi hii katika kiwanja Na. 2005/2/1 Sam Nujoma/Mpakani, Sinza, Dar es Salaam. Jumla ya shilingi bilioni 16.1 zilitumika katika ujenzi huo. Kwa sasa Taasisi hii inaendesha mafunzo katika majengo hayo baada ya kuhamia hapo Agosti, 2012. Kukamilika kwa majengo hayo kutaiwezesha Taasisi hii kuongeza udahili wa wanafunzi kufikia 1,500 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2012 – Februari, 2013, Taasisi hii ilidahili wanafunzi wapya 736. Aidha, Taasisi hii imetoa mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo kwa wanafunzi 585 waliosajiliwa katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, ambao walikuwa wanaendelea na mafunzo. Katika kipindi hicho, jumla ya wanafunzi 1,136 walifanya mitihani ya mwisho na wanafunzi 409 walifaulu mitihani hiyo na kupata sifa ya kusajiliwa kuwa Mawakili wa Kujitegemea. Wanafunzi 861 walitakiwa kurudia mitihani mbalimbali *(Supplementary Examinations)* ya kukamilisha mafunzo yao wakati wanafunzi 43 walishindwa mitihani.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa fedha kupitia Wizara yangu kwa ajili ya kuwapa ruzuku wanafunzi wahitaji wa Taasisi hii kwa ajili ya kugharamia mafunzo. Tangu Julai, 2012 hadi sasa jumla ya Shilingi 2,232,558,500.00 zimetolewa na Serikali kwa ajili ya ruzuku kwa wanafunzi hao. Aidha, mchakato wa kurejea Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Mwaka 2004 umeanza ambapo suala la Mikopo kwa Wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Februari, 2013, Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto *(Institute of Judicial Administration)*, kilidahili wanafunzi 551 wa Mwaka wa Kwanza wa Stashahada ya Sheria na Wanafunzi 634 wa Cheti cha Sheria. Kulikuwa na Wanafunzi 273 wa Mwaka wa Pili wa Stashahada ya Sheria waliokuwa wanaendelea na mafunzo. Jumla ya wanafunzi 706 walihitimu mafunzo, ambapo 223 walitunukiwa Stashahada

ya Sheria na 483 walitunukiwa Cheti cha Sheria. Aidha, Chuo kiliendesha mafunzo ya awali *(Induction Course)* kwa ajili ya Mahakimu Wakazi wapya 290 waliokuwa wameajiriwa kufanya kazi katika Mahakama za Mwanzo sehemu mbalimbali hapa nchini. Mafunzo hayo ni sehemu ya Mpango Mkakati wa Chuo ya kuanzisha na kuendesha mafunzo mahususi na endelevu kwa Majaji, Mahakimu na Watumishi wengine wa Mahakama ya Tanzania. Vile vile, Chuo kimefikia asilimia 50 ya ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kiume 300 linalotarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inahakikisha uboreshaji wa mfumo wa teknolojia ya habari, elimu na mawasiliano, unapewa umuhimu wa kutosha. Katika kutekeleza azma hiyo, hatua ya kuunganisha kwenye Mfumo mmoja wa mawasiliano *(WAN),* Makao makuu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Divisheni ya Mashtaka na Kanda ya Dar es Salaam imeanza. Katika kutekeleza hili, usimikaji wa *Local Area Network (LAN),* ambayo ni ya kisasa, yenye uwezo wa kusafirisha na kupokea sauti, picha na takwimu, imeanza kufungwa Makao Makuu. Lengo ni kurahisisha, kuboresha mawasiliano na kuongeza ufanisi wa kazi. Aidha, Tovuti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali *(www.agctz.go.tz)* imeendelea kufanya kazi ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa mbalimbali kwa jamii. Pia, *Software* ya kutunza kumbukumbu za vitabu vya maktaba imekamilika na imeanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali ikiwemo kushiriki katika vipindi vya redio na runinga juu ya masuala ya Katiba na Haki za Binadamu, mikataba, uandishi wa sheria, uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi, masuala ya haki jinai pamoja na majukumu ya Ofisi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kuandaa mtandao wa kompyuta ujulikanao kama *Case Docket Management System,* utakaowezesha utunzaji wa nyaraka mbalimbali za mashauri nchini. Mfumo huu utakapokamilika, utaimarisha upatikanaji

wa takwimu za kesi na masuala mengine ya uendeshaji mashauri. Ofisi pia ipo katika hatua za usimikaji wa mfumo wa eletroniki kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu za uendeshaji mashauri katika ofisi zote za mikoa baada ya kazi ya kufunga mfumo kukamilika katika Makao Makuu na Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imekamilisha usimikaji wa mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu *(Data Center),* ambao lengo lake ni kuunganisha mifumo ya utunzaji kumbukumbu za Taasisi zilizo chini ya Wizara. Sambamba na uimarishaji wa mifumo ya teknolojia, Wizara iliendelea na jukumu la kutoa elimu kwa umma kwa njia ya vipindi vya redio na runinga kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu utoaji na usimamizi wa haki. Vilevile, Wizara imeingia Mkataba wa makubaliano na Kampuni Tanzu ya Serikali ya China ya *ZTE Corporation* ili kufanya upembuzi yakinifu wa kusimika mfumo wa *e-justice* katika Mahakama na Magereza ili kurahisisha usikilizaji wa kesi. Upembuzi huo yakinifu umekwishaanza na unaendelea kufanyika. Mpango huu wa kusikiliza kesi kwa kutumia mfumo maalum wa *e-justice* ilikuwa ni ahadi yangu wakati nikiwasilisha bajeti ya mwaka 2012/2013 Bungeni. Utaratibu wa kutekeleza Mradi huu unaendelea kwa kuratibiwa na Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* iliwajengea uwezo wa kitaalamu Mawakili kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wanasheria na Wataalam wengine walio katika Wizara mbalimbali na Idara za Serikali.

Mafunzo haya yalihusu nyanja za kujadili, kuandika na kuhakiki mikataba kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa hatua zote za majadiliano ya mikataba ili kuweza kubaini matatizo kabla ya mikataba kusainiwa na hatimaye kuwa na mikataba yenye maslahi kwa Taifa. Vilevile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo katika Mapambano Dhidi ya Rushwa *(STACA)*. Kazi zilizofanyika kwa Mwaka 2012/2013 kutokana na Mradi huu

ni kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali zinazokinzana, kufanya mapitio ya mafaili ya kesi za rushwa kwa kuzitolea ushauri, maandalizi ya Hadidu za Rejea kwa ajili ya kupata mtaalam mwelekezi wa kutengeneza mwongozo wa maadili kwa waendesha mashtaka na kuandaa majarida *(journals)* mbalimbali ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na jukumu la kuratibu na kutekeleza Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria kwa Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Sheria ambazo ni Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Sekretarieti inayoratibu huduma ya msaada wa Kisheria *(Legal Aid Secretariat)*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai hadi Februari, 2013, Programu imetekeleza kazi zifuatazo: Kukamilisha ujenzi wa majengo ya kudumu ya Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo *(Law School of Tanzania)*; Kuendesha mafunzo ya Jinsia kwa Watumishi toka Taasisi zinazotekeleza Programu kwa lengo la kupata wakufunzi watakaoendelea kutoa mafunzo haya ndani ya Taasisi husika; na kutayarisha andiko la mchakato wa kuandaa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria. Aidha, wahisani wamekubali kuongeza kipindi cha utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka mmoja zaidi hadi Juni, 2014 ili kukamilisha malengo yaliyochelewa kufikiwa. Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria ilipaswa kuisha Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Mahakama ya Tanzania imekarabati na kujenga Mahakama kama ifuatavyo:-

(i) Ukarabati wa Jengo la Mahakama Kuu Dar es Salaam na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu unaendelea.

(ii) Ujenzi wa mabweni ya Chuo cha Mahakama Lushoto unaendelea.

(iii) Ujenzi wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi uko katika hatua ya mwisho ambapo unategemewa kukamilika mwezi Juni, 2013.

(iv) Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya Kisarawe umekamilika.

(v) Ujenzi wa Mahakama Kuu Bukoba umekamilika na awamu ya pili ya ujenzi wa Jengo la Mahakama Kuu Shinyanga unaendelea.

(vi) Magari 33 yamenunuliwa yakiwemo magari 32 ya Waheshimiwa Majaji na basi moja kwa ajili ya Watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kuleta ufanisi na tija kazini, jumla ya watumishi 579 wa Wizara na Taasisi zake wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali nje na ndani ya nchi ikiwa ni pamoja na mafunzo kazini *(on job training).* Watumishi 13 wamepandishwa vyeo na watumishi 15 walihudhuria mikutano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kuiwakilisha Wizara katika masuala mbalimbali. Aidha, Tume ya Utumishi wa Mahakama hadi kufikia mwezi Februari, 2013 imefanya vikao viwili vya kawaida na vikao viwili vya dharura ambapo watumishi 17 waliajiriwa katika masharti ya kudumu na malipo ya pensheni; Mahakimu 98 walithibitishwa katika cheo pamoja na kuthibitisha kazini Hakimu mmoja. Tume kupitia vikao hivyo ilishughulikia masuala saba ya kinidhamu ambapo sita walirejeshwa kazini na mmoja alifukuzwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilikamilisha mchakato wa kumpata Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Msajili Mkuu wa Mahakama, Msajili wa Mahakama ya Rufani na Msajili wa Mahakama Kuu. Tume pia ilifanya ziara Katika Mikoa ya Mwanza, Mara na Kagera, kwa lengo la kutoa elimu kwa Watumishi wa Mahakama na Kamati za Maadili za Mikoa na za Wilaya kuhusu utendaji wake. Aidha, Tume imekagua Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya katika Mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Arusha,

Manyara, Dodoma, Morogoro na Pwani. Lengo la ukaguzi huu ni kufuatilia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi na kupata mafanikio mbalimbali. Hata hivyo, Wizara pia imeendelea kukabiliwa na changamoto. Baadhi ya Changamoto hizi ni kama ifuatavyo:-

(i) Baadhi ya Taasisi kukosa Ofisi zake za kudumu na hivyo kutumia gharama kubwa kwa ajili ya kulipia pango.

(ii) Bajeti inayotengwa kwenye Wizara na Taasisi zake imeendelea kuwa pungufu ikilinganishwa na mahitaji halisi ya kutekeleza majukumu ya Wizara ambayo yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka.

(iii) Wizara inakabiliwa na upungufu wa rasilimali watu katika Taasisi zake, hali ambayo inaathiri ufanisi wa utoaji haki kwa Wananchi.

(iv) Baadhi ya Wananchi kukosa imani na vyombo vya utoaji haki kutokana na baadhi ya watumishi wasio waadilifu kuendelea kulalamikiwa kwa kujihusisha na vitendo vya rushwa.

(v) Suala la mikopo kwa wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo limekuwa tatizo kubwa kwa Wizara na kwa wanafunzi husika ambao ni wahitimu wa Shahada ya Kwanza. Hali hii inatokana na Sheria ya Bodi ya Mikopo inayowaruhusu wanafunzi wa Shahada ya Kwanza *(undergraduate)* peke yake kupata mikopo hiyo.

(vi) Uwezo na uelewa mdogo wa Wananchi walio wengi kutumia vyombo vya kutoa haki na huduma za Kisheria kuhusu mfumo uliopo wa Sheria.

(vii) Mazingira ya kazi yasiyoridhisha kwa watumishi

walio wengi yanayotokana na maslahi duni na uhaba wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuzipatia ufumbuzi changamoto nilizozielezea, Wizara pamoja na Taasisi inaendelea kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuendelea kuomba na kufuatilia vibali ili kujaza nafasi zilizo wazi katika Muundo na kurejea Miundo ili itosheleze mahitaji ya Taasisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

(ii) Kuboresha mazingira ya kazi kwa kujenga na kukarabati Majengo ya Mahakama na Ofisi za Wizara na Taasisi.

(iii) Kuendelea kuainisha vipaumbele vya Wizara na Taasisi zake na kujenga hoja ya kuongezewa Bajeti kulingana na uwezo wa Serikali.

(iv) Kuwajengea watumishi uwezo na ujuzi wa taaluma zao.

(v) Kuimarisha uwajibikaji na uadilifu kwa kusimamia vyema Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utekelezaji wa majukumu.

(vi) Kufanya mawasiliano na Uongozi wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na kupendekeza Marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ya Mwaka 2007 kufanyika ili kulipatia ufumbuzi tatizo la Mikopo kwa Wanafunzi wenye Shahada ya Kwanza ya Sheria.

(vii) Kuendelea kutoa elimu ya Sheria na kusogeza huduma za Kisheria kwa Wananchi.

(viii) Kuongeza idadi ya Mawakili wa Serikali, Majaji, Mahakimu na Watumishi wa kada nyingine ili kuongeza kasi ya uendeshaji wa mashauri mbalimbali nchini. Lengo ni

kulipatia ufumbuzi suala la mlundikano wa mashauri mahakamani na msongamano wa Mahabusu na Wafungwa Magerezani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/ 2013, sasa napenda kulielezea Bunge lako Tukufu Mpango na Malengo ya Wizara yangu kwa Mwaka 2013/2014 kama ifuatavyo:-

(i) Kutoa elimu na habari kuhusu utoaji wa haki kwa jamii.

(ii) Kuimarisha utoaji wa huduma za Kisheria.

(iii) Kuhakiki na kushiriki majadiliano ya mikataba mbalimbali.

(iv) Kuboresha miundombinu ya utoaji haki.

(v) Kusikiliza na kuendesha Mashauri nchini.

(vi) Kufanya tafiti na tafasiri za Sheria.

(vii) Uandishi wa Sheria na Hati za Serikali.

(viii) Kuimarisha Taasisi za Mafunzo ya Sheria.

(ix) Kuimarisha shughuli za Usajili, Ufilisi na Udhamini.

(x) Kuimarisha Haki za Binadamu na Utawala Bora.

(xi) Kuratibu mchakato wa Mabadiliko ya Katiba.

(xii) Uratibu na utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria na Miradi ya Maendeleo.

(xiii) Kuimarisha Usimamizi na Uwajibikaji katika rasilimali.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2013/2014 Wizara itatekeleza Mpango na Malengo yake ambayo yamezingatia maelekezo yaliyotolewa na Serikali katika Mwongozo wake wa Utayarishaji Mpango na Bajeti kwa kuzingatia Vipaumbele vya Taifa na Kisekta vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mpango wa Pili wa Mwaka mmoja mmoja, MKUKUTA II na Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2010 – 2015). Wizara ya Katiba na Sheria ikiwa moja ya Wizara zilizo chini ya Nguzo ya Tatu ya MKUKUTA II ya Utawala Bora na Uwajibikaji, mkazo na msukumo utawekwa katika kuhakikisha kunakuwa na rasilimali za kutosha na mikakati ya utekelezaji wa mpango vinawekwa ili kuimarisha Utawala Bora, Utawala wa Sheria na uwajibikaji katika kusimamia matumizi ya rasilimali na upatikanaji wa haki kwa wakati ikiwa ni pamoja na kukamilisha mchakato wa mabadiliko ya Katiba kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mpango na Malengo ya Wizara yangu yamelenga kutoa kipaumbele cha kusogeza huduma za utoaji haki karibu na Wananchi kwa kuendelea kuimarisha na kujenga miundombinu muhimu ya utoaji haki, kujenga uwezo wa watumishi na kuongeza vitendea kazi katika Sekta ya Sheria. Malengo yafuatayo yatatekelezwa:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea Kuboresha Mfumo wa matumizi ya TEHAMA katika usikilizaji wa mashauri na utunzaji kumbukumbu pamoja na takwimu mbalimbali. Hivyo, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea kupanua mtandao wa kielektroniki kwa ajili ya kusikiliza au kuendesha Mashauri na shughuli mbalimbali za kiofisi.

(ii) Kuandaa Sera na Mkakati wa TEHAMA kwa Wizara na Mahakama.

(iii) Kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu kwa kutumia mtandao wa kompyuta.

(iv) Kuongeza matumizi ya kompyuta katika shughuli mbalimbali za kiofisi;

(v) Kuimarisha mafunzo ya ujuzi wa TEHAMA.

(vi) Kutayarisha programu mbalimbali zitakazojadiliwa kwenye vyombo vya habari kwa ajili ya kuelimisha umma kuhusu masuala ya Sheria, Haki za Binadamu na Utawala Bora na majukumu ya Wizara pamoja na Taasisi zake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea na mchakato wa kutunga Sheria itakayoratibu Utoaji wa Huduma za Kisheria kwa Umma na kutambua watoa huduma za msaada wa Kisheria kwa umma ikiwa ni pamoja na Wasaidizi wa Kisheria *(Paralegals)*. Aidha, Wizara itaendelea kupokea na kushughulikia malalamiko mbalimbali toka kwa Wananchi yanayohusu upatikanaji wa haki zao.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itahakikisha kuwa maslahi ya Taifa yanapewa kipaumble katika mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Aidha, mashirikiano haya yanakuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo ya Wananchi kwa ujumla. Katika kutekeleza lengo hili, ofisi imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kushiriki katika masuala ya Mtangamano wa Kikanda kwa masilahi ya Taifa.

(ii) Kutoa ushauri wa kisheria na kufanya majadiliano ya mikataba ya kibiashara na Mikataba ya Mahusiano ya Kikanda na Kimataifa *(Contracts & Treaties).*

(iii) Kuimarisha uwezo wa kutayarisha taarifa mbalimbali zinazojadiliwa katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa.

(iv) Kushiriki katika mikutano ya Kamati mbalimbali za uanachama wa vyombo mbalimbali vinavyohusika na uendeshaji wa mashauri ya jinai, madai, kikatiba na haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka 2013/2014, Wizara yangu kupitia Mahakama, imepanga kuendelea na ujenzi wa Mahakama Kuu ya Shinyanga na kuanza ujenzi wa Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma, Mara, Lindi na Morogoro. Aidha, Kanda Maalum ya Mahakama Kuu Ilala na baadaye Temeke na Kinondoni, zitaanzishwa ili kuweza kusogeza huduma karibu zaidi na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kazi, Mahakama itaanza ujenzi wa nyumba za Majaji katika Mkoa wa Dar es Salaam na pia kuboresha masjala za Mahakama Kuu, Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo kwa kuanzia na zile zilizoko mijini. Aidha, Mahakama pia itafanya upanuzi wa Jengo la Mahakama Kuu Dodoma na kuanza ujenzi wa Mahakama za Mwanzo za Bunda, Ludewa, Bariadi, Kawe, Mkomazi, Mailimoja, Lukuledi, Gairo, Mangaka na Nyamikoma.

Mheshimiwa Spika, Mahakama pia ipo katika hatua za awali za kuanzisha Programu Maalum ya Ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mikoa, Wilaya na Halmashauri husika. Ni matumaini yangu makubwa kuwa, Programu hiyo itasaidia katika kufanikisha lengo kuu la Wizara la kusogeza huduma karibu na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, itaendelea kuimarisha Ofisi mpya zilizoanzishwa katika Mikoa na Wilaya kwa kuzijengea uwezo wa kuendesha mashauri mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika utoaji haki kwa ujumla. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itafungua Ofisi mpya katika Mikoa ya Geita, Simiyu, Katavi na Ofisi moja katika Wilaya ya Tarime. Vilevile, Wizara itafanya ukarabati wa Jengo la Ofisi

za Wizara (Makao Makuu) na kukamilisha ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya *RITA.* Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itaendelea kuimarisha Ofisi zake za Kanda na itaanzisha Ofisi nyingine za Kanda za Kilimanjaro, Mbeya na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri katika ngazi mbalimbali za Mahakama, kupitia Programu Maalum ya Kumaliza Mlundikano wa Mashauri ya Nyuma 1,918 yaliyoko Mahakama ya Rufani, 12,093 Mahakama Kuu, 329 yaliyoko Mahakama Kuu - Divisheni ya Biashara, 1,780 yaliyoko Mahakama Kuu - Divisheni ya Kazi, 5,393 yaliyoko Mahakama Kuu - Divisheni ya Ardhi, 25,370 yaliyoko Mahakama za Hakimu Mkazi, 21,538 yaliyoko Mahakama za Wilaya na 197,715 yaliyoko Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mahakama pia itaongeza kasi ya usikilizaji wa mashauri katika ngazi za Mahakama za Mikoa (*RMs* na Wilaya) kwa kutenganisha shughuli za Kimahakama na za Kiutawala. Vilevile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendesha Mashauri ya Madai, Katiba na Jinai na kushughulikia mashauri ya zamani na mengine mapya yatakayopokelewa.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka 2013/2014 Wizara yangu itaendelea kufanya mapitio ya Mfumo wa sheria zinazosimamia huduma za jamii kwa wazee, sheria zinazomlinda mlaji na sheria za makosa ya jinai. Kutafsiri Sheria kutoka Lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili, kufanya uchambuzi wa hukumu za kesi za Mahakama ya Rufani ili kuainisha misingi ya kisheria na kuziweka kwenye Tovuti ya Tume ya Kurekebisha Sheria. Aidha, Wizara yangu itafanya mapitio ya Sheria mbalimbali ili kuhakikisha kuwa hazikinzani na Katiba ya Nchi na Misingi ya Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwa na Mfumo wa Sheria nchini unaokidhi mahitaji ya jamii katika kujiletea maendeleo kiuchumi, kijamii na kiteknolojia, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kusimamia uandishi, tafsiri na urekebu wa Sheria mbalimbali za Nchi.

(ii) Kutayarisha Maazimio mbalimbali ya Kimataifa ambayo Nchi imeweka saini ili yaridhiwe na Bunge.

(iii) Kuwezesha upatikanaji wa Sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuimarisha Taasisi za Mafunzo ya Sheria kwa kuanzisha ushirikiano maalum wa maendeleo ya watumishi kati ya Mahakama, Chuo cha Uongozi wa Mahakama na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuimarisha shughuli za Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *(RITA)* ili kuhakikisha kwamba, lengo la Taasisi hii la kuwa Wakala linafikiwa kwa ufanisi. Katika Mwaka wa Fedha 2013/ 2014, Wakala unatarajia kuupeleka Mfumo wa Usajili wa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano *(Under 5 Births Registration Initiative - U5BRI)* hadi ngazi ya Serikali za Mitaa, ili kupunguza mlundikano wa vizazi ambavyo havijasajiliwa na kumwezesha mtoto kupata cheti cha kuzaliwa ambacho ni haki yake ya msingi. Mpango huu unatarajiwa kuanza rasmi katika Mkoa wa Mbeya na kuendelea kuutekeleza katika Mikoa ya Simiyu, Geita, Shinyanga na Mwanza. Katika Mfumo huu, utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa mara ya kwanza hutolewa bila tozo kwa watoto wote walio na umri wa chini ya miaka mitano. Aidha, Wakala pia utatekeleza mkakati wa kusajili watoto wa umri kati ya miaka 6 hadi 18 *(6 - 18 Birth Registration Initiative)* waliopo mashuleni kwa kutumia Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wakala unatarajia kuanzisha mazungumzo kati yake na *NIDA* pamoja na Uhamiaji, ili kuona namna ya kupunguza gharama za usajili kwa kutumia Mifumo ambayo tayari ipo kwa ajili ya uandikishaji na uchapishaji wa vyeti.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imedhamiria kuhakikisha kuwa Sheria na taratibu zilizowekwa na mamlaka mbalimbali kuhusu haki za binadamu zinafuatwa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu mbalimbali. Kwa kuzingatia hilo, Ofisi imedhamiria kufanya yafuatayo:-

(i) Kutoa ushauri wa kisheria ulio bora katika masuala ya Katiba na Haki za Binadamu.

(ii) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa masuala ya haki za binadamu nchini kwenye Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya Haki za Binadamu ambayo Nchi imeridhia na kuziwasilisha kwenye vyombo husika kwa ajili ya majadiliano.

(iii) Kufanya ukaguzi katika maeneo yanayohifadhi mahabusu na wafungwa ili kutoa ushauri wa namna ya kuboresha.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, itaendelea kulinda, kukuza na kuhifadhi Haki za Binadamu na Utawala Bora. Katika mwaka 2013/2014, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, itaendelea kukamilisha uchunguzi wa mashauri ya uvunjwaji wa Haki za Binadamu ambao haukukamilika; kufanya tafiti kuhusu Haki za Binadamu na Utawala Bora; kupitia Miswada na Sheria ili kuangalia kama zinakidhi vigezo vya kimataifa na vya kikanda ili kulinda Haki za Binadamu na Utawala Bora; na kukagua Magereza na Vituo vya Polisi na sehemu nyinginezo wanamozuiliwa watu. Aidha, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itaendelea kushughulikia malalamiko yaliyosalia na yatakayopokelewa, yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia maadili ya Mahakimu, Wizara yangu kupitia Tume ya Utumishi wa Mahakama, itaendelea kuzijengea uwezo Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya kwa Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara Tanga, Dodoma na Singida, kwa kuzipatia mafunzo ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Tume

itaendelea na kazi ya kukagua Kamati za Maadili za Mkoa na Wilaya kwa Mikoa ya Mtwara, Lindi, Mbeya, Rukwa na Katavi. Lengo likiwa ni kuona kama zinatekeleza majukumu yake kwa misingi ya sheria na taratibu. Tume itaitisha vikao vinne vya kawaida kwa ajili ya kujadili na kuamua masuala mbalimbali ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuratibu jambo kubwa na la kihistoria nchini mwetu ambalo ni mchakato wa mabadiliko ya Katiba. Awamu ya kwanza ya ukusanyaji wa maoni ya Wananchi na Makundi mbalimbali imekamilika. Hivi sasa Tume ya Mabadiliko ya Katiba inaendelea na uchambuzi wa maoni hayo ili kuandaa Rasimu ya Katiba itakayowasilishwa kwenye Mabaraza ya Katiba. Aidha, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara yangu kupitia Tume ya Mabadiliko ya Katiba, inategemea kufanya mambo yafuatayo ili kukamilisha mchakato huu wa mabadiliko ya Katiba:-

(i) Kusimamia Mikutano ya Mabaraza ya Katiba.

(ii) Kuchambua maoni yatakayotolewa na Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba.

(ii) Kuchapisha Ripoti na Rasimu ya Katiba.

(iv) Kuwasilisha Rasimu ya Katiba katika Bunge Maalum la Katiba.

(v) Kutoa elimu na kuhamasisha Wananchi kushiriki katika Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa mchakato huu wa mabadiliko ya Katiba, kupitia kwenu Waheshimiwa Wabunge, ninaomba muwahamasishe Wananchi wa Majimbo yenu ili waweze kujitokeza kwa wingi katika kutoa mawazo kuhusu Rasimu ya Katiba kupitia kwa Wajumbe wanaounda Mabaraza ya Katiba. Nawahamasisha na kuziomba Taasisi, Asasi za Kiraia, Jumuia za Kidini, Vyama vya Siasa na Makundi mengine yote, kuunda

Mabaraza ya Katiba. Aidha, ninawaomba Wajumbe wa Mabaraza kutoa mawazo yao kwa uwazi, uhuru na bila ya hofu yoyote. Pia nipende kuwahakikishia Wananchi kuwa, Tume inafanya kazi zake kwa uhuru na uwazi na kwamba, maoni yote yaliyotolewa na yatakayotolewa na Wananchi, Taasisi, Asasi za Kiraia na Makundi mengine, yanaheshimiwa na kufanyiwa kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Muda wa Kati *(Medium Term Strategy)* wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria na Miradi ya Maendeleo, kwa kuendelea kuziwezesha Taasisi zinazotekeleza Programu hii kuboresha Mfumo wa Sheria na kuimarisha mazingira ya kisheria yanayoongeza fursa ya Wananchi ya kupata haki kwa wakati ili kuwezesha jamii kutumia muda wao mwingi katika kujihusisha na kazi za maendeleo ya kiuchumi na kijamii, badala ya kupoteza muda huo wakitafuta haki. Aidha, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imekwishaanza kujiandaa kukamilisha na hatimaye kufunga Programu kwa kuanza kutekeleza kazi ya kufanya tathmini ya hali ya sasa ya Sekta hii *(Legal Sector Assessment)* ili kujua kiwango cha maendeleo kilichofikiwa, kubaini changamoto zinazoikabili Sekta hii na kutambua fursa zilizopo na ambazo zinaweza kutumika kikamilifu katika mipango hiyo ya kuboresha sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kubuni mbinu na kuanzisha Miradi mbalimbali ya Maendeleo ya kuboresha huduma zitolewazo na Taasisi mbalimbali za Sheria, ili kuweza kufikia dira yetu ya 'haki sawa kwa wote na kwa wakati'. Kama ambavyo nililiarifu Bunge lako Tukufu mwaka uliopita kwamba, Wizara yangu imebuni na itaanzisha Mradi wa *e-justice*; ninafurahi kulialifu Bunge lako Tukufu kwamba, tayari hatua za awali za Mradi huu zimekwishaanza na Serikali ya China imeridhia kufadhili Mradi huu. Tayari kazi ya upembuzi yakinifu wa Mradi huo inafanywa na Kampuni ya *ZTE Corporation,* iliyokasimiwa kazi hiyo na Serikali ya China. Kutegemeana na taarifa ya upembuzi yakinifu wa Mradi huu itakayoandaliwa, Wizara yangu itatekeleza Mradi huu kwa awamu tatu. Awamu ya kwanza ikiwa ni majaribio *(Pilot*

*Study)* kwa Mkoa wa Dar es Salaam, kisha kuhusisha Mikoa yote yenye Kanda za Mahakama Kuu kwa awamu ya pili na awamu ya tatu kukamilisha Mradi kwa kufikia Mikoa yote Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia umuhimu wa kuwepo na Mikataba mizuri yenye maslahi kwa Taifa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, itaendelea kuwajengea uwezo wa kitaalam Mawakili wa Serikali katika nyanja za kujadili, kuandika na kuhakiki mikataba kupitia Mradi wa *UNDP* unaofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa *(UNDP).* Katika uendeshaji wa mashauri ya rushwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kutekeleza Mradi wa Uimarishaji wa Mapambano Dhidi ya Rushwa Tanzania *(STACA),* kwa kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali katika uendeshaji wa mashauri ya rushwa, ununuzi wa vitendea kazi, uimarishaji wa mfumo wa utunzaji na usimamizi wa kumbukumbu za mashauri kielektroniki *(Case Docket Management System).*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imezingatia lengo hili katika mipango yake ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na usimamizi madhubuti wa rasilimali mbalimbali za Serikali. Katika kufanikisha lengo hili, mambo yafuatayo yatafanyika:-

(i) Kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha katika Ofisi za Makao Makuu na Mikoa kwa Taasisi zote za Wizara.

(ii) Kufanya ukaguzi wa vifaa mbalimbali vilivyopo na vinavyonunuliwa katika Ofisi zote.

(iii) Kutayarisha ratiba ya utekelezaji wa mpango kazi wa malengo yaliyopangwa na Wizara na Taasisi zake ili kuwezesha utekelezaji na utoaji wa taarifa.

(iv) Kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango ya Wizara.

(v) Kuimarisha uwajibikaji na uadilifu katika utendaji wa kazi katika ngazi mbalimbali.

(vi) Kuwaongezea watumishi maarifa na ujuzi katika maeneo yao ya kitaalam ili wawe na tija wakati wa kutekeleza majukumu yao hasa katika maeneo ambayo yameonekana kuwa na changamoto nyingi katika kuleta ufanisi wa utendaji.

(vii) Kuandaa Mpango thabiti wa rasilimali watu kwa Wizara na Taasisi na kuchambua mahitaji ya ujuzi kwa kila eneo la utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wadau wetu wa maendeleo kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuboresha Sekta yetu ya Sheria. Kwa namna ya pekee, napenda kushukuru Nchi za Canada na Denmark ambazo kupitia Mashirika yao ya Kimataifa ya Maendeleo ya *CIDA* na *DANIDA,* wameisaidia sana Wizara yangu katika kushawishi Mashirika na nchi nyingine wahisani, kuelekeza misaada yao katika kuboresha Sekta ya Sheria. Nayashukuru pia Mashirika na Taasisisi za Kimataifa zifuatazo; Benki ya Dunia *(WB),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Watoto *(UNICEF)*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo *(UNDP)* na Taasisi ya Maendeleo ya Kimataifa ya Serikali ya Uingereza *(DFID).*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Sheria kwa ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2012/2013 kama yalivyobainishwa katika Hotuba hii. Ninapenda kumshukuru Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Angellah Kairuki (Mbunge), Jaji Mkuu - Mheshimiwa Othmani Chande, Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Mheshimiwa Frederick Mwita Werema, Jaji Kiongozi - Mheshimiwa Fakih A.R. Jundu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria - Ndugu Fanuel E. Mbonde, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania - Ndugu Hussein Kattanga, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Ndugu George Masaju, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania - Ndugu Ignas Paul Kitusi, Mkurugenzi wa Mashtaka - Dkt. Eliezer M. Feleshi, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria - Bi. Winifrida Korroso, Katibu Mtendaji Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

- Bi. Mary Massey, Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo - Mheshimiwa Dkt. Gerald Ndika, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa *RITA* - Ndugu Philip Saliboko, Wakurugenzi wa Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote, kwa ushirikiano na kazi kubwa waliyoifanya katika kuandaa Mpango na Bajeti hii kwa wakati. Ni matarajio yangu kwamba, Wizara itaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2013/2014 kama walivyofanya nitekeleze majukumu yangu na wajibu wangu kwa ufanisi hadi sasa. Mwisho, natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, kwa kufanikisha uchapishaji wa Hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, tukitambua kwamba, Sekta ya Sheria ndiyo jiwe la msingi katika Utawala wa Serikali na kwa kuzingatia umuhimu wa Sekta ya Sheria katika kuchochea maendeleo ya nchi kiuchumi, kisiasa, kijamii, kisayansi na kiteknolojia, Wizara ya Katiba na Sheria inao wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba, inakuza, inaimarisha na inalinda amani na utulivu na kudumisha haki za binadamu na Utawala wa Sheria nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Wananchi wote na Waheshimiwa Wabunge, kuhakikisha kuwa azma ya Serikali ya kulinda Amani, Utulivu na Haki za Binadamu inazingatiwa, inaendelezwa na kupewa kipaumbele kwa manufaa ya Taifa letu na kwa kizazi kijacho.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara ya Katiba na Sheria ilitengewa jumla ya Sh. 186,323,718,000. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2013 jumla ya Sh. 86,005,210,966.19 zilikuwa zimekwishatumika. Ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014. Wizara yangu inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Sh. 230,687,333,000 kwa ajili ya Taasisi, Idara na Vitengo vya Wizara. Matumizi ya Kawaida yanaombewa jumla ya Sh.195,427,547,000. Kati ya fedha hizo, Sh.152,890,448,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh.42,537,099,000 ni kwa ajili ya Mishahara. Miradi ya Maendeleo inaombewa jumla ya Sh. 35,259,786,000. Kati ya fedha hizi, Sh. 24,000,000,000 ni za ndani na Sh.11,259,786,000 ni fedha za nje. Mchanganuo

wa matumizi ya bajeti kwa mafungu ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 8 - Tume ya Mabadiliko ya Katiba: Matumizi Mengineyo Sh. 33,944,588,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama: Matumizi ya Mishahara Sh. 161,882,000, Matumizi Mengineyo Sh. 2,871,716,000. Jumla Sh. 3,033,598,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Matumizi ya Mishahara Sh. 2,174,186,000, Matumizi Mengineyo Sh. 8,332,865,000, Matumizi ya Maendeleo (nje) Sh. 826,000,000. Jumla Sh. 11,333,051,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 35 - Mkurugenzi wa Mashtaka: Matumizi ya Mishahara Sh. 4,383,211,000, Matumizi Mengineyo Sh. 6,460,826,000, Matumizi ya Maendeleo (nje) Sh. 2,167,759,000. Jumla Sh. 13,011,796,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 40 – Mahakama: Matumizi ya Mishahara Sh. 30,980,157,000, Matumizi Mengineyo Sh. 86,600,000,000, Matumizi ya Maendeleo (ndani) Sh. 20,000,000,000, Matumizi ya Maendeleo (nje) Sh. 2,716,668,000. Jumla Sh. 140,296,825,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria: Matumizi ya Mishahara Sh. 2,447,110,000, Matumizi Mengineyo Sh. 8,028,651,000, Matumizi ya Maendeleo (ndani) Sh. 4,000,000,000, Matumizi ya Maendeleo (nje) Sh. 3,898,840,000. Jumla Sh. 18,374,601,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora: Matumizi ya Mishahara Sh. 1,814,993,000, Matumizi Mengineyo Sh. 3,795,802,000, Matumizi ya Maendeleo (nje) Sh. 1,034,169,000. Jumla Sh. 6,644,964,000.

Mheshimiwa Spika, Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria: Matumizi ya Mishahara Sh. 575,560,000, Matumizi

Mengineyo Sh. 2,856,000,000, Matumizi ya Maendeleo (nje) Sh. 616,350,000. Jumla Sh. 4,047,910,000.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa mwaka 2013/ 2014 inatarajia kukusanya jumla ya kiasi cha Sh. 5,250,454,700 kama maduhuli ya Serikali. Mchanganuo wa makusanyo kwa mafungu husika ni kama ifuatavyo: Fungu 16 - Sh. 3,002,000; Fungu 40 - Sh. 2,261,303,900; Fungu 41 - Sh. 2,983,648,800; Fungu 55 - Sh. 2,500,000. Jumla Sh. 5,250,454,700.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa maombi ya fedha kwa kila Fungu umeainishwa kwenye Randama zilizoandaliwa kwa kila Fungu na kuwasilishwa hapa Bungeni rasmi. Hata hivyo, nitaleta pia mapendekezo ya nyongeza kidogo ambayo tumepewa asubuhi hii ya shilingi bilioni 30 ambazo tutaziweka kwenye mgawanyo unaohusika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA**: Hoja hii imeungwa mkono, tunaendelea na hatua inayofuata.

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi wakati Viongozi mbalimbali walipokuwa wanaleta nyaraka zao Mezani, huwa tunatumia Kifungu cha 99(5), ambacho kinasema hivi: "Asubuhi ya siku ambayo Waziri amepangiwa kuwasilisha hoja ya makadirio ya Wizara yake, Waziri, Mwenyekiti wa Kamati inayohusika au Mjumbe yeyote atakayeteuliwa kwa niaba yake na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara husika, wataweka Mezani nakala ya taarifa zao kwa kuzingatia mpangilio wa shughuli za Bunge. Ndiyo maana nikasema kwamba, vingine naviona hapa na vingine sivioni.

Mheshimiwa Tundu Lissu, ameniletea ingawa nimeona *distribution* yake siyo nzuri, lakini tunakubali, naomba

mzingatie hivyo. Kuweka Mezani ni pamoja na kuweka hapa kwangu, mnaposema na mimi naiona. Siyo kuwekewa mbuzi kwenye gunia halafu mnasema mnasema mmepata *document.*

Nashukuru sana. Sasa nimwite msemaji wa Kamati iliyohusika na suala hili; Mheshimiwa Gosbert Blandes.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, naomba kutoa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/ 2014.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na 117(11), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inahusisha Mafungu manane; Fungu 8 - Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama, Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Fungu 35 - Mkurugenzi wa Mashtaka, Fungu 40 - Mahakama, Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria, Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata muda wa kutosha wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake

kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Mathias Chikawe - Waziri wa Katiba na Sheria, akishirikiana na Naibu Waziri - Mheshimiwa Angellah Kairuki. Katika maelezo yake, Waziri aliieleza Kamati kuhusu utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa kipindi cha mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi wa Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati ulizingatiwa. Kwa yale maeneo ambayo utekelezaji upo katika hatua za awali, Kamati inasisitiza Wizara ikamilishe utekelezaji wa maagizo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara ya Katiba na Sheria inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

Ukomo wa bajeti umeendelea kuwa changamoto kubwa kwa Wizara kwani kiasi cha fedha kinachotengwa kwa Wizara kimekuwa hakikidhi mahitaji halisi ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake; Ucheleweshwaji wa mashauri mahakamani pia ni changamoto inayoendelea kuwa kikwazo katika mfumo wa utoaji haki nchini; Vitendo vya rushwa kuendelea kujitokeza katika baadhi ya vyombo vya utoaji haki, hali ambayo inasababisha Wananchi kukosa imani na vyombo vya utoaji haki; Serikali kuchelewa kuwasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo kumeendelea kuwa kikwazo kikubwa kwa Wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa vitendo *(The Law School of Tanzania)*, kwani sheria iliyounda Bodi ya Mikopo haiwapi fursa ya kukopa wanafunzi waliomaliza Shahada ya Kwanza ya Sheria.

Mazingira duni ya kufanyia kazi kwa Watumishi wa Wizara pamoja na Taasisi zake hususan ukosefu wa majengo

ya Mahakama za Mwanzo, Ofisi za Mawakili wa Serikali pamoja na Taasisi zingine; upungufu wa watumishi katika Taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria, bado ni changamoto inayotakiwa kufanyiwa kazi, upungufu huu unasababisha ufanisi kupungua au baadhi ya kazi kutotekelezeka kwa wakati; uwezo mdogo wa Wananchi walio wengi kutumia vyombo vya kutoa haki na huduma za kisheria na uelewa mdogo wa Wananchi kuhusu mfumo uliopo wa Sheria na Mahakama nchini; Serikali kupitia Mahakama kutotoa machapisho ya Ripoti za Maamuzi ya Mahakama kuanzia mwaka 1998 – 2006 *(The Tanzania Law Reports 1998 - 2006)* kwa Umma na badala yake kutumika na Mahakama peke yake, kumeendelea kuwa kikwazo kwa Mawakili ambao hushindwa kufanya rejea ya Maamuzi hayo kwa kuwa machapisho hayo hayajawekwa tayari ili yaweze kuuzwa kwa Mawakili wa Kujitegemea kwa lengo la kuwarahisisshia kufanya rejea; Wasaidizi wa Sheria wa Majaji kufanya kazi bila kuapishwa kama Maafisa wa Mahakama *(Judicial Officers)* kwa muda wa miaka mitatu mfululizo toka waajiriwe mwaka 2010 huku wakiwa wanafanya kazi nyeti sana inayohusisha kuwasaidia Waheshimiwa Majaji katika kutoa haki. Kutoapishwa huko kumeendelea kuwanyima baadhi ya haki na stahiki zingine ambazo Mahakimu na Maafisa wengine wa mahakama wanazipata; hivyo, kuwafanya wajisikie wanyonge na kujihisi kuwa wao siyo sehemu ya Mahakama na hivyo kupunguza ari ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati na kwa kuzingatia majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake, Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Wizara na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Tume ya Mabadiliko ya Katiba mnamo tarehe 7 Machi, 2013. Katika ziara hiyo, Kamati ilielezwa kazi mbalimbali zinazofanywa na Tume na hatua ambayo Tume imefikia katika ukusanyaji wa maoni ya Wananchi. Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba katika kuratibu mchakato mzima wa Mabadiliko ya Katiba.

Kamati ilipotembelea Tume iliambiwa kuwa, zoezi la ukusanyaji wa maoni ya Wananchi limekwishakamilika; hivyo, Tume kuendelea na zoezi la kutathmini na kuchambua maoni hayo, kupitia na kuchambua michango, mawazo, taarifa na mapendekezo yaliyokusanywa na kufanyiwa tathmini siku za nyuma kwa madhumuni ya kuandaa Rasimu ya Katiba Mpya ili iweze kuchambuliwa kwenye Mabaraza ya Katiba. Pamoja na hayo, Kamati inashauri ifuatavyo:-

Moja, Kamati inashauri Serikali kufuatilia kwa makini utendaji kazi wa Tume hii bila kuathiri uhuru wa Tume ili kuiwezesha nchi kufikia lengo la kupatikana kwa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wakati mwafaka.

Mbili, Kamati inashauri kwamba, bajeti ya Bunge la Katiba ifahamike na kuletwa Bungeni mapema kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/ 2013, Tume ya Utumishi wa Mahakama - Fungu 12, ilitengewa kiasi cha Sh. 977,101,000. Kufikia Februari, 2013, Tume ilikuwa imepokea kiasi cha Sh. 709,279,940, kiasi hiki cha fedha kimetumika kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Tume kuajiri Mahakimu 17 kwa masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni. Aidha, Tume imeendelea na jukumu lake kubwa la kumshauri Rais kuhusu uteuzi wa Jaji Mkuu na Majaji wengine wa Mahakama Kuu. Aidha, kwa mwaka huu wa fedha wa 2013/2014, Tume ya Utumishi wa Mahakama imetengewa kiasi cha shilingi 1,471,716,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi 161,882,000 ni kwa ajili ya mishahara. Hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kama ilivyokuwa mwaka jana, jambo ambalo Kamati inaona siyo jema kwani kutenga fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kila mwaka hakutaisaidia Mahakama kupiga hatua za kimaendeleo.

Kamati katika majadiliano ya Makadirio ya Bajeti ilishauri Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria kuiongezea fedha Tume hii ili iweze kutimiza majukumu yake kwa ufanisi

zaidi. Kiasi cha shilingi 1,471,716,000 kilichotengwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 hakikidhi mahitaji ukilinganisha na majukumu mazito iliyonayo Tume ya Utumishi wa Mahakama.

Kamati inatoa pongezi kwa Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Othman Mohamed Chande, kwa kukubaliana na ushauri wa Kamati kutekeleza maagizo ya kuiongezea Tume ya Utumishi wa Mahakama kiasi cha fedha hadi kufikia shilingi 2.9 bilioni ili kuiwezesha Tume kifedha kutoka Mfuko wa Mahakama kwa lengo la kuziwezesha Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya kufanya kazi zao kama inavyotakiwa kupitia Barua yenye Kumb. Na. CAB.75/197/01 ya tarehe 8 Aprili, 2013 iliyotumwa kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria na kunakiliwa kwa Katibu wa Bunge. Wizara iendelee kuwaelimisha Wananchi kuhusu uwepo wa Tume hii pamoja na majukumu yake ili ifahamike na Wananchi wengi zaidi na hatimaye kuwawezesha Wananchi kutoa malalamiko pale kunapotokea ukiukwaji wa maadili kwa baadhi ya Watendaji wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia utekelezaji wa majukumu na makisio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, Kamati ilishauri ifuatavyo kuhusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Fungu 16:-

Moja, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iimarishe Kitengo cha Mikataba kwa kuwajengea uwezo wa fedha na rasilimali watu ili Kitengo hiki kiweze kushiriki kikamilifu katika kuingia Mikataba mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa.

Mbili, Kamati inashauri Kitengo cha Uandishi wa Miswada kinapokuwa kinaandaa Miswada kwa lengo la kuileta Bungeni, kiandae Miswada kwa Lugha ya Kiswahili na Kiingereza ili hatimaye inapokuwa imepitishwa na Bunge, kuwepo na sheria moja yenye Lugha ya Kiingereza na Kiswahili ili kuwawezesha Wananchi wengi kunufaika na Sheria hiyo kwa kiwango kikubwa.

Tatu, Kamati inashauri kwamba, kwa kuwa kasi ndogo

ya kushughulikia mashauri inatokana na sababu mbalimbali ikiwemo uhaba wa watumishi, ni vyema Serikali ikaiwezesha ofisi hii kibajeti ili iweze kuajiri watumishi wa kutosha.

Nne, asilimia saba tu ya bajeti nzima ya mwaka 2013/2014 imetengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambayo ni kidogo sana kuleta maendeleo katika Sekta ya Sheria. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya mwaka 2013/2014 ni shilingi 11,333,051,000 na kati ya hizo, shilingi 826,000,000 pekee ndizo zilizotengwa kwa Miradi ya Maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kuanza kutenga fedha nyingi zaidi ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Tano, Serikali iboreshe maslahi ya watumishi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuwapa motisha watumishi hao kufanya kazi kwa bidii na kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia bajeti ya Wizara, Kamati ilielezwa kazi zinazofanywa na Mkurugenzi wa Mashtaka ikiwa ni pamoja na kusimamia vyema uendeshaji wa mashauri ya jinai na uratibu wa kazi zinazofanywa na Vyombo vya Upelelezi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza uwezo wa fedha kwa ajili ya kuiwezesha Kurugenzi ya Mashtaka kutekeleza vyema mpango wake wa kutenganisha suala la upelelezi na uendeshaji wa mashtaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi zilizofanywa na Ofisi ya Kurugenzi ya Mashtaka kwa kufungua ofisi zake katika Kanda za Morogoro, Pwani na Njombe. Aidha, Kamati inaishauri Kurugenzi ya Mashtaka kuongeza kasi zaidi kufungua Ofisi katika kila Wilaya, hasa katika Wilaya mpya ili kurahisisha uendeshaji wa Mashtaka nchini.

Kamati inashauri kwamba, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali iongezewe Mawakili wa Serikali kwani Mahakama inajitahidi kuongeza idadi ya Mahakimu, hivyo ni vyema mawakili nao wakaongezwa ili kuwe na uwiano wa kiutendaji kati ya Mawakili na Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia utekelezaji wa

majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake, Kamati ilibaini kuwa Wizara imejitahidi katika kujenga na kukarabati mahakama zilizo katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Tarehe 18 Machi, 2013 Kamati ilifanya ziara katika Wilaya ya Kisarawe na kujionea Jengo la Kisasa la Mahakama ya Mwanzo na Mahakama ya Wilaya ya Kisarawe. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hiyo. Aidha, Kamati inashauri Wizara kununua vifaa vya kisasa kama kompyuta kuliko kutumia *typewriter na* kununua samani za ndani kwa ajili ya Mahakama zote nchini, kwani uzoefu unaonesha kwamba, samani zinazotengenezwa ndani ya nchi zinadumu muda mrefu zaidi kuliko zinazotengenezwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa kuona Serikali haikupeleka kiasi chochote cha fedha za maendeleo kati ya kiasi cha shilingi 17,213,116,000 zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Suala hili linatia shaka kama kweli Serikali ina utashi wa dhati wa kumaliza changamoto ya ukosefu wa majengo, uchakavu na upungufu wa vifaa katika mahakama. Aidha, Kamati imebaini kwamba, kitendo cha Serikali kutokutoa fedha iliyokuwa imepangwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, kimekwamisha Miradi ya Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo za Kawe, Bunda, Mangaka, Gairo, Bariadi, Lukuledi na Mkomazi. Kamati inaishauri Serikali kuzitoa fedha hizo mapema ili kuwezesha miradi ya ujenzi wa Mahakama kuendelea kama ilivyokuwa imepangwa.

Kamati inashauri Mahakama ipewe fedha za kujenga majengo ya Mahakama Kuu kwenye Mikoa ya Kigoma, Mara, Lindi, Morogoro, Singida, Manyara, Katavi, Njombe, Simiyu na Pwani ambako Wananchi husafiri mwendo mrefu kwa kutumia gharama nyingi kutafuta haki zao kwenye mikoa mingine zilipo Kanda za Mahakama Kuu. Aidha, Mahakama inahitaji ongezeko la watumishi wa fani mbalimbali wanaofikia 3455 ili kuweza kutoa huduma kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi

mbalimbali zinazofanywa na Uongozi wa Mahakama katika kupunguza mlundikano wa mashauri Mahakamani (*Back logs*). Mahakama ya Mwanzo kwa mfano iliingia Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ikiwa na idadi ya mashauri 124,959 yaliyosalia toka miaka ya nyuma na kusajili mashauri mapya 650,140, hivyo kuwa na jumla ya mashauri 775,140. Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba, 2012, Mahakama ya Mwanzo ilisikiliza na kutolea uamuzi mashauri 577,425, sawa na asilimia 89 ya mashauri yaliyofunguliwa na hivyo kubaki na mashauri 197,715.

Kamati imeridhishwa sana na kasi hii na kuamini kuwa kama itaendelea hivyo, inaweza kumaliza kabisa tatizo la mlundikano wa mashauri mahakamani. Pamoja na jitihada hizi, Kamati inashauri Mahakama ije na njia bora zaidi ya upimaji wa utendaji kazi wa Mahakimu na Majaji ili kuongeza ufanisi na utendaji wa Mahakama kwenye kazi za msingi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kukubaliana na ushauri uliotolewa na Kamati wa kuondokana na utaratibu wa uendeshaji wa mashauri mahakamani kwa kuandika mwenendo wa mashauri kwa njia ya mkono na badala yake kufikiria kutumia njia ya kisasa inayofanana na *Hansard* katika baadhi ya divisheni za Mahakama. Kamati ilijulishwa kwamba, Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu Wa China, zinaendelea kufanya upembuzi yakinifu wa Mradi mkubwa wa *Tele-justice* utakaoiwezesha Mahakama kuendesha Mashauri na kurekodi mienendo ya kesi kama ilivyo *Hansard.*

Kamati inaishauri Serikali kutilia mkazo na kusukuma upembuzi yakinifu kwa haraka zaidi ili Mahakama iweze kuondokana haraka na mfumo wa zamani wa kurekodi mienendo ya kesi kwa njia ya mkono.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha Mfuko wa Mahakama kibajeti ili Mfuko huo uweze kukidhi haja za mahitaji ya Mahakama. Aidha, Kamati inaishauri Serikali itoe motisha kwa Mahakimu wanaofanya kazi katika mazingira mugumu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa jumla ya shilingi 12,986,298,000. Kati ya fedha hizo, fedha za matumizi ya kawaida zilikuwa shilingi 9,544,571,000 na shilingi 3,441,727,000 zilikuwa fedha za nje kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Hadi kufikia Februari, 2013, fedha zilizopokelewa kutoka Hazina na kutumika zilikuwa shilingi 4,483,399,491.64, sawa na asilimia 47 ya bajeti nzima iliyopangwa; hivyo, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

- Kasi ya utoaji wa fedha zinazotengwa na Wizara na kupitishwa na Bunge zitolewe kwa wakati ili kuwezesha ufanikishaji wa utekelezaji wa shughuli hizo.

- Serikali kuweka kipaumbele Miradi ya Maendeleo na kutenga fedha za ndani kwa ajili hiyo kuliko kutegemea fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kazi nzuri inayofanywa na Tume ya kurekebisha Sheria, ikiwa ni pamoja na kukamilisha Taarifa ya Mfumo wa Haki za Madai *(Civil Justice System)*, inayofanywa na Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania. Aidha, Kamati inaona kwamba, taarifa hizo zitasaidia sana kuboresha mifumo ya utoaji haki nchini hasa katika nyanja ya madai lakini pia kuboresha mfumo wa Sheria za Kimila. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba, Serikali ikamilishe haraka taarifa ya mapitio ya sheria zinazosimamia usuluhishi na utatuzi wa migogoro ya ardhi, kwani migogoro ya ardhi imekuwa mingi na mfumo wake wa utatuzi haukidhi haja hivyo ni vyema mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi ukarekebishwa. Aidha, Ibara ya 107 ya Katiba inasema: "Mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama na hivyo Kamati inashauri Sera ya Mabaraza ya Ardhi ya Vijijini kuwa chini ya Wizara ya Ardhi iangaliwe upya na ikiwezekana Mabaraza hayo yawe chini ya Mahakama."

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na

Utawala Bora - Fungu 55. Kamati inashauri na kupendekeza ifuatavyo:-

Kiasi cha shilingi shilingi 4,047,910,700 kilichotengewa Tume ni kidogo sana kikilinganishwa na majukumu makubwa iliyonayo kama yalivyoainishwa katika Ibara ya 130(1)(a) - (h) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa ikisomwa pamoja na Kifungu Na. 6(1)(a) - (0) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Na. 7 ya Mwaka 2001, ambayo pamoja na mambo mengine ni kuhamasisha uhifadhi wa haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi.

Matukio ya uvunjwaji haki na vitendo vya kujichukulia sheria mkononi vinaongezeka; hivyo, ni vyema Tume ikaongeza jitihada zake za kutoa elimu kwa Umma juu ya umuhimu wa kuheshimu Sheria.

Tume iongeze kasi ya uchunguzi wa matukio ya uvunjwaji wa haki na kutoa ripoti zake mapema ili kuwawezesha Wananchi kujua hali ya Haki za Binadamu nchini. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuipatia fedha za kutosha ili iweze kuchapa Ripoti za Haki za Binadamu za kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake ya kuisimamia na kuishauri Serikali, Kamati ilifanya ziara tarehe 5 Aprili, 2013 kwenye Jengo la Wakala wa Usajili wa Vizazi, Vifo na Ufilisi (*RITA TOWER),* lililopo Mtaa wa Makunganya, Jijini Dar es Salaam. Kamati imetambua kazi nzuri inayofanywa na Serikali kupitia Wakala kwani ujenzi umesimamiwa vizuri na uko katika hatua nzuri. Jengo hili litapunguza kero ya kupanga pamoja na uhaba wa ofisi. Aidha Jengo litauongezea Wakala kipato kwa kupangisha ofisi za ziada. Hata hivyo, Kamati inaomba Serikali kutoa fedha za ujenzi kwa Wakala haraka kwani Jengo hilo linajengwa kwa ubia kati ya *RITA* na *NSSF*. Hadi sasa fedha zote kati ya shilingi bilioni 35 zinazotakiwa kugharamia Mradi zimetolewa na *NSSF*, *RITA* walipaswa kutoa shilingi bilioni 17 sawa na asilimia 69 ya

gharama za mradi. Kamati inaitaka Serikali kuupatia Wakala fedha hizo mapema iwezekanavyo ili zilipwe, kukwepa riba kubwa itakayotekea endapo fedha zitachelewa kulipwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba, utekelezaji wa Mpango wa Kusajili Watoto Chini ya Umri wa Miaka Mitano unaojulikana kama *U5BRI - Under Five Birth Registration Initiative,* ukilenga kupunguza mlundikano wa vizazi ambavyo havijasajiliwa, usambazwe katika wilaya zote nchini ili kuhakikisha watoto wote chini ya miaka mitano ambao hawajasajiliwa wanasajiliwa. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuuwezesha kibajeti Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini ili uweze kutekeleza mpango wake ilioubuni wa *U5BRI Underfive Birth Registration Initiatives ili* kuongeza kiwango cha usajili na kutoa vyeti hasa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia, namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria - Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Naibu Waziri - Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki na Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Mheshimiwa Jaji Frederick Werema, kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Vilevile, nawashukuru Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria na Wakuu wa Taasisi pamoja na Maafisa Waandamizi wa Wizara na Taasisi zake, kwa ushirikiano waliotupatia.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu Sekta ya Sheria, Haki za Binadamu na Utawala Bora, umesaidia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Tulishaacha mchezo huo, sisi hatuna muda. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, samahani sana.

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Dkt. Pindi Hazara Chana | - | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. William Mganga Ngeleja | - | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu | - | Mjumbe |
| 4. Mhe. Nimrod Elirehema Mkono | - | Mjumbe |
| 5. Mhe. Halima James Mdee | - | Mjumbe |
| 6. Mhe. Fakharia Khamis Shomar | - | Mjumbe |
| 7. Mhe. Nyambari C. M. Nyangwine | - | Mjumbe |
| 8. Mhe. Jaku Hashim Ayoub | - | Mjumbe |
| 9. Mhe. Felix Francis Mkosamali | - | Mjumbe |
| 10. Mhe. Gosbert Begumisa Blandes | - | Mjumbe |
| 11. Mhe. Rukia Khasim Ahmed | - | Mjumbe |
| 12. Mhe. Mustapha Boay Akunaay | - | Mjumbe |
| 13. Mhe. Ramadhan Haji Saleh | - | Mjumbe |
| 14. Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu | - | Mjumbe |
| 15. Mhe. Deogratias Aloys Ntukamazina | - | Mjumbe |
| 16. Mhe. Jason Samson Rweikiza | - | Mjumbe |
| 17. Mhe. Ali Khamis Seif | - | Mjumbe |
| 18. Mhe. Abdallah Sharia Ameir | - | Mjumbe |
| 19. Mhe. Mariam R. Kasembe | - | Mjumbe |

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, namshukuru Ndugu Haika Mtui na Ndugu Matamus Fungo, Makatibu wa Kamati hii, kwa kuratibu kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante, hivyo hivyo hata Waziri wa Katiba na Sheria, kuwashukuru watu wake, kawashukuru ofisini siyo hapa kutumia muda wetu.

Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii na kama inawezekana muda ambao Kamati haijaumalizia nikopeshwe mimi.

**SPIKA:** Hakuna cha kukopa hapa. (*Kicheko*)

**MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, naomba kuwasilisha Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Wizara ya Katiba na Sheria, kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/14 na ninaomba nifanye hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za kudumu za Bunge lako Tukufu za mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika**,** Ofisi ya Waziri wa Katiba na Sheria, imeanzishwa kwa mujibu wa kipengele cha 12 cha Nyongeza ya Waraka wa Rais uliochapishwa kama Tangazo la Serikali Na. 494 la tarehe 17 Desemba, 2010. Majukumu ya Ofisi hii yameainishwa katika Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la Mwaka 2010 (*The Ministers [Assignment of Ministerial Functions] Notice*, 2010) lililochapishwa katika Gazeti la Serikali kama Tangazo la Serikali Na. 494A la tarehe 17 Desemba, 2010.

Kwa mujibu wa Nyongeza ya Pili ya Tangazo hilo, pamoja na mengine, Ofisi ya Waziri wa Katiba na Sheria imekasimiwa majukumu ya masuala ya kikatiba, uendeshaji na utoaji wa haki, uendeshaji mashtaka na Haki za Binadamu. Kwa sababu ya matukio ya hivi karibuni yanayohusu utendaji wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba katika mchakato wa

Katiba Mpya na kwa kuzingatia umuhimu wake katika mustakbali wa Taifa letu, tunaomba kuanza na masuala yanayoihusu Tume na uendeshaji wa mchakato huo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 33.944 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 ya Sheria za Tanzania. Kwa mujibu wa Maelezo ya Makadirio ya Matumizi Mengineyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 yaliyoletwa mbele ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala mwezi uliopita, hadi kufikia tarehe 25 Februari, 2013, Tume ilishapokea shilingi bilioni 18.473 kutoka Hazina na ilikwishatumia shilingi bilioni 14.968, sawa na asilimia 81 ya fedha zilizopokelewa.

Kwa mujibu wa maelezo hayo, shilingi bilioni 3.504 ambazo hazijatumika zimetengwa kwa ajili ya kulipia madeni kutokana na huduma za uchapishaji wa Mwongozo wa Mabaraza ya Katiba, uratibu wa mchakato wa kupatikana Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba na gharama nyingine za uendeshaji wa Ofisi.

Maelezo ya Tume yanaonesha kwamba, shillingi bilioni 15.471 ambazo hazijatolewa na Hazina zitatumika kwa ajili ya kusambaza nakala milioni moja za Rasimu ya Katiba Mpya (shilingi bilioni 3.848); elimu kwa umma juu ya Rasimu ya Katiba Mpya (shilingi milioni 400); kuratibu na kuendesha Mabaraza ya Katiba kwa nchi nzima (shilingi bilioni 4.734); na shilingi bilioni 6.488 kwa ajili ya matumizi mengine pamoja na stahili za Wajumbe na Sekretarieti.

Mheshimiwa Spika, katika Maoni yetu ya mwaka jana, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ililalamikia kile ilichokiita "... matumizi yasiyoelezeka na yasiyokubalika ya fedha za umma hasa hasa katika mazingira ambayo Wananchi wanahubiriwa na Watawala kwamba miradi ya maendeleo yao ya kiuchumi na kijamii haitekelezeki kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti ya Serikali." Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilidai kwamba, shilingi bilioni 14.633 zilizotengwa kwa ajili ya

kuwalipa Wajumbe na Watendaji wa Tume posho mbalimbali, zilikuwa zinatishia kuigeuza heshima ya kutumikia waliyopewa Wajumbe wa Tume kuwa hongo ya Serikali.

Madai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuitaka Serikali ilieleze Bunge hili Tukufu gharama zote za kila Mjumbe wa Tume, Sekretarieti na Watumishi wengine wote wa Tume ili Wabunge na Wananchi wa Tanzania wafahamu kodi wanazolipa zinavyotumika katika mchakato wa Katiba Mpya, yalikataliwa na Serikali kwa hoja kwamba taarifa hizo ni siri kati ya mwajiri na mwajiriwa.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu linaombwa kuidhinisha shilingi bilioni 33.944, kiasi kile kile kilichoidhinishwa mwaka jana, kwa ajili ya matumizi ya Tume kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/14. Kiasi hiki ni pamoja na shilingi bilioni 12.193 kwa ajili ya kulipia posho za vikao kwa Wajumbe wa Tume 34 na Sekretarieti 160; shilingi bilioni 1.728 ambazo zitalipia posho ya kujikimu kwa ajili ya Wajumbe na Sekretarieti wanaposafiri ndani ya nchi kikazi; na shilingi bilioni 1.650 kwa ajili ya kulipa gharama za nyumba za Wajumbe na Sekretarieti wanaotoka nje ya Dar es Salaam. Aidha, kuna shilingi milioni 18 zinazoombwa kwa ajili ya kugharamia chakula kwa Wajumbe wa Tume na Sekretarieti watakaokuwa wamepata maambukizi ya UKIMWI; shilingi milioni 60 kwa ajili ya usafiri wa ndani; shilingi milioni 50 kwa ajili ya gharama za malazi kwa Wajumbe wa Tume na Sekretarieti wanaposafiri kikazi; shilingi milioni 423 kwa ajili ya chai na vitafunwa; na shilingi milioni 50 kwa ajili ya wahudumu wanaosaidia kazi za Tume wakiwa mikoani wakati wa kushiriki kwenye Mabaraza ya Katiba na zoezi la upigaji kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Bunge lako Tukufu linaombwa kuidhinisha shilingi milioni 60 za kulipia maji kwa matumizi ya Ofisi za Tume; shilingi milioni 30 kwa ajili ya kulipia gharama za usafiri wa basi na taxi kwa Wajumbe na Sekretarieti watakaposafiri ndani ya nchi kikazi; na shilingi milioni 103 kwa ajili ya kulipia gharama za simu za mikononi.

Mheshimiwa Spika**,** Bunge lako Tukufu linaombwa

kuidhinisha posho na ulaji zaidi ya huu kwa ajili ya Wajumbe na Sekretarieti ya Tume. Ulaji huu mwingine unajumuisha shilingi milioni 604 kwa ajili ya posho kwa Wajumbe wa Tume na Sekretarieti wakati wa Bunge Maalum la Katiba.

Maelezo ya Tume yamejaribu kuhalalisha matumizi ya fedha hizi za ziada kwa kuzibatiza jina la *hardship allowances*, yaani posho ya mazingira magumu, wakati Vikao vya Bunge Maalum la Katiba vitafanyika Dar es Salaam au hapa Dodoma!

Vilevile, katika ulaji huu mpya zipo shilingi milioni 266 zinazoombwa kwa ajili ya chakula na viburudisho wakati wa Vikao vya Bunge Maalum la Katiba; shilingi milioni 12 nyingine kwa ajili ya huduma za chakula na viburudisho kwa shughuli zinazohusiana na Tume; na shilingi milioni 185 kwa ajili ya kulipia usafiri wa basi na taxi. Aidha, kuna shilingi milioni 30 za utengenezaji wa *T-shirts* na kofia kwa Wajumbe wa Tume na Sekretarieti wakati wa kushiriki kwenye zoezi la uhamasishaji kuelekea upigaji wa kura ya maoni; shilingi milioni 40 nyingine kwa ajili ya utengenezaji wa sare wakati wa maadhimisho mbalimbali ya Kitaifa; na shilingi milioni 12 kwa ajili ya posho za kujikimu kwa Watumishi wa Tume watakaohudhuria kwenye maadhimisho mbalimbali ya Kitaifa.

Zaidi ya hayo, kuna shilingi bilioni 1.307 zinazoombwa kwa ajili ya posho za kujikimu kwa ajili ya Wajumbe na Sekretarieti ya Tume wanaposafiri ndani ya nchi wakati wa kushiriki kwenye zoezi la upigaji wa kura ya maoni; na shilingi milioni 218 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya magari ya Tume wakati wa kushiriki zoezi la uhamasishaji kuelekea upigaji wa kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Bunge lako Tukufu linaombwa kuidhinisha jumla ya shilingi bilioni 19.039 kwa ajili ya posho za aina mbalimbali na malipo mengine yanayowahusu Wajumbe na Sekretarieti ya Tume kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/14. Hii ni zaidi ya asilimia 56 ya bajeti yote inayoombwa kwa ajili ya Tume. Kwa ulinganisho,

posho na malipo mengine yanayowahusu Wajumbe na Sekretarieti ya Tume yalikuwa shilingi bilioni 14.633 au asilimia 43 ya bajeti yote ya Mwaka wa Fedha uliopita. Hii ina maana kwamba, gharama za moja kwa moja za Wajumbe na Sekretarieti ya Tume zitaongezeka kwa zaidi ya shilingi bilioni 4.406 au zaidi ya asilimia 30 ya gharama za mwaka jana kama Bunge lako Tukufu litaidhinisha maombi haya!

Mheshimiwa Spika, maombi haya ya mabilioni ya fedha za Wananchi yanatoa uvundo na harufu mbaya ya ufisadi na hayaelezeki na wala kukubalika kwa misingi ya kisheria na kwa rekodi ya utendaji kazi wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Kwanza kabisa, kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Mabadailiko ya Katiba, Tume ina Wajumbe wasiozidi thelathini pamoja na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wake.

Kwa maana hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua uhalali wa maombi ya shilingi bilioni 12.193 kwa ajili ya posho za vikao kwa Wajumbe 34 wa Tume wanaotajwa katika kijifungu 210321 cha kasma 210300 kwenye randama ya Fungu 08 linalohusu Tume.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua Wajumbe hawa wanne wa ziada ni akina nani na wameteuliwa lini kuwa Wajumbe wa Tume? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kuelezwa, inakuwaje Tume iwe na Wajumbe 34 wakati Sheria iliyoiunda inataka Tume yenye Wajumbe wasiozidi thelathini?

Pili, kwa mujibu wa kazi za Tume kama zilivyoainishwa katika kifungu cha 9 cha Sheria; na kwa mujibu wa utaratibu wa utendaji kazi wa Tume kama ulivyofafanuliwa katika Sehemu ya Nne ya Sheria; na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 22(1) cha Sheria hiyo, Wajumbe na Sekretarieti ya Tume siyo Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba. Badala yake, uhusiano pekee wa kisheria uliopo kati ya Tume na Bunge Maalum ni ule uliotajwa katika Vifungu vya 20(3), 20(4)

na 25(2) vya Sheria vinavyomruhusu Mwenyekiti wa Tume kuwasilisha Rasimu ya Katiba Mpya kwenye Bunge Maalum na kuwaruhusu Mwenyekiti na Wajumbe kutoa ufafanuzi utakaohitajika wakati wa majadiliano katika Bunge Maalum.

Hii ina maana kwamba, mara baada ya kuwasilisha Rasimu ya Katiba Mpya, Mwenyekiti wa Tume anakuwa *functus officio*, yaani hana kazi nyingine yoyote ya kufanya kwenye Bunge Maalum. Aidha, Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume hawana kazi nyingine yoyote ya kufanya katika Bunge Maalum hadi hapo watakapohitajika na Bunge Maalum kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa jambo lolote linalohusu Rasimu ya Katiba Mpya.

Wakishatoa ufafanuzi utakaohitajika walioitiwa, nao pia wanakuwa *functus officio*. Kwa sababu hizo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua uhalali wa shilingi bilioni 1.055 ambazo Bunge lako Tukufu linaombwa kuziidhinisha kwa ajili ya posho, chakula na viburudisho na usafiri wa basi na taxi kwa Wajumbe wa Tume na Sekretarieti wakati wa Vikao vya Bunge Maalum la Katiba.

Tatu, kwa mujibu wa Kifungu cha 33(2) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, jukumu pekee la Tume katika hatua ya uhalalishaji wa Katiba Mpya ni kutoa elimu ya uraia na uhamasishaji juu ya Katiba inayopendekezwa kwa muda usiozidi siku thelathini kuanzia siku ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Kwa kazi ya mwezi mmoja tu, Wajumbe na Sekretarieti ya Tume wanaombewa shilingi bilioni 1.307 kwa ajili ya posho za kujikimu. Kwa mahesabu hayo, kila Mjumbe wa Tume, Katibu na Naibu Katibu pamoja na Wakuu wa Vitengo saba vya Tume na madereva wa kila mmoja wao, watalipwa wastani wa shilingi milioni 16.756 kwa mwezi huo mmoja au shilingi 558,547 kama posho ya kujikimu kwa kila siku moja.

Mheshimiwa Spika, katika nchi ambayo Wauguzi katika hospitali za umma wanalipwa mshahara wa kuanzia wa takriban shilingi 360,000 kwa mwezi na Walimu wa shule za msingi wanaanzia shilingi 250,000 na wale wa sekondari shilingi 325,000 kwa mwezi, malipo haya kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba yana uvundo na harufu mbaya ya rushwa kwa Wajumbe wa Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, kwa vile kifungu cha 14(2) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kinatamka kwamba Wajumbe wa Tume na Sekretarieti "watalipwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za nchi", Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM iliambie Bunge lako Tukufu ni Sheria na Kanuni zipi za nchi yetu ambazo zimetumika kuhalalisha malipo haya makubwa kwa Wajumbe na Sekretarieti na Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM itoe kauli rasmi mbele ya Bunge lako Tukufu kama kuna uhalali wowote wa kutumia fedha za wananchi wa Tanzania ili kununua 'chakula maalum' *(special foods)* kwa ajili ya Wajumbe na Sekretarieti ya Tume watakaopata UKIMWI kwa sababu ya kuendekeza ngono zembe na starehe zao binafsi wakati wanatakiwa wafanye kazi ya Tume. Vinginevyo, Bunge lako Tukufu lielezwe kwa ufasaha ni kwa namna gani mchakato huu wa Katiba Mpya unatazamiwa kusababisha maambukizi ya UKIMWI kwa Wajumbe na Sekretarieti ya Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Serikali kujificha nyuma ya pazia la 'siri ya mwajiri na mwajiriwa' hakutoshi tena, kwani ni kulizuia Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake kikatiba wa kuisimamia Serikali chini ya Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura ya 2 ya Sheria za Tanzania. Aidha, ni haki kwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kujua uhalali wa malipo haya kwani, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(a) ya Katiba, Bunge lako Tukufu "laweza kumuuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yako katika wajibu wake...."

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua shilingi milioni 218 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya magari ya Tume zitatumikaje ndani ya kipindi cha siku thelathini za uhamasishaji na kuelimisha wananchi kupiga kura ya maoni kwa Katiba Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ina maana kwamba hata kama kila Mjumbe wa Tume, Katibu, Naibu Katibu na wakuu wa vitengo saba vya Tume watapewa gari moja kwa kila mmoja wao kwa kipindi hicho, kila gari itatumia wastani wa shilingi 186,325 kwa siku kwa ajili ya mafuta tu! Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni safari zipi hizo za Tume ambazo zitalazimu matumizi ya *full tank* ya mafuta kila siku kwa mwezi mzima? Huu, kama Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alivyowahi kusema, ni 'wizi mtupu'! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amlipaye mpiga zumari ndiye achaguaye wimbo. Baada ya Tume kulipwa mabilioni yote tuliyoyapigia kelele kwenye Maoni yetu ya mwaka jana, kuna ushahidi kwamba Tume imekuwa inacheza wimbo uliochaguliwa na CCM na Serikali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi Februari ya mwaka huu, Tume ilichapisha Mwongozo Kuhusu Muundo, Utaratibu wa Kuwapata Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya (Mamlaka za Serikali za Mitaa) na Uendeshaji Wake. Mwongozo huo ulisainiwa na Mwenyekiti wa Tume Jaji Joseph Sinde Warioba na ulianza kutumika tarehe 1 Machi, 2013. Ingawa Tume imedai kwamba Mwongozo huo ulitolewa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba Mwongozoulitolewa kinyume na matakwa ya Sheria hiyo na kwa lengo la kuinufaisha CCM na washirika wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 17(8) cha Sheria kinailazimu Tume kubuni "... utaratibu unaofanana ambao utatumika katika kila upande wa Jamhuri ya Muungano katika ukusanyaji na uchambuzi wa maoni ya wananchi, uendeshaji wa Mabaraza na uandaaji wa ripoti." Katika utekelezaji wa majukumu yake, Tume inatakiwa kufuata

msingi huu mkuu "isipokuwa kama mazingira yatahitaji vinginevyo....". Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba, kwa kiasi kikubwa, Tume iliweka utaratibu unaofanana ambao ulitumika katika hatua ya ukusanyaji wa maoni ya wananchi katika kila upande wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Tume haikuweka utaratibu wowote wa maana wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya masuala yote yanayohusu Katiba Mpya ili kuwaandaa wananchi kuchangia maoni yao kwa Tume wakiwa na uelewa wa kutosha. Badala yake, wakati wa mikutano ya Tume ya kupokea maoni ya wananchi, wajumbe wa Tume walipewa jukumu la kuwaeleza wananchi juu ya Katiba Mpya kwa muda usiozidi nusu saa. Hii ilifanyika katika mikutano yote ya Tume katika kila upande wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, pili, muda uliowekwa na Tume wa kukusanya maoni ya wananchi ulikuwa mdogo sana ukilinganisha na ukubwa wa nchi yetu na wingi wa Watanzania. Katika Majimbo karibu yote ya uchaguzi, Tume iliendesha wastani wa mikutano saba kwa kila Jimbo kwa lengo la kukusanya maoni ya wananchi lakini huu ni wastani tu, katika Majimbo mengi, Tume ilifanya mikutano minne au mitano tu. Hili pia lilifanyika katika kila upande wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, tatu, katika mikutano yote ya ukusanyaji maoni, wananchi walitakiwa kutoa maoni yao kuhusu Katiba Mpya kwa muda wa dakika tano kila mmoja na mikutano yenyewe ilichukua muda wa masaa matatu ikiwa ni pamoja na muda wa kutambulishana wajumbe wa Tume na mambo mengine yaliyo nje ya kuchukua maoni ya wananchi. Hii ilifanyika hata kwa Wabunge wakati Tume ilipokuja kuchukua maoni ya Wabunge hapa Dodoma. Utaratibu huu ulitumika katika kila upande wa Jamhuri ya Muungano.

Aidha, utaratibu unaofanana katika kila upande wa Jamhuri ya Muungano ulitumika pia kukusanya maoni ya

makundi maalum kama vile vyama vya siasa, taasisi zisizokuwa za kiserikali, mashirika ya kidini na hata taasisi za kiserikali na viongozi wake, wa sasa na waliostaafu.

Mheshimiwa Spika, wakati Tume iliweka utaratibu unaofanana katika kila upande wa Jamhuri ya Muungano wakati wa zoezi la kukusanya maoni ya wananchi, Tume hiyohiyo iliweka utaratibu tofauti na wa kibaguzi katika hatua ya kuunda Mabaraza ya Katiba ya Wilaya.

Kwanza, Tume iliweka ngazi mbili za uchaguzi wa wajumbe wa Mabaraza kwa upande wa Tanzania Bara wakati kwa upande wa Zanzibar Tume iliweka ngazi moja tu ya uchaguzi. Hivyo, kwa mfano, aya ya 6.1.4 ya Mwongozo wa Tume imeweka Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji au Mtaa "ambao utakuwa na agenda moja tu ya kuwapendekeza kwa kuwapigia kura watu wanne ambao majina yao yatawasilishwa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata." Hii ni ngazi ya kwanza ya uchaguzi wa wajumbe wa Mabaraza kwa upande wa Tanzania Bara na kazi yake ni kupendekeza tu.

Baada ya hapo, majina ya watu walioshinda katika uchaguzi wa ngazi ya Kijiji au Mtaa yatawasilishwa kwa Afisa Mtendaji wa Kata "ambaye ataitisha Kikao Maalum cha Kamati ya Maendeleo ya Kata, ambacho ... kitachagua majina manne ..." ya wajumbe wa Baraza la Katiba la Wilaya. (aya ya 6.1.8, 6.1.9 na 6.1.10). Hii ni ngazi ya pili na ndiyo inayoamua nani awe mjumbe wa Baraza la Katiba la Wilaya kwa upande wa Tanzania Bara na nani asiwe.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zanzibar, ngazi ya uchaguzi ni moja tu, Mkutano wa Shehia ambao, kwa mujibu wa aya 6.3.4 ya Mwongozo wa Tume, "... utakuwa na agenda moja tu ya kuwapigia kura ya siri watu watatu ... ambao majina yao yatawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa au Katibu wa Halmashauri ya Mji au Wilaya ambapo Shehia hiyo ipo." Kwa utaratibu huu, wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya kwa upande wa Tanzania Bara wamechaguliwa na watu wanne au watano tu ambao

ni wajumbe wa *WDC* wakati wajumbe wa Mabaraza ya hayo kwa upande wa Zanzibar wamechaguliwa na watu wote walioshiriki katika Mkutano wa Shehia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya kwa upande wa Zanzibar wana uhalali wa kisiasa kwa sababu wanawakilisha matakwa ya wananchi waliowachagua moja kwa moja bila mchujo, wakati wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya kwa upande wa Tanzania Bara hawana uhalali wowote wa kisiasa kwa sababu wanawakilisha maslahi ya CCM ambayo ndiyo inayotawala asilimia zaidi ya themanini ya *WDC* zote ambazo ndio zilizowachuja wajumbe hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili linalothibitisha kwamba utaratibu wa Tume ni wa kibaguzi ni katika uendeshaji wa mikutano ya uchaguzi wa wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya. Kwa mujibu wa aya ya 6.1.4 ya Mwongozo wa Tume, kwa upande wa Tanzania Bara Mkutano Maalum wa Kijiji au Mtaa "... utaendeshwa na Mwenyekiti wa Kijiji au Mtaa, ambapo Afisa Mtendaji wa Kijiji au Mtaa atakuwa Katibu wa Mkutano na ndiye atakayewasilisha majina ya wananchi walioomba kuingia kwenye Baraza la Katiba la Wilaya."

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa upande wa Zanzibar kwa mujibu wa aya ya 6.3.5 ya Mwongozo wa Tume, "Mkutano wa Shehia utachagua Mwenyekiti na Katibu wa Mkutano huo kutoka miongoni mwa wananchi waliohudhuria Mkutano. Katibu ndiye atakayewasilisha kwenye Mkutano majina ya wananchi wote walioomba kuwa wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya...." Karibu Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa wote wa Tanzania Bara ni wanachama na makada wa CCM, ilhali zaidi ya 90% ya Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa wote ni wanachama na makada wa chama hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, mikutano ya uchaguzi wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya kwa upande wa Tanzania Bara imeendeshwa na makada wa CCM wakati

kwa upande wa Zanzibar mikutano imeendeshwa na viongozi waliochaguliwa na wananchi walioshiriki katika mikutano hiyo bila kujali itikadi au uanachama wao katika vyama vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana, karibu nchi nzima ukiacha Zanzibar, kwa mujibu wa taarifa ilizo nazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, wananchi wengi wasiokuwa wanachama wa CCM ambao walipata kura nyingi katika kura za mikutano ya uchaguzi ya Vijiji na Mitaa walienguliwa kwenye michujo iliyofanyika katika Kamati za Maendeleo za Kata zilizowekwa kwa mujibu wa Mwongozo wa Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata mahali ambapo wananchi wasiokuwa wana CCM walifanikiwa kupenyeza katika chekecheke la mchujo wa *WDC*, wamefanyiwa mizengwe na wana CCM ili waondolewe katika orodha ya wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni yaliyomkuta Bwana Beatus Kipeya aliyechaguliwa mjumbe wa Baraza la Katiba la Wilaya ya Arusha Mjini kwa kupitia Kata ya Sombetini. Mara baada ya Bwana Kipeya kuchaguliwa kwenye kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Sombetini cha tarehe 8 Aprili, 2013, siku hiyo hiyo Katibu wa CCM Wilaya ya Arusha Allan G. Kingazi alimwandikia Mkuu wa Wilaya ya Arusha barua ya malalamiko juu ya kuchaguliwa kwa Bwana Kipeya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumpa Mkuu wa Wilaya 'salaam za Chama' chao, Katibu wa CCM Kingazi alilalamika kwamba Afisa Mtendaji wa Kata ya Sombetini amemruhusu "... raia wa Burundi Bwana Beatus Ndanyahubwi Kipea (ambaye katika kugombea ametumia jina la Beatusi Kipea ili asijulikane kama ni Mrundi – ila mtu wa Kigoma yaani Muha) kugombea nafasi ya Ujumbe wa Baraza la Katiba la Wilaya na akashinda, kinyume na maagizo ya Tume ya Katiba, kwamba Mjumbe ni lazima awe Raia wa Tanzania." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo mengi kuhusu 'Urundi' wa Bwana Kipeya, Katibu wa CCM Kingazi anamwambia Mkuu wa Wilaya yafuatayo: "... (N)ashauri matokeo ya Uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Katiba ufutwe na utangazwe upya. Aidha, Afisa Mtendaji huyo achukuliwe hatua za kinidhamu kwa kuvuruga kwa makusudi uchaguzi wa Muundo wa Baraza la Katiba la Wilaya." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu cha kwanza cha kushangaza kuhusu barua ya Katibu wa CCM Kingazi ni kwamba aliyetumiwa malalamiko ni Mkuu wa Wilaya ambaye, kwa mujibu wa Ibara ya 42(3), 44(3) na 46(3) ya Katiba ya CCM Toleo la 1982, Mkuu wa Wilaya ni mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Wilaya, Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya na Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya. Kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na Mwongozo wa Tume, Mkuu wa Wilaya hana mamlaka yoyote kushughulikia jambo lolote linalohusu uchaguzi wa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya. Kwa maana hiyo, sababu pekee ya Mkuu wa Wilaya ya Arusha kuandikiwa malalamiko haya ni kwa sababu ni kada wa CCM! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiacha Afisa Uhamiaji wa Mkoa wa Arusha, watu wengine wote walionakiliwa barua ya malalamiko ya Katibu wa CCM Kingazi ni makada wa CCM. Hivyo basi, nakala za malalamiko hayo zinaonyeshwa kupelekwa kwa Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Katibu wa CCM Mkoa, Mkuu wa Mkoa (ambaye pia ni mjumbe wa vikao vyote vya kikatiba vya CCM katika ngazi ya Mkoa), Afisa usalama wa Taifa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji la Arusha. Wote hawa hawahusiki kisheria kwa namna yoyote ile katika mchakato wa uundaji wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya. Chombo pekee ambacho kinahusika kisheria na mchakato wa kuunda Mabaraza hayo na ambacho kilitoa Mwongozo wa namna ya kuyaunda, yaani Tume, hakikuandikiwa wala kunakiliwa barua ya malalamiko ya Katibu wa CCM Kingazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara tu baada ya Afisa Uhamiaji Mkoa wa Arusha Bwana R. Gowelle kupata nakala yake,

alimwandikia Bwana Kipeya barua ya 'wito wa kufika ofisi ya uhamiaji Mkoa wa Arusha', ambapo alimtaka kufika ofisini kwake 'bila kukosa wala kutuma mwakilishi.' Cha kushangaza ni barua hiyo imenakiliwa kwa Afisa Mtendaji Kata ya Sombetini, Mwenyekiti wa Mtaa wa Kirika A, Sombetini na Balozi wa Mtaa wa Zurich, Sombetini.

Mbali na Afisa Mtendaji Kata ambaye alikuwa mlalamikiwa, wengine wote walionakiliwa barua ya Afisa Uhamiaji Mkoa ni makada wa CCM na kwa taarifa za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ndio walikuwa chanzo cha malalamiko ya Katibu wa CCM Kingazi. Kwa taarifa za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Bwana Kipeya ni raia halali wa Tanzania anayetoka katika Jimbo la Muhambwe katika Wilaya ya Kasulu ya Mkoa wa Kigoma. Dhambi pekee na kubwa aliyoifanya na kustahili kusumbuliwa na Idara ya Uhamiaji ni kugombea na kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Katiba la Wilaya ya Arusha wakati yeye sio mwanachama wa CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina ushahidi unaoonyesha kwamba njama za kuhakikisha kwamba wanaCCM pekee ndio watakaochaguliwa kuwa wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya kwa upande wa Tanzania Bara zilipangwa katika ngazi za juu kabisa za CCM. Mnamo tarehe 3 Machi, 2013, siku mbili tu baada ya Mwongozo wa Tume kuanza kutumika, Katibu wa *NEC* ya CCM, Uhusiano wa Kimataifa Dkt. Asha-Rose Migiro alituma barua pepe kwa wajumbe na watendaji wa Sekretarieti ya *NEC* ya CCM yenye kichwa cha habari: 'MUHIMU!! MABARAZA YA KATIBA YA WILAYA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barua pepe ya Dkt. Asha-Rose Migiro inasema: "Naandika kuhimiza kazi ya kuwatia hamasa Makatibu wa Mikoa wasimamie kikamilifu mchakato wa kuundwa kwa Mabaraza ya Wilaya ya Katiba. Kama mnavyofahamu Tume ya Katiba imeshatoa taarifa rasmi kwenye vyombo vya habari ... kuhusu zoezi hili muhimu. Sambamba na hatua za awali tulizochukua baada ya kupata rasimu ya mwanzo ya Mwongozo wa Tume, hivi sasa

tunatakiwa tuongeze juhudi za ushiriki wetu na kutayarisha makundi husika kama tulivyokwishaongea." *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walipiga Makofi kwa muda mrefu)*

**SPIKA:** Inatosha.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kuagiza 'mawasiliano kati ya SUKI na Makatibu wa Mikoa' kuhusu mambo ya kufanya, Dkt. Asha-Rose Migiro alimalizia barua yake kwa maneno yafuatayo: "Tafadhali wanakaliwa msisite kutoa maoni, ushauri na mbinu bora zaidi za kutimiza azma yetu katika suala hili muhimu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanakiliwa wa barua pepe ya Dkt. Asha-Rose Migiro ni pamoja na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Zakhia Meghji, Mheshimiwa Muhamed Seif Khatib na Bwana Nape Nnauye, Katibu Mwenezi wa *NEC* ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku moja baadaye, Bwana Nape Nnauye aliwaandikia 'wanakiliwa' wenzake kama ifuatavyo: "nashauri ikiwezekana kwa sababu ya unyeti wa swala hili tupate taarifa kila siku/au walau siku tatu ya hali halisi inavyoendelea katika kila Mkoa, ni vizuri idara ikaandaa checklist ya mambo muhimu ya kupima kama mchakato unakwenda vizuri au la! Mfano ... idadi ya walioandaliwa kugombea katika kila eneo, idadi ya waliohamasishwa kuhudhuria na kupiga kura, n.k." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, njama za CCM kuteka nyara mchakato wa Katiba Mpya zinahusu pia mchakato wa uhalalishaji wa Katiba Mpya kwenye kura ya maoni. Mnamo tarehe 18 Desemba mwaka jana, Katibu wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Francis K. Mwonga, aliwaandikia barua Makatibu wote wa CCM wa Mikoa kuwapa 'Maelekezo ya Kikao cha Sekretarieti ya Halmashauri

Kuu ya Taifa na Makatibu wa CCM wa Mikoa Kilichofanyika Dar es Salaam Tarehe 10/12/2012.' *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Maelekezo hayo inasema: "Wakati wa kupiga kura ya maoni kuhusu Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mawasiliano yafanywe na wahusika ili vituo vya kupigia kura visiwe mbali sana na wananchi." Maneno haya yameandikwa hata kabla Tume haijamaliza zoezi la kukusanya maoni ya wananchi na tayari Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM inawaelekeza makada wake mikoani kufanya mawasiliano na 'wahusika' juu ya namna ya kupanga vituo vya kupigia kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 56(a) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 ya Sheria za Tanzania, mamlaka inayohusika kupanga vituo vya kupigia kura ni Msimamizi wa Uchaguzi, yaani Mkurugenzi wa Jiji, Mkurugenzi wa Manispaa, Mkurugenzi wa Mji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya. Wasimamizi hawa wa uchaguzi wamelalamikiwa kwa miaka mingi na vyama vya upinzani kwa kupendelea CCM na wagombea wake katika chaguzi mbalimbali. Hawa ndio wanaotakiwa wawasiliane na Makatibu wa CCM Mikoa ili wapange vituo vya kupigia kura ya maoni juu ya Katiba Mpya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mawasiliano haya ya viongozi wa ngazi za juu za CCM yanathibitisha kwamba mchakato wa Katiba Mpya umeiingiliwa na kuhujumiwa kwa kiasi kikubwa na CCM. Aidha, mawasiliano haya yanathibitisha kauli iliyotolewa mbele ya Bunge lako Tukufu na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wakati wa mjadala wa hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba "...viongozi wa kiserikali kama vile Wakuu wa Wilaya na wa Mikoa waliwahamasisha Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Madiwani kuhakikisha kwamba wagombea wote wasiokuwa wa CCM, hasa wa CHADEMA, wanaenguliwa katika chaguzi za Vijiji, Mitaa au Kata." Aidha, mawasiliano haya yanathibitisha kauli ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba Mabaraza ya Katiba ya Wilaya yaliyochaguliwa kwa utaratibu "...ni Mabaraza ya CCM na sio Mabaraza ya Katiba ya Watanzania wote." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yote ambayo tumeyasema hapa yanathibitishwa pia na Tume yenyewe. Tarehe 29 Aprili, 2013, Mwenyekiti wa Tume Jaji Warioba alikiri kwenye mkutano wa waandishi habari kwamba "... sehemu kubwa ya matatizo yaliyojitokeza yalisababishwa na misukumo na misimamo ya kisiasa na kidini." Mwenyekiti Warioba amekiri kwamba kuna wajumbe wamejazwa katika Mabaraza ya Katiba ya Wilaya:

"Hao waliojazana kwenye Mabaraza wanadhani wanakuja kupiga kura, hapana.... Tume inazingatia uzito wa hoja zilizotolewa na wananchi na si idadi ya watu waliotoa maoni." Kwingineko, Mwenyekiti Warioba amekaririwa na vyombo vya habari akikiri kwamba kulikuwa na rushwa katika mchakato wa uchaguzi wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya. Hata hivyo, licha ya kukiri kuwepo kwa matatizo makubwa kama haya katika mchakato wa kuunda Mabaraza hayo, Mwenyekiti Warioba na Tume yake wamekataa madai ya kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi wa Mabaraza kwa hoja kwamba kufanya hivyo kutachelewesha kupatikana kwa Katiba Mpya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kauli ya Mwenyekiti wa Tume ni ya kinafiki na ya kujikosha kutokana na makosa ya Tume yenyewe. Hii ni kwa sababu Tume yake ilitahadharishwa mapema juu ya uwezekano mkubwa wa matatizo hayo kujitokeza. Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kiliitahadharisha Tume mapema mwezi Februari ya mwaka huu kwamba rasimu ya Mwongozo wa Tume itazaa Mabaraza ya kiCCM na italeta manung'uniko mengi ya wadau ambao wataenguliwa kwenye ngazi ya *WDC* ambazo zinatawaliwa na CCM kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, CHADEMA iliishauri Tume iachane na mapendekezo ya kuziweka *WDC* kuwa ni kikao cha uchaguzi wa wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya na badala yake wajumbe wa Mabaraza wachaguliwe moja kwa moja na wananchi kama ilivyopendekezwa kwa upande wa Zanzibar. Jaji Warioba na Tume yake walikataa kata kata mapendekezo haya ya CHADEMA. Kama alivyosema Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni: "... (L)icha ya Tume ya

Mabadiliko ya Katiba kupatiwa maoni ya wadau kwamba utaratibu huo utaharibu mchakato wa Katiba Mpya, Tume ilikataa kata kata kuubadilisha Muundo wa Mabaraza haya. Ni wazi kwamba Tume inafahamu inachokifanya. Ni wazi vilevile kwamba Tume inafahamu matokeo ya hicho inachokifanya, yaani kuundwa kwa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ambayo ni ya wanaCCM."

Mheshimiwa Spika, Jaji Warioba na Tume yake hawawezi wakasikika sasa hivi wakisema kwamba vyama vya kisiasa na taasisi za kidini ndio zenye makosa kwa kuvurugika kwa mchakato wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya! Aidha, Tume iliyotengeneza Mwongozo uliosababisha wanachama wa CCM 'kujazana' katika Mabaraza ya Katiba ya Wilaya haiwezi sasa ikalalama na kudai kwamba haitaangalia idadi ya waliotoa maoni bali itaangalia uzito wa hoja! Katika hili Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania kama kuna uhalali wowote kutumia shilingi bilioni 4.734 kwa ajili ya kuratibu na kuendesha Mabaraza ambayo Tume imesema maoni ya wengi katika Mabaraza hayo hayatafuatwa.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo, kukataa kwa Tume kufuta matokeo ya uchaguzi wa Mabaraza ambayo Tume yenyewe inakiri umevurugwa, ni uthibitisho tosha kwamba ndivyo Tume ilivyodhamiria tangu mwanzoni. Mabaraza haya ya kiCCM ni matunda ya moja kwa moja ya Tume kukiuka utaratibu uliowekwa na kifungu cha 18(3) cha Sheria ulioilazimu Tume kuunda Mabaraza ambayo "... yatashirikisha na kuwakutanisha wawakilishi toka makundi mbalimbali ya wananchi katika jamii."

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli mbele ya Bunge lako Tukufu kama CCM au viongozi na makada wake wamefanya mawasiliano yoyote na vyombo vitakavyosimamia kura ya maoni juu ya Katiba Mpya kama zinavyoashiria nyaraka za CCM ambazo tumezielezea hapa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM itoe kauli juu ya uhalali wa mawasiliano haya wakati mchakato wa kutengeneza Katiba

Mpya haujakamilika na wala Sheria husika za Uchaguzi hazijafanyiwa marekebisho ili kuruhusu kura ya maoni kufanyika kihalali, hasa kwa upande wa Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 10 cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kinafafanua kwamba "Tume itakuwa na mamlaka na uhuru kwa kadri itakavyokuwa muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu na mamlaka yake chini ya Sheria hii na haitaingiliwa na mtu au mamlaka yoyote." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyaraka za CCM ambazo tumezielezea hapa zinaonyesha dhahiri kwamba CCM imeingilia uhuru na mamlaka ya Tume. Kwa uchache kabisa, nyaraka hizi zinaonyesha viongozi wa ngazi za juu kabisa wa Sekretarieti ya *NEC* ya CCM wamefanya makosa ya kula njama kutwaa mamlaka ya Tume kwa kuwatumia Makatibu wa Mikoa wa CCM 'kusimamia kikamilifu mchakato wa kuundwa kwa Mabaraza ya Wilaya ya Katiba.' Kwa mujibu wa kifungu cha 21(2)(b) cha Sheria, "mtu yeyote ... atakayejifanya kuwa mjumbe wa Tume au Sekretarieti ... atakuwa ametenda kosa."

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 21(3) kinaelekeza adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kwa muda usiopungua mwaka mmoja na usiozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili, kwa mtu yeyote atakayepatikana na hatia na kosa hilo.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM itoe kauli mbele ya Bunge hili Tukufu kama iko tayari sasa kuwachukulia hatua tajwa za kisheria Dkt. Asha-Rose Migiro, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Muhamed Seif Khatib, Bwana Nape Nnauye na wengine wote waliotajwa katika nyaraka za CCM kwa uhalifu walioufanya dhidi ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, baada ya ushahidi wote huu, hakuwezi kuwa na ubishi kwamba utaratibu mzima wa kuundwa kwa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ni haramu. Hakuwezi kuwa na ubishi tena kwamba uharamu huu una lengo moja tu: kuhakikisha kwamba Katiba Mpya itakayopatikana kwa mchakato huu haramu "... itakuwa ni Katiba Mpya kwa jina tu, mambo mengine ya msingi yatabaki vilevile (yalivyo katika Katiba ya sasa). Kwa maneno mengine, itakuwa ni Katiba ile ile, ya watu wale wale, wa chama kile kile.

"Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni: "Katika mwaka wa kwanza wa mchakato wa upatikanaji Katiba Mpya, Tume ya Mabadiliko ya Katiba imethibitisha hofu tuliyokuwa nayo toka mwanzo kwamba lengo la mchakato wa Katiba Mpya uliowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ni kuhakikisha kwamba mabadiliko pekee yakayokuwepo ni yale yenye kulinda matakwa ya CCM na Serikali yake au yale pekee yatakayokuwa na baraka za "*status quo*."

Mheshimiwa Spika, katika Maoni ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tulitangaza kwamba CHADEMA itajitoa ushiriki wake katika mchakato wa Katiba Mpya endapo mambo yafuatayo hayatapatiwa ufumbuzi hadi kufikia mwisho wa mwezi huu, yaani tarehe 30 Aprili, 2013:-

(i) Kufutwa kwa uchaguzi wa Wajumbe wa Mabaraza ya Wilaya ya Katiba uliofanywa na Kamati za Maendeleo za Kata na badala yake wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya wachaguliwe moja kwa moja na wananchi wa Kata husika bila kuchujwa na *WDC*;

(ii) Serikali ilete mbele ya Bunge hili Tukufu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba yatayofanyia maeneo yafuatayo marekebisho:

(a) Vifungu vyote vinavyohusu uwakilishi katika Bunge Maalum la Katiba wa taasisi zilizoainishwa katika Sheria

ya Mabadiliko ya Katiba ili kuweka wazi namna wawakilishi wa taasisi hizo watakavyopatikana kutoka kila taasisi na idadi yao kwa kila taasisi;

(b) Vifungu vyote vinavyohusu ushirikishi wa wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba kutoka Zanzibar katika mijadala inayohusu mambo yasiyokuwa ya Muungano ya Tanzania Bara ili kuhakikisha kwamba wajumbe wa Zanzibar ambao hawatakuwa pungufu ya theluthi moja ya wajumbe wote watashiriki katika mijadala inayohusu mambo ya Muungano tu na sio mambo ya Tanzania Bara yasiyokuwa ya Muungano;

(c) Vifungu vyote vinavyohusu mamlaka ya Rais kuitisha tena Bunge Maalum la Katiba baada ya Bunge hilo kuwa limeshapitisha Rasimu ya Katiba Mpya kwa lengo la kufanya marekebisho katika Rasimu kabla haijapelekwa kwenye kura ya maoni ili kumwondolea Rais uwezo wa kubadilisha maamuzi yaliyopitishwa na Bunge Maalum;

(d) Vifungu vyote vinavyohusu mamlaka ya Kikatiba na ya kisheria yatakayoiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuendesha na kusimamia kura ya maoni ili kurekebisha hali ya sasa ambayo Katiba na Sheria za Uchaguzi za nchi yetu hazitambui uwepo wa kura za maoni na utaratibu wa namna ya kuiratibu, kuisimamia na kuiendesha;

Mheshimiwa Spika, madai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni hayajatimizwa hadi tunatoa Maoni haya. Mwenyekiti wa Tume Jaji Warioba amesema waziwazi kwamba uchaguzi wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya, ambayo Tume inakiri ulivurugwa na mivutano ya kisiasa na kidini, hautarudiwa na Mabaraza hayo yataendelea. Aidha, Mwenyekiti wa Tume amewaasa wale wanaolalamikia uchaguzi wa Mabaraza hayo wapeleke malalamiko yao kwenye Tume ili yashughulikiwe. Ushauri huu wa Tume hauna maana yoyote kwa sababu Mwongozo uliotolewa na Tume yenyewe haujaweka utaratibu wowote wa kufungua na kushughulikia malalamiko yoyote yanayotokana na uchaguzi wa Mabaraza hayo!

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali, Waziri Mkuu aliahidi – wakati wa kuhitimisha hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu – kwamba Serikali italeta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kabla ya mwisho wa Mkutano huu wa Bajeti. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imetafakari sana ahadi hii ya Waziri Mkuu. Pamoja na kwamba ni ahadi ya maneno tu, kama ilivyokuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwamba marekebisho yote yanayohitajika katika Sheria hiyo yatakamilika hadi kufikia Novemba 2012, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeona ni vema iipe muda Serikali wa kuleta marekebisho tajwa ndani ya Mkutano huu wa Bunge la Bajeti. Kipindi hiki pia kitaenda sambamba na Tume kutoa Rasimu ya Kwanza ya Katiba Mpya kwa ajili ya kuanza kujadiliwa na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, endapo hadi kufikia mwisho wa kipindi hicho Serikali itakuwa haijaleta Muswada wa marekebisho yanayotakiwa; au endapo Muswada utakaoletwa hautakidhi matakwa ya kuboresha mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya, basi CHADEMA itawaalika wanachama, wafuasi na mashabiki wake Tanzania nzima, pamoja na taasisi za kiraia na za kidini, vyama vya siasa na Watanzania wote wenye nia njema na Taifa hili kuhamasisha Watanzania kuikataa Rasimu ya Katiba Mpya kwenye kura ya maoni itakayofanyika kwa ajili ya kuihalalisha Katiba hiyo.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Kenya imepata Katiba Mpya mwezi Agosti 2010 baada ya mchakato uliochukua zaidi ya miaka kumi na moja. Kwa mujibu wa Dkt. Patrice L.O. Lumumba *(Kenya's Quest for a Constitution: The Postponed Promised, The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi, 2008)* aliyekuwa Katibu wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya Kenya, kwanza Serikali ya KANU chini ya Rais Daniel Arap Moi na baadaye Serikali ya *NARC* chini ya Rais Mwai Kibaki, zilijaribu kuteka nyara mchakato wa Katiba Mpya ya Kenya kwa kuandaa Rasimu ya Katiba Mpya ambayo ilipopelekwa kwenye kura ya maoni mwaka 2005 ilikataliwa na wananchi wa Kenya.

Mheshimiwa Spika, kama inavyojulikana, baadaye Kenya ilifanya Uchaguzi Mkuu wa Desemba 2007 kwa mujibu wa Katiba ya zamani ya Kenya ya mwaka 1969. Matokeo ya uchaguzi huo chini ya Katiba ya zamani yaliingiza Kenya katika machafuko makubwa ya kisiasa yaliyosababisha mauaji ya maelfu ya Wakenya. Kwa sababu ya machafuko hayo, Kenya imeingia katika vitabu vya historia kuwa nchi ya pili katika Bara la Afrika, baada ya Hassan al-Bashir wa Sudan, yenye Rais na Naibu Rais walioko madaraka lakini wanakabiliwa na mashtaka ya uhalifu dhidi ya ubinadamu *(crimes against humanity)* katika Mahakama ya Kimataifa ya Jinai.

Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Zimbabwe nayo imepata Katiba Mpya mwezi Februari ya mwaka huu baada ya mchakato uliochukua zaidi ya miaka kumi na sita. Mwaka 2000, Chama Tawala cha *ZANU PF* cha Rais Robert Mugabe kiliwapelekea wananchi wa Zimbabwe Rasimu ya Katiba Mpya iliyotokana na mchakato uliotawaliwa na chama hicho kuanzia mwanzo hadi mwisho. Katika kura ya maoni iliyofanyika mwaka huo, Rasimu hiyo ya Katiba Mpya ilikataliwa kwa kura nyingi na wananchi wa Zimbabwe. Matokeo yake, Zimbabwe iliingia katika giza kuu la machafuko ya kisiasa na kijamii yaliyopelekea ukiukwaji wa kutisha wa haki za binadamu na hatimaye Zimbabwe kutengwa kimataifa kwa kufukuzwa katika Jumuiya ya Madola na kuwekewa vikwazo vya kiuchumi na kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, baadaye, *ZANU PF* iliyofikiria kwamba inaweza kutawala kwa mabavu ya kijeshi, ilipoteza wingi wake Bungeni na hatimaye ililazimika kufanya maridhiano na vyama vya upinzani na makundi mengine ya kijamii yaliyopelekea kusainiwa kwa Makubaliano Makuu ya Kisiasa *(Global Political Agreement).* Chini ya Makubaliano hayo, Bunge la Zimbabwe liliunda Kamati ya Katiba ya Bunge iliyokuwa na wajumbe sawa kwa kila kimoja cha vyama vikuu vya kisiasa vya nchi hiyo. Kamati hiyo ya Bunge, iliyokuwa na Wenyeviti Wenza Watatu, Makamu Wenyeviti Wenza Watatu na wajumbe tisa kwa kila chama, ndiyo iliyoandaa Rasimu ya Katiba Mpya ya Jamhuri ya Zimbabwe

iliyopigiwa kura ya maoni na kupitishwa na wananchi wa Zimbabwe mwezi Februari ya mwaka huu. Baadhi ya Wabunge wa Bunge lako Tukufu walishiriki katika kura ya maoni hiyo kama sehemu ya ujumbe wa waangalizi wa Chama cha Mabunge ya *SADC*.

Mheshimiwa Spika, mifano ya Kenya na Zimbabwe inatosha kuwaonyesha kwamba wanajidanganya wale wote wanaodhani kwamba kuwa chama tawala chenye Wabunge wengi na mabavu ya kijeshi inatosha kubaki madarakani hata kwa hila na uchakachuaji. Saa ya mabadiliko inapogonga, hakuna mabavu ya kijeshi wala Usalama wa Taifa wala mapesa mengi wala ukatili wa aina yoyote unaoweza kuzuia wimbi la mabadiliko hayo! Bunge lako Tukufu litafanya vema kujifunza kutokana na historia ya wenzetu.

Mheshimiwa Spika, hifadhi ya Haki za Binadamu. Katiba ya nchi yetu inatambua na kuhifadhi haki za binadamu na wajibu muhimu. Sehemu ya Tatu ya Katiba yetu imefafanua haki hizo kwa kirefu. Kama sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa, Tanzania vilevile imeridhia mikataba mbalimbali ya haki za binadamu kama vile Tangazo la Ulimwengu la Haki za Binadamu *(Universal Declaration of Human Rights – UDHR), 1948;* Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa *(International Covenant on Civil and Political Rights – ICCPR),* 1966 na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni *(International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights – ICESCR), 1966.* Aidha, Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na za Wananchi *(African Charter on Human and Peoples Rights – ACHPR), 1981.*

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwepo kwa msingi huu wa kikatiba na kisheria, hali ya haki za binadamu imezidi kuzorota kwa kiasi kikubwa katika nchi yetu kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeelezea mara nyingi katika Bunge lako Tukufu. Kwenye Maoni haya, Mheshimiwa Spika, tunaomba tufanye marejeo ya taarifa rasmi za kitafiti za mamlaka za umma za kiserikali na za taasisi zisizokuwa

za kiserikali kuhusiana na matumizi ya nguvu za vyombo vya dola na jinsi ambavyo zinahatarisha haki za binadamu zilizohifadhiwa na Katiba yetu. Taarifa hizi rasmi zinahusu uchunguzi wa kifo au mauaji ya mwandishi wa habari Daudi Mwangosi katika Kijiji cha Nyololo, Wilaya ya Mufindi, Mkoani Iringa mnamo tarehe 2 Septemba, 2012, wakati akifanya kazi ya kukusanya habari kwa niaba ya Kituo cha Televisheni cha Channel Ten katika mkutano wa ndani ulioandaliwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18(b) na (d) ya Katiba inahifadhi haki ya kila mtu "... kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi"; na "... haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbali mbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu ya jamii." Aidha, kwa mujibu wa ibara ya 22(1) inatamka bayana kwamba "kila mtu anayo haki ya kufanya kazi." Kwa misingi hii ya Kikatiba, Marehemu Daudi Mwangosi alikuwa na haki zote kisheria kukusanya habari katika mkutano wa CHADEMA katika Kijiji cha Nyololo siku alipouawa.

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu pia inatambua na kuhifadhi "... uhuru wa kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika, kushirikiana na watu wengine na kwa ajili hiyo kutoa mawazo yake hadharani na kuanzisha na kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi na kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo." (Ibara ya 20(1), ni muhimu kutambua hapa kwamba 'aya nyakuzi' *(clawback clauses)* zilizokuwa zinaweka masharti na vizingiti vya 'kwa mujibu wa sheria' vilivyokuwa vinazuia raia kufaidi haki na uhuru unaotambuliwa na Ibara za 18 na 20 viliondolewa na Sheria ya Marekebisho ya Katiba, Sheria Na. 1 ya 2005.

Kwa maana hiyo, hakuna sheria nyingine yoyote inayoweza kufunga au kupunguza uhuru na haki zilizotolewa na vifungu hivi isipokuwa masharti yaliyoko kwenye Ibara ya 30 ya Katiba yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Sura ya Sita ya Katiba inaunda Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na kuipa majukumu na mamlaka ya kuyatekeleza majukumu hayo. Kwa mujibu wa ibara ya 130(1) ya Katiba, majukumu ya *CHRAGG* ni pamoja na kuhamasisha hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii; kupokea malalamiko ya uvunjaji wa haki za binadamu na kuyachunguza; na, kama itabidi, kufungua mashauri mahakamani ili kuzuia uvunjaji wa haki za binadamu.

Mara baada ya mauaji ya Marehemu Mwangosi kutokea, Tume ya Haki za Binadamu ilifanya uchunguzi wa mazingira na sababu za mauaji hayo. Baada ya uchunguzi huo, Tume iliandaa Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Uchunguzi wa Tukio Lililopelekea Kifo cha Daudi Mwangosi Kilichotokea Septemba 2, 2012 Kijijini Nyololo. Taarifa hiyo ilitolewa hadharani na kwa vyombo vya habari tarehe 10 Oktoba, 2012.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Uchunguzi inaeleza kwamba "... Tume ilizingatia zaidi masuala ya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Hivyo basi, Tume ilitilia maanani Katiba ..., sheria mbalimbali na mikataba ya kimataifa na ya kikanda inayohusu haki za binadamu ambayo Tanzania imeridhia." Katika uchunguzi wake Tume ilibaini mambo yafuatayo:-

(1) Tarehe 2 Septemba, 2012 CHADEMA kiliruhusiwa na Kamanda wa Polisi wa Wilaya ya Mufindi kufanya mikutano ya ndani na kuzindua matawi mapya lakini jioni ya tarehe 1 Septemba, 2012 Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa Michael Kamuhanda alizuia CHADEMA kufanya mikutano iliyoruhusiwa. Kwa mujibu wa Tume ya Haki za Binadamu, Kamanda wa Polisi wa Wilaya ndiye '"*Officer in charge*" wa Polisi wa eneo husika kama sheria inavyotaka.'

(2) Viongozi wa CHADEMA kilifanya mazungumzo na Mkuu wa Upelelezi wa Jinai Mkoa wa Iringa "... na kuruhusiwa kufungua matawi yao bila ya kuwa na mikutano ya hadhara."

(3) Msajili wa Vyama vya Siasa aliwaandikia barua viongozi wa vyama vya siasa kuwataka kusitisha shughuli zao kwa sababu ya sensa ya watu na makazi iliyokuwa inafanyika wakati huo.

(4) Wakati shughuli ya uzinduzi wa tawi la Nyololo ukiendelea, Kamanda Kamuhanda alifika eneo hilo na kuamuru viongozi wa CHADEMA wakamatwe na wafuasi wa CHADEMA walipinga kukamatwa kwa viongozi wao.

(5) Kamanda Kamuhanda aliamuru kupigwa kwa mabomu ya machozi ili kuwatawanya wananchi waliokusanyika katika ofisi za tawi hilo la CHADEMA.

(6) Baada ya mabomu ya machozi kupigwa, wananchi walitawanyika na kukimbia ovyo, lakini Marehemu Mwangosi "... alizingirwa na Askari, aliteswa na hatimaye inadaiwa alipigwa bomu na kufa papo hapo.

(7) Marehemu Mwangosi aliuawa umbali wa takriban mita 100 kutoka ilipo Ofisi ya CHADEMA tawi la Nyololo.

(8) Katika tukio hilo wananchi kadhaa walijeruhiwa kwa mabomu, wakiwemo mwandishi wa habari wa gazeti la Nipashe Godfrey Mushi, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake CHADEMA Wilaya ya Mufindi, Winnie Sanga na Mkuu wa Kituo cha Polisi Mufindi Asseli Mwampamba "aliyekuwa akifanya jitihada za kumuokoa marehemu Daudi Mwangosi."

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu, "... Tume imejiridhisha kuwa tukio la lililopelekea kifo cha Daudi Mwangosi limegubikwa na uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora." Taarifa ya Tume inafafanua kuwa, "... Tume imejiridhisha kuwa Jeshi la Polisi limevunja haki ... ya kuishi, haki ya kutoteswa na kupigwa, haki ya usawa mbele ya sheria na haki ya kukusanyika na kutoa maoni."

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na amri ya Kamanda Kamuhanda ya kupiga marufuku mkutano wa CHADEMA, Taarifa ya Tume inasema kwamba katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamanda Kamuhanda "... alikiuka Sheria ya Vyama vya Siasa ... kifungu cha 11(a) na (b) na Sheria ya (Jeshi la) Polisi ... kwa kuingilia kazi za *OCD* wa Mufindi na kutoa amri ya kuzuia shughuli za CHADEMA wakati yeye hakuwa *'Officer in-charge'* wa polisi eneo husika. Kwa maana hiyo amri aliyoitoa haikuwa halali kwa kuwa ilitolewa na mtu ambaye hakuwa na mamlaka kisheria kutoa amri hiyo. Haya ni matumizi mabaya ya madaraka, hivyo ni ukiukwaji wa misingi ya utawala bora."

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu ilihoji pia hatua ya Msajili wa Vyama vya Siasa John Tendwa kuwaandikia barua viongozi wa vyama vya siasa kuwataka kusitisha shughuli zao kwa sababu ya sensa. Kwa mujibu wa Taarifa ya Tume, hatua hiyo "... ilikiuka misingi ya utawala bora kwani maelekezo yaliyotolewa ndani ya barua hiyo yanakinzana na Sheria ya Takwimu, Na. 1 ya mwaka 2002 inayotoa fursa kwa wananchi kuendelea na kazi zao wakati wa sensa...." Barua hiyo pia "... ni kinyume na Sheria ya Vyama vya Siasa ... inayotoa fursa kwa vyama vya siasa kufanya shughuli zake bila kuingiliwa."

Mheshimiwa Spika, katika hili ni muhimu kunukuu mapendekezo ya Tume ya Haki za Binadamu kwa kirefu: "Jeshi la Polisi na Msajili wa Vyama vya Siasa waepuke kufanya maamuzi au matendo yanayoibua hisia za ubaguzi au upendeleo miongoni mwa jamii wakati wanapotekeleza majukumu yao kisheria. Mfano, Jeshi la Polisi lilizuia mikutano ya CHADEMA kwa sababu ya sensa wakati huo huo ... CCM walikuwa wakifanya uzinduzi wa kampeni huko Zanzibar.

Aidha, rai ya Msajili wa Vyama vya Siasa haikuzingatiwa kwa upande wa CCM Zanzibar huku CHADEMA walishurutishwa na Polisi kutii rai hiyo." Aidha, Taarifa ya Tume inasisitiza kwamba "demokrasia ya mfumo wa vyama vingi iheshimiwe na kulindwa."

Mheshimiwa Spika, sio Tume ya Haki za Binadamu pekee iliyofanya uchunguzi wa mauaji ya Marehemu Mwangosi. Baraza la Habari Tanzania *(MCT)* na Jukwaa la Wahariri Tanzania *(TEF),* taasisi mbili huru zinazojihusisha na masuala ya habari Tanzania, nazo zilifanya uchunguzi wa pamoja. Taarifa yao inayojulikana kama Ripoti ya Timu Maalum ya Uchunguzi Iliyoteuliwa na Baraza la Habari Tanzania *(MCT)* na Jukwaa la Wahariri Tanzania *(TEF)* Kuchunguza Mazingira Yaliyopelekea Kuuawa kwa Mwandishi wa Habari Daudi Mwangosi Septemba 2, 2012 Katika Kijiji cha Nyololo, Wilaya ya Mufindi, Mkoani Iringa, imeunga mkono Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya *MCT/TEF,* matokeo ya uchunguzi wao "... yanadhihirisha bila wasi wasi kwamba Polisi kwa makusudi waliwavurumisha Waandishi waliotoka Iringa wakati wakikusanya habari za shughuli za CHADEMA katika kijiji cha Nyololo. Zaidi ya hapo, Daudi Mwangosi mwenyewe aliuawa akiwa mikononi mwa Polisi huku wakisimamiwa moja kwa moja na Kamanda ... Kamuhanda." Ripoti inakubaliana na Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu kabla ya Mwangosi kuuawa, "... maelewano yalifikiwa katika ya *RCO* na maofisa wa CHADEMA na kamanda (*RCO*) (aliwa)amuru maofisa wake kutotumia nguvu dhidi ya watu waliokusanyika kwenye ofisi ile.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hali hiyo maelewano ilibadilika mara baada ya Kamanda Kamuhanda kufika katika eneo la tukio. Kwa mujibu wa Ripoti ya *MCT/TEF,* "mashuhuda wanaeleza kuwa RPC alimwita *RCO* na kumuonya wazi kuhusu kushughulikia kwa amani masuala ya CHADEMA katika eneo la awali la utulivu." Baada ya hapo, "inaelekea *RCO* alijitoa kuelekea eneo la umwagaji damu ... na hivyo usimamizi wa utoaji amri katika eneo la umwagaji damu ... ulibakia kwa mkuu wake ambaye ni *RPC* Michael Kamuhanda."

Mheshimiwa Spika, sawa na Taarifa ya Tume, Ripoti ya *MCT/TEF* inaweka lawama za vurugu zilizotokea Nyololo

kwenye miguu ya Kamanda Kamuhanda: Vurugu zilianza pale Kamanda Kamuhanda alipoamuru kukamatwa kwa viongozi wa CHADEMA waliokuwepo. "Kufuatia amri hiyo ... Polisi ... waliingia kwa nguvu katika ofisi ya CHADEMA wakipiga mabomu ya machozi na kuwaamuru viongozi hao wajisalimishe." Kwa mujibu wa Ripoti ya *MCT/TEF*, viongozi wa CHADEMA walitii amri hiyo na "... kujisalimisha kwa kuketi na kuinua mikono yao juu." Hata hivyo, "... wakati makada wa CHADEMA walitii maagizo ya viongozi wao ya kuketi chini na kuinua mikono yao juu, Polisi walifyatua risasi na mabomu ya machozi na kuwapiga makada hao na waandishi kwa virungu."

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya *MCT/TEF* inakubaliana na Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu juu ya jinsi Marehemu Mwangosi alivyouawa. "Alipoangalia nyuma, Daudi Mwangosi aliona kikundi cha Polisi wakimpiga mwandishi mkuu wa gazeti la Nipashe wa Iringa, Godfrey Mushi.... Wakati mwandishi Godfrey Mushi akiwa bado anapigwa na Polisi, marehemu Mwangosi aliwakimbilia akiwaomba waache kumdhuru zaidi Mushi kwa kuwa alikuwa Mwandishi tu. Polisi hawakumsikiliza. Badala yake wakamburuta mwandishi huyo ambaye tayari alikuwa amepoteza fahamu na kumweka kwenye gari lao na wakamgeukia Daudi Mwangosi mwenyewe, wakampiga kwa nguvu mpaka akapoteza fahamu."

Mheshimiwa Spika, hata amri ya Mkuu wa Kituo cha Polisi Mafinga Mwampamba kuwataka Askari Polisi waache kumpiga marehemu Mwangosi haikusikilizwa na Askari hao. Ili kujiokoa, marehemu Mwangosi alimkumbatia *OCS* Mwampamba na "baadaye kumwangukia miguuni mwake kuepuka kipigo zaidi." Kwa mujibu wa Ripoti ya *MCT/TEF,* "picha za mgando zinaonyesha Polisi mmoja akipiga bomu la machozi tumboni mwa marehemu Mwangosi kwa karibu kabisa." Bomu hilo liliusambaratisha mwili wa marehemu Mwangosi aliyekufa papohapo. Kwa sababu marehemu Mwangosi alikuwa chini ya miguu ya *OCS* Mwampamba, "naye pia alijeruhiwa vibaya."

Mheshimiwa Spika, siku moja baada ya mauaji ya Daudi Mwangosi, Kamanda Kamuhanda alinukuliwa na vyombo vya habari akidai kwamba marehemu Mwangosi alifariki "kutokana na kitu kizito kilichotupwa na waandamanaji." Aidha, siku iliyofuata Kamishna wa Operesheni wa Jeshi la Polisi Paul Chagonja alidai kwamba baada ya ghasia kudhibitiwa, marehemu Mwangosi alikimbilia walipokuwa Polisi na "kitu kama bomu kikarushwa na kundi la watu wanaokimbia hovyo na kumlipua Mwangosi."

Mheshimiwa Spika, madai haya yanakanushwa na Ripoti ya *MCT/TEF* inayomnukuu shuhuda mwanamke aliyeshuhudia mauaji hayo na kubainisha kwamba marehemu Mwangosi "aliuawa chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa *RPC* Michael Kamuhanda." Ripoti hiyo pia imeelezea kwa kirefu jinsi Jeshi la Polisi lilivyotoa taarifa zinazokinzana juu ya kuhusika kwake na mauaji ya Mwangosi. Hivyo, kwa mfano, wakati Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi alidai tarehe 4 Septemba, 2012 kwamba marehemu aliuawa na bomu la machozi ambalo 'halikulipuliwa kitaalamu na Polisi', Kamanda Kamuhanda alitokea kwenye televisheni siku iliyofuata "akitangaza habari za kuwatupia lawama wafuasi wa CHADEMA kwa kutupa kitu kizito kilicholipuka na kumuua Mwangosi...."

Mheshimiwa Spika, kwa miaka miwili mfululizo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imezungumzia kwa kirefu vitendo vya mauaji ya raia wasiokuwa na hatia ambavyo vimekuwa vinafanywa na vyombo vya dola hasa Jeshi la Polisi. Kama tulivyowahi kusema kwa kunukuu matokeo ya utafiti uliofanywa katika nchi za Afrika Mashariki na Mradi wa Haki za Binadamu wa Jumuia ya Madola na kuchapishwa mwezi Juni, 2006, '"watu wa Tanzania ... wanakabiliwa na tatizo la kuwa na Jeshi la Polisi ambalo mara nyingi lina sifa ya ulaji rushwa, matumizi ya mabavu na kuwa na chombo katili cha serikali." Kwa mujibu wa utafiti huo, "aina hii ya uendeshaji wa shughuli za Polisi inapingana na madai ya kuwepo kwa demokrasia yanayotolewa na Serikali ya Tanzania."

Mheshimiwa Spika, sasa Taarifa ya Uchunguzi wa Kifo cha Mwandishi wa Habari wa Channel Ten Bwana Daudi Mwangosi, iliyoandaliwa na Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Nchimbi na kuchapishwa tarehe 9 Oktoba 2012 imethibitisha ukweli wa kauli hii na ukweli wa madai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya matumizi ya nguvu ya Jeshi la Polisi.

Baada ya kuzunguka huku na huko ikijaribu kulisafisha Jeshi la Polisi, Taarifa ya Kamati hiyo inasema: "Hapakuwepo na uhalali wa kutumia Bomu la Kishindo kwani lengo la ulipuaji wake ni ili watu waogope na kukimbia." Aidha, Kamati hiyo iliyoongozwa na Jaji Mstaafu Stephen Ihema, inakiri kwamba "hapakuwepo umuhimu wa kutumia Bomu la Kishindo kwa sababu hata ingekuwa ukamataji tayari Askari Polisi wapatao sita walikuwepo eneo la tukio." Kwa misingi hiyo, "... Kamati imeona kwamba ... tukio la kuuawa Bwana Daudi Mwangosi na kuumizwa baadhi ya Askari Polisi halikustahili kabisa."

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli kama inakubaliana na matokeo ya taarifa hizi tatu zilizoandaliwa na taasisi za kiserikali kama vile Tume ya Haki za Binadamu, Kamati ya Jaji Ihema na *MCT/TEF* juu ya kuhusika kwa Jeshi la Polisi na mauaji ya marehemu Daudi Mwangosi. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iteo kauli mbele ya Bunge lako tukufu kama inakubaliana na Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu kwamba kitendo cha Kamanda Kamuhanda kupiga marufuku mkutano halali wa CHADEMA kilikuwa ni kinyume cha Sheria ya Jeshi la Polisi, Sheria ya Vyama vya Siasa na ukiukwaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli kama – baada ya ushahidi wa taarifa hizi tatu - iko tayari kuiomba radhi CHADEMA kwa kuisingizia kuhusika na kifo cha marehemu Daudi Mwangosi. Mwisho, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli mbele ya Bunge lako Tukufu kama iko tayari kuilipa familia ya marehemu Mwangosi fidia kwa mujibu wa sheria

kwa kitendo cha Serikali kusababisha mauaji yake bila 'uhalali.'

Mheshimiwa Spika, Serikali na chama ambacho sera zake zinakiuka haki za binadamu na misingi ya utawala bora inapoteza uhalali (*legitimacy*) ya kuendelea kutawala. Hapa ndipo CCM na Serikali yake ilikoifikisha nchi yetu: Waandishi wa Habari wanauawa kwa sababu ya kufanya kazi yao halali ya kutafuta habari za mambo yanayohusu umma kama mikutano ya vyama vya siasa.

Watanzania hawastahili Serikali ya aina hii. Kama alivyosema Baba wa Taifa katika kitabu chake Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania: "Hatulazimiki kuendelea na uongozi mbovu wa Chama na Serikali. Wala tukiendelea na hali hii, bila kubadili uongozi wa Chama na Serikali, sina hakika kama tutafika huko salama. Masuala muhimu ya nchi yetu hayatashughulikiwa.... Na masuala mengine muhimu ... yataachwa yajitatue yenyewe.

Nasema katika hali kama hiyo sina hakika kama tutafika salama; na tukifika salama tukiwa na uongozi huu huu wa Chama na Serikali mbele kutakuwa ni giza tupu. Majuto ni mjukuu, huja baadaye."

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya marefu, naomba kukushukuru na wewe binafsi na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ambayo sijayasema yaingizwe katika rekodi Rasmi za Bunge lako Tukufu, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Kwa maana hii, ni kwamba watakaoweza kuchangia asubuhi hii watakuwa kama wachangiaji wanne. Nitaanza na Mheshimiwa Jasson Rweikiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mheshimiwa Sabreena Sungura na Mheshimiwa Raya Ibrahim na kisha atafuatia Mheshimiwa Pindi Chana. Tutaangalia itakavyokuwa, Mheshimiwa Rweikiza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii, nichangie katika hotuba ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inaendeshwa kwa utawala wa sheria na huu ndiyo msingi wa utawala bora. Kwa hivyo, Wizara hii ni muhimu kama zile Wizara nyingine, lakini cha kushangaza tumesikia hotuba ya Waziri, hotuba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, fedha inayopewa Wizara hii haitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile, muda wa dakika kumi nilionao ni mdogo sana, nizungumzie Mahakama. Mahakama ndiyo mhimili mkubwa wa kutenda haki katika nchi hii lakini inasikitisha sana kwamba Mahakama inafanya kazi katika mazingira magumu sana, haipati fedha kama inavyotakiwa. Tumemsikia aliyewasilisha maoni ya Kamati anasema mwaka wa fedha huu tunaomalizia sasa hivi, fedha iliyotengwa ni shilingi bilioni 17.2 kwa ajili ya maendeleo ya Mahakama haikutolewa hata senti tano. Mahakama inafanya kazi kwa shida sana. Sasa katika hali kama hii ni vigumu kutegemea kwamba utawala wa sheria utaonekana vizuri.

Mheshimiwa Spika, watu wanakwenda Mahakamani kesi zinachelewa kumalizika, haziishi upesi. Kule Bukoba mtu anakwenda Kituo cha Polisi kumlalamikia mtu kwamba amemwibia au amemtukana, anaambiwa mlete mshtakiwa kwa gharama zako wewe mwenyewe, msafirishe. Akiwekwa mahabusu au rumande pale ulimpie chakula. Sasa kama hii ni bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani au Katiba na Sheria, sijui lakini ni katika mfumo mzima wa utendaji haki. Ukweli ni kwamba fedha inayotengwa kwa ajili ya Wizara ya Katiba na Sheria bado haitoshi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, matokeo yake wananchi hawaendi tena Mahakamani, wala Polisi kulalamika, wanachukua sheria mkononi ile tunayoita *mob justice*. Mtu ana manung'uniko dhidi ya mtu, anamtuhumu hata kama ni uongo, anatafuta ndugu na marafiki zake

wanamuadhibu kwa kumpiga na wengine wanawaua kwa sababu akienda kule Mahakamani anaambiwa agharamie yeye mwenyewe, uwezo huo hana. Kaonewa lakini anaambiwa agharamie hizo gharama za kumpeleka mtu Mahakamani. Niiombe sana Serikali iongeze fedha kwenye mafungu ya Wizara ya Katiba na Sheria na hasa fungu la Mahakama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kutenda haki, kwa mfano Mahakamani pale kama nilivyosema, kuna Mahakama yenyewe, Waendesha Mashtaka ambao ni Polisi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ukiangalia zile Idara nyingine zina nafuu kidogo; Polisi wana magari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali watu wake wana magari na vifaa vya kufanyia kazi, Mahakama haina vifaa hivyo. Mahakimu hawana nyumba, hawana magari, hawana motisha, kwa kweli hali inakuwa ni mbaya sana. Niiombe sana Serikali itoe fedha kwenye idara ya mahakama na Wizara ya Katiba na Sheria kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, isiwe kwamba tunatenga fedha hapa na tunapitisha bajeti inakuwa ni kama ukomo, *ceiling*. Tunasema kiasi fulani kimetolewa kwa Wizara fulani lakini hizo fedha haziendi, inakuwa ni kama tumeweka kiwango cha mwisho cha ukomo. Zile fedha ziende zitumike kufanya kazi iliyokusudiwa katika Idara iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, nimemsikia Msemaji wa Kambi Rasmi ya CHADEMA, yeye anasema Kambi Rasmi ya Upinzani, mimi nasema siyo ya Upinzani ni ya CHADEMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anazungumzia Mabaraza ya Katiba, Tume, ninamshangaa sana ni kwa nini anapenda kupotosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anapenda kupotosha umma kwa sababu wao walisema wakiingia madarakani siku 100 na Katiba Mpya, wangeipata wapi? Siku mpya wangeipata wapi Katiba? *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa!

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Tumeanzisha mchakato wa kutafuta Katiba Mpya...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa!

**WABUNGE FULANI:** Kaa chini.

**SPIKA:** Naomba uendelee Mheshimiwa. *(Makofi)*

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Siyo jambo dogo hili! Tumepiga hatua kubwa sana kwenye mchakato huu. Wananchi wote wametoa maoni yao, wote waliotaka kutoa maoni yao wametoa maoni yao. Wamehudhuria vikao vile vilivyoandaliwa kwa uhuru na uwazi, wametoa maoni yao. Tume imeundwa na inafanya kazi yake vizuri. Wanategemea Tume waende kwa miguu nchi nzima? Wajumbe thelathini na wangapi sijui, wazunguke nchi nzima kwa miguu? Ni lazima watumie magari, walale hotelini, wafanye kazi yao, anatoa takwimu za uongo, sijui posho shilingi ngapi, za kubuni, si za kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka tu kusema kwamba mchakato huu ni mkubwa, Mabaraza yameundwa, vilevile yamehusisha wananchi wote, kuanzia kwenye vijiji na mitaa, wananchi wote wamepiga kura kwa haki na uwazi kuchangua wajumbe wa Mabaraza haya. Hakuna upendeleo wala kufichaficha, kila mwananchi amehusika kwenye Mabaraza haya, yatakaa yajadili Rasimu ya Katiba, tutakwenda hadi Bunge Maalum la Katiba, amelisema, tutakwenda hadi kwenye kura ya maoni, kuna tatizo gani? Wenyewe walitaka watoe Katiba ya kuweka tu Wabunge wao, Tundu Lissu Mwanasheria atunge Katiba aseme ndiyo Katiba ya nchi! Katiba inatungwa na watu kwa ajili ya watu, lazima watu washiriki kuanzia mwanzo mpaka mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namshangaa sana anapolalamika kwamba sijui gharama gani, sasa alitegemea ifanyike namna gani, bila gharama? Lazima mchakato huu uwe na gharama kubwa na gharama hizi tunatoa wananchi wenyewe katika kodi, ndivyo ilivyotegemewa na ndivyo ilivyo. Kwa hiyo, si vizuri kusimama pale na kupotosha wananchi kwamba, mchakato huu umetekwa na CCM, ooh mchakato huu umekuwa sijui namna gani, siyo kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaunga mkono hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria lakini niombe kwamba Wizara ipewe fedha za kutosha na Mahakama iongezewe mafungu ili iweze kufanya kazi zake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis atafuatiwa na Mheshimiwa Sabreena Sungura na Mheshimiwa Raya.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitaanza kuzungumzia Mahakama. Chombo cha Mahakama ni muhimu kwa nchi yoyote, siyo Tanzania peke yake lakini kuna mambo nimeyaona ambayo kwa Mahakama yetu kidogo sijui ni kwamba tuna Majaji wachache au umekuwa kama ndiyo utaratibu, kwa sababu ziko Mahakama kama nane; Mahakama ya Rufaa, Mahakama Kuu, Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara, Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi, Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo, zote hizi ukiziangalia utendaji wake hakuna hata Mahakama moja iliyomaliza mashauri au kesi. Kila mwaka zinalimbikizana, badala ya kesi kumalizika, zinazaa kesi nyingine.

Sasa najiuliza, hivi kweli tuko *serious* kama Mahakama kuwasaidia wananchi? Unapokuwa na kesi huwezi kulala,

harakati zako zote zinakuwa haziko kwenye utaratibu mzuri. Sasa ningeona hiki chombo wakati kuna mfuko wa Mahakama, shilingi bilioni 20 zile walizopewa ambazo walisema watapunguza hizi kesi, nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, hili kweli linatendeka?

Mheshimiwa Spika, tunajua kuna utaratibu mmoja, mtu unapompa kazi umfuatilie. Unajua Mahakimu hawafuatiliwi, kwa nini? Mtu anakuwa na kesi, hajui kwa wiki mimi natakiwa amalize kesi ngapi, kwa mwezi amalize kesi ngapi, kwa mwaka amalize kesi ngapi? Sasa mtu huyu kama hutamwekea utaratibu au Mkaguzi ambaye atakuwa akiwakagua Majaji kwa mujibu wa utaratibu wa kesi wanazopangiwa, ndio mambo yanakuwa hivi. Mheshimiwa Waziri naona hawa Majaji lazima kuwe na utaratibu wa kuangalia na kufuatilia ili kujua ni kesi ngapi wanazisikiliza kwa wiki, mwezi na mwaka. Nafikiri huu utakuwa ushauri mzuri na hata Jaji atakuwa anajua kwamba wiki hii lazima nimalize idadi fulani ya kesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja katika mabadiliko ya Katiba. Najua Tume wanatakiwa ifikapo Aprili, 2014 wawe wamekamilisha mchakato mzima wa Katiba na tuwe na Katiba yetu. Siyo vibaya na Mwenyezi Mungu atawasaidia. Tume imepewa utaratibu wa kukusanya maoni na tumeona jinsi zoezi hilo lilivyokwenda. Wamepewa uwezo kuanzia Mikoa, Wilaya, vikundi maalum na kadri watakavyojipangia. Utakuta utaratibu huu wa kura za maoni, wakati walipokuja kule Zanzibar walikuwa wanafanya Kishehia. Mchakato mzima ule umekwenda, hasa tukichukua mfano wa Mkoa ambao nilikuwepo mimi wa Mjini Magharibi, utakuta Tume walikuwa wakifika pale wanapofanyia ile shughuli ya mchakato ameachiwa Sheha.

Huyu Sheha maskini hajawezeshwa, uwezo wake ni mdogo. Anatakiwa atafute sehemu ya mkutano, atafute viti vya wajumbe wa Tume, Sheha huyo huyo atafute kivuli cha kukaa wajumbe wa Tume, Sheha huyohuyo uwezo hana, anaweza kutafuta vitu mahali popote, kama ni viti au nini, akipeleka inakuwa ni mvutano, aah kachukua viti au

maturubai kwenye vyama. Sasa akachukue wapi na yeye uwezo hana? Nyumbani kwake kitu hicho anaweza akawa hana, akachukue wapi? Suala hili nilikuwa nataka niwatabanaishe Tume waangalie na kuhakikisha kwamba, wanapompa mtu kazi, wampe na uwezo wa kuitekeleza kazi hiyo, najua vifungu hivyo Tume wanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isitoshe mchakato ule ulivamiwa na vijana. Kwa nini ulivamiwa na vijana na ukakosa nguvu? Utakuta anakuja Mwenyekiti au mhusika wa Tume anasema kwamba, mtu yeyote anaweza kwenda Shehia yoyote akavamia na akatoa maoni. Kweli watu wamevamia, watu walewale walikuwa wanajirejea, mtu wa Shehia husika hawezi kufika pale, Masheha waliopewa kazi ya kusimamia wakawa wananung'unika.

Sasa ukakuta ule utaratibu badala ya kuwa mzuri, ukawa na vurugu. Wazee wanashindwa kwenda, walipowekwa watu hao wanaotoa maoni siyo pa heshima, mtu anawekwa chini, mahali pana vumbi, mvua inanyesha mahali pale unakuta pana maji, sasa utakuta mtu mzima na heshima zake hawezi kwenda, ikawa wanaokwenda ni vijana. Huko mbele kuna kura za maoni, jamani tuangalie ni vipi tutajipanga ili shughuli yetu iweze kuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kuzungumza juu ya *RITA*. Hapa nitazungumza kuhusu wosia. Watanzania wengi bado hatujapata elimu ya kutayarisha wosia. Watu wanakufa, kesi zinakwenda kwenye Mahakama, watu wanacheleweshwa kupata haki zao, kesi zinachelewa kumalizika. Nataka Mheshimiwa Waziri akifika hapa aje anielezee, *RITA* na uhifadhi na uandikaji wa wosia ameuweka kwenye kiziba gani kwa sababu, *RITA* haijafanya kazi ya kupita kuelimisha na kuwafahamisha wananchi au kutoa elimu katika Vijiji, Miji na Mikoa.

Hili ni suala zuri kwa sababu tunakokwenda siku hizi umri wetu ni mdogo, siku hizi tunaona vijana wetu wanamiliki mali nyingi, sasa kama hakutakuwa na wosia hapa katikati kutatokea vurugu, kutofahamiana au kuumizana. Naomba

kitengo hiki kifanye bidii kupita kwenye Mikoa na jamii ili kutoa elimu itakayowasaidia Watanzania kuweza kujua jinsi ya kuandika na kuhifadhi wosia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije katika ofisi ya *DPP*. Ofisi ya *DPP* inafanya kazi nzuri na tunaipongeza lakini kuna mvutano ambao nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri akija hapa anifafanulie, juu ya ofisi ya *DPP* na ofisi ya TAKUKURU. TAKUKURU anasema kesi zangu za rushwa haziendi kwa sababu *DPP* hazitoi. *DPP* anasema kwamba mimi nafanya kazi kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi. Sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri aje kuifahamisha jamii huu mvutano uliopo katikati hapa unaashiria kitu gani? Kwa sababu Serikali inataka rushwa iondoke na *DPP* anafanya kazi kwa mujibu wa sheria, sasa jambo hili ili liweze kufanyika, kutendeka na kutoa hisia kwa wananchi ili waweze kuiamini Serikali yao, ni vipi Serikali italisimamia ili tumwone *DPP* anafanya kazi bila matatizo na TAKUKURU anamuamini *DPP* kwa mujibu wa shughuli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia kidogo juu ya Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo. Katika ukurasa wa 45 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumza vizuri na tumemwelewa, lakini bado changamoto zipo kwa sababu hawa wanafunzi wapo, ruzuku inakwenda kwenye Wizara hiyo ninakubali, lakini na wanafunzi bado wanatakiwa kupata mikopo, bila ya mkopo huwezi kusoma. Kama kuna sheria inazuia wanafunzi hawa wasiwezi kupata mikopo, iletwe hapa Bungeni, tuirekebishe ili hawa wanafunzi na wao waweze kupata mikopo kama wanavyopata wanafunzi wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nakuja kwenye Tume ya Haki za Binadamu. Bado hii Tume yetu ya Haki za Binadamu haijatusaidia kwa sababu imerundika mashauri 6,891....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, nitamwita Mheshimiwa Sabreena kwa dakika tano na Mheshimiwa Raya dakika tano.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa, napenda kuweka kumbukumbu sawa kwamba, mchangiaji wa kwanza amepotosha umma kwa kusema Chama cha CHADEMA kilisema kitakamilisha mchakato wa Katiba ndani ya siku 100. Sivyo, Ilani ya CHADEMA ilisema itaanza mchakato wa marekebisho ya Katiba ndani ya siku 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani. Pili, ninapenda Serikali itwambie, ilivyoamua kuweka shilingi milioni 18 kwa ajili ya wajumbe wa Tume ambao wanaweza wakapata maambukizi ya UKIMWI, mimi naona suala hili ni kuitabiria jamii yetu mabaya. Je, ulifanyika mchakato wa kuwapima Wajumbe hawa kabla hawajaingia kwenye kazi hiyo na watajihakikishiaje kwamba ni wajumbe wangapi wamepatwa na dhoruba hiyo ndani ya mchakato huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja sasa kwenye suala zima la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Wanasheria wa Wizara. Serikali imekuwa na *double standard*, Wanasheria ni haohao wenye *same qualification* lakini *scale* za mishahara yao ni tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka Serikali leo ije itwambie Mwanasheria wa Wizara yupo pale kufanya kazi gani? Kesi zote za Wizara zinazopelekwa pale, Mwanasheria wa Wizara anabakia tu kama mshauri, wasimamizi wa kesi hizo ni Wanasheria wa *Attorney General*. Sasa wale watu wa Wizara pale tumewaweka wafanye kazi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikataba yote inayopelekwa Wizarani inapita tu, inapelekwa kwa *Attorney General*. Kuna

nini huko kwenye Ofisi ya *Attorney General?* Mnawacheleweshea Watanzania maendeleo. Mikataba inachelewa, kesi zinachelewa tunaambiwa zipo kwa *Attorney General*. Sasa wale Wanasheria waliopo katika Wizara wanafanya kazi gani jamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri sasa ni wakati muafaka ndugu yangu *Attorney General* utaratibu wa zamani urejeshwe kwamba Wanasheria wa Wizarani na Wanasheria wa Ofisi ya *AG*, wote wabakie kwamba ni ma-*State Attorneys* na wapewe mshahara unaolingana.

*(Hapa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikuwa anatikisa kichwa)*

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Ndiyo unaweza ukatikisa kichwa, lakini leo hii mtu ambaye ni *Principal Legal Officer* wa Wizara...

**SPIKA:** Kanuni inasema uzungumze na mimi sio na watu wanaotikisa vichwa vyao. Zungumza na mimi. *(Kicheko)*

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** ...anakuwa ni mdogo kwa *State Attorney* hata kama ana-*experience* ya kutosha, ana uzoefu wa kazi wa muda mrefu wa kutosha, mnawaondolea watu *morale*, mnawakatisha tamaa. Kwa hiyo, ni lazima mfikirie kurejea upya utaratibu wa zamani ambapo watu wote walikuwa wanaajiriwa kama *State Attorneys* ili mambo yaweze kwenda sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalopenda kugusia ni suala nzima la ucheleweshaji wa kesi kwenye Mahakama zetu. Kumekuwa kuna mlundikano mkubwa wa kesi na hatuelewi kwa nini, ni muda mrefu toka enzi na enzi kesi zimekuwa zikichelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda tu kuwausia wenzangu wa *DPP*, ni vyema sasa tukaanza *system* ya *pre-bargaining.* Wenzetu wa USA, asilimia 96 ya kesi zao za *criminal* zinakuwa *solved* kwa kutumia mfumo wa *pre-bargaining* kwamba *DPP*

anafanya mazungumzo na watuhumiwa, wanamaliza hiyo kazi kabla ya kupoteza muda na pesa ya Mahakama, wanamaliza nje kabisa, wanapokwenda pale inakuwa tu ni suala la utekelezaji lakini sisi kesi zetu zimekuwa zinachukua muda mrefu haziishi. Kwa hiyo, tungefanya hii *system* ya *pre-bargaining* kwamba mtu anakubali kosa mapema, *in extent charge* zao zinakuwa *reduced*. Nafikiri suala hili litakuwa ni suala la msingi sana na la umuhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, napenda moja kwa moja nigusie Tume ya Haki za Binadamu... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante muda umeisha, Mheshimiwa Raya.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii. Najikita katika maeneo matatu ambayo nitayazungumzia katika Wizara hii na miongoni mwa hayo nilijaribu kuyazungumzia katika Bunge la Bajeti lililopita la mwaka jana, lakini bado inaonekana kuna uzito fulani katika utekelezaji au pamoja na jitihada hizo imekuwa ni changamoto na bado ni tatizo, ni suala zima la mashauri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amelieleza vizuri, yaani hotuba yake imeonyesha matumaini ya kushughulikia mashauri pamoja na kupunguza msongamano wa kesi Mahakamani. Mashauri yana gharama nyingi yaani mtu mpaka shauri lake liishe ni gharama kubwa sana na Watanzania wengi siyo wote wenye uwezo wa kumudu kushughulikia mashauri yao kwa gharama ambayo Serikali imeweka.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ama maoni yangu katika suala hili ni kupunguza gharama za mashauri. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kurasa za 45 na 46 ameeleza mikakati ya kukabiliana na changamoto hii ambapo ni pamoja na kuongeza idadi ya Mawakili na idadi

ya watumishi lakini shauri wangu kwa hapa ni kuwa na *limitation* ya *time* katika mashauri. Kesi inapofunguliwa basi angalau isizidi miaka miwili iwe imemalizika, nadhani hiyo itakuwa njia ya kupunguza msongamano wa mashauri mengi yaliyopo Mahakamani. Vilevile itasaidia Watanzania wengi kupata haki zao kwa muda muafaka kama ambavyo wanatarajia na siyo ambavyo wanavyopata kwa sasa. Kwa hiyo, nashauri kuwe na *limitation* ya *time* katika mashauri yaani yasizidi miaka kadhaa katika kuendeshwa Mahakamani. Nadhani hilo litakuwa ni suala zuri pamoja na kupunguza gharama kwa watu ambao wanatakiwa wafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo nitaliongelea ni suala zima la rushwa katika Mahakama zetu. Tunaona bado rushwa ni tatizo kubwa, rushwa ni changamoto katika Mahakama zetu. Inafikia wakati *judgement* imetoka basi upewe ile *judgement* yako, haujakaa sana umekaa miezi sita, yaani mtu chini ya miezi sita huwezi kupata *judgement unless* una undugu na mtu yeyote ama vinginevyo labda umetoa pesa ili upatiwe *judgement* yako ambayo ni haki yako unatakiwa uipate mara tu baada ya kutolewa na isizidi muda kadhaa lakini inafika miezi sita mtu bado hajapata *judgement.*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika Mahakama, ku-*release order* kutoka Mahakamani pia inachukua muda mrefu sana labada uwe unajuana na mtu ama vilevile utangulize pesa ndiyo upate haki yako.

Mheshimiwa Spika, aidha, ukija kwenye suala la kumpata Jaji bado inakuwa ni tatizo kubwa kwa watu kuwapata Majaji, Mahakimu na Mawakili ambao watakuja kuwasimamia katika kesi zao. Nakumbuka niliwahi kulizungumzia na kidogo limegusiwa katika hotuba ya Waziri kwa matumaini lakini bado tunataka kuona utekelezaji, jinsi ambavyo Watanzania, wananchi ambao wanakabiliwa na mashtaka yao, wanakabiliwa na kesi zao Mahakamani, Serikali inawasaidia kama katika *Act* ilivyoelezwa kwamba inatakiwa Mtanzania ambaye hana uwezo basi Serikali

imwone, imsaidie, impe Wakili na imueleweshe lakini unakuta mtu hana uwezo, hakuna maelekezo yoyote, hajui aanzie wapi, hajui amalizie wapi ili apate haki yake. Haki inafinywa, haki inazuiwa, inatumiwa na watu ambao hawastahili kuitumia na inatumiwa na watu kwa kupeana tuseme. Mtu ambaye ni maskini hata anapokwenda Mahakamani anaona tu anapoteza muda wake na pesa, haendi kupata haki yake kwa sababu kwa sasa hivi haki zinanunuliwa na siyo kutolewa Mahakamani. Kwa hiyo, tunashauri Serikali iliangalie sana hilo, kupitia Wizara hii ilitazama hilo suala la rushwa katika Mahakamani zetu na kuwapatia wananchi haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ambalo napenda kuliongelea, ni kutofikiwa kwa Mahakama ama kuwa na Mahakimu wachache. Hatuwezi kuwa na *accessibility* ya *justices* endapo tutakuwa na hali ambayo tunayo sasa kwamba Hakimu anatoka Bagomoyo, Hakimu huyohuyo anasubiriwa Chalinze katika Mahakama ya Wilaya aende akasikilize kesi nyingine, tunakwenda wapi, tunafanya nini? Kinachotakiwa, wasomi wapo wengi mitaani, vijana wengi wame-*qualify* kuwa Mahakimu, lakini ajira bado ni kikwazo, inakuwa ni tatizo kwa vijana hawa kupatiwa ajira. Hivyo basi, ili tuwe na *accessibility* ya *justices* katika Mahakama zetu, ni vizuri kuongeza Mahakimu, kuajiri watu na vilevile kuboresha mazingira ya wafanyakazi wetu hasa Majaji... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA**: Ahsante. Sasa nitamwita Rukia Kassim Ahmed, atafuatiwa na Mheshimiwa Pindi Chana.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndiyo chanzo kikubwa cha migogoro katika nchi hii kwa watu kutokuelewa sera

na sheria zilizopo katika nchi hii. Sera na sheria zipo lakini zimefungiwa katika makabati tu, wananchi hawazielewi hata wale wanaotakiwa kutekeleza zile sera basi pia hawazielewi, hili ni tatizo kubwa ambalo linasababishwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, migogoro mikubwa inayohusiana na Muungano, inatokana na watu kutokujua sera na sheria. Kwa mfano, katika Bunge hili, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge humu hawajui hata maana ya Jamhuri ya Muungano. Kuna Waheshimiwa Wabunge humu wamethubutu kusema kuwa sisi Wazanzibari hatupaswi kuingia katika Bunge la Katiba kwa kujadili mambo yanayohusiana na Bara. Tena la kusikitisha hasa, watu hawa ni watu wakubwa, watu ambao wapo katika Chama kikubwa kinachojiita ni chama mbadala, wanafikia mahali wanatwambia sisi Wazanzibar hatuna haki ya kuingia katika mchakato wa kujadili Katiba ya nchi hii, hii yote ni uelewa mdogo wa sera na sheria zinazohusu Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge humu katika Bunge la Tisa walithubutu kusema Geita kuna watu wanaozidi milioni moja na kidogo wanawakilishwa na Wabunge wanne lakini pia Zanzibar kuna watu milioni moja na kidogo wanaowakilishwa na watu zaidi ya 50. Hii yote ni uelewa mdogo wa sera na sheria ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wa kulaumiwa ni Wizara hii kwa kutokutoa taaluma na wakawafanya Wabunge wa Bunge hili kujua nini sera na sheria ya Muungano. Naomba Wizara hii itoe taaluma kwa Waheshimiwa Wabunge kabla ya Bunge la Katiba ili isije ikatuletea matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa nataka niende kwenye Mahakama. Ucheleweshaji wa kupata haki, hilo ni tatizo kubwa na kwa kweli linaleta mzozo mkubwa katika nchi. Ucheleweshaji wa kesi Mahakamani, watu kutopata haki yao mapema ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba, ukurasa wa nane, Waziri mwenyewe amesema Mahakama ya Rufaa imesikiliza kesi kwa asilimia 13, Mahakama Kuu imesikiliza kesi asilimia 30, Mahakama ya Biashara imesikiliza kesi asilimia 22, hili ni tatizo. Kwa sababu haki inapochelewa kupatikana watu wanakosa imani hata na Serikali, watu wanakosa imani na chombo hiki cha Mahakama.

Kwa hiyo, hii milundikano wa kesi upungue. Kuna watu wamelundikana katika mahabusu au katika jela ambao wana kesi ndogo ndogo. Kwa mfano, kibaka pengine akampora mtu simu, pengine kuna mtu kaiba kuku anawekwa katika jela, hawa watolewe, waende Kariakoo kule wakasafirishe mitaro, wakasafishe soko lile ile pekee yake ni adhabu na ni aibu wataona haya.

Mheshimiwa Spika, wakipelekwa kule, wakaenda kusafisha watu wakiwaona hawa wamekamatwa kwa kesi pengine ya kuiba kitu kama hiki, mtu atakuwa na taharuki mara ya pili haibi tena itakuwa funzo na mlundikano kwenye jela zetu utapungua. Hata katika mahabusu zetu, utakuta vilevile kuna mlundikano kama huo.

Mimi nashauri Serikali iangalie zile kesi ndogo ndogo watu watolewe kwa njia kama hiyo. Katika Mikoa yetu huko kuna sehemu za kusafisha, wapelekwe wakasafishe pia iwe ni hukumu yao na tutapunguza ule mlundikano.

Mheshimiwa Spika, halafu pia katika haya Magereza yetu, kuna watoto wadogo ambao wamechanganywa na watu wakubwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge muda wako umekwisha. Msemaji wa mwisho mchana huu ni Mheshimiwa Pindi Chana.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kupata nafasi.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajikita kwenye Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Wakati sheria hii inapitishwa mimi nilikuwa ni Mwenyekiti na ninashukuru Mungu bado ni Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuielezea. Kwanza nianze na Bajeti ya Tume, Tume tumepitisha bajeti shilingi bilioni takribani 33. Hela hizi kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba ni ndogo na nitatoa sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walikuja mara ya kwanza, hii ni bajeti ya pili, walituomba shilingi bilioni 40 na kulikuwa na kazi nyingi za kufanya. Kwenye Kamati tukasema baadhi ya kazi zipunguzwe, tukaenda shilingi bilioni 33 na sasa hivi wamepewa *ceiling* ya kipindi kilichopita shilingi bilioni 33. Sasa wakati wa kujadili tulisema hawa wajumbe wa Tume walipwe posho au mishahara? Tukachukua mifano ya nchi ambazo zimebadilisha Katiba mfano wa Ghana na Kenya. Kenya walikuwa wanalipwa *dollar* na Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya Kenya walikuwa wanaruhusa *donors* kutia pesa kwenye Tume, kwa hiyo, walikuwa na pesa za kutosha. Kwa hiyo, sisi tukasema hii ni *call* kwa ajili ya nchi, tunaomba mfanyeni kwa viwango na malipo wanayolipwa yamepitishwa na *Standing Orders* kwa utaratibu maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatujaanza leo kuwa na hizi Tume, tumewahi kuwa na Tume ya Kukusanya Maoni kutoka Chama Kimoja kwenda Vyama Vingi, tumewahi kuwa na Tume ya ku-*fast track East Africa Community* kwenda kwenye *Political Federation,* hebu tuangalie Tume mbalimbali zimekuwa zinalipwa shilingi ngapi halafu tuangalie Tume ya Mabadiliko ya Katiba inalipwa shilingi ngapi? Pale ndipo tuta-*justify* kama wanalipwa fedha nyingi ama hawalipwi lakini utaona wanajitolea kwa maslahi ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Watanzania wajue kwamba posho wanayolipwa Wajumbe wa Tume kwa kweli ni kwa kujitolea. Kwa sababu taarifa hizi zipo wazi wala

siyo za kificho angalieni Tume mbalimbali zimekuwa zikilipwa kiasi gani ukilinganisha na Tume mbalimbali ambazo zimeshakuwepo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema kwamba Tume imekuwa inachukua maoni katika baadhi ya maeneo, inapofika kwenye Wilaya inachukua Kata kadhaa. Ni kweli tungetamani iende kwenye Kata zote. Kutokana na bajeti tuliyowapa, kwa kweli ni vigumu kufika katika Kata zote.

Aidha, katika kufanya tafiti au kukusanya maoni tunafanya *sampling,* kuna *purposeful sampling*, *snow ball sampling, random sampling* na kuna wasomi wengi hapa, sasa leo tunataka Watanzania milioni 45 wote wakatoa maoni, sijui hiyo ripoti itakuwaje? Huwa tunafanya *sampling*! Kwa hiyo, maudhui ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa kweli yapo sawasawa na sheria hii ililetwa Bungeni na tulijadili Wabunge wote 357. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la elimu, sisi Wabunge tukipitisha sheria hapa lazima tukawaelimishe watu wetu, tukawape *feedback* iwe ni bajeti, iwe sheria, ni jukumu letu. Tulipopitisha hii sheria tena tukasema isije *under certificate of urgency,* tukaambiwa twende tukawape elimu watu wetu Majimboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa kutoa elimu ilikuwa ni jukumu la Wabunge, Taasisi za Kidini, *NGO's* na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Vyama vya Siasa. Leo hii Dkt. Asha-Rose Migiro akiwasiliana na wanachama wa CCM au Nape anaambiwa kwa nini umewasiliana na wanachama wako, hiyo sijapata kuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeruhusu Vyama visajiliwe, leo hii tuna vyama 18 vilivyosajiliwa, kila chama kina utaratibu wake. Kwa hiyo, mimi ninasema *big up* Nape, *big u*p Dkt. Asha-Rose Migiro muwasiliane na mkishindwa hiyo kazi, tutasema mtupishe wataingia wengine. Kwa hiyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo suala wanalosema wadau kwamba Mabaraza yamechukuliwa wanaCCM. Mimi sielewi, Tanzania *population* ni milioni 45 leo hii tukisema tufanye *statistics* wanaCCM ni wengi, haikwepiki na ndiyo maana humu Bungeni CCM ni wengi maana yake waliotupa ridhaa huko nje CCM ni wengi. Sasa unashangaa nini kuona Mabaraza CCM ni wengi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesema twende tukashindane, sasa mwenzio anakimbia wewe unasema mshike huyo, rudi nyuma. Leo kuna Vyama vinasajiliwa, tumeruhusu. Sasa hivi kuna vyama 18 vilivyosajiliwa, Chama kitachokuwa kimesajiliwa leo, *followers* wake hawatafanana na Chama kilichosajiliwa miaka ya nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuliposema wakachaguliwe wajumbe, wala hatukusema watokane na vyama, wanachaguliwa Watanzania wajumbe kwenda kwenye Mabaraza na uchaguzi huo umefanyika wazi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaunga mkono hoja hii asilimia mia moja na suala hili la Katiba lije haraka na lifuate muda unaostahili. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Nadhani ni kengele ya kwanza, tunaendelea. *(Makofi)*

**SPIKA** Naona ni kengele ya pili imeishagonga tayari.

Waheshimiwa Wabunge, tutakaporudi, tutakuwa na wachangiaji wachache na hii Wizara ni ya siku moja kwa hiyo tutakuwa tunamaliza. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipokuwa tumesitisha Shughuli za Serikali mchana, nilikuwa nimwite Mheshimiwa Anna Abdallah, atafutiwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri halafu mtoa hoja. Mheshimiwa Anna Abdallah!

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria. Awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na kueleza kwamba asubuhi hukuwa umepata taarifa hii ya Upinzani hapo Mezani, lakini baadaye ukatuambia kwamba umeipata. Sisi wengine tumeipata alipokuwa anachangia mtoa hoja wa mwisho ule mchana. Kwa hiyo, imebidi tufanye kazi kweli ya haraka haraka kuisoma. Sasa nafikiri, tuelezane wazi kwamba tabia hii sio nzuri, hizi taarifa inabidi tuzipate wote mapema, tupate nafasi ya kuzisoma ili tuweze kuchangia vizuri.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi niliposikiliza pale hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani tangu mwanzo mpaka mwisho wa hotuba yake amezungumzia habari ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba mpaka pale mwisho aliposema na hayo mengine yaliyoko humo basi yachukuliwe, baada ya kitabu kukipata nikaanza kuangalia nikasema alaah, kumbe alikuwa na mengine ya kusema. Mimi nilidhani alikuwa na hilo tu moja la Tume ya Katiba. Nataka niseme kwamba wanatunyima na wanawanyima Watanzania haki ya kujua yale yote yanayosemwa na Kambi Rasmi ya Upinzani kwa sababu tu ya kuchelewa kutupa hivi vitabu.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kusema hayo, naomba niseme, maelezo yaliyotolewa hasa kuhusu Tume hususan kumtaja binafsi Mheshimiwa Warioba, ninasema kwanza haikuwa haki na maneno yaliyotumiwa yalikuwa ni

ya kumvunjia heshima na vilevile kwa umri wake Mheshimiwa Jaji Warioba ukilinganisha na umri wa Mheshimiwa Tundu Lissu, nataka kusema Mheshimiwa Jaji Warioba anastahili heshima ya asili kutoka kwa Mheshimiwa Tundu Lissu. Kwa kweli nasema Bunge hili lisitumike kudharau watu, kunyanyasa watu, kusema maneno ya kashfa kwa ajili ya watu, tena hasa watu hawa waliotuzidi umri, mimi nafikiri hatutendi haki hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata wenzangu waliokuwa wanasema tunaunga hotuba hii mkono, nasema kama wanaunga maudhui, lakini maneno yale ya kashfa sidhani kama hata Wabunge wanawake wanayaunga mkono maneno yale. Kwa kweli si vyema kuvunjiana heshima tunapotaka kuweka pointi yoyote ili ieleweke. Tunaweza tukaeleza maelezo yetu vizuri bila hata kumkashfu mtu na yakaeleweka na yakaingia. Hivi sasa mnawakimbiza watu tu ambao pengine walikuwa wanadhani kwamba Chama hiki ni kizuri sana lakini kwa maneno ya namna hii mnawakimbiza tu watu ambao wangependa kujiunga nacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, ninaomba nijikumbushe kwamba kwa rekodi tuliyonayo, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria aliwahi kuwa Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria kwa muda mrefu tu, lakini alipokuwa yeye Katibu mambo mengi waliyopendekeza kuletwa Serikalini mpaka sasa hayajatekelezwa. Sasa natarajia kwamba maadam yeye sasa ndio yuko kwenye chungu basi yale yaliyoshindikana wakati yeye akiwa Katibu kule kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria yaletwe Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nazungumzia hususan Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971. Sheria ya Ndoa imetolewa taarifa na nina hakika na Tume ilizunguka sana kupata maoni ya watu na taarifa yao ipo tulikwisha kuisoma. Sheria ya Ndoa inaruhusu mtoto wa miaka 15 kuolewa kwa ridhaa ya mzazi ama mlezi lakini Sheria ya Mtoto tafsiri ya mtoto ni mtoto wa miaka 18, lakini kwa Sheria ya Ndoa inavunja hata Sheria ya

Bunge yenyewe iliyoweka tafsiri ya mtoto. Mtoto wa miaka 15 anaweza kuolewa eti kwa ruhusa ya mzazi lakini mtoto huyu wa miaka 15 akibakwa ni kesi lakini akibakwa kwa ruhusa ya wazazi wake sio kesi. Sheria hii moja inawezaje kuruhusu kubakwa halafu hapohapo inaruhusu mtu mwingine atoe ridhaa ya mtoto wake kubakwa? Mimi nafikiri huku ni kutokumtendea mtoto wa kike haki, mtoto wa kike wa miaka 15 ni mtoto mdogo sana, hana uwezo kabisa wa kufikiri wala kubeba majukumu ya unyumba, iwe kwa ruhusa au bila ruhusa, hii ni kinyume kabisa cha haki ya mtoto. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, alilishughulikia hili tunaomba alete hapa Bungeni kurekebisha jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia juu ya Wabunge wa Viti Maalum. Katiba ya Nchi inaweka aina ya Wabunge. Wako Wabunge kutoka kwenye Majimbo, wako Wabunge wa Kuteuliwa na Rais, wako Wabunge waliotokana na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, yuko Mwanasheria Mkuu halafu wako Wabunge wa aina ya Viti Maalum. Mle ndani ya Katiba haijasema kwamba Wabunge wa Viti hivi watakuwa hivi, isipokuwa sheria ndio zimefafanua. Sheria ya kwanza ya ubaguzi kabisa ambayo nina hakika kabisa kwamba Tume ya Kurekebisha Sheria itaiangalia, ni kule kusema Mbunge yeyote mwingine isipokuwa wa Jimbo tu ndio anaweza kuwa Waziri Mkuu, huu ni ubaguzi kwa sababu tunao akinamama ambao wana uwezo mkubwa tu lakini hawakutoka kwenye Majimbo. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ubaguzi wa pili, Wabunge wa Viti Maalum hawapewi zile fedha kwa ajili ya kuendeleza Majimbo kwa maelezo kwamba ile fedha ni kwa ajili ya Majimbo. Sasa kwa nini Katiba ikaweka aina nyingine za Wabunge kama hili jambo lilikuwa hivyo? Ni matumaini yangu kwamba jambo hili sasa litaangaliwa na nina hakika kabisa huko tunakokwenda na hasa kwa kupitia Tume hii, jambo hili litarekebishwa.

Mheshimiwa Spika, ambalo nataka kulisemea ni

namna ya kumpata Mbunge wa Viti Maalum. Wabunge wa Majimbo wanaeleweka wanavyopatikana, Wabunge kutoka Baraza la Wawakilishi wanajulikana jinsi watakavyopatikana, wanaoteuliwa na Rais inajulikana atakavyowateua lakini cha kusikitisha kabisa katika Viti Maalum ni kwamba Wabunge wa Viti Maalum ambao ni wanawake hawakuwekewa utaratibu ukiachia ule tu unaosema kila Chama kitapata kutokana na uwiano wa kura walizozipata kwenye Uchaguzi Mkuu, hakuna utaratibu wa namna ya kuwapata. Kwa hiyo, kila Chama kimeweka utaratibu wake na mnawafanya sasa hivi wanawake wawe kama ni miliki ya vyama vya siasa. Hili halifahi, hakuna mtu anayemmiliki mwenzake hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunataka sheria itungwe hata kama mnasema mtangoja Katiba, tunataka utaratibu wa kisheria ambao kila chama utaufuata, mtu anayechaguliwa achaguliwe sio kwa mapenzi ya mtu na wala sio kwa matakwa ya mtu au ya chama chake, achaguliwe kwa sababu amechaguliwa hata kama ni kwa Viti Maalum. Kwa hiyo, tunapenda kabisa kwamba jambo hili lisahihishwe kwa sababu linadhalilisha baadhi ya Wabunge wanawake hasa Wabunge vijana wanawake. Kwa hiyo, napenda jambo hili lisahihishwe liwe mwisho kabisa kama tulikosea huko nyuma tulikosea lakini lazima utaratibu wa kuwapata Wabunge hawa uwekwe vizuri na iwe utaratibu wa kisheria na ikiwezekana hao akinamama wote wakachaguliwe ili na wenyewe basi mtindo wa kuwabagua kwamba hawawezi kupata hiki na kile, hawezi kuwa Waziri Mkuu litakuwa limekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini suala la kuwa na hakika ya kuwa na akinamama ndani ya Bunge hili, hilo ni lazima lizingatiwe. Piga ua, akinamama ni asilimia 51.1 ya watu wote wa nchi hii. Sasa hivi huko tunakokwenda tunahitaji uwakilishi wa nusu kwa nusu. Tunachohitaji ni utaratibu utakaofanywa ili akinamama hawa waingie katika Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninasema kwa tafrani

zinazotokea humu Bungeni za maneno na mipasho na kadhalika, kama Wabunge akinamama wasingekuwemo humu ndani ya Bunge, sijui kungekuwaje? Mimi nataka kusema Wabunge wanawake ni mhimili wa amani humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanasemwa wamenyamaza, mara wasemwe hili tunanyamaza, kila jambo linalosemwa kuhusu mwanamke humu ndani tungesimama wote, ingekuwa tafrani kubwa sana. Mimi napenda kuwapongeza akinamama, tuendelee na moyo huo, sisi ni mhimili wa amani... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri...

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 68(7) kwenye Kanuni zetu za Bunge, sina sababu ya kukisoma kwa sababu kifungu kile kinaeleweka vizuri 68(8) kuhusu Mwongozo.

Mheshimiwa Spika, kama alivyorejea kusema Mheshimiwa Anna Abdallah kwamba kulikuwa na sababu za kupata kitabu hiki mapema lakini bahati mbaya hatukukipata mapema. Mimi nilivyokipata, nimejaribu kusoma lakini ukisoma labda kitabu cha wengine Mheshimiwa Spika, cha kwangu hakina ukurasa wa 19, kiko wazi, kiko *blank* hapo kwenye ukurasa wa 19 lakini pia ukurasa wa 26 hakuna kitu yaani zimerukwa.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo ninaotaka kuomba,

je, kama kurasa hizo zinazo-*miss* ziko taarifa ambazo zimeandikwa inawezekana sio nzuri sana na zingepaswa labda ziondolewe kama tungekuwa tumeziona, lakini hazipo katika kumbukumbu zetu za *Hansard* kipi kinachoenda hiki au kile ambacho kimerukwa baadaye wanaweza wakasema wanataka kukirudisha kiwe ni kumbukumbu za kudumu za Bunge. Kwa sababu pia ukisoma ukurasa wa 27 pale, kuna maneno ambayo yanakuwa kama ya uchochezi kiwango fulani, kwenye *paragraph* ya pili ukurasa 27. Sasa nina wasiwasi na hizo kurasa zinazo-*miss* na ndiyo nasema naomba Mwongozo wako kitabu hiki kwa kuwa na upungufu huo unaelekeza nini?

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo.

**SPIKA:** Sawa. Tutakaa kwenye Kamati ya Kanuni kuweza kuweka utaratibu ni wakati gani taarifa zinazopaswa kuwekwa hapa Mezani ziwe zimemfikia Spika si wakati wa asubuhi ingawa Kanuni ya 99(5) inaelekeza kwamba zile *documents* zinazowekwa Mezani ziwepo kwa Spika.

Kwa hizo kurasa unazosema naona kama labda wachapaji waliruka, ndio sasa zinasambazwa lakini ni kweli kwamba kumekuwa na kuleta taarifa ki-*pressure, pressure* namna hii, nadhani hili tutalirekebisha katika siku zijazo.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SAID SULEIMAN SAID:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni juu ya Hati ya Muungano. Wakati Watanzania tumo katika mchakato wa kuandika Katiba Mpya, bado kuna kiu cha kutofahamika ilipo Hati ya Muungano iliyosainiwa na Waasisi Wakuu wa zile zilizokuwa Dola Mbili Huru; yaani Mwalimu Nyerere kwa Dola ya Tanganyika na Mzee Karume kwa dola ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naungana na wale Watanzania wenzangu waliotangulia kutaka kujua ni wapi ilipo Hati ya Muungano? Kuna wapo waliothubutu kwenda Mahakamani mwaka 2007 kuidai Hati kama ipo basi ioneshwe hadharani.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar alipoitwa Mahakamani alisema hata yeye hajawahi kuiona hati hiyo na akawataka walalamikaji washirikiane naye kuitafuta na kujua wapi ilipo Hati hiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed aliyewahi kuwa Waziri katika Serikali zote mbili na Katibu Mwenezi wa CCM Zanzibar, aliwahi kuuliza swali hapa Bungeni akitaka kuelezwa wapi ilipo Hati ya Muungano. Jibu alopata ni kwamba nakala moja ipo Ofisi ya Rais, Ikulu Dar es Salaam, lakini mpaka hii leo haijaoneshwa hadharani. Sasa swali langu ni kuwa, kama Hati ya Muungano ipo, Serikali zetu zote mbili zinaogopa nini kuionyesha hadharani?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ni kutokana na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83, Toleo la mwaka 2012, Sehemu ya Nne kuhusu utaratibu wa utendaji kazi wa Tume, Kifungu namba 17(4), kinachoeleza kuwa katika kutekeleza majukumu yake chini ya sheria hii, Tume itapitia na kuchambua michango, mawazo, maoni, taarifa na mapendekezo yaliyokusanywa na kufanyiwa tathmini siku za nyuma ikiwemo kifungu 17(4)(e) Hati za Muungano wa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hizi ni baadhi ya hati zilizotajwa na sheria hii kama Tume katika kutekeleza majukumu yake itazitumia katika kutayarisha rasimu ya Katiba Mpya. Hapa swali langu ni je, Tume imeshaiona Hati hiyo au imeshakabidhiwa Hati hiyo ya Muungano? Ikiwa Hati hiyo haipo, uhalali wa Muungano wetu uko wapi? Hii si inaonesha kwamba, uundwaji wa Muungano wetu haukuwa wa Kisheria na hivyo kuwa msingi wake ulikuwa mbaya tokea mapema kabisa ulipoundwa mwaka 1964.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias

M. Chikawe; Naibu Waziri wa Sheria na Katiba, Katibu Mkuu wa Wizara, Mheshimiwa Jaji Kiongozi, Mheshimiwa Jaji Mkuu, Mtendaji Mkuu wa Mahakama Alhaji Husein Katanga pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye mikakati mizuri ya kuboresha utoaji wa huduma kwa watendaji ulio bora zaidi. Nawaombea Mungu awatangulie malengo yatekelezeke vema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhaba wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo Singida, napenda kuikumbusha Serikali pamoja na Mahakama za Mwanzo chache zilizopo Mkoani Singida kwani sio Kata zote zina majengo ya Mahakama za Mwanzo, bado kuna tatizo kubwa la upungufu wa Mahakimu Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Chikawe amelieleza Bunge kuwa tayari anao Mahakimu wapya, napenda kujua kwa Mkoa wa Singida tumepewa Mahakimu wangapi ili kusaidia kuondoa mrundikano wa kesi nyingi ambazo zinahitaji kusikilizwa. Vile vile kuwapunguzia kazi Mahakimu waliopo kwani karibu kila Hakimu ana vituo viwili au zaidi. Nasubiri majibu ya Serikali ili wananchi wa Singida walionituma wasikie, pia nisiwasumbue kwenye vifungu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu majengo ya Mahakama za Wilaya zote za Mkoa wa Singida; inasikitisha sana pamoja na juhudi za kuikumbusha hapa Bungeni mara nyingi kuwa Mahakama zote za Wilaya za Mkoa wa Singida zinatumia majengo ya Mahakama za Mwanzo. Napenda kujua ni Wilaya ngapi za Mkoa wa Singida zimetengewa fedha za kujenga Mahakama za Wilaya tafadhali.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwatengenezea maeneo mazuri ya kufanyia kazi Mahakimu wa Wilaya ni kuwaongezea moyo wa kujituma. Nasubiri majibu ya Mheshimiwa Mathias Chikawe yenye kutia moyo kwa Mahakimu wa Mahakama hizi, uongozi wa Mkoa wa Singida na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Mahakama Kuu

Mkoani Singida; napenda kuleta kilio cha wananchi wa Singida ambacho hata Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba, Mheshimiwa Mathias Chikawe anafahamu vizuri. Naendelea kusikia ujenzi wa Mahakama Kuu mikoa ya wenzetu ambayo iliomba baada ya sisi wa Singida, lakini imeshatupita.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali inieleze kulikoni kucheleweshwa Mradi huu kwa kiasi kikubwa. Kosa letu ni nini ili tujirekebishe. Nasubiri majibu yenye faraja kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kutambua juhudi za Mtendaji Mkuu wa Mahakama Husein Katanga; nimeshindwa kujizuia kusema ukweli kuwa kwa muda mfupi Ndugu Husein Katanga ameonesha uwezo wa juu wa kupanga mikakati ya utekelezaji wa majukumu yake. Tatizo nililoligundua ni kwamba, Serikali haijamuunga mkono ipasavyo kwani fedha anazopewa ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuongeza fedha katika Bajeti ya Idara hii muhimu sana kwa Watanzania, nitashukuru sana kupata majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nafasi ya Wabunge Viti Maalum; napenda kuishauri Serikali kutoa ushirikiano kwa Tume ya Katiba ya Mheshimiwa Jaji Mstaafu Warioba, juu ya kuangalia dirisha lenye heshima kwa Wabunge Viti Maalum kuingia Bungeni ili ifike mahali Wabunge Viti Maalum wapate heshima na haki kama Wabunge wa Majimbo. Suala hili lichukuliwe kwa uzito wa pekee.

Mheshimiwa Spika, kuhusu posho za wazee wa Mahakama; pamoja na Serikali kuendelea kutangaza posho za wazee wa Mahakama, lakini bado kiwango ni kidogo sana. Ni vema sasa kiangaliwe kiwango ambacho kitadumu muda mrefu na kiwe kiwango cha kuwafanya wasinunuliwe au kushawishika na rushwa ambayo ni adui wa haki.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nimalizie kwa

kuwapongeza Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri mwenye dhamana na Mheshimiwa Angellah Kariuki, Naibu Waziri kwa mshikamano wao mzuri ambao umeongeza ufanisi ndani ya Wizara hii ya Katiba na Sheria. Hivyo, naunga mkono hoja hii Mungu awatangulie.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongezewa fedha Wakala wa Vizazi na Vifo *(RITA)*; napenda kutoa niliyonayo moyoni kuhusu kitengo hiki cha vizazi na vifo *(RITA)* kwamba Taasisi hii inayo Mtendaji Mkuu chapakazi na mwadilifu mno na amejitahidi kutekeleza wajibu wake wakishirikiana na wasaidizi wake, bali bado hajafanikiwa vizuri kwa sababu fedha anazotengewa kila Bajeti ni ndogo mno, zinampa nafasi finyu ya kwenda mikoani ndiyo maana asilimia ya usajili wa watoto chini ya miaka mitano bado ni mdogo sana na kuna Mikoa kama Mbeya, Shinyanga, Simiyu, Geita na Mwanza bado uko chini sana.

Mheshimiwa Spika, hata Singida bado watoto wengi wanahitaji kusajiliwa. Ningependa kujua Serikali itafanya jitihada za kuwaongezea fedha Wakala wa *RITA* ili wasiendelee kukaa ofisini wakati kazi ziko mikoani, tusiwavunje moyo watendaji kama hawa wenye ari ya kazi. Nasubiri majibu ya Serikali yenye afya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ya uandikishaji wa Vizazi na Vifo kufanyiwa marekebisho; nimeona ni vema kuikumbusha Serikali kuwa Sheria ya Uandikishaji wa Vizazi na Vifo imepitwa na wakati. Hivyo, napenda kujua ni lini Serikali italeta Muswada huu hapa Bungeni ili tuweze kuifanyia marekebisho. Ni vema iwe ni Sheria kuwa kila anayesoma awe na cheti cha kuzaliwa, anayeomba kazi, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia kuondoa adha pale kijana anapopata nafasi ya kwenda kusoma au kufanya kazi nje ya nchi kupata *Passport* bila shida. Hivyo, sheria ifanyiwe marekebisho kila kijana awe na cheti cha kuzaliwa. Nasubiri maelezo yenye kuonesha uzito wa suala hili.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu

ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Kawe; kwa miaka mitatu mfululizo, Serikali imekuwa ikiahidi mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, itajenga upya Mahakama ya Mwanzo kutokana na ile ya awali kuwa gofu hali iliyopelekea mashauri yote kusikilizwa katika Ofisi ya Mtendaji Kata. Hali inayosababisha usumbufu mkubwa! Naomba kupata kauli ya mwisho kutoka Serikalini kwa maana ya Wizara ya Katiba na Sheria. Ni lini, Mahakama hiyo itajengwa na kwa gharama kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchakato wa Katiba, nitazungumzia mambo mawili:-

Kwanza, idadi ya wananchi waliochangia/toa maoni ya Katiba; wakati tukiwa katika mchakato muhimu wa Katiba kumekuwa na sintofahamu nyingi juu ya ushiriki wa wananchi. Naomba Serikali iliambie Bunge hili Tukufu, mpaka sasa tukiwa tunaelekea katika mchakato wa Baraza, ambapo Tume itatoa Rasimu kwanza ya Katiba ili Mabaraza yajadili kama ilivyoelekezwa na kifungu 18 (2).

Pili, kuhusu Bunge la Katiba; kwa mujibu ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, sura 83, Toleo la mwaka 2012, kifungu namba 29(1) na (2) gharama za Bunge maalum la Katiba zitalipwa kutokea Mfuko Mkuu wa hazina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, taarifa ambazo zimewasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu, kupitia Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ambayo ndio ina jukumu la kupitisha Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, ambayo pia fungu la Tume ya Mabadiliko ya Katiba iko ndani yake, hazioneshi fedha hizo ziko wapi na ni kiasi gani ambacho kimetengwa kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *The Law School of Tanzania*; kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu sana kutoka kwa wanafunzi wa Taasisi ya Sheria kwa vitendo (*The Law School of Tanzania*) kutokana na kutowepo kwa utaratibu unaoeleweka utakaotoa fursa kwa wanafunzi

waliomaliza Shahada ya kwanza ya Sheria kukopa toka kwa Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, hii inatokana na ukweli kwamba, Sheria iliyounda Bodi ya Mikopo haiwatambui. Utaratibu pekee uliopo ni kwa Wizara ya Sheria na Katiba kwa kutumia mafungu yake na kwa vigezo inavyovijua yenyewe kutoa ufadhili/msaada/mkopo kwa wanafunzi wa *Law School*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hoja hii imejadiliwa kwa kipindi kirefu sana, naomba Serikali iliambie Bunge hili Tukufu ni lini Serikali itawasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ili kuwezesha uwepo wa mfumo ulio wazi na huru kwa wanafunzi wote wenye sifa za kupata mkopo.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio mwisho kwa umuhimu, naomba kupata kauli ya Serikali juu ya mchakato uliomalizika hivi karibuni, wa Mabaraza ya Katiba ambao umelalamikiwa sana na wadau wengi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa Hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Mahakama zote hapa nchini zimekithiri kwa rushwa. Haki za Watanzania wengi maskini zinapotea kwa sababu ya rushwa. Mahakimu wengi wamefanya Mahakama ni *deal*/kesi za wanyonge ni mtaji wa kupata fedha. Hii ni hatari kubwa sana kwani Mahakama ni eneo pekee ambapo mwananchi anategemea kupata haki yake. Serikali ina mpango gani mahususi kuondoa rushwa kwenye chombo hiki muhimu?

Mheshimiwa Spika, kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu kwenye Ofisi za Serikali kuanzia ngazi za Vijiji, Kata, hadi Wilaya.

Watendaji wa Vijiji na Kata wametumia nafasi zao kuwakamata wananchi wanaochelewa kutoa michango ya maendeleo na kuwafungia kwenye Ofisi za Vijiji na Kata kwa zaidi ya siku tatu (3) hadi siku saba (7), wanachanganywa wanawake na wanaume.

Mheshimiwa Spika, mfano halisi Kata ya Sungwa, Tarafa ya Uliyankuru, Wilaya ya Kaliua kila leo wananchi wananyanyaswa. Nimeongea na Mkurugenzi wa Urambo juu ya jambo hili, lakini bado tatizo linaendelea. Serikali ieleze Bunge ni Sheria gani inaruhusu Ofisi za Vijiji na Kata kutumika kama mahabusu?

Mheshimiwa Spika, mahabusu za Polisi zimekuwa zikikiuka taratibu na Sheria na kuweka watu mahabusu bila chakula na mbaya zaidi wanakaa kule siku nne (4) hadi wiki moja. Sheria inasema ndani ya masaa 48 mahabusu afikishwe Mahakamani. Kituo cha Polisi Usinge, Kaliua; Ulyankuru, Wilaya ya Kaliua wanawaweka watu pale wiki nzima hadi siku kumi na nne (*14 days*) halafu wanawaachia bila hata kuwafikisha Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu haki za watoto; Tanzania tumesaini Mkataba wa Haki za Watoto tarehe 1 Juni, 1990 na kuridhia 1991. Pia tumesaini mkataba wa Afrika juu ya Haki za Watoto mwaka 2003. Bado matukio mengi ya kukiukwa kwa haki za watoto hapa nchini yanaongezeka kila leo. Watoto wanabakwa, wanalawitiwa, wanapigwa, wanachomwa kwa moto katika maeneo mbalimbali ya miili yao. Hata watoto wa mitaani wameongezeka kutokana na kuongezeka ukatili kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado haijaweka utaratibu makini wa kukomesha ukatili kwa watoto. Kesi zinazohusu ukatili wa watoto bado zinachelewa sana wakati huu watuhumiwa wako mitaani wanaoendeleza vitendo vibaya kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, lipo dawati maalum kwa ajili ya

watoto, lakini bado halijatoa suluhisho la kudumu kwani watendaji wanachukua rushwa na kuficha ukweli.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali haiweki kitengo maalum cha Mahakama/Mahakama ya dharura kushughulikia kesi zote zinazohusu haki za watoto ili haki zao zipatikane kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, Tume ya haki za binaadamu inafanya kazi nzuri sana, lakini hawawezeshwi na Serikali kuwa na rasilimali za kutosha kutimiza wajibu wake kwa ufanisi. Serikali ituambie kwenye Bajeti hii ni Ofisi ngapi za Tume zitafunguliwa kwenye Mikoa na Wilaya hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, Tume ipatiwe vyombo vya usafiri waweze kwenda vijijini kusaidia wananchi wanaonyimwa haki zao. Wapatiwe Wanasheria wa kutosha (*Manpower)* kushughulikia masuala wanayoyaibua kwenye jamii. Tume ipatiwe fedha za kukaa vijijini kuchunguza kesi wanazokutana nazo. Suala la uchunguzi linahitaji muda na pesa ili haki iweze kupatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, zipo kesi zimekaa Mahakamani miaka zaidi ya kumi (10). Mashahidi wa kesi hizo wanafariki, watuhumiwa wanafariki bado kesi ipo Mahakamani. Serikali iweke utaratibu wa dharura wa kuhakikisha kesi zote zilizokaa Mahakamani zaidi ya miaka kumi (*10 years*) zifanywe kwa dharura kwa muda maalum, ziishe haki za watu zipatikane kwani wamechoka kusubiri haki zao na wengine wamekata tamaa. Siyo haki ni ukiukwaji wa haki kwa wakati.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, naungana na maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi na vyumba vya Mahakama; kutokana na kuongezeka kwa idadi ya Majaji, Mahakimu na watumishi wengine Ofisi za Majaji na Mahakimu (*Chambers*) hazitoshi. Mahakimu wanashirikiana maofisi kama makarani. Serikali ikope fedha popote kuongeza

majengo ya Mahakama. Katika mchango wangu wa 2011/ 2012 na 2012/2013 nilisema haya, sijui kama Serikali ilipokeaje?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mabaraza ya Ardhi; hakuna sababu ya kuwa na Mabaraza haya, Mahakama inatosha. Mabaraza haya yafutwe, iwapo mashauri ya ardhi yenye thamani zaidi ya shilingi milioni 50 yanafanyika Mahakama Kuu kwa nini ya chini hapa yasifanyike katika Mahakama za chini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Tele-justice*; Mradi utakaoiwezesha Mahakama kuendesha mashauri na kurekodi mienendo ya kesi kama ilivyo *Hansard* ili kuharakisha kumaliza mashauri kwa muda mfupi. Kama mradi wa nchi ya China unakuwa mgumu, kitafutwe chanzo nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya Mawakili; kwa uwakili ni fani inayohitaji mafunzo ya vitendo ya kina, naona mafunzo yanayotolewa na *Law School* hayatoshi kwa ajili hiyo nashauri Ofisi ya *AG* iwe ndiyo inayotoa mafunzo ya vitendo kama ilivyokuwa huko nyuma (*in order to avoid compromising legal professional standards*).

Mheshimiwa Spika, kuhusu muda wa kukaa Mahakamani; Mahakimu au Majaji kama hawatafanya kazi wasiwaweke watu bure Mahakamani, shauri liahirishwe mapema.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa kuzungumzia mambo makuu mawili; ucheleweshaji wa kesi na upungufu wa wafanyakazi katika ngazi ya Wilaya na Mkoa (Wanasheria – *State Attorneys*).

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukishuhudia idadi kubwa ya mahabusu hata kwa wale wenye kesi zenye kupewa dhamana, lakini wanapelekwa gerezani, hivyo, kupelekea mrundikano wa Mahabusu gerezani, mfano

gereza la Wilaya ya Tarime ambalo hupokea watu toka Wilaya mbili Tarime na Rorya.

Mheshimiwa Spika, gereza hili la Tarime lina mrundikano mkubwa wa Mahabusu ambao wengi wao ni wenye kesi zenye dhamana lakini wananyimwa kwa sababu za upungufu wa maadili kwa watendaji wa Mahakama. Vile vile kumekuwepo na ucheleweshaji mkubwa wa kesi na hata zile zisizo na ushahidi. Ikizingatiwa *nature* ya kesi wapewazo wananchi wa Tarime/Rorya ambapo kwa kiasi kikubwa ni ubambikaji wa kesi unaofanywa na Jeshi la Polisi kwa maslahi binafsi na sio ya umma.

Mheshimiwa Spika, kuna kesi mtu/watu wamekamatwa kwa kosa la jinai, lakini ghafla unaombwa fedha (rushwa). Mara wakosapo hubadilishiwa kesi na kuwa *Armed Robbery /murder* kitu ambacho si haki na ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambapo inatuambia kila raia ana haki ya kuishi na kutenda kazi ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni wakati muafaka sasa Wizara ikemee kitendo hiki/hivi na kuhakikisha kesi zote zenye kutoa/pewa dhamana zipewe. Zile ambazo hazina basi upelelezi ufanyike haraka, maana kesi nyingi Tarime/Rorya ni za kisiasa ambapo watu hubambikwa kesi.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo hupelekea kesi kuchelewesha ni kuchelewa kwa upelelezi pamoja na upungufu wa wafanyakazi wenye kutoa haki za kisheria (Mahakimu na Mawakili) ni wachache sana ambao hawakidhi mahitaji na hivyo kupelekea ucheleweshaji wa kesi. Vile vile kuna upungufu wa majengo (Mahakama za Mwanzo), Mahakama Kuu, Ofisi ni duni/chakavu ambazo hazina hata vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba uwezekano wa kujengwa Mahakama katika Wilaya ya Rorya pamoja na gereza ili kuweza kupunguza mrundikano wa mahabusu/ wafungwa katika gereza la Tarime kitu ambacho kinaweza kupelekea maambukizo ya magonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu suala la upatikanaji wa Katiba mpya Tanzania. Katiba ni suala la Watanzania wote, Katiba sio suala la Vyama vya Siasa Katiba. Suala la upatikanaji wa Katiba mpya bado halijakaa sawa. Kuna malalamiko kwa makundi yaliyo pembezoni kwa mfano, walemavu, wanawake na hata Watanzania wasiojua kusoma na kuandika bado hawajaelimishwa kuhusu Katiba mpya. Ni kwa nini Serikali isiongeze muda wa kutosha ili tupate Katiba iliyokuwa bora na ambayo imewashirikisha Watanzania wote?

Mheshimiwa Spika, suala la Mahakama na kero mbalimbali zinazozikabili Mahakama zetu. Mahakimu wengi wanafanya kazi katika mazingira magumu, majengo mengi ya Mahakama ni chakavu, pia kuna mrundikano wa kesi za muda mrefu ambazo zinasababishwa na Bajeti ndogo ya Wizara hii. Ni lini Serikali itahahakikisha Wizara hii ya Katiba na Sheria inatengewa fedha za kutosha ili kukarabati majengo ya Mahakama kama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya, na kadhalika na kununua vifaa vya kisasa?

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Watanzania ambao wanafikisha kesi zao Mahakamani hasa walio pembezoni aidha, wameshtaki au wameshtakiwa baadhi yao hawajui Sheria, vile vile hawana uwezo wa kuweka mawakili. Wengi wamekuwa wakidhulumiwa haki zao kwa sababu hawajui Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hukumu zote za kesi zinazotetewa na Mahakama zinatolewa kwa Lugha ya Kiingereza na baadhi ya Watanzania hawajui Kiingereza. Ni lini Serikali itahakikisha hukumu zote zinazotolewa na Mahakama zinatolewa kwa lugha ya Kiswahili?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mawakili wa Serikali; baadhi ya Mawakili wa Serikali wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu. Vile vile hata kuhatarisha

maisha yao wamekuwa wakiendesha (kusikiliza) kesi za mauaji na kadhalika, lakini cha kushangaza Mawakili hawa wa Serikali wanapomaliza kesi Mahakamani, wanatumia usafiri wa daladala kwa sababu hawana usafiri wao binafsi. Ni lini Serikali itaboresha maslahi ya Mawakili hawa wa Serikali kwa mfano, vitendea kazi, makazi bora ya kuishi (kisasa) na kadhalika?

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, Dola imejengeka kwa mihimili mitatu (3) ambapo ni Bunge, Serikali na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Bunge kazi yake moja ya Kikatiba ni kutunga Sheria na Serikali wajibu wake ni kuzitekeleza Sheria hizo. Kutunga Sheria ni suala moja na utekelezaji wake wa Sheria hilo ni jambo lingine.

Mheshimiwa Spika, haifanani hata kidogo Serikali kutozitekeleza baadhi ya Sheria wakati Miswada ya Sheria hizo inatoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Bunge la tisa (9) kwenye Mkutano wake wa Aprili mwaka 2013 ilitunga Sheria mbili zinazohusiana na Sekta ya Mifugo. Sheria hizo ni Sheria namba 12 ya mwaka 10 inayoitwa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji ya mwaka 2010 (*Time Live Stock Identification Registration and Traceability* Act 2010) na Sheria ya pili ni Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula na Mifugo Namba 13 ya mwaka 2010 (*The Grazing Land and Animal Feed Resources*).

Mheshimiwa Spika, Sheria mbili hizo ni muhimu mno kwa ufugaji bora na uhifadhi wa mazingira yetu. Bahati mbaya mpaka leo karibu miaka mitatu (3) Sheria hizo hazijatekelezwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho anieleze kwa nini Sheria hizo hazijatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna mrundikano

mkubwa wa mashauri katika Mahakama zetu katika daraja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mahakama Kuu ya Divisheni ya Ardhi ilichukua mashauri ya zamani na ya sasa, jumla 5393 ambayo kwa kasi ya sasa ni mashauri 427 ndio yaliyotatuliwa. Kwa kasi hiyo mashauri 5393 yatachukua miaka sita (6) na miezi mitatu (3). Hali hiyo inatisha! Ipo haja hatua maalum zichukuliwe ili kuongeza kasi ya kuyatatua mashauri yaliyoko Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, mashauri yaliyoko Mahakamani, Mahakama za Hakimu Mkazi hivi sasa ni 25,370 na uwezo ni mashauri 612 kwa miezi sita. Ili kuyamaliza mashauri 25,370 itakuwa muda wa miaka 20 na miezi saba (7) bila ya kuongezeka mashauri mengine.

Mheshimiwa Spika, ipo haja Serikali iziwezeshe Mahakama ili mashauri yaliyoko Mahakamani yaweze kupata ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. DESDERIUS JOHN MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Elimu juu ya Katiba ya Nchi ni muhimu, Wananchi wengi hawana uelewa wa kutosha juu ya Katiba ya Nchi yao ambayo ni Sheria Mama na muhimu kwa kila raia kuwa na uelewa wa kutosha. Nashauri pamoja na kuwepo kwenye masomo kama *topic* au mada mojawapo, tutenge fedha za kutosha kuhakikisha kunakuwepo makala za mara kwa mara za rejea ama kila wiki au kila mwezi. Vilevile Katiba iwe inapatikana hivi sasa, Katiba ilikuwa bidhaa adimu hadi pale tulipoanza kuandika Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, zimetungwa Sheria ili sote tuzifuate lakini Sheria ya Rushwa inavunjwa kwa kiwango kikubwa na wasimamizi wa Sheria Mahakamani na Polisi. Ni vizuri kumaliza dosari hii. Lazima vyombo hivyo viwe na utaratibu wa kuheshimu Sheria wanazosimamia ama Wizara zinazohusika wahakikishe stadi au *research* zinafanyika kujua

sababu ili kumaliza dosari hii. Wilaya ya Nkasi hatuna Mahakama ya Wilaya kwa maana ya Jengo na Hakimu pia.

Mheshimiwa Spika, zoezi la Katiba linaenda vizuri na madai ya Wabunge hasa wa CHADEMA ni kuogopa kivuli chao tu, hapajakuwa na dosari kubwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wajumbe wa Tume wasipangwe kwenda kufanya kazi maeneo wanayotokea, wapangwe sehemu nyingine ili kuleta ufanisi.

**MHE. UMMY ALLY MWALIMU**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, kwa kusimamia vyema utekelezaji wa mipango na malengo ya nchi katika utoaji haki, kusimamia Utawala wa Katiba na Sheria Nchini. Hata hivyo, ningependa kupata maelezo katika masuala yafuatayo:-

Je, ni lini tafrisi ya Kiswahili ya Sheria ya Mtoto Namba 21 ya 2009 itakamilika?

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Mtoto mwaka 2009 kwa lengo la kulinda na kukuza haki za mtoto Nchini kwetu. Hata hivyo, bado jamii haina uelewa wa Sheria hii kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uelewa mdogo wa Lugha ya Kiingereza, ambayo ndiyo imetumika kutengeneza Sheria hii. Hivyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri anipatie majibu ni lini Sheria hii itatafsiriwa kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili ili iweze kueleweka vizuri na Wananchi hasa walio vijijini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ndoa, Mirathi na Sheria nyingine Kandamizaji Dhidi ya Wanawake; ni lini mchakato wa kuzifanyia marekebisho utakamilika?

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), aya ya 186(f), inaelekeza Serikali kuzifanyia marekebisho Sheria za Mirathi na zile zinazooenekana kuwakandamiza Wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usipopingika kuwa uwepo wa Sheria za Mirathi (za kimila) na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, bado wanawake wengi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo haki ya kurithi mali, toka kwa wazazi au waume pale wanapofariki. Sheria ya Ndoa inayoruhusu mtoto wa kike wa umri wa chini ya miaka 18 kuolewa inadidimiza jitihada za nchi katika kumpatia elimu mtoto wa kike, kupunguza vifo vya wanawake wajawazito na pia jitihada za kumkomboa mwanamke kiuchumi. Hivyo, hakuna ubishi kuwa Wanawake wa Tanzania wangependa sasa kupata kauli ya mwisho ya Wizara ni lini Sheria za Mirathi, Sheria za Kimila na Sheria ya Ndoa zitaletwa Bungeni ili ziweze kufanyiwa marekebisho na hivyo kuwezesha kulinda na kukuza haki za wanawake na wasichana nchini?

Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengewa kwa mwaka 2013/2014 kwa ajili ya mpango wa kusajili watoto chini ya umri wa miaka mitano? Kwa mujibu wa *TDHS - Tanzania Demographic and House Hold Survery* ya mwaka 2010, inaonyesha kuwa ni asilimia 16 tu ya watoto wa umri wa miaka mitano waliosajiliwa na Mamlaka husika na kati ya hao ni asilimia nane tu waliopata vyeti vya kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, hali hii hairidhishi kabisa, ni lazima tuongeze jitihada katika suala hili. Hivyo, ninaomba Wizara ilieleze Bunge lako Tukufu ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Kusajili Watoto Chini ya Umri wa Miaka Mitano kwa Mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAWA ABDULRAHMAN GHASIA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pia napenda kuipongeza Wizara kwa kuanzia na Waziri pamoja na Viongozi wote ambao wanaunda Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, majengo ya Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara hayaridhishi; kwanza, eneo yalipo siyo mazingira mazuri kufanyia kazi hata kidogo na majengo yenyewe yana nafasi finyu tena yapo kajificheni. Ningependa

kufahamu kama kuna mkakati wowote wa kujenga majengo mapya ya kisasa na kwenye mazingira wezeshi kwa shughuli muhimu kama za Mahakama kutoa haki.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida ni vizuri mfanyakazi yeyote kupongezwa pale anapofanya vizuri ili kumtia moyo wa kuendelea kufanya vizuri na hivyo kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ni utaratibu kwa Watumishi wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama kupewa Tuzo na Nishani kama ishara ya kuthaminiwa mchango wao kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, sijawahi kuona hata siku moja Watumishi wa Mahakama wakipongezwa kupitia Siku ya Wafanyakazi Duniani au eneo lolote au katika mazingira ya shughuli zozote. Ndiyo kusema Watumishi wa Mahakama hawana haki ya kupongezwa wanapofanya vizuri?

Kutokana na utaratibu huu wa kutotambua wanaofanya vizuri hamwoni kwamba unawakatisha tamaa wafanyao vizuri na hivyo kupunguza ufanisi wa Mhimili huu muhimu kwa kutoa haki?

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara ni kubwa kuliko zote Mkoani Mtwara, lakini Halmashauri hii ina Mahakama za Mwanzo zisizozidi au chini ya tatu zinazofanya kazi. Je, lini Mahakama za Mwanzo zitajengwa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara ili kuwapunguzia Wananchi adha ya kwenda umbali mrefu kutafuta haki?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono haja.

**MHE. HAMOUD ABUU JUMAA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nafasi hii, nami niweze kutoa mchango wangu katika Bajeti ya Wizara ya Kabiba na Sheria ya mwaka 2013/2014. Napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa Bajeti yake nzuri, iliyoandaliwa kwa umakini mkubwa ili kukidhi mahitaji na kukabiliana na changamoto katika Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, sote tunajua Taifa letu kwa sasa tupo kwenye mchakato wa upatikanaji wa Katiba mpya, itakayokidhi matarajio ya wengi kwani mchakato huu umekabidhiwa kwa Wananchi ili watoe maoni yao kipi kiwepo kwenye Katiba mpya. Kwa hali hiyo, napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada zake katika kusimamia mchakato mzima na kufikia hatua kubwa katika mchakato huu. Pia naipongeza Serikali kwa jitihada kubwa za kuongeza Majaji katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Kufanya hivyo, kunaongeza ufanisi katika utendaji wa shughuli za Mahakama ngazi ya Mahakama Kuu na Rufani.

Mheshimiwa Spika, hali ya uendeleshaji wa mashauri mengi hapa nchini inasikitisha sana, kwani kesi nyingi zimekuwa zikichelewa kusikilizwa na hivyo kuchukua muda mrefu kutolewa hukumu. Kwa namna hiyo, huwanyima haki pande zote mbili zinazohusika. Hali hii ni hatari sana kwa mustakabali wa utoaji haki nchini kwani ikumbukwe kwamba, haki inayocheleweshwa ni sawa na haki iliyonyimwa (*Justice Delayed is Justice Denied*). Naishauri Serikali iongeze idadi ya Watumishi hasa Mahakimu na Mawakili wa Serikali wa Kada mbalimbali ili kuongeza kasi ya uendeshaji wa mashauri mbalimbali nchini kwa lengo la kulipatia ufumbuzi suala la mlundikano wa mashauri Mahakamani linalosababisha pia msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani.

Mheshimiwa Spika, bado kumekuwa na changamoto kubwa kwa waajiriwa wapya waliopangiwa kutoa huduma katika Mahakama za Mwanzo Nchini. Mageuzi hayo katika mfumo wa Mahakama yana changamoto zake kwani vijana hao wasomi walioajiriwa itabidi wakakae na kufanya kazi kwenye maeneo ya vijijini ambako katika mazingira ya kawaida, imekuwa ni vigumu kwa vijana wengi kuyaafiki. Nashauri Serikali iboreshe miundombinu ya Mahakama za Mwanzo, ikiwa ni pamoja na utoaji wa motisha kwa Mahakimu hawa wapya ili waweze kutekeleza majukumu yao katika mazingira rafiki.

Mheshimiwa Spika, suala la Serikali kuingia mikataba

mibovu na makampuni mbalimbali hasa ya kigeni, ni jambo linalosumbua Jamii ya Watanzania. Hali hii inatafsiriwa kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambayo imepewa dhamana kuishauri Serikali kabla ya kuingia mikataba hiyo kuwa, haipo makini ama inajihusisha na rushwa au watumishi wake hawana utaalam wa kutosha kuhusiana na Mikataba hii ya kigeni. Naishauri Serikali ilichukulie eneo hili kwa umuhimu wa kipekee, kwani lina athari hata kwenye uchumi wa nchi yetu. Aidha, Serikali izidi kutoa mafunzo ya kutosha kwa Mawakili waliopo ili kupunguza gharama kubwa zinazotumika kulipia makampuni binafsi hasa katika maeneo mapya ya makosa ya kutakatisha fedha *(Money Laundry, Asset Forfeiture and Recovery and Trans National Crimes*).

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado kumekuwa na changamoto katika Mahakama zetu. Jambo hilo hutokana na kuwa na watumishi wasiokuwa waadilifu katika utendaji kazi wa kila siku. Hali hiyo imekuwa ikiwapa usumbufu Wananchi kwa kiwango kikubwa sana na hufikia mahali hata kupoteza haki zao za msingi. Vilevile ni ukweli usiopingika kwamba, kumekuwa bado na manun'guniko upande wa Wananchi kwamba, kuna kasoro za uandishi wa kesi na mashauri Mahakamani pamoja na utoaji wa hukumu zenye utata mkubwa.

Tuhuma hizi japo hazina ushahidi wa moja kwa moja, bado haziwezi kubezwa na hivyo, napenda kuishauri Serikali hususan upande wa Mahakama, kutoa mafunzo ya mara kwa mara hasa kwa Majaji au Mahakimu wapya kuhusu namna bora ya uendeshaji wa mashauri katika ngazi ya Mahakama ili kudumisha imani kwa chombo hiki muhimu katika utoaji wa haki. Aidha, napenda kusisitiza kwamba, Serikali izidishe kasi ya ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu ili kufikia lengo la kuwa na Mahakama Kuu kwa kila Mkoa kuliko ilivyo kwa hivi sasa ambapo Mahakama Kuu ya Tanzania ina Kanda 13 tu ambazo hazikidhi mahitaji ya Wananchi. Hali hiyo huleta usumbufu na gharama kwa Wananchi pindi wanapohitajika katika Mahakama hizo kwani hutakiwa kusafiri kutoka mahali walipo.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia Hotuba hii. Naomba niseme wazi kwamba, Serikali haijaitendea haki Wizara hii. Pesa ya Bajeti iliyotengwa ni ndogo ukilinganisha na changamoto nyingi zinazoikabili Wizara.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utaanza kujielekeza katika upungufu mkubwa wa waendesha mashtaka nchini ukilinganisha na idadi ya Majaji na Mahakimu waliopo ili kuleta ufanisi katika kuendesha. Jaji mmoja ni lazima ahudumiwe na Mawakili wawili, vivyo hivyo kwa Mahakimu ni vyema kuwe na uwiano katika kuajiri Mahakimu na Mawakili wa Serikali. Pale ambapo Mahakama inapewa kibali cha kuajiri, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ipewe kibali cha kuajiri Mawakili wawili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa idadi ya wanafunzi wanaohitimu Shahada ya Sheria imeongezeka, ni vyema Serikali ikawa na dhamira ya dhati ya kuongeza ajira za Mawakili wa Serikali na Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nitumie fursa hii kuishauri Serikali kuwa pale ambapo Serikali haitoi kibali cha ajira ya Mawakili wa Serikali, ni vyema Ibara ya 59(b)(3) ya Katiba na kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Mashtaka, vinavyomruhusu *DPP* kuteua Waendesha Mashtaka vikatumika ipasavyo. Ni vyema *DPP* atengewe pesa za kutosha kuwalipa waendesha mashtaka watakaowateua. Utaratibu huu utatuwezesha kuondokana na pengo la Waendesha Mashtaka linaloikabili Nchi hii kuimarisha mfumo wa kutenganisha mashtaka na upelelezi.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, atueleze wamejipanga vipi kuongeza Waendesha Mashtaka na kuwapeleka katika Mahakama za Wilaya na Mwanzo ili kuendana na mfumo mpya wa ajira wa Mahakama ambao sasa inaajiri na kupeleka Mahakimu Wahitimu wa Shahada ya Sheria kuanzia ngazi ya Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Iringa una Wilaya tatu za Iringa, Mufindi na Iringa na Mkoa wa Njombe una Wilaya nne za Makete, Ludewa na Wanging'ombe. Wilaya hizi zote saba bado ziko chini ya Mahakama ya Mkoa wa Iringa kwa kuwa bado Mahakama ya Hakimu Mkazi Njombe haijaanzishwa Kisheria. Mpaka leo hii Wilaya ya Kilolo hakuna Mahakama ya Mwanzo. Wananchi wa Kilolo wanapata huduma hiyo kutoka Mahakama ya Wilaya ya Iringa. Hii yote ni kutokana na kutokuwepo kwa miundombinu ya kimahakama katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Iringa, Mahakama ya Mwanzo Mlolo, inatembelewa na Hakimu kutoka Mahakama nyingine ya Mwanzo. Pia Wilaya ya Kilolo, Mahakama ya Mwanzo ya Mahenge inatembelewa na Hakimu kutoka Mahakama nyingine.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri atakapojumuisha anieleze ni lini Mahakama hizo za Mwanzo za Mlolo na Mahenge na Wilaya ya Kilolo zitaongezewa Mahakimu kwani hivi sasa wapo wachache sana na kusababisha mlundikano wa kesi.

Mheshimiwa Spika, pia Mahakama zetu nyingi majengo yake ni chakavu, hakuna vifaa vya kutosha, kama mashine ya chapa, *computer* na hakuna umeme. Uangaliwe uwezekano wa kuweka *solar.*

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iangalie uwezekano wa kuboresha mishahara na maslahi ya Majaji na Mahakimu kwa kuwa ipo chini sana ukilinganisha na uzito wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichangie kuhusu posho za Wazee wa Baraza. Serikali ifikirie mpango wa kuwaongezea posho na kuwaboreshea baadhi ya huduma. Wapatiwe ofisi wakati wanasubiri kesi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, gharama za kukata shauri Mahakamani bado ni kubwa kiasi ambacho si Wananchi wote wanaoweza kuzimudu na hivyo, hupelekea baadhi yao kukosa haki zao kwa kutokuwa na pesa za kutosha katika kukata shauri. Vilevile mashauri huchukua muda mrefu sana Mahakamani kwa kuchelewa kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zilizofanywa na Wizara hii, bado *speed* ya uendeshaji wa mashauri katika Mahakama takriban zote ni ndogo sana na kupelekea zaidi ya miaka miwili kwa kusikilizwa shauri. Muda mrefu katika kesi za mashauri Mahakamani hupelekea Wananchi kukosa imani na Mahakama zao na vilevile Wananchi hukosa haki zao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika suala hili, maoni yangu naitaka Serikali kupunguza gharama za kukata shauri.

Mheshimiwa Spika, pia au Serikali kwa ujumla iweke muda maalumu *(time limitation)* ya kusikiliza mashauri. Kwa mfano, kesi za mashauri zisizidi miaka miwili Mahakamani kabla ya kutolewa hukumu.

Mheshimiwa Spika, suala la rushwa bado ni tatizo katika Mahakama zetu kwani imefikia wakati hadi kuitisha faili kwa karani jibu ni kwamba halionekani, lakini ukijulikana au ukitoa pesa faili lako hupatikana. Hivyo basi, suala hili nalo huwanyima haki zao wasio na pesa na vilevile hupelekea kesi kuchukua muda mrefu. Mfano, kupata *Order* ya Mahakama pia *issue;* kupata *judgement* pia si chini ya miezi sita; na *delay* yote hii ni kwa kuwa wanataka pesa (rushwa).

Mheshimiwa Spika, Wizara iliangalie hili kunusuru haki za watu wasio na pesa. Iboreshe mazingira ya kazi kwa wafanyakazi na wala rushwa wawajibishwe ili wengine nao wasiendelee.

Mheshimiwa Spika, bado hatuna Mahakimu wa

kutosha katika Mahakama zetu, hali ya kuwa mtaani wapo pia wenye sifa lakini hawana ajira; hivyo, ni vyema kuajiri Mahakimu wa kutosha katika Mahakama zetu. Kwa mfano, Hakimu wa kutoka Bagamoyo ndiye huyo huyo anasubiriwa na Mahakama ya Wilaya ya Chalinze. Ninashauri kuongeza Mahakimu katika Mahakama za Wilaya kutapelekea *accessibility to Justice.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Mkurugenzi wa TAKUKURU atakuwa *appointed* na Mheshimiwa Rais, basi ni vyema apitishwe na Bunge, yaani awe *confirmed* au *approved* ndani ya Bunge kama njia inayotumika kuwapata au katika mchakato wa Mawaziri wa Kenya. Baada ya kuteuliwa, Bunge nalo huwapitisha.

Mheshimiwa Spika, bado Wananchi wetu wengi hawazijui Sheria na taratibu za kufungua kesi na jinsi ya kumpata Wakili wa Serikali kwa wale wasiokuwa na uwezo wa kuwalipa Mawakili.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iwe na utaratibu maalumu wa kuwaelewesha ambao watahitaji msaada wa Mawakili hali ya kuwa hawana uwezo wa kuwalipa.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, bajeti haikidhi haja kwa kiwango kikubwa mno.

Mheshimiwa Spika, nitalipeleka jambo hili katika mjadala wa Bajeti ya Serikali itakapowasilishwa siku chache zijazo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto zilizopo katika Wizara hasa juu ya usimamiaji wa haki na Sheria, tengeo la jumla ya shilingi bilioni 18.4 kwa miradi na matumizi ya kawaida halitoshi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya miundombinu ikiwemo majengo ya Mahakama na nyumba za Watumishi hayawezi tena kufumbiwa macho kwani hadhi ya Mahakama inaendelea kupungua.

Mheshimiwa Spika, vitendea kazi kama vyombo vya usafiri, samani na kadhalika, vina upungufu mkubwa unaochangia utendaji hafifu wa Mahakama nchini kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa watumishi, unaochangiwa na changamoto nyingine kama nilivyoainisha hapo juu, nalo ni tatizo kubwa linalosababisha Mahakama nyingi kuelemewa na hivyo Magereza nyingi kuwa na msongamano wa watuhumiwa huku baadhi yao wakiwa na makosa madogomadogo kama wizi wa mahindi mabichi kadhaa na kadhalika. Kesi nyingi huchukua muda mrefu kabla ya hukumu (zikiwemo zile zinazohusu makosa ya kawaida sana).

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ione haja ya kuongeza tengeo katika bajeti yake kwa ajili ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya kuona namna bora ya kuhusisha jamii katika kutatua kesi zinazotokana na makosa madogo na ya kati; kwa mfano, matumizi ya safu za uongozi wa kimila pale ambapo bado zina nguvu *(chiefdom),* uongozi wa kidini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vilevile utaratibu wa kitaalam ujulikanao kama *Alternative Dispute Resolutions (ADR),* utiliwe mkazo. Kiundwe chombo mahususi cha *ku-compile* changamoto zote za Idara ya Mahakama na kutoa mapendekezo ya ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Spika, nina maombi maalum kwa ajili ya Tunduru. Kwanza, naomba gari la Mahakama. Jiografia ya Tunduru iwe kichocheo cha kuipa Tunduru kipaumbele; tunaomba sana.

Pili, naomba ajira za Mahakamu na Watumishi wa Mahakama; *Tunduru is a disadvantaged district due to remoteness, poor accessibility et cetera.* Tunaomba *special consideration*.

Tatu, naomba tengeo la fedha kwa ajili ya majengo hasa Mahakama ya Wilaya.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali ilitenga zaidi ya shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Machame. Ramani na eneo la ujenzi vyote vilikuwa tayari, lakini katika mazingira ya kutatanisha, Mahakama hii haikujengwa Machame, bali ilihamishiwa katika Mji wa Bomang'ombe (Hai Mjini).

Mheshimiwa Spika, eneo palipokusudiwa kujengwa Mahakama hiyo ni eneo ambalo kihistoria na kimila, palikuwa ndipo penye Baraza la Kichifu lililosimamia masuala yote ya utoaji haki katika Tarafa za Machame na Lyamungo. Jengo lililopo limechakaa sana na ni hatari kutumika.

Mheshimiwa Spika, maadam awali palionekana umuhimu wa kujenga Mahakama hii Machame, bado umuhimu huo upo na sana sana umeongezeka. Eneo linalotegemea Mahakama hii ni zaidi ya vijiji 25, kata sita na idadi ya wakazi zaidi ya 150,000.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua vilevile *Status ya Project* iliyohamishiwa Mji Mdogo wa Bomang'ombe imefikia wapi na itakamilika vipi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Serikali ione umuhimu wa kuirejesha Mahakama ya Mwanzo Machame katika bajeti ya mwaka 2013/2014.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuiomba Serikali ijaribu kuiangalia kwa umakini Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kwa sababu chombo hiki ni chombo cha Kikatiba, lakini bajeti yake haitoshelezi kabisa kusimamia majukumu yake. Lakini cha ajabu, Serikali imekuwa haifanyii kazi mapendekezo ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Mfano mzuri ni mapendekezo ya kesi ya Daudi Mwangosi kuhusu kulipwa fidia kwa mkewe na kuwasomesha

watoto wa Marehemu, lakini hakuna lililozingatiwa. Sasa Serikali itueleze: Kwanini haizingatii ushauri wa chombo kilichoundwa kikatiba?

Mheshimiwa Spika, nashauri utaratibu wa upatikanaji wa Majaji uwe wa kupigiwa kura, yaani nafasi ya Jaji Mkuu ipatikane kwa kushindanishwa.

**MHE. AMINA NASSORO MAKILAGI**: Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi kwa Wizara, naomba kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, sheria zinazowakandamiza wanawake kama vile Sheria ya Ndoa, Mirathi na Sheria ya Ardhi nilijua zitawasilishwa Bungeni ili ziweze kufanyiwa marekebisho ili tatizo la kuolewa watoto wadogo walio chini ya miaka 18, Mirathi, wanawake kumiliki ardhi, yapatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, kumejitokeza tabia ya wananchi kuchukua sheria mkononi na kuchoma moto nyumba za baadhi ya viongozi hasa wanawake, majengo ya Serikali na Ofisi za Chama.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua, ni hatua gani zilizochukuliwa kwa wale wote waliohusika ili kutoa fundisho kwa wengine?

Mheshimiwa Spika, vile vile hivi karibuni kumejitokeza vitendo vya mauaji ya wanawake Mkoa wa Mara Wilaya ya Butiama na mauaji ya vikongwe Mkoa wa Geita.
Pia ningependa kujua ni hatua gani zimechukuliwa ili kudhibiti vitendo hivyo na kuchukua hatua kali kwa wale wote waliohusika na mauaji hayo ili kutoa fundisho kwa wengine?

Je, ni hatua gani zilizochukuliwa kwa wale wote wanaomdhalilisha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Bungeni?

Pia ni hatua gani zinazochukuliwa juu ya Wanasiasa wanaovunja Sheria kwa kuwapotosha wananchi kupitia Mikutano ya hadhara?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufinyu wa bajeti, nashauri Serikali ione uwezekano wa kuongeza fedha katika Wizara hii kwa ajili ya matumizi ya ujenzi na ukarabati wa Mahakama, kuajiri Mahakimu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ucheleweshaji wa kesi, ni vyema sheria hii ya mwendo wa kesi ikaangaliwa upya ili kuwa na ukomo wa kumaliza kesi Mahakamani kuliko ilivyo sasa. Kesi zinachukua muda mrefu sana, hivyo wananchi walio wengi hasa wanyonge kukata tamaa na kupoteza haki zao.

Mheshimiwa Spika, wapo baadhi ya Mahakimu ambao ni wala rushwa. Ni vyema kufanya uchunguzi na watakaobainika kuchukuliwa hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B.BLANDES:** Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kuajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wenye Shahada ya Sheria *(LLB),* jambo ambalo ni jema. Waheshimiwa Mahakimu hawa tangu waajiriwe hawajapangiwa Vituo vya Kazi. Wapo wamekaa bila kazi katika Mahakama za Wilaya, hawajapangiwa kazi yoyote, hata hawaruhusiwi kuahirisha kesi Mahakamani, hata mishahara ya baadhi yao haijatumiwa karibia miezi kumi. Ni jambo la kukatisha tamaa sana kupita maelezo. Vijana hawa hawajui wafanye nini, wametelekezwa kama watoto yatima hadi wanajuta ni kwanini waliomba nafasi za Uhakimu. Ni kwanini Serikali haichukui hatua za makusudi na za haraka sana ili kunusuru mgogoro huu?

Mheshimiwa Spika, *Nolle Prosequi(no further Prosecution)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya mwenendo wa makosa

ya Jinai *CPA*, inampa madaraka Mkurugenzi wa Mashtaka *(DPP)* kumfutia mashtaka mshitakiwa yeyote pale anaporidhika kuwa hakuna ushahidi wa kutosha kuendelea kumshitaki.

Mheshimiwa Spika, kwa siku za hivi karibuni Ofisi ya *DPP* imekuwa na kigugumizi cha hali ya juu sana cha kutumia mamlaka haya kwa kuogopa vyombo vya habari na masuala ya kisiasa.

Naomba nishauri Ofisi ya *DPP* ifanye kazi kwa mujibu wa Sheria, kwani kutofanya hivyo, raia wengi wasio na hatia wanateseka bila sababu ya msingi na hakuna fidia yoyote wanayolipwa. *DPP Office*, isiogope maneno ya Mtaani, maneno ya kisiasa, chuki binafsi kukomoana au jambo lolote la kumnyima mtuhumiwa haki yake ya *Nolle Prosequi (no further Prosecution)*. *DPP* na timu yake wawe wepesi kutoa *Nolle Prosequi* haraka iwezekanavyo ili mradi wahakikishe haki inatendeka na *Nolle Prosequi* haitolewi katika mazingira ya rushwa au shinikizo lolote.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii ili kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali, bado kuna changamoto kubwa katika Wizara hii hasa katika Kitengo cha Mahakama, uelewa wa wananchi kuhusu mambo mbalimbali ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, Mahakama imekuwa inalalamikiwa sana kuhusu utoaji wa haki kwa wananchi. Wananchi wamekuwa wanabambikiwa kesi tofauti kabisa na zao za awali. Hata hivyo, Taasisi hii imekuwa inatuhumiwa sana kwa rushwa, jambo linaloifanya Taasisi kukosa imani kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara na Serikali kwa ujumla kutafuta njia nzuri ya kushughulikia kesi za wananchi ili kurudisha imani za wananchi kwa Taasisi hii.

Mheshimiwa Spika, pia kesi nyingi na ndogo ndogo zimekuwa zinachukua muda mrefu bila kupatiwa ufumbuzi huku watuhumiwa wakiachiwa ndani bila kupewa dhamana; huku kutokuelewa sheria kwa wananchi hawa kukichukuliwa kama faida kwa Watendaji wa Mahakama na Askari Polisi.

Mheshimiwa Spika, asilimia kubwa ya wananchi hazijui sheria nyingi za msingi au muhimu katika maisha yao ya kila siku. Jambo hili limefanya kudhulumiwa haki zao mara kwa mara. Nashauri Serikali kutafuta mfumo wa kuwaelimisha wananchi kuzijua Sheria mbali mbali ili kuwaepusha na matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, Katiba ndiyo sheria mama katika nchi yoyote inayofuata misingi madhubuti ya Sheria. Sheria yoyote ni lazima izingatie misingi ya Katiba ya Nchi. Nchi yetu ina Katiba, lakini Katiba yetu ina utata ambao umeleta manung'uniko na malalamiko kwa muda mrefu, jambo ambalo limepelekea leo kuleta mjadala wa mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, jambo hili la kuridhiwa kujadiliwa kwa suala la Katiba, litasaidia sana kutatua baadhi ya kero zilizomo katika Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar endapo nia thabiti ya marekebisho hayo yatafuata zaidi maoni ya walio wengi na siyo maamuzi ya mtu.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Tume ya Kuratibu Maoni ya Wananchi amekuwa akitoa maelezo kupitia vyombo vya habari kwamba suala la mabadiliko ya Katiba ni jambo ambalo halitochukuliwa vile wanavyotaka watoaji wa maoni hayo.

Kauli hiyo ya Mwenyekiti haiashirii kuwepo kwa uadilifu na uaminifu juu ya uratibu huo wa maoni ya wananchi juu ya mabadiliko ya Katiba. Wananchi walio wengi wanaona kwamba suala la utoaji wa maoni ni kama kiini macho, lakini

Katiba iliyokusudiwa imeshatayarishwa zamani na ndiyo Mwenyekiti anayeshughulikia suala hilo akadai kama yuko tayari wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, maelezo yaliyotolewa ni Waziri wa Katiba na Sheria yanakinzana kabisa na maelezo yanayotolewa na Mwenyekiti anayesimamia uratibu wa maoni ya wananchi juu ya mabadiliko ya Katiba. Ni vyema basi Mheshimiwa Jaji Warioba akajikita katika maoni ya wananchi na siyo yale tu anayoona yeye kwamba yanafaa badala ya kuwasilisha maoni ya wananchi, jambo ambalo linaweza kuleta ufa mkubwa na vurugu zisizokwisha, ambapo baada ya kusonga mbele likaweza kuturejesha nyuma. Ni vyema maoni hayo yakaangalia Muungano wa nchi zote mbili.

Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa Mahakama katika utoaji haki hautoshi, unadhalilisha. Ni wazi kwamba Serikali imeshindwa kabisa kulisimamia jambo hili ambapo mara nyingi washukiwa wa makosa wanadhalilishwa. Lakini mwisho wake washukiwa huonekana kwamba hawana makosa, na baadhi ya makosa kuonekana na sura za kisiasa. Ni maoni yangu kwamba kwa wale ambao watachukuwa hatua kwa nia tu ya kuwadhalilisha wananchi wengine kwa kutumia nafasi zao na ikathibitika kwamba hakuna uthibitisho wa kosa, ni lazima aliyedhalilishwa alipwe fidia.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba Serikali haiko makini katika kuangalia na kuimarisha majengo ambayo yanatumika katika kutoa haki. Majengo ni dhaifu, hayatoshi na hayaonyeshi sura kwamba ni sehemu ya kutolea haki. Majengo yanaonekana kama maeneo yasiyo na amani na imani na wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, mihimili mitatu ambayo ni Serikali Bunge na Mahakama; muhimili wa tatu, yaani Mahakama haujatumika vizuri katika kusimamia kazi zake. Hivyo ni wazi sasa muhimili huu ufanye kazi zake ili utendaji huo usiambatane na misingi ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri haki zitendeke, zitekelezwe. Kuna wajibu wa makusudi wa Serikali kuhakikisha kwamba imeajiri Mahakimu wengi ili iweze kusimamia kutoa haki kwa kesi nyingi ambazo zimelundikwa kwa muda mrefu bila kutolewa maamuzi, na hivyo kuwafanya washukiwa ama kukaa ndani kwa muda mrefu au kwa wale walio nje na wanaoendelea na kesi kukosa kuendelea kufanya shughuli zao za kimaendeleo, kwani hawawezi kwenda popote katika shughuli zao kwa kuhofia kuonekana kwamba wamekimbia.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na utamaduni wa Mahakimu kuendesha kesi kwa muda wanaotaka wenyewe na hivyo kesi kulundikana na kusababisha kuwepo kwa mianya ya rushwa. Hivyo basi, ni vyema Serikali ikaangalia upya kwa kupitia Wizara husika namna bora ya kuendesha kesi hizo. Aidha, kwa kuongeza idadi ya watumishi wakiwemo Mahakimu; upanuzi wa ukarabati wa Mahakama ili kuziwezesha kuwa za kisasa zaidi ili kufanya kazi kwa ufanisi na tija; ukarabati ama ujenzi wa Mahakama mpya lazima uendane sambamba na uwekaji wa vifaa vya kisasa kama *Computer* na vinavyofanana na hivyo ili kuziwezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni vyema kikatumika Kiswahili wakati wa hukumu ili kumrahisishia mtuhumiwa kuelewa mwenendo mzima wa shauri na hatima ya hukumu.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa Wizara husika na Serikali ikaangalia namna ya utoaji elimu kwa Umma ili Umma uweze kuzitambua sheria mbalimbali na pia waweze kuzitii bila shuruti.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwamba katika

kipindi chake cha Utawala hadi sasa ameteua Majaji zaidi ya 50 ambao wameweza kusikiliza kesi kwa haraka na kuwawezesha Watanzania kupata haki zao kwa wakati na kutekeleza kwa vitendo dira ya Mahakama ya kutoa haki kwa wote na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hii inaonyesha jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais anavyowajali Watanzania kwa kuona haki za Watanzania zinapatikana na kuonekana katika jamii.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2012/2013 zilitengwa Shilingi bilioni moja na laki tatu kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Mahakama, lakini fedha hizo hazikutolewa na Hazina. Katika bajeti hii Serikali imetenga Shilingi bilioni moja na laki tano kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo hazitoshi, kwani kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa, ujenzi wa Mahakama Vijijini unagharimu zaidi ya Shilingi milioni nne na laki tano na Mahakama za Mijini, ujenzi unagharimu Shilingi milioni mia tano na laki tano. Hivyo kwa fedha iliyotengwa, ina maana tutajenga Mahakama tatu tu. Bila kufanya ukarabati wowote katika Mahakama, mfano, Mkoa wa Morogoro kuna mahitaji ya Mahakama 54 za Mwanzo na Mahakama za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itafute fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Mahakama zetu ili wananchi waweze kufikiwa na huduma na kuweza kupata haki zao.

Mheshimiwa Spika, hitaji la Mahakama limekuwa kubwa sana, mfano kwenye Wilaya mpya 19 ikiwemo ya Gairo – Morogoro hakuna Mahakama; Mikoa mipya ya Geita, Simiyu, Njombe na Katavi hazina kabisa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, gazeti la *Daily News* 22/4/2013 limetangaza tenda ya kujenga majengo ya Utawala ya Mikoa na Wilaya mpya ambapo jumla ya majengo 23 yatajengwa, lakini katika majengo hayo, hakuna hata Mahakama moja inayojengwa wala vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itazame upya iweze kuweka kipaumbele ili wananchi waweze kupata huduma za Mahakama ili haki zao zisipotee hasa kwa akina mama ambao wamekuwa wakikata tamaa kufuatilia haki zao, kwani inawalazimu kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za Mahakama.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu utawala bora. Mahakama za Wilaya ziko kwenye Ofisi na majengo ya Mamlaka nyingine. Mahakama za Mwanzo ziko kwenye Ofisi za Kata, mfano Mahakama ya Mwanzo ya Mlali Mvomero iko kwenye Ofisi za Serikali ya Kata. Sasa endapo inatokea kesi inawahusisha viongozi wa Serikali za Kata: Je, Hakimu ataweza kusimamia sheria na kutenda haki, wakati ndiyo wamempa jengo kuendesha shughuli za Mahakama?

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na migogoro mingi ya ardhi nchini kati ya wakulima na wafugaji, wananchi na wawekezji na migogoro ya Vyama vya Siasa hasa wanapoendesha Mikutano ya hadhara, jambo ambalo limepelekea Serikali kuunda Tume mbalimbali katika kushughulikia migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imepewa mamlaka kikatiba kulinda kukuza na kutetea Haki za Binadamu na misingi ya utawala bora ni vyema sasa Serikali ikaijengea uwezo Tume kwenye Rasilimali Fedha na Rasilimali Watu ili kupunguza gharama za Serikali kuunda Tume kila linapotokea tatizo la uvunjifu wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tume ya Haki za binadamu ina mamlaka kikatiba ya kutoa elimu na kusuluhisha migogoro, naamini kabisa Tume ikiwezeshwa itasaidia kutatua kero nyingi za wananchi na kupunguza mlundikano wa kesi mbalimbali katika Mahakama zetu, kwani Tume itakuwa imezipatia ufumbuzi kwa njia ya usuluhishi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani iliyowasilishwa na Mheshimiwa Tundu Lissu.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni lini Serikali italipa Washauri wa Mahakama za Mwanzo posho zao nchini? Kwa mfano hai, ni kama nilivyowasilisha kwako madai ya Washauri wa Mahakama za Mwanzo wa Ifakara pamoja na jitihada zao za kufuatilia kwa barua.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Mahakama za Mwanzo ambazo ndizo zinakuwa kimbilio za Watanzania asilimia 75 - 80 waishio Vijijini?

Mheshimiwa Spika, tumepitisha Sheria hapa Bungeni inayotaka Hakimu wa Mahakama za Mwanzo wawe na shahada lakini hizo Mahakama za Mwanzo hazina nyumba za Watumishi, majengo ya Mahakama, lakini katika Mahakama nyingi nchini ndiko rushwa imekithiri. Vile vile wananchi wengi wanahukumiwa kwa kukosa Wanasheria wa kuwasaidia. Je, Serikali ina mpango gani wa msaada wa kisheria kwa wananchi wa Vijijini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ucheleweshwaji wa kesi, Magereza nchini zinajaa kutokana na watu wengi kubaki mahabusu au kwa kufungiwa dhamana au masharti ya dhamana kushindikana. Mfano, hati ya nyumba ambapo maeneo mengi Wilayani Serikali haijapima viwanja wala haijatoa hati za nyumba, hivyo sheria zirekebishwe ili kupata masharti nafuu ya dhamana.

Mheshimiwa Spika, ni wakati sasa Serikali ipeleke elimu ya sheria kwa wananchi ili waondokane na kuhukumiwa bila kujijua.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba baada ya wananchi mbalimbali kupigiwa kura kwenye Mikutano Mikuu ya Kijiji, Mtaa na kuchaguliwa na kushinda kwa kura nyingi na kuongeza, lakini majina yalipopelekwa kwenye kikao cha Kata ambapo kwa kawaida Wajumbe wa Baraza la

Maendeleo ya Kata ni Diwani na Madiwani, Mtendaji Kata, Wataalam katika Kata, Viongozi wa Vyama vya Siasa, Wawakilishi wa *NGO's* na Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji.

Sasa wananchi wanashangaa, kwa nini uchaguzi wa Wajumbe katika Kata waliohusika kuteua Wajumbe ni Diwani na Wenyeviti tu ambapo uteuzi huo umelalamikiwa mahali pengi? Ni vyema suala hilo lingeangaliwa upya.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Spika, napongeza juhudi za Wizara na Taasisi zote kwa umoja wa dhamira na azma ya kutenda na kusimamia hifadhi ya haki. Haki huzaa amani, upendo na mshikamano kwa kustawisha ustawi wa maendeleo ya jamii, uchumi na uwajibikaji bora wa utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii hutambulisha mazingira ya hamasa ya matarajio ya shabaha na malengo ya uhai wa hatma ya kusadikika demokrasia na siasa kuwa zitazaa uwakilishi wa hiyari ya jamii kujiongoza na kujisimamia.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 ulikuwa wa uchaguzi wa Madiwani na Wabunge. Serikali ilitambua kasoro ya kazi za Ubunge kuhitaji muda wa nyongeza wa kusikilizwa na kuamuliwa madai ya malalamiko ya kasoro na hitilafu kwa Kanuni za Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, pana kesi za madeni ya kasoro na hitilafu zilizopo katika Mahakama za Mikoa. Hatima ya kesi hizo ni vurugu za utashi wa maono yasiyo na mwongozo. Je, ni lini patatolewa muda wa nyongeza wa kuzaa uvumbuzi kwa madai ya malalamiko ya hizo kesi za uchaguzi za Madiwani.

Mheshimiwa Spika, bima ya uhai wa utulivu wa siasa za uchaguzi hujengwa na vitendo ya haki zilizotendeka katika chaguzi zilizopita.

Mheshimiwa Spika, naomba kauli elekezi itolewe kupitia Bunge hili kuhusu usalama na uendelevu. Je, utatekelezwa vipi na Mahakama ziahirishe kesi hizo badala ya kuzifuta.

Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali na kauli ya Mahakama Kuu kwa umoja wake watadhibiti mwonekano wa fikra hasa dhidi ya Serikali na dhidi ya Mahakama kuwa ni Wakala wa kudhulumu haki za utawala bora wa demokrasi na siasa kwa watu wa tabaka la chini la Madiwani.

Mheshimiwa Spika, naomba kukumbusha kwamba Wizara hii ina mhimili wa Mahakama. Ni fursa chanya na ni wajibu mtambuka wa kuondoa mapishi ya mizozo na migogoro ya kuegemewa na wanasiasa kuezua imani ya Umma kwa mafanikio ya wema mpana ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile *DPP* apatiwe fursa ya kutoa Bungeni semina ya utambulisho wa maana na wajibu wa Ofisini hii.

Mheshimiwa Spika, Ofisi hii ndiyo maono ya hekima na busara pana, hivyo tuepuke malipuko ya kuisuta kwa dhana ya asiyejua maana, hana sifa ya kuzua jambo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, natanguliza sana shukrani zangu kwa kupata fursa hii ya kuchangia kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Spika, nasema kwa kifupi kwa kuwa ninayoyaona mimi yanayohitaji marekebisho ni kidogo sana kwani yaliyo mengi yapo sawa, hii ni kadri nionavyo mimi.

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kuipongeza Serikali kwa jitihada za kuongeza idadi ya Mahakimu tofauti na hapo mwanzo japo wanafanya kazi katika mazingira

magumu kutokana na maeneo wanayofanyia kazi hasa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, ukomo kumaliza kesi kwa mwaka. Mbali na kuongeza idadi ya Mahakimu basi uwepo utaratibu wa kisheria wa Hakimu kumaliza angalau kesi kwa idadi fulani ili kupunguza mlundikano wa kesi ili kuokoa fedha za walipa kodi ambazo zinatumika kulisha mahabusu na wafungwa. Uwepo wa ukomo wa chini wa idadi ya kesi ni mzuri japo una changamoto zake kulingana na aina ya kesi.

Mheshimiwa Spika, njia nyingine ya kupunguza mlundikano Magerezani, ni kuhesabu miaka au muda wa mahabusu walioutumia Gerezani kabla ya hukumu ili wakihukumiwa basi ule muda walioutumia uingizwe katika muda wa hukumu atakayopata.

Mheshimiwa Spika, majengo ya Mahakama nyingi hapa Tanzania ni chakavu na bado hayajakidhi kabisa idadi ya mashauri yaliyopo. Napenda kuishauri Serikali iliangalie kwa umakini suala hili ili mlundikano wa watu Magerezani na kesi Mahakamani zipatiwe ufumbuzi wa kudumu pia adhabu mbadala itiliwe mkazo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Wizara hii muhimu ya Katiba na Sheria ambayo inasimamia haki, sheria na uhuru wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, nianze na uboreshaji wa mazingira ya kazi na ujenzi wa majengo. Mhimili huu wa sheria ni muhimu sana lakini Serikali imekuwa haitoi fedha za kutosha kulingana na majukumu ya mhimili huu ulivyo. Miundombinu bado iko nyuma sana kwa maana ya majengo ya Mahakama nyingi za Wilaya nchini ni mabovu, yamechakaa na kuwa makazi ya bundi (magofu). Usafiri kwa Mahakimu ni mgumu, hawana magari ya kufanyia kazi vya kutosha. Hawana vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi maofisini, kama *computer,* bado

wanatumia *typewriter* kizamani ambazo huchelewesha kupatikana kwa taarifa za kazi na kuweka mlundikano pia upotevu wa taarifa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kubadilisha Sheria Tanzania. Tume hii ipiganie kubadilisha sheria nyingi zilizopitwa na wakati kwani sheria kandamizi kama vile umiliki wa ardhi kwa mwanamke bado ni tata na hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali hawa *paralegal* wazunguke sana vijijini kutoa elimu ya sheria mbalimbali. Pia katika sheria au kusimamia masuala ya mashauri, lugha ya Kiswahili itumike ili wananchi waelewe kwa ufasaha misingi ya haki zao badala ya kuingia gharama ya kutafuta Mawakili wa kuwasimamia kwa gharama kubwa au kukata tamaa kabisa na kumuachia Mungu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, Mji Mdogo wa Himo ulitangazwa rasmi na Serikali mwaka 2000. Mwaka 2002, watu wenye nia mbaya kuzuia maendeleo ya mji huo, kwa kutumia Mawakili ambao lengo lao ni kutafuta fedha, wakaanzisha kesi Mahakamani kuzuia mji huo usipimwe na wala usijengwe.

Mheshimiwa Spika, kitu kinachonisikitisha kama Mbunge ni kuona jinsi Mahakama inavyotumika kuzuia maendeleo ya wananchi. Kesi hiyo imekaa Mahakamani kuanzia mwaka 2002 hadi leo mwaka 2013 zaidi ya miaka 11, kesi haiongelewi, kesi haimaliziki, mji haupimwi wala haujengwi, kisa kuna kesi Mahakamani. ni maoni yangu kwamba Mahakama zinatumika vibaya kwa manufaa ya watu wachache wenye nia ovu. Ni kwa nini kesi inayozuia maendeleo ya wananchi ikae Mahakamani kwa miaka 11? Huu utawala wa sheria uko wapi? Wananchi wakidai kuna rushwa Mahakamani inayozuia haki na maendeleo yao yasipatikane tunasema nini? Ni lazima Serikali izuie utapeli huu. Nina majina ya wananchi 400 wanaotaka kupimiwa viwanja kwenye Mji wa Himo lakini imeshindikana kupimiwa

viwanja hivo kisa kuna kesi Mahakamani, kesi iliyoko Mahakamani kwa miaka 11.

Mheshimiwa Spika, suala hili nimelifikisha mbele ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali atoe msukumo wake kwa kuwa halijamalizika. Hii kesi ya bandia inaidhalilisha sana Serikali. Naomba Serikali itoe tamko juu ya kesi hii ya bandia inayozuia Mji wa Himo kupimwa na kujengwa.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kutanguliza kuunga mkono Hoja ya Waziri. Pamoja na kuunga mkono, nieleze changamoto kwenye Wizara hii na pili nieleze kero kwenye Jimbo la Longido.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Serikali haiipatii Wizara hii fedha za kutosha. Serikali inapogawa maeneo ya utawala mfano Mikoa, Wilaya Mpya, yote yanahitaji Mahakama za Mikoa na Mahakama za Wilaya. Kuna mahitaji katika maeneo mengi nchini. Tunashauri Serikali iitengee Wizara fedha za kutosha ili majengo ya Mahakama yajengwe kwenye maeneo yanayohitajika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni usafiri wa Mahakimu. Tatizo hili ni kubwa hasa kwa Wilaya za pembezoni. Hakimu anahitaji kuzunguka kwenye Tarafa mbalimbali jambo hili ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni muhimu Mahakimu kujengewa nyumba za kuishi kama watumishi wengine.

Mheshimiwa Spika, napenda nieleze kero za Wilaya ya Longido. Wilaya ya Longido imetengwa kwenye Wilaya ya Monduli mwaka 2007. Huduma ya Mahakama iliyoko Monduli ni mbali sana, kilometa 150 jambo ambalo inawawia wananchi vigumu kutumia huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Longido ina Tarafa nne (4) ambazo ni mbali na Makao Makuu mfano, Tarafa ya

Enduimet ni km.75 toka Makao Makuu (W), Tarafa ya Ketumbeine km.60, Tarafa ya Engarenaibor km.44.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Longido haina jengo la Mahakama ya Wilaya. Haina Mahakama ya Mwanzo, bado Mahakimu wanakosa eneo la kuendeshea mashauri ya Mahakama pamoja na usafiri wa kufikia Tarafa nilizozitaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Wilaya ya Longido ni ya zamani tofauti na Wilaya ambazo zimegawanywa mwaka jana lakini bado tuna mahitaji makubwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, naomba Serikali isikilize ombi hili kwani ni la muda mrefu kuanzia Waziri Bakari Mwapachu mpaka sasa kila Waziri anayeingia anatoa ahadi na kuondoka bila kutekeleza ahadi hii, kwa sasa Serikali iangalie tena kero hii ya Jimbo la Longido.

Mheshimiwa Spika, nawaombea mafanikio mema.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii kuhusu bajeti ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iharakishe ukarabati wa Mahakama za Mwanzo za Mwamagembe na Ukimbu (Kayui).

Mheshimiwa Spika, aidha, naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kujenga Mahakama za Mwanzo kwa ajili ya Kata za Idodyandole, Ipande, Aghondi, Rungwa, Kitaraka na Saijaranda.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria. Mambo mengi yaliyopangwa ndani ya hotuba hii ni mema iwapo yatafuatwa na kutekelezwa kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa msisitizo tu, kwamba mchakato wa kuunda Katiba Mpya, ungefaa kama kufikia mwaka 2014, mchakato huu ungekamilika na Katiba Mpya kupatikana.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 59 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, ametamka kwamba Tume ya kukusanya maoni ya Katiba Mpya, itayaheshimu na kuyafanyia kazi ipasavyo maoni yote yaliyotolewa na yatakayotolewa na wananchi, Taasisi, Asasi za kiraia na makundi mengine. *TGNP* na Chama cha Wabunge Wanawake kimeshiriki kutoa maoni yake katika Tume ya Kukusanya Maoni. Naomba maoni na mapendekezo yaliyotolewa yazingatiwe kwa faida ya wanawake wote Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa suala la uwakilishi Bungeni, bado wanawake wanasisitiza uwakilishi wa asilimia 50 kwa 50 upatikane/uwepo na sio ndani ya Bunge tu hata katika vyombo vingine vya maamuzi ngazi ya juu Serikalini. Naiomba Tume ya maoni ya Katiba ijitahidi kukamilisha mapema uundwaji na upatikanaji wa Katiba mpya ili mapendekezo mengine yaliyotolewa na *TGNP* na Chama cha Wabunge Wanawake, yaweze kutumika katika uchaguzi wa mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, siyo maoni yote yaliyotolewa yanajenga au yatajenga. Tuweke utaifa mbele, tuangalie amani ya nchi yetu na watu wake. Maoni yanayotolewa ambayo hayajengi na hayatajenga nchi na Utaifa wa nchi yetu. Ni vyema yakaachwa, na kwa hili Tume inahitaji kuchukua na kufanya maamuzi magumu pale inapoona maoni yaliyotolewa hayatafaa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Liwale haina Mahakama ya Wilaya. Mahakama inayotumika sasa hivi ni Mahakama ndogo ambayo ilikuwepo enzi za mkoloni kabla Wilaya ya Liwale haijawa wilaya mwaka 1975. Mahakama hii ilikuwa ni Mahakama ya Tarafa ya Liwale, na mpaka sasa Wilaya inaendelea kutumia kibanda hiki kidogo

kinachofanana na Mahakama za Mwanzo. Katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, ni lini Wilaya ya Liwale itapata jengo kubwa la Mahakama linalolingana na hadhi ya Wilaya?

Mheshimiwa Spika, siyo kitu chema sana kudai jengo la Mahakama kubwa na zuri, kwani Mahakama siyo mahali pazuri. Lakini jengo hili chakavu la Mahakama liko katikati ya Mji na hivyo kuleta sura mbaya ya Mji wetu wa Liwale.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikilalamika kuhusu jengo hili kuu kuu, ila Mahakama sasa ni mwaka wa tatu, ni vyema Serikali itujengee jengo lingine jipya la Mahakama.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina jukumu kubwa la kutoa haki kwa wananchi na sasa jukumu kubwa la kusimamia na kuleta Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Kibaha Mjini, tunayo kero kubwa sana ya Mahakama ya Mwanzo. Jengo la Mahakama ya Mwanzo kwanza liko kwenye eneo la barabara likitizama uwanja wa bwawani pale Maili Moja.

Mheshimiwa Spika, kama hii haitoshi, jengo hili ni la udongo na miti na linavuja kiasi kwamba haiingii akilini kama kweli hili ni jengo la Serikali, tena Mahakama inayotakiwa kusikiliza malalamiko, na makosa mbalimbali ya wananchi na kuyatolea maamuzi ya haki. Hata watumishi katika Mahakama hii waweza kutoa maamuzi mabaya kwa ajili ya athari wanazopata kutokana na mazingira haya mabaya ya jengo hili la Mahakama wanapotendea kazi zao.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Serikali itoe majibu kuwa ni lini jengo jipya la Mahakama ya Mwanzo litajengwa na kukamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi wa Kibaha Maili Moja. Naomba Waziri atolee jambo hili maelezo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za kibajeti (yaani kifedha) tulizonazo, ni wazi kwamba sasa Idara ya Mahakama ni lazima nayo iendane na teknolojia ya kisasa. Kwa sasa hivi, maelezo ya watuhumiwa, watuhumu na mashahidi huchukuliwa kwa kunukuliwa na kuandikwa na Hakimu, tena kimuhtasari katika jalada husika. Jambo hili huchangia katika mambo matatu. Kwanza, ni kazi ngumu, lakini Hakimu kuweza kurekodi tofauti na maelezo au maana halisi ya maelezo ya wahusika; pili, ni rahisi kuruka au kukataa maelezo hayo na tatu ni rahisi kukaribisha rushwa kwa kubadili maana halisia ya maelezo na hata kupotea au kupotezwa kwa maelezo na faili ya kesi husika.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Serikali iweke mitambo ya kisasa ya kurekodi maelezo ya watuhumiwa, watuhumu, mashahidi na hata Mahakimu na Wazee wa Mabaraza au Mahakama ili ukweli wa maelezo ya wahusika yaweze kutunzwa na hata hapo hukumu inapoandikwa Mahakimu waweze kuzingatia maelezo sahihi ya sauti ya wahusika. Hii ni rahisi na ni mfano halisi wa jinsi *Hansard* ya Bunge inavyorekodi majadiliano mbalimbali ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kuwa Wizara ina jukumu kubwa la kusimamia mchakato wa Katiba mpya ambayo ndiyo sheria mama ya nchi yetu. Ninashauri uwepo umakini mkubwa ili nchi ipate Katiba itakayoleta utengamano, amani na msukumo wa maendeleo kwa wananchi, Katiba itakayotoa changamoto za kuipeleka Tanzania katika hatua bora za kimaendeleo yenye kumwajibisha kila Mtanzania ashiriki katika ujenzi wa Taifa huku akihakikishiwa usalama na maisha bora.

Mheshimiwa Spika, niitakie Wizara kila la kheri. Naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, Kitabu cha hotuba ya Waziri kinaelezea vizuri changamoto mbalimbali na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo. Mojawapo ya changamoto hizo ni, uwezo na uelewa mdogo wa wananchi walio wengi kutumia vyombo vya

kutoa haki na huduma za kisheria kuhusu mfumo uliopo wa Sheria (ukurasa wa 45) na Wizara inapendekeza mkakati wa kuendelea kutoa elimu ya Sheria na kusogeza huduma za kisheria kwa wananchi (ukurasa wa 46).

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, tatizo la msingi zaidi kwa wananchi wengi Vijijini na Mijini ni kwamba raia wengi hawazifahamu haki zao za kikatiba na kisheria. Ujinga wa raia wengi kuhusu haki zao mbalimbali ni chanzo kikuu cha dhuluma na hujuma mbalimbali ambazo wananchi (hasa wa Vijijini) hufanyiwa na Polisi na vyombo vya kutoa haki. Wananchi wanapobambikiwa kesi au taratibu za utawala bora zinapovunjwa, wananchi wengi hawajui wafanye nini kwa sababu aina ya haki iliyovunjwa hawaifahamu. Wizara ina mpango gani wa kuwaelimisha wananchi kuhusu haki zao kama zinavyosimamiwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora?

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mambo ambayo Wizara imejipangia kufanya mwaka 2013/2014, ni “Kutafsiri Sheria kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili” (ukurasa wa 54). Naipongeza Wizara kuendelea na zoezi hili ambalo litasaidia kuondoa kikwazo cha lugha kwa uelewa wa wananchi wa sheria. Ninavyokumbuka, tafsiri ya sheria zetu kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili ni pendekezo lililotolewa pia katika Mkutano wa Bunge la Bajeti wa mwaka 2012/2013 na baadhi ya Wabunge (pamoja na mimi). Naipongeza na kuihimiza Wizara iongeze juhudi zaidi katika shughuli hii ili hatimaye sheria zote ziwe katika lugha ya Kiswahili. Swali langu hapa ni hili: Je, Wizara imepanga kutafsiri Sheria ngapi kwa Kiswahili? Mwaka 2012 ilitafsiri sheria ngapi? Wizara ina mpango mkakati wowote wa kukamilisha zoezi la tafsiri la sheria zetu zote?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono ushauri wa Kamati ya Katiba na Sheria kwamba Miswada yote mipya ya sheria inafaa iandaliwe kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Ushauri huu ukitekelezwa, Serikali itakuwa imefanikiwa kuifanya sheria kuwa karibu na wananchi kwa kuwa itakuwa katika lugha wanayoifahamu. Wizara ijipange ili itekeleze ushauri huu.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho nitakaloongelea ni ucheleweshwaji wa mashauri ambao pia umetajwa na taarifa ya Kamati. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 7 - 15, imetaja mashauri mbalimbali ambayo yanaonyesha kuwa kuna mashauri mengi ambayo hayajashughulikiwa. Tatizo hasa ni nini?

Mheshimiwa Spika, mfano wa kutisha wa ucheleweshwaji wa mashauri niliuona katika Gereza la Kahama nilipolitembelea mwaka 2012. Gereza hili lina mahabusu kutoka Wilaya ya Mbogwe, Bukombe na Kahama. Mahabusu wengi wamo ndani kwa tuhuma ndogo ndogo, ingawa wengine wanakabiliwa na tuhuma za jinai.

Niliongea na Mahabusu na lalamiko lao kubwa lilikuwa kucheleweshwa kwa kusikilizwa kwa mashauri. Baadhi ya mashauri hayajasikilizwa kwa zaidi mwaka au hata miaka miwili. Ushauri wangu kuhusu ucheleweshwaji wa mashauri ya mahabusu wa Bukombe na Mbogwe katika Gereza la Kahama ni huu ufuatao:-

(1) Pendekezo langu la mwaka 2012 kuhusu Wizara kujipanga ili adhabu mbadala ianze kutumika, lifikiriwe haraka. Njia hii itasaidia kupunguza msongamano katika Magereza kama ya Kahama.

(2) Tatizo linalowakabili mahabusu wa Bukombe na Mbogwe ni kwamba mashauri yao yanasikilizwa katika Mahakama za Bukombe. Inabidi wasafirishwe kutoka Kahama hadi Ushirombo. Tatizo ni kwamba kuna wakati ambapo gari lipo na wakati mwingi hakuna gari. Wizara itawasaidiaje mahabusu hao ili mashauri yao yaharakishwe kusikilizwa?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nkasi ilianzishwa, leo hii ina umri wa miaka 37, ajabu hatuna Hakimu wa Wilaya. Ina wakazi wapatao 420,000 na Kata 17, Tarafa tano, Vijiji 98 Vitongoji 12. Wananchi wanapata taabu sana, wanafika Namanyere, Hakimu kutoka Sumbawanga hafiki Namanyere, wananchi wanapoteza

nauli zao na muda wao, acha gharama za chakula na malazi. Je, hii ni utawala bora?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nkasi imekamilika kwa kila Idara, maana hakuna Idara haina Mkuu wake, kasoro ni huyo Hakimu wa Wilaya, Idara mpya kabisa ya TAKUKURU nayo ina Bosi wa Wilaya, hata Uhamiaji, *OCD* Afisa Usalama wa Wilaya wote wako.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanateseka, wengine wanatembea kwa miguu wafike Wilayani halafu Hakimu hayupo. Je, huo ni uungwana? Nauli yake ni juu sana, mfano mtu wa Kala, Wampembe lazima apitie Sumbawanga, Itindi hakuna njia, ni mguu njiani. Kwa mfano, kutoka Kabwe hadi Namanyere Kilometa 67, kutoka Itindi hadi Namanyere Kilometa 85, kutoka Kirando hadi Namanyere kilometa 60, kutoka Namanyere hadi Sumbawanga kilometa 100, kutoka Wampembe hadi Namanyere kilometa 100 na kutoka Kala hadi Namanyere kilometa 150.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu mhimili huu wa Mahakama ukaongezewa fedha za kutosha hususan za miundombinu kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama za Mwanzo Wilaya na Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, maombi ya Mahakama ya Mwanzo Ludewa na Manda Ludewa itajengwa lini? Kwani ni Bajeti ya tatu sasa ninakumbushia.

Mheshimiwa Spika, huduma za *RITA* ni muhimu zikawa *Decentralized.* Ni lini maeneo ya *Local Government* yatapata huduma hii ya Wakala *RITA* Vijijini na Wilaya zote nchini?

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni lazima iwe na tafsiri ya Kiswahili kwa Sheria zote. Ni lini jambo hili litafanyika?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Je, Bajeti ya Bunge la Katiba ipo wapi?

Mheshimiwa Spika, aidha, taarifa za Tume ya Haki za Binadamu kwa mujibu wa kanuni zinapaswa kuwasilishwa Bungeni: Ni lini taarifa hizi zitaletwa Bungeni?

Mheshimiwa Spika, aidha, napongeza uwazi uliotumika kuwapata Wajumbe 19,182 wa Baraza la Katiba.

Mheshimiwa Spika, usikilizwaji wa mashauri napongeza, ila unapaswa kuongeza kasi. Mahakama Kuu takwimu zinaonyesha kuwa *Speed* inapaswa kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, napongeza suala la *Paralegals* na naomba sheria ije haraka Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria za Migogoro ya Ardhi, nashauri Mabaraza yawe chini ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, vile vile napendekeza kwamba *Law Reform Commission* irekebishe Sheria zilizopitwa na wakati, mapema.

Mheshimiwa Spika, Maazimio, *"International Concentions"* ni muhimu tukawa na Idara *(department)* inayoonyesha maazimio tuliyoridhia na utekelezaji wake. Hivi sasa ni vigumu sana kufuatilia maazimio yaliyopitishwa. Aidha, tunahitaji *Matrix*, Vitabu na *CD*.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana huduma ya *registration USBRI* na naomba isambazwe mapema sana. Je, wale ambao ni *six years,* inakuwaje?

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu uimarishaji wa mafunzo kwa vitendo *(Law School).* Wanafunzi hawa ni muhimu sana wakazingatiwa katika Bodi ya Mikopo, hivyo ningeomba kujua jitihada za Wizara.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kiendelee kutoa elimu kwa wafanyakazi wengi, na kikidhi *quality* ya kufundisha Majaji na Mahakimu. Aidha, wakati umefika sasa wa kutoa huduma za Kimahakama kwa mitandao *(E-Judiciary)* na hivyo kuhama kutoka *typewriter* kwenda *computer*.

Mheshimiwa Spika, kodi ya pango imekuwa kubwa na hivyo ipo haja ya kupata majengo ya Wizara ili yatumike kwa ajili ya Mahakama nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa bajeti na raslimali watu, tunahitaji *political will*. Vile vile kuwepo na *House Allowance* kwa Mahakimu na Majaji ambao hawana nyumba.

Mheshimiwa Spika, ni lini Kamati ya Maadili ya Mkoa na Wilaya za Njombe zitapewa elimu?

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati *KSU* ilishauri uwepo utaratibu wa *OPRAS* kwa Majaji – *Open Performance Apraisal System* ili kupunguza *back log.* Je, Wizara imefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na kazi nzuri ambazo Wizara na Taasisi yake wamekuwa wakifanya, Kamati ya *KSU* itahitaji kuonana na *Law Reform Comission, LHRC* na Kutembelea Chuo cha Mahakama Lushoto na Mahakama ya Wilaya na Mwanzo Mkoani Dodoma katika kipindi hiki cha Bunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenasheria Mkuu wa Serikali!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, najua kwamba umeshalitolea uamuzi jambo hilo, lakini kwa kweli ni kinyume na Kanuni kwamba ili uweze kufahamu kama taarifa hii inastahili kuwasilishwa Bungeni, ni lazima kwanza uwe umeiona na kuna Kanuni inasema ziwasilishwe siku mbili kabla ya kufika hapa. Hata hivyo, hili limefanyika lakini nafikiri kwenye Kamati ya Uongozi tulizungumze vizuri.

Ninachosema ni kwamba nafikiri tuepuke kama Wabunge kufanya mambo kama wanafunzi wanaoficha kazi zao kwa ajili ya kuwashtukizia wenzao kwenye mitihani au kwenye semina.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Mathias Meinrad Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria ambaye ameiweka Mezani kwako asubuhi ya leo. Aidha, napenda kutumia nafasi hii kufafanua baadhi ya hoja na kutoa majibu kwa maswali yaliyoulizwa kuhusu Ofisi ninayoiongoza ambayo Waziri ameiombea fedha.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niseme kwamba ninaunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kuna mambo ambayo yamesemwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ambayo inaongozwa na Dkt. Pindi Hazara Chana na ambayo ilisomwa na Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe. Nawashukuru sana, naishukuru sana Kamati kwa ushauri iliotoa, ushauri mahsusi kuhusu Ofisi yangu na Divisheni zake lakini pia kwa moyo waliotupa na tunaupokea ushauri wao kwa moyo mmoja kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu suala la weledi kwenye suala la mikataba, Wabunge wengine pia wamechangia suala hili. Naomba kutoa taarifa Bungeni kwamba tumeanza kutoa mafunzo mahsusi yaani *specialised training* kwenye eneo la mikataba kwa ufanisi yaani badala ya kusoma tu, lakini tunatumia pia mikataba ya zamani kama ni njia ya kujifunza namna ya kusonga mbele. Kwenye maeneo ya gesiasilia, uchimbaji wa mafuta, mikataba ya uchimbaji wa madini, yote hiyo tunaifanyia kazi na zimeshatengwa fedha kwa ajili hiyo, shilingi 2,340,211,000/= zimetengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Waandishi wa Miswada, tunapokea ushauri kwamba Miswada iandikwe kwa lugha ya Kiswahili na kwa Kiingereza. Kazi hii imeanza

isipokuwa tu niseme kwamba zipo changamoto za kibajeti pamoja na mafunzo ambazo tumeamua na zenyewe kuzishughulikia.

Mheshimiwa Spika, kwenye usimamizi wa Mashauri ya Jinai, mafunzo yatatolewa. Tunashukuru kwamba zimetengwa fedha za kutosha kwa ajili hiyo kwa mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hoja ya Muswada wa Marekebisho wa Sheria ya Bodi ya Mikopo, naomba kutoa taarifa kwamba leo saa 4.30 asubuhi tulipokea Rasimu kutoka kwenye Wizara inayohusika. Tunaahidi kwamba tutaishughulikia na baada ya kupitia kwenye vyombo vya maamuzi, tutaleta Muswada huo hapa Bungeni mapema iwezekanavyo. Hili suala ni muhimu kwa kila Mbunge na kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la lingine ni lile ambalo dada yangu Mheshimiwa Sabreena Sungura alikuwa analizungumzia.

Kwanza, namshukuru sana, nilipokuwa natikisa kichwa nilikuwa nakumbuka kwamba Waheshimiwa Wabunge walitunga sheria ambayo iliweka mahusiano kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Maafisa Sheria katika Wizara na katika Serikali za Mitaa. Nampongeza sana kwa kutetea maslahi ya Wanasheria wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lilitunga Sheria Na. 4 ya Mwaka 2005 na sheria hiyo inaweka mahusiano ya Mawakili wa Serikali na Maofisa wengine wanatekeleza majukumu ya sheria katika Wizara, Idara na Serikali za Mitaa.

Kama inavyofahamika, mamlaka haya ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni ya Kikatiba. Jukumu la kuishauri Serikali kwenye mambo ambayo yameainishwa kwenye sheria hiyo ambayo Bunge lilitunga, ni mamlaka ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, mtu yeyote anayetekeleza mamlaka hayo, ni yule mtu ambaye kwa mujibu wa sheria, ameelekezwa kufanya hivyo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Maafisa walioko Wizarani, kwa kweli naomba kutumia nafasi hii kuwaomba kwamba Sheria inawataka kwenye Sheria ambayo imetungwa hapa Bungeni Kifungu cha 26 cha Sheria ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wajiandikishe kwenye daftari la Wanasheria na sisi wako wengine tunawatumia, siyo kwamba hatuwatumii, tunawatumia na wengine ni wazuri, isipokuwa katika suala la maslahi, yaani mishahara, ni vizuri tufanye tofauti. Tofauti ya msingi ni kwamba mimi sihusiki na mishahara yao. Mishahara yao inahusiika na sehemu ambayo wanafanyia kazi. Ila ninahimiza kwamba suala hili na lenyewe tutaliangalia ili maslahi ya Wanasheria hawa nayo yasiwe haba.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa majengo, ni kweli kuwa tuna tatizo na tunachukua hatua za kulikabili. Kwa kweli ukosefu wa Ofisi za kukaa pamoja na majengo katika Wilaya na katika Mikoa ni kweli yapo na tunashukuru kwamba safari hii fedha tulizozipata zinatuwezesha kusonga mbele. Hivyo hivyo kwenye Watumishi wachache na kuongeza bajeti *DPP* pamoja na suala la kufungua Ofisi za Kanda, kwa bajeti ambayo tumefanya, nafikiri tutaanza kuendelea.

Kuhusu suala la Mheshimiwa Shibuda la kuongeza muda wa kusikiliza mashauri ya kesi za Uchaguzi wa Madiwani; kama mnavyofahamu Muswada wenye mapendekezo hayo ulishawasilishwa hapa Bungeni na ukasomwa mara ya kwanza. Kwa hiyo, hili jambo bado liko kwenye hatua hii.

Kuhusiana na suala la Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba Serikali itoe tamko kuhusu taarifa za uchunguzi wa mauaji wa Mwandishi wa Habari, Marehemu Daudi Mwangosi; ni kweli kuwa Tanzania imeridhia mikataba mingi, lakini mikataba ile siyo zaidi ya Katiba yetu. Ina-*supplement* Katiba. Katiba ni ya kwanza mikataba ile inafuata. Kwa

mujibu wa Katiba yetu, hakuna mtu ambaye anaruhusiwa kutoa uhai wa mtu mwingine bila kufuata utaratibu wa kisheria. Kwa ajili hiyo, tukio ambalo linahusiana na Marehemu Daudi Mwangosi, ni kwamba upelelezi wake umekamilika na kwamba mtu atakayehusika atapelekwa Mahakamani. Nafikiri huo ndiyo utaratibu. Sasa kusema kwamba tutoe tamko, nafikiri tusubiri kwanza utaratibu huo wa Kimahakama.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni hili la ushauri wa Ofisi ya *DPP*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga hoja mkono na ninashukuru kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja zilichochangiwa na Waheshimiwa Wabunge kwa Taasisi mbalimbali zilizoko katika Wizara ya Katiba na Sheria. Yako maeneo mengi yaliyochangiwa, lakini kutokana na ufinyu wa muda, nitatoa majibu kwa maeneo machache na Mheshimiwa Waziri atajibia maeneo mengi zaidi kwa kina. Baada ya kusema hayo, naomba sasa kujibu hoja hizo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwanza na hoja zilizotolewa na Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, ambapo katika hoja ya kwanza Kamati ilieleza kuwa ni vyema taratibu za kuhakikisha kwamba wananchi walio wengi wanaipata haki kwa kupata huduma za kisheria zikamilishwe mapema. Serikali imekwishafanya maamuzi, hivi sasa Wizara ya Katiba na Sheria inaandaa taratibu za kuandika Muswada wa Sheria ambao pindi utakapokamilika katika mwaka huu wa fedha utawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kutungiwa Sheria.

Kamati pia imetutaka kutulia mkazo upembuzi yakinifu wa mradi mkubwa wa *Tele- Justice* na kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kupitia hotuba yake

ya asubuhi alivyokuwa ameeleza, hivi sasa zoezi la upembuzi yakinifu linakaribia kukamilika, na hivi sasa Kamati ya Ufundi iko katika Mikoa mbalimbali ya Kanda zetu ili kuweza kufanya utafiti, lakini pia kuweza kupata takwimu sahihi kabla ya kusimika mitambo hiyo ambayo itasaidia sana kuendesha mashauri Mahakamani kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Tume ya Kurekebisha Sheria, tumetakiwa kukamilisha haraka taarifa ya mapitio ya sheria zinazosimamia usuluhishi na utatuzi wa migogoro ya ardhi pamoja na Sera ya Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, kwani hivi sasa ni Wizara zaidi ya tatu zinashughulikia utatauzi wa migogoro ya ardhi. Tumepokea ushauri huu, na taarifa kuhusiana na sheria husika imekwishakamilika na tunatarajia wakati wowote katika mwezi huu wa Mei mwaka huu 2013 itawasilishwa Serikalini kwa ajili ya hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, tumetakiwa pia kupitia Tume ya Haki za Binadamu, wametakiwa kuongeza jitihada za kutoa elimu kwa Umma kuhusiana na uelewa na kuheshimu sheria; tumepokea ushauri huu, tutazingatia na kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali iipatie fedha za kutosha Tume ya Haki za Binadamu ili waweze kuchapa ripoti zao za kila mwaka; ushauri huu pia tumeupokea, lakini hivi sasa kutokana na ufinyu wa bajeti ndiyo maana wamekuwa wakishindwa kutekeleza kuchapisha ripoti zao kwa wakati. Lakini tutakuwa tukiendelea kujenga hoja ili fedha zaidi ziweze kutolewa na waweze kuendana na wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana Wakala, Ufilisi na Udhamini *(RITA)*, wametakiwa kuharakisha Mpango wa Usajili wa Watoto Walio na Umri wa Chini ya Miaka Mitano na kwamba mpango huu usambazwe katika Wilaya zote nchini ili kuhakikisha kuwa watoto wote walio chini ya umri wa miaka mitano ambao hawajasajiliwa waweze kupata usajili. Tumepokea ushauri huu na ndiyo maana hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri pia, kwenye hili alilisemea kuwa tunao mpango mahsusi kabisa na kwa mwaka huu, tutaanza na Mikoa mitano; Mkoa wa Mbeya, Shinyanga, Simiyu, Geita

pamoja na Mwanza, kwani katika ripoti ya Tanzania *Demographic Household Surveyor* ya mwaka 2010 ndiyo ambayo iliainishwa kwamba ina kiwango cha chini kabisa cha usajili; na kama mnavyofahamu ni 6.2% ya watoto walio chini ya umri wa miaka miatano ndiyo wamesajiliwa na umri mwingine zaidi ya miaka sita kwenda juu ni 7.7% tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunalitilia mkazo, na ukiangalia katika bajeti hii, tumetenga Shilingi bilioni moja kuhakikisha mpango huu unatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali ihakikishe inaipatia fedha *RITA* kiasi cha Shilingi bilioni 17 ili zilipwe kwa ujenzi wa *RITA* linalojengwa kwa ubia na *NSSF* ili kukwepa riba kubwa itakayojitokeza endapo fedha hizo zitachelewa kulipwa. Ushauri huu wa Kamati tunaupokea. Hivi sasa Wizara ya Katiba na Sheria inafanya mawasiliano na Hazina ili kuweza kufanikisha azma hii.

Kuhusiana na hoja mbalimbali za Mbunge mmoja, mmoja Mheshimiwa Ali Khamis Seif yeye alitaka kasi ya kumaliza mashauri ya ardhi iongezwe. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Mahakama imekuwa ikijitahidi sana na kuanzia mwaka 2012 ambapo Majaji kumi walioteuliwa kwa mara ya mwisho mahsusi kabisa, Mheshimiwa Jaji Mkuu aliwapangia waweze kusikiliza mashauri ya ardhi.

Mwaka 2012 waliweza kumaliza mashauri 908 ya ardhi na hivi sasa wapo wanakamilisha mashauri mengine 131 na kasi kwa kweli imekuwa ikienda vizuri sana. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mashauri haya yatapungua na ni lengo la Mahakama kumaliza kabisa mashauri haya ya ardhi ambayo mengi yao yamekuwa ni ya muda mrefu.

Mheshimiwa Augustine Mrema - Mbunge wa Vunjo, ameomba tuharakishe kesi ya ardhi inayomhusisha Augustino Temu na wenzake 768 kwamba kesi hii imekaa muda mrefu, imechukua takribani miaka 11. Ni kweli kesi hii imechukua

muda mrefu, lakini sababu kubwa iliyopelekea ucheleweshaji ni maombi mbalimbali ambayo yalikuwa yakitolewa na wadaawa waliotaka kujiunga kwenye kesi hii na pingamizi mbalimbali za awali ambazo zilikuwa zimeandikishwa. Tunao mpango mkakati na tumeiweka kesi hii katika mkakati maalum wa Mahakama wa kuondoa mashauri ya zamani na tunaamini itamalizika haraka iwezekanavyo. Tuombe tu ushirikiano wa pande zote ili kesi hii iweze kumalizika mapema.

Mheshimiwa Silvestry Koka pamoja na Mheshimiwa Mustapha Akunaay wameitaka Serikali kupitia Mahakama ijitahidi kuongeza matumizi ya *TEHAMA* katika kurekodi mashauri. Ushauri huu tunaupokea na hivi sasa tulishaanza awamu ya kwanza ambapo mitambo ilisimikwa katika Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu pamoja na *Division* zote tatu za Mahakama Kuu; *Division* ya Biashara, *Division* ya Ardhi pamoja na *Division* ya Kazi. Kama ambavyo nimeeleza awali kupitia mradi wa *Tele-Justice* ambao tunao, tunaamini azma hii itaweza kuzingatiwa na tutaikamilisha.

Mheshimiwa Diana Chilolo ametoa rai tuangalie uwezekano wa kuongeza posho za Wazee wa Baraza. Ushauri huu tunaupokea na ndiyo maana hata mwaka 2012 posho ya Wazee wa Baraza iliongezwa. Lakini pia tunaangalia uwezekano wa kuwapatia vivutio vingine, mfano huduma ya afya kupitia Mfuko wa Jamii ili na wenyewe waweze kupata huduma hii ya afya, kwani tunaamini kiwango hiki cha fedha wanachopatiwa bado hakitoshi kulinganisha na kazi kubwa na nzuri wanayoifanya kwa ajili ya Mahakama.

Mheshimiwa Keissy, Mbunge wa Nkasi Kaskazini ameelezea mahitaji ya Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Nkasi. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge mara moja tutapeleka Hakimu katika Mahakama ya Wilaya ya Nkasi.

Mheshimiwa Raya Khamis pamoja na Mheshimiwa Esther Matiko, wameongelea masuala ya rushwa iliyoko katika Mahakama. Suala hili kwa kweli tumekuwa tukiliongelea mara kwa mara katika Bunge hili, tunatambua

wote kwamba rushwa ni kosa la jinai, lakini pia zipo kanuni za Maadili za Mahakimu wetu na Majaji ambazo wanaongozwa nazo, na zipo Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya ambazo zimekuwa mara zote zikifanya kazi nzuri. Pindi itakapothibitika kuwa kuna tuhuma za rushwa na kwamba kweli wametenda vitendo hivyo, Tume imekuwa ikiwachukulia hatua wote waliohusika na vitendo hivyo.

Kwa hiyo, nitoe tu rai kwa Waheshimiwa Wabunge, endapo watakuwa na ushahidi watakapokuwa wanasikia, basi waweze kufikisha malalamiko haya katika Kamati za Maadili ngazi ya Wilaya kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, lakini katika Kamati za Madili za Mikoa kwa Mahakimu wa Wilaya pamoja na Mahakama za Hakimu Mkazi. Mheshimiwa Eugine Mwaiposa, ameelezea tatizo la wananchi wengi kukosa Elimu ya Sheria za Msingi, jambo linalopelekea wananchi hao kudhulumiwa haki zao.

Mheshimiwa Spika, tunapokea ushauri huu, tunaelewa tatizo hili. Lakini Serikali imekuwa ikiweka mikakati mbalimbali ya kuongeza uelewa wa Sheria kwa wananchi. Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa ikiendesha vipindi mbalimbali katika runinga zetu, katika redio lakini pia tumekuwa tukitoa makala katika magazeti.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtoa Hoja!

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuhitimisha hoja yangu ambayo nimeileta kwako leo asubuhi. Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wachangiaji wote waliotoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ambayo wangependa Wizara yangu iyachukue ili kuboresha utendaji katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni ya jumla tu hasa kuhusu hotuba ya Kambi ya Upinzani. Siyo hotuba

mbaya, isipokuwa tu, kwa ujumla, lugha iliyotumika, kidogo hairidhishi. Unapodhani kwamba Tume ya Marekebisho ya Katiba ni sehemu ya ulaji na unawatazama Wana-Tume wale, unasema Mzee Warioba ndio mlaji mwenyewe, au Salim Ahmed Salim ndio mlaji, kwa kweli unasema ah, labda angesema jambo lingine au lugha nyingine, kwani hawa wazee tunawaheshimu sana. Ni wazee ambao wanafanya kazi hii kwa kujitolea tu. Hawapati kitu chochote ukiondoa labda sifa itakayotokana na kazi nzuri ambayo watakuwa wamefanya mwisho, kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nasema pengine Mheshimiwa alitumia lugha hii kwa kuteleza tu. Sidhani kama alikusudia kuwafikiria wazee wale ni walaji. Nina uhakika kabisa hilo halimo kichwani mwake. Lakini nafikiri katika ujumla tu wa kudhani Serikali basi ni walaji, basi akadhania na Tume ni walaji. Tume ile ni ya watu makini sana, hawawezi wakaruhusu aina yoyote ya ufisadi utokee ndani ya Tume ile. *(Makofi)*

La pili, majibu yangu pia yatazingatia hoja na maoni ambayo yametolewa huko nyuma katika michango iliyotolewa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu na hotuba nyingine, nitajaribu kutoa majibu, maana mengine hayakuelezwa vizuri, nitachukua nafasi hii kuyaeleza hayo yaliyotolewa katika hotuba hizo zilizopita. Lakini kabla sijaanza kutoa majibu kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani, naomba nitoe majibu ya taarifa ilitolewa leo hapa na Mwenyekiti au Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge, zilitolewa hoja mbalimbali. Moja ilikuwa ni juu ya changamoto ya ucheleweshaji wa mashauri Mahakamani, inayoendelea ambayo wanasema ni kikwazo katika mfumo wa utoaji haki hapa nchini.

Kwanza, niseme, hiyo ni changamoto kubwa na Wizara na Mahakama tunatambua kwamba idadi ya

mashauri ni mengi sana Mahakamani na kesi ya kuyashughulikia haijawa nzuri ya kuridhisha. Sasa tumechukua hatua mbalimbali ya kupambana na changamoto hii.

Moja, tunajaribu kuhakiki takwimu za mashauri katika Mahakama zote nchini na tumepitia katika Mahakama kadhaa, tumegundua kuwa kesi nyingine zilizoko pale zinaitwa kesi lakini siyo kesi, kwenye majalada hakuna kitu. Kwa hiyo, tunapitia na kuhakiki na tutagundua baadaye kwamba tuna kesi ngapi ambazo kweli zipo na zinahitaji kushughulikiwa. Takwimu tulizonazo sasa zinaonyesha kama tuna kesi nyingi, lakini kwa utafiti huu wa Masjala chache ambazo tayari wataalamu wa Mahakama wamezipitia, wamegundua kwamba jambo hili siyo kweli, lakini tunangoja taarifa yao kamili, ndiyo tutajua kwa uhakika zaidi kuwa ni kesi ngapi zipo na mlundikano huu ni wa kiasi gani hasa, na tutazidi kutafuta njia za kuukabili.

La pili tulilofanya, tumejaribu kuongeza idadi ya Mahakama kwenye *Extended Jurisdiction.* Kwa kipindi hiki kifupi, tumeongeza kama thelathini hivi ili waweze kujaribu kusaidia kupunguza kesi ambazo zipo katika Mahakama zetu kuu. Sasa tunaandaa *Program* Maalum tunaita *Cleanup Program* kwa ajili ya kupunguza kesi za zamani ambazo zimelundikana katika Mahakama zetu. Maandalizi haya yamekwishakamilika, tulikuwa tunangoja bajeti hii na ninaomba Waheshimiwa Wabunge mtupitishie bajeti hii ili tuanze na na *Cleanup Program* yetu ya kuondoa mashauri yaliyopo katika Mahakama zetu ambayo hayajashughulikiwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nimewatolea leo asubuhi takwimu mmeziona, siyo nzuri na wala haziridhishi. Kwa hiyo, nawaomba mtupitishie bajeti ili tuanze progaramu hii tufanye kazi. Pia tutajaribu sana kadri inavyowezekana, kutumia njia mbadala za kumaliza mashauri. Kuna Waheshimiwa Wabunge wamezungumza hapa, nafikiri alikuwa ni Mheshimiwa Akunaay, nafikiri amezungumza kuhudu *ADR* na ni muhimu sana. Jambo hili siyo la kupenda, ni jambo la kisheria liko ndani ya sheria na sisi tutalitekeleza ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine iliyozungumzwa, Waheshimiwa Wabunge walisema kuwa kuna vitendo vya rushwa vimeendelea kujitokeza na hali hii inasababisha wananchi kukosa imani na Mahakama kama chombo cha utoaji haki. Ushauri huu tumeupokea. Tatizo la rushwa katika nchi yetu, tatizo la rushwa duniani ni tatizo kubwa sana. Katika nchi yetu tunazo hatua mbalimbali ambazo tumezichukua kupambana na tatizo hili. Tunacho chombo cha TAKUKURU ambacho kinajitahidi na tunaendelea kukiongezea nguvu mwaka hadi mwaka ili waweze kupambana na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini Waheshimiwa Wabunge pia mtakubali kuwa vitendo vya rushwa vimepungua katika Mahakama zetu kutokana na juhudi za makusudi ambazo tumezifanya sasa hivi katika kupambana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ukosefu wa majengo ya Mahakama za Mwanzo na niseme Mahakama zote; Serikali tunalitambua tatizo hili, tuna upungufu mkubwa sana wa majengo ya Mahakama. Huko nyuma wakati wa Ukoloni, majengo haya yalikuwa yanajengwa na Halmashauri. Sasa Halmashauri hazijengi tena, na kwa kipindi fulani tukasema Mahakama ndiyo itajenga. Sasa Mahakama bajeti yake imekuwa finyu kila mwaka, na hata mwaka huu tumeomba, lakini bado ni finyu. Kwa hiyo, tutachukua hatua za makusudi kupambana na jambo hili. Tumeeleza katika mikakati yetu kwamba tunatakiwa kujenga Mahakama na tutajenga Mahakama za Mikoa; kwanza *High Courts* katika Mikoa minne, halafu tutajenga Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Kati kwa kadiri uwezo utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizungumzia pia suala la machapisho ya ripoti za maamuzi ya Mahakama, yaani *Tanzania Law Reports* kuanzia mwaka 1998 mpaka mwaka 2006 kwa ajili ya Mawakili na kwa ajili ya Umma. Ni kweli, taarifa hizi hazipatikani, Mawakili wanapata taabu sana wakienda Mahakamani, sana sana akiwa na Hakimu au Jaji rafiki, ndio anaweza akatoa kopi pale kwake, lakini hawajapata nafasi ya kuzinunua.

Mheshimiwa Spika, sasa jambo hili, tunasema Mahakama inatengeneza kwa ajili ya watumishi wake. Bado hatujaweka utaratibu ni jinsi gani tutazipata hizi. Nimeongea na wenzangu kwa kirefu sana, hizi *Law Reports* tuwaachie *Private Sector* wazitengeneze, waziuze, tumeona *private sector* yetu kidogo kwa upande huu iko dhoofu, ni *weak*. Kwa hiyo, tunadhani labda hapo baadaye Wizara itakaa tena na kujipima ubavu na kuona kama Wizara inaweza ika-*undertake* jukumu hili na baadaye basi vitabu hivi vikauzwa kwa watu wote ambao watavihitaji ili kuvitumia.

Mheshimiwa Spika, *issue* nyingine iliyoletwa mbele yetu ni kuhusu Wasaidizi wa Sheria wa Majaji kwamba wanafanya kazi bila kuapishwa kama Maafisa wa Mahakama *(Judicial Officers)* toka walipoajiriwa. Sasa tumeliona hili. Vijana hawa wanafanya kazi za kuwasaidia Majaji, lakini katika kufanya kazi hiyo, wanakutana na mambo mengi, wanaona mambo mengi mazito, na kwa kweli wangepashwa waapishwe ili waweze kutunza siri za mambo hayo wanayoyaona. Baada ya kugundua hilo, tunasema kwamba kwa sasa hivi Mahakama ina jumla ya Wasaidizi wa Majaji 70 na wamegawanywa kwenye Vituo kama 13 hivi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi ilishatoa maagizo kwamba watu hawa waapishwe. Kwa hiyo, taratibu sasa hivi zimekwishaandaliwa na vijana hawa wataapishwa na Jaji Kiongozi, atakwenda kuwafuata katika Vituo hivyo 13, atawaapisha mmoja baada ya mwingine na tutakuwa tumeondokana na tatizo hili, tukiamini sasa watu wataheshimu viapo vyao na watafanya kazi kwa uaminifu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilituelekeza kwamba Mahakama ya Tanzania ishughulikie ununuzi wa vifaa vya kisasa kama vile kompyuta kuliko kutumia *typewriters* na pia kununua samani za Ofisi zinazotengenezwa nchini kwa ajili ya Mahakama zote Tanzania. Ushauri huu tumeupokea, ni ushauri mzuri. Hata hivyo, ipo changamoto ya Mahakama nyingi, kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge tunaotoka Vijijini kule umeme hakuna, kwa hiyo, katika

Mahakama za Mwanzo zile, ukisema sasa utapeleka kompyuta, utategemea kuweka *solar* na hiyo *solar* yenyewe inabidi nayo iingie katika bajeti ya ujenzi wa hiyo Mahakama. Lakini hili ni jambo ambalo tunaweza kulitekeleza katika sehemu zile ambapo umeme unapatikana kwa urahisi na hakuna matatizo ya nishati hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ili-*raise* suala la kusema kwamba kitendo cha Serikali kutokutoa fedha zilizokuwa zimetengwa mwaka wa fedha 2012/2013 kimekwamisha miradi ya ujenzi wa Mahakama za Mwanzo za Kawe, Bunda, Mangaka, Gairo, Bariadi, Lukuledi na Mkomazi. Kitendo hicho kishughulikiwe kwa fedha hizo kutolewa mara moja.

Mheshimiwa Spika, napenda niamini kwa ahadi ambayo tunaendelea kupewa na Wizara ya Fedha kwamba mwaka bado haujakwisha; “ninyi kwanini mnakuwa hivyo? Subirini ndani ya mwaka huu tutatekeleza ahadi zetu.” Kwa hiyo, nasi tunasubiri na tunaamini tukipata pesa hizo angalau tutakwenda haraka haraka, tuwaweke ma-*contractor* wafanye kazi kwa sababu pesa hizi hazitakuwa nyingi, kusema tutashindwa kuzitumia kwa kipindi kifupi Ni suala tu la kuweka watu waanze kazi. Kwa hiyo, tunategemea na sisi tunasubiri kama mnavyosubiri Waheshimiwa Wabunge. Tuendelee kusubiri, na Hazina watatekeleza ahadi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania ishughulikie upatikanaji wa fedha za kujenga majengo ya Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma, Mara, Lindi, Morogoro, Singida, Manyara, Katavi, Njombe, Simiyu na Pwani. Kati ya Mikoa 26 ya Tanzania Bara, kuna Mahakama Kuu katika Mikoa 13 tu. Mpango wa Serikali ni kuwa na Mahakama Kuu katika kila Mkoa.

Mheshimiwa Spika, ili kutimiza dhamira hii, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, kwamba mwaka ujao wa fedha, yaani mwaka huu mkipitisha bajeti hii, na nimesema kwenye bajeti yangu kwamba Wizara yangu itakamilisha ujenzi wa Mahakama Kuu ya Shinyanga na kuanza kujenga

Mahakama Kuu katika Mikoa ya Singida, Kigoma, Mara, Lindi, Manyara na Morogoro. Tutaendelea na ujenzi katika Mikoa iliyobaki kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete amelisisitiza sana. Amesema katika miaka miwili ijayo, ni lazima tumalize ujenzi wa Mahakama Kuu katika Kanda zote na katika Mikoa yote. Kwa hiyo, sisi tutafuatilia na wenzetu wa Hazina nina hakika wataendelea kutuelewa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Tanzania ishughulikie upatikanaji wa Watumishi wa fani mbalimbali wanaofikia 3,455 ili kuweza kutoa huduma kwa ufanisi; ushauri huu umepokelewa. Mahakama tayari imepewa kibali cha kuziba nafasi 139 zilizoachwa wazi, na Serikali itaendelea kuziba pengo hilo kadri uwezo wa kifedha utakavyoongezeka. Mawasiliano na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyotolewa na Kamati, inasema kwamba Mahakama ya Tanzania ishughulikie namna bora zaidi ya upimaji wa utendaji kazi wa Mahakimu na Majaji ili kuongeza ufanisi wa utendaji wa Mahakama.

Nakubaliana na suala hili sana na toka awamu ya kwanza nilipokuwa Waziri wa Katiba na Sheria mpaka awamu hii, jambo hili lipo moyoni mwangu na nimekuwa ninalizungumza sana na wenzangu wa Mahakama na wenzangu bahati nzuri wamelikubali. Sasa wameandaa utaratibu ambao utakuwa na uwezo wa kupima utendaji kazi wa kila Jaji anafanya kazi kiasi gani. Wale wanaosikiliza kesi kumi kwa mwaka na wale wanaosikiliza kesi 100 kwa mwaka, sasa atajulikana, na hatua zitachukuliwa kwa yule ambaye hatekelezi wajibu wake. Haya wamefanya wenyewe, wamekubaliana, sasa kilichobaki ni utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwangu kama Kiongozi, ni kutizama na kusukuma na kuhakikisha jambo hili linafanyika

na kutekelezwa. Kwa sababu ni muhimu tujue, haiwezekani Majaji ninyi wote mnapata mshahara sawa, wote mnapata marupurupu sawa, halafu mmoja anafanya kazi kwa mwaka anaamua kesi 200, mwingine kwa mwaka anaamua kesi 10 au hata chini ya hapo. Haiwezekani! Hatuwezi kufanya kazi namna hiyo! Ni lazima tuwe na njia ya kupima ni kitu gani kinafanyika. Wazungu wanasema, "*what you can't measure, does not exist.* Kwa hiyo, ukishindwa kupima, ina maana hakuna. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na uwezo wa kupima na tutaendelea kuwasisitizia wenzetu ili waweze kufanya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la Mahakama kwamba itoe motisha kwa Mahakimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Motisha hapa nina hakika inayozungumziwa labda ni pesa au mikopo mbalimbali na kadhalika. Sisi tunasema, ni Sera ya Serikali kutoa motisha kwa wafanyakazi wote pamoja na Mahakimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Lakini ushauri huu tunaupokea na Serikali imeanza kutoa motisha kwa wafanyakazi na tutaendelea kufanya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilikuwa na maoni kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria. Kamati inasema: "Serikali ifuatilie kwa makini utendaji kazi wa Tume ya Mabidiliko ya Katiba bila kuathiri uhuru wa Tume ili kuwezesha nchi kupata Katiba mpya kwa wakati." Ushauri huu umepokelewa na unatekelezwa bila ya kuathiri uhuru wa Tume. Serikali kwa muda wote toka Tume hii imeundwa, imekuwa na sera ya *Eyes On, Hands Off*. Tunatazama, tunawa-*facilitate* lakini hatuwaingilii.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe ni mfano, nimekwenda Tume kutembea kuangalia ni nini kinaendelea. Lakini siyo kukagua kazi, wala kuuliza mnafanya nini, au mtafanya nini? Sizungumzi nao, hawazungumzi na mimi na mimi sitaki, kwa sababu mambo mengine usipoyajua ni bora zaidi kuliko ukiyajua. Mimi nikiyajua, pengine ni matamu sana, nitayasema. Nikiyasema nitakuwa nimeshaharibu, afadhali nisiyajue na siyajui, ninashukuru. Kwa hiyo, nawapongeza

Tume, wameendelea na msimamo wao wa kufanya kazi kama *Independent Board* na ndiyo kitu pekee kinachowaletea heshima na kitakachoendelea kuwaletea heshima katika kazi hii*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine tulishauriwa kwamba Serikali ishughulikie utoaji wa fedha zinazotengwa kwa matumizi ya Wizara na kutolewa kwa wakati. Ushauri huu utazingatiwa. Pesa zinapotolewa, sisi tutazitumia kama tulivyopanga. Zisipotolewa, tunasikitika kama wengine.
Mheshimiwa Spika, tulishauriwa kwamba Serikali iweke kipaumbele katika kutekeleza miradi ya maendeleo na kutenga fedha za ndani kwa ajili hiyo kuliko kutegemea fedha za nje. Ushauri huu ni mzuri na mimi ninauzingatia sana. Ukitegemea mambo ya nje, huwezi kuwa na uhakika kama zitakuja, ama zitakuja lini. Ukiwa nazo mwenyewe ndani, basi una hakika zaidi ya kufanya mambo yako kama ulivyopanga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Kamati ya Sheria ilikuwa na mambo yafuatayo; wanasema Bajeti ya Bunge la Katiba ifahamike mapema na kuletwa Bungeni. Hili nimeulizwa hata nilipoingia hapa, Mheshimiwa Machali ameniandikia ki-*note* anasema zungumza kuhusu bajeti ya Bunge la Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu tuliojiwekea, bajeti ya kuendesha Bunge la Katiba haiko Wizarani kwangu. Bajeti hii itasimamiwa na Ofisi ya Bunge. Kwa hiyo, pesa zake sasa hivi ziko kwenye *Consolidated Fund*, itakapofika wakati wanazihitaji, watazitumia. Vivyo hivyo, kwenye uchaguzi, ile *referendum* itakayofanyika, fedha zile haziko Ofisini kwangu, wala Ofisi ya Tume. Zitakuwepo kwenye Tume ya Uchaguzi ambayo ndiyo itasimamia hiyo *referendum* na hizo zenyewe pia nazo ziko kwenye *Consolidated Fund* zitakapohitajika zitatolewa. Kwa hiyo, usipoziona kwenye bajeti hii ,ni kwamba hazipaswi kuwepo humu na hazipo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikuwa na neno moja la kusema kuhusu Tume. Walisema Tume ya Utumishi wa Mahakama iendeleze juhudi za kuelimisha wananchi kuhusu

uwepo wa Tume na majukumu yake ili kuwawezesha wananchi kutoa malalamiko yao juu ya ukiukwaji wa maadili ya Utumishi wa Mahakama. Nami nasema, Tume inaupokea ushauri huo na sisi tutaendelea kuwaasa waendelee kuzingatia ushauri huu mzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, kabla zijakwenda kwenye hoja ya Mbunge mmoja mmoja, nirudi kwenye hoja ya Mheshimiwa wa Kambi ya Upinzani aliyoitoa hapa Bungeni asubuhi hii. Kama wengine, hotuba hii imechelewa sana kutufikia, kwa hiyo, nasi tumeipata mchana ule, tumekwenda kuisoma kadri tulivyoweza kuisoma. Tutajaribu kujibu hoja zote au nyingi zilizoletwa katika hotuba ile.

Bahati nzuri hotuba hii kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka 30 na hii ni kati ya kurasa 42 imezungumza kuhusu Tume ya Katiba Mpya, na kurasa zilizobaki, imezungumzia kuhusu haki za binadamu, lakini hususan kesi ya Marehemu Mwangosi. Kwa hiyo, ni mambo mawili ya msingi, nami nitajaribu kwenda nayo kama yalivyokuja.

Mheshimiwa Spika, niseme mapema kabisa kwamba umetumika muda mwingi sana na kurasa nyingi katika hotuba ya Kambi ya Upinzani, ukurasa wa 14 - 17 ulikuwa ukimzungumzia mtu anayeitwa Beatus Kipea kwamba ameunguliwa katika Orodha ya Wajumbe waliochaguliwa, kutoka Kata ya Sembetini na kwamba imefanywa hivyo kwa sababu yeye siyo mwana-CCM.

Kwanza niseme kwamba taarifa hii siyo sahihi. Sitaki kusema ni ya uwongo, lakini nasema siyo sahihi. Aliyempa taarifa hii au aliyeandika taarifa hii, hakumwambia ukweli, kwa hiyo, naye akafanya jambo ambalo siyo sahihi. Bwana Beatus ni Mjumbe halali. Hadi kufikia tarehe 25 Mwezi huu wa Mei, taarifa nilizonazo mimi, Bwana huyu ni Mjumbe halali, na bado ni Mjumbe, na katika matangazo ya Wajumbe wote watakaokwenda kwenye Mabaraza ya Kata, jina lake limo na litatangazwa.

Mheshimiwa Spika, nashangaa kuambiwa kwamba kafutwa, sijui kwa sababu gani. Ndiyo maana nasema jambo hili siyo sahihi. Taarifa zangu hizi nimeletewa leo. Sina Kawaida ya Kuongea na Tume, lakini kwa hili nimeziomba. Wakaniambia Mratibu wa Tume ameleta taarifa rasmi kwamba Bwana huyo yumo na katika majina yatakayotolewa atakuwemo. Sasa inapoandikwa hapa zimetumika *page* 14, 15, 16, na 17 kuzungumzia jambo ambalo siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, unataka kujiuliza ukurasa wa 1 - 30 umesema nini ambacho ni sahihi? Maana *page* hizi tatu zote siyo sahihi. Hizi nyingine zimesema nini cha sahihi? Lakini tutakwenda nazo taratibu, nami nitajaribu kujibu hoja kwa hoja. Lakini hili suala la Bwana Beatus siyo la kweli, ni la uwongo. Wananchi mlijue hivyo! Bwana Beatus kama yupo mwenyewe anaweza kuthibitisha, maana hili limethibitishwa na Viongozi wa Tume, wanasema yumo katika majina ya wale watu wa Mabaraza na atatangazwa rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilikuwa ni uhalali wa malipo ya Shilingi bilioni 12.1 kwa ajili ya posho ya vikao kwa ajili ya Wajumbe 34 wa Tume. Wajumbe wa Tume hawapo 34, Wajumbe wa Tume wapo 32. Wapo Wajumbe 30, halafu wana Mwenyekiti wao na Makamu wake. Waliowekwa ngazi sawa na Wajumbe hawa, ni Katibu na Naibu wake, unapata watu 34. Lakini Wajumbe wa Tume hawapo 34. Kwa hiyo, kama ilitolewa picha hiyo, basi picha hiyo siyo sahihi ni picha potofu. Wajumbe wenyewe pamoja na Mwenyekiti wao na Makamu ni 32, halafu wanaongezwa juu yao ambao wako katika *level* sawa, kwa maana ya kulipwa posho sawa, ni Katibu na Naibu wake. Kwa hiyo wanakuwa watu 34 katika ngazi sawa.

Sasa kama waliitwa wote ni Makamishna, basi ni makosa kwa sababu wote siyo Makamishna, ila sasa posho hizi ndiyo zile ambazo zimepangwa na kukubaliwa kimsingi, kwamba watalipwa posho hii. Zimekubalika na Sheria za Fedha na sisi wenyewe tumepitisha bajeti ya kwanza hivyo hivyo, bajeti hii inaendelea tena, sasa hata sijui,

hazijaongezwa! Ni posho zile zile tulizokubali *last year* na ndiyo hizo hizo wanazopewa mwaka huu. Sasa kinachogomba ni nini?

**SPIKA:** Naomba Waziri ujibu, hakuna kusikiliza mtu ambaye hahusiki na maelezo haya. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukweli ndiyo huo. Posho hizi ni za kuwalipa viongozi hawa na viongozi hawa walilipwa posho za namna hii mwaka 2012, wataendelea kulipwa hivyo mpaka watakapomaliza kazi yao. Kama itakuwa ni Mwezi Aprili ama baadaye, basi tutaona. Lakini tumeweka bajeti ya mwaka mzima, maana bajeti ni makadirio. Zitakapohitajika, zitalipwa; zisipohitajika hazilipwi.

Kuhusu uhalali wa kuwa na Wajumbe 34 badala ya 30 kulingana na sheria hili ndiyo nimelieleza. Kwa kweli hakuna Wajumbe 34, wapo Wajumbe 32, ukijumlisha Mwenyekiti na Makamu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhalali wa maombi ya fedha za matumizi ya Shilingi bilioni 33.94 zilizoombwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Kama mtakumbuka na Mheshimiwa Pindi Chana ametukumbusha hapa, mwaka 2012 tulipoomba kwenye Kamati Shilingi bilioni 40, zikapunguzwa zikafika Shilingi bilioni 33. Mwaka huu ukomo wa bajeti tuliyopewa na watu wa Hazina na Mipango wakasema hizo hizo, na mtaumia nazo, hizo hizo. Lakini sasa kwa kupewa hizi, kuna mambo yataathirika. Kubwa ni haya Mabaraza ya Kata ya Katiba. Kwa sababu vichwani mwetu tulikuwa tunafikiria tufanye siku nne, lakini haiwezekani. Kwa hiyo, tutafanya siku mbili badala yake, ili angalau kuwa ndani ya bajeti hii ya Shilingi bilioni 33.9.

Mheshimiwa Spika, tuliomba zaidi, lakini tukaambiwa ukomo ni huo huo. Kwa hiyo, sasa inabidi tuji-*adjust*. Kwa hiyo, tunaathirika na tutaathirika kiasi kwa sababu hatuna pesa hizi tena za kuweza kufanya Mabaraza. Tungeweza kufanya Mabaraza siku nne labda, lakini inaongeza pesa nyingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uhalali wa matumizi ya fedha wakati wa Bunge Maalum la Katiba. Kwa mujibu wa Sheria, mnafahamu kwamba Mwenyekiti wa Tume ndio atawasilisha Rasimu ya Katiba kwenye Bunge Maalum la Katiba. Lakini Mwenyekiti wa Tume, anaweza kutoa ufafanuzi unaohitajika wakati wa majadiliano kwenye Bunge Maalum la Katiba. Kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu tajwa, Tume imetenga fedha hizo kwa ajili ya kuwalipa posho Wajumbe wa Tume na Sekretarieti wakati wa Bunge Maalum la Katiba, kuwezesha kuwasilisha Rasimu ya Katiba na kutoa ufafanuzi kuhusu rasimu hiyo. Hivyo basi, siyo sahihi kusema kuwa Mwenyekiti akishawasilisha Rasimu ya Katiba, anakuwa hana kazi nyingine ya kufanya kwamba, yeye sasa ni *fanctus ofisio.*

Mheshimiwa Spika, *process* hii ya kuwasilisha, kweli anakwenda mle ndani, labda atakwenda peke yake, lakini anabebwa na wenzake. Wakati wote hii Tume ndiyo inayomsapoti. Iko naye, itamwacha siku ile wakishaambiwa haya, sasa *referendum* imefanyika na Katiba imeshapatikana, hatahitajika tena. Tutawafukuza siku hiyo hiyo kweli! Kama ndiyo itakuwa tarehe 26 mwezi wa Nne, basi wajue kazi yao inakwisha tarehe 26 mwezi wa Nne mwakani. Kama haitakuwa siku hiyo, itakuwa siku hiyo ambapo watakuwa wamekamilisha kazi hii. Hatuwezi kuwalipa kama hawaendi kufanya kazi. Huo ndiyo utaratibu wetu! Hawawezi kulipwa kama hawaendi kufanya kazi. Kama nilivyosema mwanzo, hii siyo Tume ya Ulaji, hii ni ya kufanya kazi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhalali wa matumizi ya fedha wakati wa kutoa elimu ya uraia kabla ya kura za maoni; kwa mujibu wa Kifungu 33 (2), Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83; Tume inawajibika kuhamasisha na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu Katiba inayopendekezwa kabla ya kura ya maoni. Kwa msingi huo, Wajumbe wa Tume na Sekretarieti wote watalazimika kuzunguka nchi nzima kutoa elimu katika kipindi hicho. Fedha zilizotengwa ni hizo, sasa sijui hata kama zitatosha. Wataizunguka nchi hii yote kujaribu kuwaeleza wananchi kwamba, jamani, Katiba ile ambayo

tumezungukanayo sasa ni hiyo, itoleeni maamuzi; kama mnaitaka semeni ndiyo, kama hamuitaki semeni siyo. Basi.

Mheshimiwa Spika, lakini ni lazima wazunguke. Watafanya kazi hiyo na yale matangazo ya redio na magazeti na *television* na runinga, yataendelea. Lazima yaendelee. Sasa pesa hizi sina hata uhakika kama zitatosha, maana mwaka huu bajeti yenyewe imefinywa sana. Uhalali upo kwa sababu kazi hii ni ya Tume. Nina hakika Vyama vitasimama, vitakwenda kuhamasisha wananchi wake kwa nguvu sana kwenda kusema jambo hili. *As it is,* wengine wameshaanza, Mheshimiwa nimekuona; nilifurahi kweli, Katiba haipatikani wapi? Itapatikana wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Lissu anaifahamu. Kwa hiyo, kampeni zitakuwepo na zinaendelea, zimeshaanza kama hivyo, bado! Mtaendelea kufanya na sisi na Chama cha Mapinduzi kitafanya, lakini Tume ndiyo wenye kazi hii na hicho tunaingilia kazi ya Tume, lakini tuna wajibu wa kuwaelimisha wananchi wetu waelewe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, uhalali wa matumizi ya fedha kwa ajili ya chakula maalum kwa Wajumbe wa Sekretarieti watakaokuwa wamepata *UKIMWI,* duh. Katika utungaji wa bajeti kuna *cluster* tano. *Cluster* ya kwanza kabisa, inawekwa inasema kuhudumia watumishi ambao wana *UKIMWI,* maana hili ni suala mtambuka kwa jamii. Sasa haina maana kwamba Wana-Tume wale wana *UKIMWI* au Sekretarieti, hatujui, mimi sijui. Lakini tunaweka bajeti, endapo wapo, watatumia ili waweze kutufanyia kazi vizuri. Kwenye Wizara yangu mimi wapo na tunayo hiyo bajeti na tunawahudumia ipasavyo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kila Wizara hapa ukiangalia, kila Wizara ina bajeti hiyo kwa sababi, ni *cluster* mojawapo katika zile *cluster* 5 za bajeti. Ni lazima iwekwe. Hawa ni watumishi, tunataka watuhudumie, lakini wanahitaji hudumja ya Serikali na Serikali inaweka. Kwenye Tume, sijui kama wapo! Lakini bajeti tunaiweka, kama wapo watatumia.

Hatuwezi kuyatangaza haya mambo hadharani, hata kama wangekuwepo, siwezi nikakwambia wapo watano au sita.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala kuhusu Tume kwmaba haikuweka utaratibu wowote wa maana wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya masuala yote yanayohusu Katiba. Hili lilizungumzwa, sasa dah, hata sijui nisemeje. Lakini niseme yafuatayo:-

Mheshimwa Spika, katika suala la kutoa elimu kwa umma kuhusu mchakato wa Katiba Mpya, Tume iliandaa programu mbalimbali za elimu na tulitumia vyombo vya habari kama redio, runinga na magazeti. Tulitoa machapisho mbalimbali yakiwemo Katiba ya Jamhuri ya Muungano yenyewe, kwa lugha nyepesi na kwa lugha yake ilivyo, Sheria yenyewe ya Mabadiliko ya Katiba kwa lugha nyepesi na kwa lugha yake ilivyokuwa, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba yenyewe, hadidu za rejea za Tume, kazi za Tume, maswali yanayoulizwa mara kwa mara, yaani *frequently asked questions,* tulichapisha tukagawa.

Mheshimiwa Spika, machapisho hayo pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Zanzibar, yalisambazwa nchi nzima kabla ya Tume haijafika kukusanya maoni ya wananchi. Elimu kwa Umma ilikuwa inatolewa na Wajumbe wa Tume kila walipofika kwenda kukusanya maoni.

Mheshimiwa Spika, lilikuja lingine, wanasema muda uliotolewa pia haukutosha, watu walipewa dakika tano-tano tu kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, lakini nasema, pamoja na hizo dakika tano, watu walipewa muda wa kuandika. Hili la watu kusema *sample* ni ndogo, kwa kweli, siyo sawa. Hakuna *sample* kubwa iliyoweza kutumika kama hii ya kwetu, nitakwambia namna gani. Pamoja na watu wale ambao mnasema walionekana wakapigwa picha, wakatoa; tulikuwa na makundi mbalimbali. Chama cha Mapinduzi chenye Wanachama wasiopungua 6,000,000 kilitoa maoni kikiwakilisha wanachama wale 6,000,000. Chama cha

*CHADEMA,* kilikwenda kutoa maoni yake, sina uhakika wana wanachama wangapi waliowawakilisha kwenye maoni yale?

**MBUNGE FULANI:** Milioni kumi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Milioni kumi.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Kwa hiyo, hapo peke yake kuna wananchi milioni 16, ambao maoni yao yametolewa. Sasa unaposema *sample* ni ndogo, ulitaka watu milioni 40 wote waweze kutoa? Maana wengine ni watoto wadogo, hawawezi kutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa Vyama hivyo viwili peke yake, *you have one of the largest samples.* Acha Vyama vingine. *CUF,* sitaki kuuliza, mna wanachama wangapi, lakini na ninyi mlitoa maoni kwa niaba ya wanachama wenu.

**MBUNGE FULANI:** Milioni 11. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Milioni 11! Sasa una milioni 11 wa *CUF,* milioni 10 wa *CHADEMA,* milioni sita wa *CCM,* una watu zaidi ya milioni 26 wametoa maoni. Ukisema *sample* ni ndogo, siyo sahihi. Ni *sample* kubwa haijapata kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume iliweka utaratibu tofauti na wa kibaguzi katika hatua za kuunda Mabaraza. Hili limezungumzwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kwa mujibu wa Kifungu 17 (8), Tume imepewa mamlaka ya kubuni na kutumia taratibu tofauti katika utekelezaji wa majukumu yake katika pande mbili za Muungano. Siyo kweli kusema kwamba, wakati wa kukusanya maoni Tume ilikuwa na utaratibu unaofanana na pande zote za Muungano. Kwa upande wa Mabaraza ya Katiba, kulikuwa na tofauti katika ngazi za

uchaguzi wa Wajumbe wa Mabaraza hayo. Kwa upande wa Tanzania Bara, ngazi ya msingi ilikuwa ni Kata, wakati kwa upande wa Zanzibar, ilikuwa ni Shehia.

Mheshimiwa Spika, katika chaguzi hizi, Tume ilikuwa inatumia mifumo iliyopo kisheria ya Uchaguzi katika ngazi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwa Zanzibar, hakuna mfumo wa kiuchaguzi katika ngazi ya Wadi, ambayo ndiyo inayofanana na Kata kwa Tanzania Bara. Kwa Tanzania Bara, kuna mfumo wa uchaguzi katika ngazi ya Kijiji na ngazi ya Mtaa. Pia Kamati za Maendeleo za Kata zimepewa mamlaka ya kufanya maamuzi mbalimbali ya kimaendeleo na chaguzi za Wajumbe wa Kamati mbalimbali katika ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Spika, tusingeweza kufanya uchaguzi katika ngazi za Kata, haiwezekani! Kata ni kubwa mno! Hakuna Kikao cha Uchaguzi wa Kata, lakini wa Kijiji kipo na ndiko tulikofanya. Tusingeweza kufanya kwenye Kata, hata kidogo! Uchaguzi huo sijui ungekuwaje? Wakazi wote wa Kata, isingewezekana. Kata zote, isingewezekana! Kwa hiyo, tukafanya kwenye Kijiji tukaja kwenye Kata. Kwenye Kata, tukatumia mfumo tu uliokuwepo wa Serikali za Mitaa, wa kupata Wawakilishi wa wanne wa wananchi. Najua zimetokea kasoro sehemu mbalimbali, zipo na hizo Tume wenyewe wanajua jinsi ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, kuna Kata imetokea imepeleka watu wa wanne, bahati mbaya watu watatu katika wanne, wale wanatoka nyumba moja. Baba mwenyewe Diwani, mke wake na mwanawe. Sasa Uwakilishi wa namna hiyo, Tume inajua. Ikasema, hapana, hili tutaliangalia vizuri jamani. Hamwezi mkapata watu kutoka kwenye vijiji vinne, badala yake mnapata watu kutoka nyumba moja? Kwa hiyo, yapo matatizo madogo madogo. Lakini kimsingi utaratibu umekamilika na kama nilivyosema asubuhi, tumekwishawapata Wajumbe wote katika Mikoa yote ambayo inahusika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mabaraza ya Katiba ya Wilaya kutawaliwa na Wajumbe wengi kutoka *CCM* na

kuondolewa Wajumbe ambao sio wa *CCM,* na hasa wa *CHADEMA.* Kama nilivyoeleza, jambo hili siyo kweli, na misingi yake chaguzi hizi haikuwa Vyama. Uwakilishi katika Mabaraza haya, siyo wa Vyama. Hauna msingi wa Vyama. Vyama vimeingilia sana mchakato huu na vimekaribia kuuvuruga. Lakini uchaguzi huu siyo wa Vyama.

Misingi ya Mabaraza haya siyo Vyama, ni Wawakilishi wa wananchi wenyewe. Wakitokea wote ni *CCM,* basi labda ni kwa sababu hapo mahali wengi ni *CCM.* Wakitokea wote ni CHADEMA, basi labda hapo mahala wengi ni CHADEMA, lakini hakuna mfumo uliotungwa eti wakachaguliwe wanachama fulani, hapana. Chama siyo sifa mojawapo ya kuwa Mjumbe wa Mabaraza haya. Uwanachama wa Chama chochote kile, siyo sifa mojawapo ya kuwa Mjumbe wa Mabaraza haya. Uwakilishi wake ulikuwa mzee mmoja, mwanamke mmoja, kijana mmoja na mtu mwingine mmoja, basi.

Mheshimiwa Spika, sasa mambo ya Vyama haya ni uvurugaji. Nami ninavionya, kama vyama vimeingilia mchakato huu, vinaharibu, viache. Havihusiki na jambo hili! Siyo lao! Hili ni jambo la Tume, Tume inatafuta maoni ya wananchi na maoni hayo hayategemei wewe unatoka Chama gani. Ila wewe katika Kijiji, chako unawakilisha, watu wamekupenda kiasi gani, basi.

Mheshimiwa Spika, kutokuwa mwanachama au kuwa mwanachama, siyo sifa mojawapo ya kuwa Mjumbe wa Baraza. Hiyo ningependa ieleweke mapema na kwa hiyo, waliochaguliwa wamechaguliwa kwa sifa zao ambazo zimetajwa katika ule Mwongozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la bwana Beatus, nimelizungumzia ipasavyo. Nafikiri limeeleweka.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mabadiliko ya Katiba, imepata Hati ya Muungano na kuitumia kama ilivyoelekezwa na Sheria? Hili ni swali linaulizwa na Mheshimiwa Said Suleiman, Mbunge wa Mtambwe.

Mheshimiwa Spika, sina hakika Sheria ni Kifungu gani kimeelekeza jambo hili, sikumbuki. Sikumbuki na Mwanasheria Mkuu hajanikumbusha kama kipo Kifungu kinachosema kwamba, lazima ipatikane Hati ya Muungano ndiyo Tume hii ifanye kazi. Kwa hiyo, jambo hili, labda pengine hatukumwelewa vizuri. Lakini kwa sababu yupo na baadaye atapata nafasi ya kusimama, anaweza akaliuliza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wametoa maoni mengi ya Tume na Tume itayazingatia. Mimi nataka niwahakikishie kitu kimoja tu kwamba, Tume hii imepokea na itaendelea kupokea maoni kutoka kwa watu mbalimbali, hasa haya Mabaraza ya Kata, yatatoa maoni yao, lakini Mabaraza mengine pia yale ambayo nimesema yanaweza kujiunda, kwa aina yoyote ile ya Vyama, ya Dini, ya *NGOs,* ya Asasi mbalimbali, wajiunde, ili watoe maoni. Ninachowahakikishia mimi ni kwamba, Tume itayapokea maoni yote na itayafanyia kazi. Kitakachofanyiwa kazi ni uzito wa hoja inayotolewa.

Mheshimiwa Spika, Tume ile ndiyo maana ina watu wenye busara, watu wazito, watakaa wataangalia hoja. Suala la kusema watu wengi wamesema hivi, kwa hiyo, hivi ndiyo iwe, pengine wingi siyo hoja. Uzito wa hoja ni muhimu zaidi kuliko wingi wa watoa hoja hiyo. Kwa hiyo, Tume itazingatia uzito wa na hoja, na hoja zote zikipelekwa kwa Tume, basi tuzipeleke nyingi kadri inavyowezekana na wengi tuzipeleke ili Tume ipate uwanja mpana zaidi wa kuweza kutafakari na kutuletea Katiba ambayo itatufaa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nijaribu kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ester Nicholaus Matiko, alizungumzia hoja ambayo pia ilizungumziwa na Kamati ya Katiba, nikaijibu kwamba ucheleweshaji wa mashauri Mahakamani ni kikwazo katika mfumo wa utoaji haki. Nilisema ni sawa, na sisi tumeliona hilo na tunaendelea na taratibu za kuboresha hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini, yeye alizungumzia kuhusu mafunzo ya Mahakimu na Majaji.

Mheshimiwa Spika, Mahakama imeendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa kada zote kadiri ambavyo bajeti inaruhusu. Kwa mwaka ujao, Mahakama inakusudia kutoa mafunzo kwa watumishi wake zaidi ya 1,000 wa ngazi mbalimbali. Kwa hiyo, suala hili tunalitilia umuhimu na sisi tunaona umuhimu wa mafunzo, Wizara na Taasisi zote ambazo ziko chini yake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jumaa pia aliendelea kuzungumzia kuhusu nyumba kwa Waheshimiwa Majaji. Katika hotuba yangu, nimesema tuna mpango wa kujenga nyumba kwa Waheshimiwa Majaji. Tumepata kiwanja pale Dar es Salaam, tutajenga nyumba zao katika kijiji kimoja. Kwa hiyo, tunategemea kufanya hivyo. Lakini katika kila mahali ambapo tuna Mahakama Kuu, tunajenga nyumba ya Jaji na tunaendelea kujenga nyumba za Mahakimu, kila tunapojenga Mahakama nyingine mpya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, amesema wafanyakazi bora kupongezwa ni kutiwa moyo na kuendelea kufanya vizuri. Anachosema ni kwamba, toka aone Sherehe za Siku ya Mei Mosi, hajapata kuona Wafanyakazi Bora kutoka Sekta ya Mahakama. Yeye anasema kupata Wafanyakazi Bora ni kutiana moyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli na mimi nakubali, ndiyo maana sisi Sekta yetu hii ya Mahakama huwa inawapongeza watumishi wanaofanya kazi kwa bidii kila mwaka kwa kuwapa zawadi ya kutambua juhudi zao. Hata hivyo, utaratibu huu wa kwenda huko kwenye *May Day* na sisi basi tutaingia, lakini unafanyika, lakini unafanyika katika ngazi ya Taasisi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ramo Makani, Mbunge wa Tunduru, alizungumza kuhusu kuzingatia *ADR.*

*ADR* ni *Alternative Dispute Resolution Mechanism,* ambayo tunatakiwa kuizingatia. Mimi nasema, sisi tunaizingatia sana. *Actually* kama nilivyosema mwanzo, haya ni matakwa ya sheria na yapo kwenye Sheria na sisi tunazingatia sana, kujaribu kutatua matatizo badala ya kwendanayo Mahakani. Lakini pia mnaweza mkaenda Mahakamani, badala ya kufanya kesi, mkatumia utaratibu huu na mkajaribu kutatua. Hii itaongeza kazi ya kupunguza mashauri yanayokwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, ambaye ndiye aliyesoma pia Taarifa ya Kamati, alikuwa na mengine ya kusema. Anasema Waheshimiwa Mahakimu wapya, hawakupangiwa vituo vipya vya kazi.

Mheshimiwa Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mahakimu hao wapya wako kwenye vituo sasa hivi. Wako kwenye vituo mbalimbali vya Mahakama wakijifunza kazi na kupata uzoefu zaidi kutoka kwa Mahakimu wenye uzoefu, na siyo kuwa wamekaa tu na hawafanyi kazi. Wako pale wanafanya *internship* na hawa Mahakimu ambao wako siku nyingi. Wao sasa tulikuwa tunasubiri tu Sheria ile ipite, Sheria imepita na Mheshimiwa Rais, amekwishaisaini. Barua wamekwishapewa sasa hivi. Vijana hawa watapewa Mahakama zao na sasa wameshapata uzoefu, watapewa Mahakama zao ili waende sasa wakaanze kazi ya kuendesha Mahakama zao wao wenyewe peke yao. Lakini kwa sasa walikuwa wamepangwa na Mahakimu wengine wakijifunza kazi na kupata uzoefu kwa Mahakimu hao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge pia alisema vilevile kwamba, mishahara ya Mahakimu wapya haikutumwa kwa wahusika. Nataka kusema kwamba kati ya Mahakimu wapya walioajiriwa mwaka 2012, ni 12 tu ambao hawakulipwa mishahara yao. Hawa hawakulipwa kutokana na kukiuka taratibu za utumishi, ambapo walikuwa watumishi wa Taasisi za Serikali na kuacha kazi badala ya kuomba kuhamishwa. Hata hivyo, mawasiliano na Ofisi ya Rais – Utumishi, yanaendelea ili kumaliza tatizo lao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Laizer na Mheshimiwa Makani, waliomba huduma za usafiri kwa Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jambo hili, Watumishi wa Mahakama wakiwa Mahakimu katika mwaka ujao wa fedha, tutanunua mabasi madogo katika Mahakama za Mikoa kwa ajili ya usafiri wa watumishi wa Mahakama, wakiwemo Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Hamad Abuu Jumaa, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo na Mheshimiwa Esther Matiko, walizungumzia suala la rushwa katika Taasisi hii ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, nasema ushauri huu tumeupokea. Lakini kama nilivyosema mwanzo, suala la rushwa haliko *confined* kwa Mahakama peke yake, ni tatizo mtambuka na tunapambana. Tunaendelea kupambana kwa kadiri tunavyoweza, lakini ni tatizo gumu na ninyi mnafahamu. Lakini hata hivyo, Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema mtakubaliana na mimi kwamba angalau vitendo vya rushwa kwenye Mahakama sasa vimepungua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Felix Mtambo, Mbunge wa Liwale, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, Mheshimiwa Sylivester Koka, Mbunge wa Kibaha walizungumzia kuhusu mahitaji ya majengo ya Mahakama katika sehemu zao. Kwa kutambua upungufu huu na uchakavu na mahitaji kwa ujumla wa majengo katika Mahakama zetu, Serikali imeanzisha *program* maalum ya ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mkoa, Wilaya na Halmashauri husika. Ni matumaini yangu kama nilivyosema kwenye bajeti yangu kuwa Serikali kwa *program* hii itasaidia kutupatia ufumbuzi wa changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, aidha, ongezeko la bajeti la Mahakama litasaidia kukabiliana na changamoto hii mwaka wa fedha huu ujao. Kama nilivyosema asubuhi, tuliongezewa katika Mahakama leo hii asubuhi kama Shilingi bilioni 20

ambazo tunategemea nazo zitaingizwa katika ujenzi wa Mahakama hizi na kupunguza tatizo hili la mahitaji ya majengo ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Dkt. Prudenciana Kikwembe yeye alizungumza kuhusu ucheleweshaji wa mashauri na amesema kuna kuongezeka sana kwa idadi ya watuhumiwa na akazungumzia upanuzi, yaani ukarabati wa ujenzi wa majengo ya Mahakama, mwenendo na tuhuma za mashauri ya jinai ziwe za Kiswahili ili washtakiwa waelewe mwenendo wa shauri na hatma yake.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kweli mashauri yanaweza yakaendeshwa kwa Kiswahili, kinachoandikwa Kiingereza ni ile hukumu, lakini mle ndani wanaweza wakasema Kiswahili. Kwa hiyo, haimnyimi mtuhumiwa kuelewa nini kinaendelea. Hilo linafanyika na kama kuongezeka kwa watuhumiwa, pia tukubaliane Watanzania tumeongezeka, hali ya maisha imebadilika *nature* ya misuguano katika jamii pia imebadilika. Sasa hivi kwenye kesi zangu Mahakamani kule kesi zilizopo nyingi utakuta ni za kijamii jamii, siyo za mtu mmoja mmoja kama zamani. Ukishtaki sasa, unamshtaki mtu mmoja, lakini ana watu wengine kama mia pale wanakwenda kama mashabiki wake. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, kesi ni nyingi. Nyingine za kidini, nyingine za kisiasa, ziko nyingi. Lakini tu ile *conflicts* ndani ya jamiii zimebadilika. Zamani ilikuwa ukimkamata kibaka mmoja, basi una-*deal* na huyo huyo. Lakini sasa ukimkamata mtuhumiwa mmoja, unaweza uka-*deal* na Chama kizima cha siasa. Kwa hiyo, *nature* ya *conflicts* katika jamii imebadilika sana. Hili tunalielewa na ni changamoto ambayo inatukabili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuzungumzia hoja aliyoitoa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu haki za binadamu kwa ujumla. Lakini sana sana yeye alizungumzia kesi ya Marehemu ambayo ipo Mahakamani. Nami kwa sababu ya kesi ile kuwepo Mahakamani sitaizungumzia hata kidogo. Nitazungumzia tu hali ya haki za binadamu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu ndani na nje tumesifika vizuri sana kwa kuzingatia haki za binadamu. Tumesifika sana! Mimi mwenyewe nimewakilisha nchi yetu sehemu nyingi ambapo kila tukisimama wanasema *status* ya haki za binadamu kwa Tanzania ni nzuri. Yapo matukio ambayo yanaweza yakawa yanatutia doa, mengine ni ajali; lakini hakuna la makusudi. Siku moja kuna mtu alizungumza, nafikiri tulikuwa kwenye Kamati akasema kuna mauaji kama vile ya kupangwa na Serikali. Hakuna kitu cha namna hiyo! Siyo Serikali hii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali hii haiwezi kupanga, haijawahi kupanga wala haitapanga mauaji ya raia wake inaowalinda. Haiwezekani! Kwa hiyo, kama yametokea matukio ambayo yameonyesha kama vile kuna uvunjifu wa haki za binadamu, matukio haya hayajapangwa na Serikali wala hayapangiki. Hakuna kikao kinachoweza kufanya hivyo ndani ya Serikali hii ninayoijua mimi na naijua. Hii Serikali nimeitumikia miaka mingi sana, uhai wangu wote nimetumikia Serikali hii. Kwa hiyo, naijua. Hakuna uwezekano wa jambo kama hilo kutokea. Kwa hiyo, hali yetu ya haki za binadamu ni nzuri, na ni nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, zinapotokea fujo mahali za aina yoyote ile, wanapokwenda Polisi kwenda kujaribu kutuliza fujo hiyo katika harakati zile akatokea raia akauawa ama akaumizwa, ukatoka pale ukasema Tanzania inavunja haki za binadamu, kwa kweli unatuonea. Ulitaka tufanyaje? Tukae tu zile fujo ziendelee, wananchi waendelee kuumizana? Sasa ikitokea hiyo, Wamarekani wenzetu wana neno lao linaitwa *Collateral Damage.* Sisi hatuwezi kutumia hilo. Sisi tunasikitishwa na kila raia anapoumia, kila raia anapokufa tunasikitishwa sana. Tunaumizwa sana!

Kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ajaribu kutuangalia katika picha hiyo na asitu-*point* kama sisi ni watu wabaya, tunapenda kuua, tunakwenda mahali, basi Polisi ua! Hapana. Hatuko hivyo na yeye anafahamu hatuko hivyo. *Ofcourse* kuna maneno ya kisiasa, lakini hayo siyo mahali pake hapa. Hapa ni Bungeni,

tunaongea *facts,* hatuongei maneno ya uongo na hatutaki kuongea maneno ya uongo.

Mheshimiwa Spika, nimejitahidi kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, sina hakika kama nimezimaliza zote. Zipo nyingi, lakini wenzangu walinisaidia pale mwanzo, wamezipunguza.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie tu kwa kushukuru sana. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono. Mheshimiwa Zambi.

**MWONGOZO**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nimesikitika kidogo hapa, natumia Kanuni ile ile ya mwongozo uniwie radhi, lakini nimeona nisimame tu kwa sababu ya kuweka mambo sawa.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri anajibu hoja hapa, limekuja suala la takwimu za wanachama wa Vyama vya Siasa ambao walihusika katika utoaji wa maoni, ikasemwa kwamba CCM wanachama milioni sita, na CHADEMA watu wakacheka cheka hapa wakasema milioni 10 na baadaye *CUF* wakasema milioni 11. Ulikuwa kama utani, watu wanacheka.

Mheshimiwa Spika, *concern* yangu hapa, hizi ni kumbukumbu sahihi za *Hansard* za Bunge. Vizazi vinavyokuja kesho kutwa, wataona kwamba mwaka huu 2013 na tarehe ya leo Serikali ilithibitisha kwamba kumbukumbu za wanachama wa Vyama hivi ndivyo zilivyokuwa jambo ambalo siamini kama liko hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali, au tupe mwongozo wako, taarifa zinaposomwa Bungeni za kiutani utani na zinarekodiwa na *Hansard:* Je, tunaziacha hivyo hivyo au tunazisahihisha, au tunathibitisha zipo sahihi?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu kaa chini tumalize moja kwanza.

*Actually,* kufuatana na kanuni zetu hapa, kama huna uhakika na kitu chochote, siyo sahihi kusema. Kwa hiyo, *Hansard* isomeke kwamba zile *figure* hazina usahihi wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nikupatie taarifa, nikujulishe kwa mujibu ya kanuni ya 77(2) ya kanuni zetu inayosema: "Mbunge yeyote aliyehudhuria anaweza kumjulisha Spika kwamba Wabunge waliopo ni pungufu ya akidi inayohitajika kwa ajili ya shughuli inayoendelea."

Mheshimiwa Spika, ili shughuli ya Bunge lako Tukufu iwe halali, akidi kwa kila kikao cha Bunge wakati wa kufanya maamuzi itakuwa ni nusu ya Wabunge wote. Tunakwenda kwenye Kamati ya Matumizi na idadi ya Wabunge ambao wako humu kwa mahesabu yangu ya haraka haraka ni Wabunge kama 133, wakati nusu inatakiwa iwe 176. Kwa mahesabu yangu, naomba kwa mujibu wa kanuni hizi, ujiridhishe kama tuna akidi ya kutosheleza kutupeleka kwenye Kamati ya Matumizi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mnajua humu ndani kuna watu wanapenda kuchelewesha tu mambo na kufanya hivi; mimi hapa huwezi kuniambia wangapi nimewaruhusu kwenda kufanya nini. Najua idadi hii inatosha kabisa. Kwa hiyo, tunaendelea, Katibu.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 8 – Tume ya Mabadiliko ya Katiba**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*……………………..Tshs. 19,596,543,000/=

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika na Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kasma 210300 ambayo mwaka wa fedha uliopita ilikuwa Shilingi bilioni 10.2, mwaka huu Shilingi bilioni 10.1, Kambi Rasmi ya Upinzani inaomba ufafanuzi wa mgawanyo wa fedha hizi kwa maana ya viwango vya posho vya Wajumbe wa Tume ya mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Waziri katika majumuisho hakutaja kabisa viwango vya posho vya Wajumbe, na Kambi Rasmi ya Upinzani imeonyesha mashaka yake siyo mwaka huu tu, hata mwaka 2012 kuhusu viwango ambavyo Wajumbe wa Tume wanalipwa na kufikia hatua ya kuviona kama viwango hivyo ni ulaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwa Shilingi hizi bilioni 12.1 zilizopo hapa, kiwango cha posho cha Mjumbe kwa kikao kimoja kwa siku wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba ni kiasi gani? Iwapo ufafanuzi utakaotolewa na Waziri hautaniridhisha, nitaomba nipewe nafasi ya kutoa hoja ya kuhamisha sehemu ya fedha hizi kupeleka kwenye vifungu vingine ambavyo Mheshimiwa Waziri mwenyewe amekiri kwamba vina pesa kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibia swali alilouliza Mheshimiwa

Mnyika kuhusiana na kasma ya 210300 ambapo ametaka kujua mgawanyo wa fedha wanazolipwa Makamishna wa Tume.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukirudia suala hili mara kwa mara. Mwaka 2012 wakati tunapitisha bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, lakini pia hata leo Mheshimiwa Waziri amelieleza hili, viwango vya posho anayolipwa Kamishna wa Tume ni stahili na ni siri ya Mjumbe mwenyewe wa Tume.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa ni kifungu hicho hicho cha Mheshimiwa Mnyika 210300. Kuna nyongeza ya Shilingi bilioni mbili. Sasa nataka nipate ufafanuzi, hiyo nyongeza ya Shilingi bilioni mbili, kwa sababu tumeambiwa kwamba kilicholipwa mwaka 2012 ndiyo ambacho kimelipwa huu.

Sasa kwanza kuna Shilingi bilioni hii mbili ya ziada. Hii Shilingi bilioni mbili ya ziada ni kitu gani na nisisitize kwamba, watupe mchanganuo wa kila Mjumbe analipwa kiwango gani, hasa ukizingatia kwamba wamesema ni vijisenti tu, na kwamba wale Wazee wanajitolea?

**SPIKA:** Nilivyosikia mimi, mgao wa Tume unalingana. *The total amount* inalingana kama ule wa mwaka 2012. Haya maswali mengine; Mheshimiwa Zubeir.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Haulingani, imeongezeka Shilingi bilioni mbili.

**MWENYEKITI:** Ndiyo imeongezeka!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Sasa haulingani basi!

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Swala langu Mheshimiwa limeshaulizwa, ni hilo lililoulizwa la kwanza.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Account Unit* …….Tshs. 40,250,000/=

Kif. 1003 – *Internal Audit Unit* ……………..…Tshs. 64,200,000/=
Kif. 1004 – *Procurement Mgt Unit*…………..Tshs. 97,480,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 – *Inform. Comm. and Techn*……Tshs. 487,000,000/=

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote 1005* kifungu namba 410600 - *Acquisition of Office and General Equipments.* Hapa mwaka 2012 inaonekana kulikuwa na Shilingi milioni 30 lakini mwaka huu kuna ongezeko zaidi ya mara tatu, Shilingi milioni 102, hebu naomba Wizara itueleze, ongezeko hili ni kwa ajili ya nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri maelezo! Mmekiona kifungu anachosema Mheshimiwa, cha 410600?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura kuhusiana na kasma 410600. Fungu hili litatumika katika kununulia *saver* itakayotumika ku-*back up* maoni ya wananchi kutokana na umuhimu wa usalama wa maoni yenyewe yanayokusanywa kwa ajili ya kumbukumbu za Kitaifa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 – *Comm. and Outreach*……. Tshs. 10,310,195,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lugola, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Chilolo, Mheshimiwa Zubeir, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Sabreena; vifungu vyenyewe havitoshi nyie wote!

Haya, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Paresso, Mheshimiwa Ngonyani na Mheshimiwa Mipata. Tuanze na Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kupata ufafanuzi katika *subvote* 1006 kifungu kidogo 220100 - *Office and General Supplies and Services*. Mwaka 2012 ilikuwa Shilingi milioni 200, lakini safari hii imetengwa Shilingi bilioni nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeomba ufafanuzi, kwa nini kiwango hicho kimekuwa kikubwa sana?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zitatumika katika kuchapishia nakala milioni moja za rasimu ya Katiba.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka ufafanuzi kwenye hiyo *subvote* 1006 kifungu 221300 kinachohusiana na *Educational Material Supplies and Services.* Mwaka 2012 ilikuwa Sh. 182,500,000/= lakini mwaka huu naona imekwenda mpaka Sh. 1,578,195,000/=. Naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zitatumika katika kutoa elimu kwa Umma hususan sasa hivi tunapoelekea katika Mabaraza ya Katiba, lakini baadaye katika Bunge Maalum na mwisho kabisa kwenye Kura za Maoni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani!

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mheshimiwa Lugola ameshanimaliza kwenye swali langu.

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Suzan Kiwanga!

**MHE. SUZAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo...

**MWENYEKITI**: Kama ni kifungu hicho wala msipoteze muda wa Spika hapa!

**MHE. SUZAN L.A. KIWANGA**: Nipo kwenye fungu hilo hilo, 220600 wanasema *clothing*, *bedding*, *footwear and services*. Miaka yote hakuna hela iliyopangwa, lakini mwaka huu shilingi milioni 40 ni za nini? Hawa watu wananunuliwa tena hivyo vitu?

**SPIKA:** Wewe uliza ni za nini? Hawa watu, watu gani? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zitatumika katika kununulia sare kwa ajili ya wajumbe wa Sekretarieti ya Tume, pindi wanapokwenda katika sherehe mbalimbali za maazimisho kwa ajili ya kutangaza kazi za Tume, lakini pia kuhamasisha wananchi waweze kushiriki katika kutoa maoni yao kuhusiana na Rasimu ya Katiba pamoja na hatua nyingine zinazofuata.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nani pale! Diana Chilolo!

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti hoja yangu imeshajibiwa.

**MHE. VITA R. M. KAWAWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 221000, *travel in country*. Mwaka jana ilikuwa sh.

70,000,000/= mwaka huu ni sh. 12,000,000/=, swali langu kwa nini zimepungua, na kifungu hiki kinahusiana na mawasiliano *and outrich*.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zimepungua kwa sababu fedha zingine tumeziweka katika kifungu cha utawala.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zubeir!

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unaniweka wa mwisho mwisho, kwa kuwa swali langu lilikuwa kwenye *clothing*, *Bedding*, *Footwear and Services*, ambalo limeshaulizwa.

**MWENYEKITI:** Tayari limeshaulizwa, Mheshimiwa Mipata!

**MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 221200, *Communications and Information,* kimepanda karibu mara tatu, naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zitatumika kama nilivyoeleza kwa ajili ya kutangaza shughuli za Tume, lakini pia kwa ajili ya kulipia vikundi mbalimbali vya sanaa na kwa ajili ya kuelimisha wananchi kutoa maoni yao.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007 – *Review Coordination Unit … …*sh. 3,348,920,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu A. Lissu!

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza kuhusu kijifungu 210400, *Personnel Allowances* – (*Discretionary*) – *Optional* sh. 604,800,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika randama ya Tume na maelezo yaliyoletwa Bungeni, hizi pesa zinasemekana ni posho za kujikimu za wajumbe wa Tume wakati wa Bunge la Katiba. Mheshimiwa Waziri ametueleza hapa kwamba pesa za Bunge la Katiba ziko kwenye *consolidated fund*, haiko kwenye bajeti hii. Sasa naomba ufafanuzi kama pesa za kuendeshea Bunge Maalum la Katiba ziko kwenye *consolidated* na hazijaidhinishwa na Bunge hili. Hizi sh. 604,800,000/= ambazo ni posho za kujimu za wajumbe wa Tume wakati wa Bunge Maalum la Katiba zikoje hapa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Bunge la Katiba litakuwa likihudumiwa na Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, lakini mwisho wa siku bado Wajumbe wale wa Tume ni waajiriwa wa Tume na watahitajika kuja katika Bunge la Katiba kutoa ufafanuzi mbalimbali, kwa hiyo bado wanawajibika chini ya Tume.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu liko kwenye *item* namba 221200, *Communications and Information*, mwaka huu wa fedha unaoisha walitengewa shilingi bilioni mbili, lakini mwaka ujao wa fedha hakuna pesa zilizotengwa. Naomba maelezo.

**MWENYEKITI**: Umepata hapo, *item* 221200! kwamba hakuna fedha safari hii.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi tumeziweka katika fungu la utawala.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko katika kifungu namba 221000 *Travel in Country*, mwaka uliopita palitumika sh. 600,000,000/=, lakini mwaka huu zimeongezeka sana zimekuwa sh. 1,493,820,000/=. Je, kuna nini hapa, tuambiwe.

**MWENYEKITI:** Jamani lakini mjue hii Tume ni ya muda, inatakiwa ieneze, inatakiwa ifanye nini, naona mnaona kama ni kitu cha kudumu. Naomba mwelewe mazingira yenyewe ya ofisi. Haya Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zitatumika na wajumbe wa Tume wanapokuwa wakisafiri mikoani kikazi hasa katika kusimamia uendeshaji wa Mabaraza ya Katiba.

**MHE. SUZAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye kasma ndogo 220600, *Clothing*, *Bedding*, *Footwear and Services*. Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kwamba fedha hizo ni kwa ajili ya sare na mambo mengine, lakini kifungu huku bado kina *appear* katika *subvote* 1007 na vile vile kina *appear* kwenye *subvote* 1001, pamoja na ile aliyouliza Mheshimiwa Suzan Kiwanga. Naomba kupata maelezo kama bado *sub-vote* hii pia ni kwa ajili hiyo na ni kwa nini?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muundo wa Tume, kipo kitengo cha uratibu wa maoni ya wananchi. Kitengo hiki ni muhimu sana tutakapokuwa tukielekea katika mchakato wa kura ya maoni. Kwa hiyo, wao watakuwa wakichapisha *T-shirt* kwa ajili ya kuhamasisha wananchi tunapoelekea katika mchakato wa kura ya maoni.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama**

Kif. 1001- *Administration and* Human
Resource *Management... ...* sh. 1,432,410,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 1001, kasma 220700, *Rental Expenses*, ambapo kwa wastani kodi imekuwa ikiongezeka kila mwaka. Mwaka huu kodi imefikia shilingi milioni 186. Mheshimiwa Waziri katika

maelezo yake, ameeleza kwamba, kuna changamoto ya kutokuwa na jengo kwa ajili ya Tume ya Utumishi wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa kodi inazidi kuongezeka kila mwaka, ningependa kupata maelezo, ni kwa nini kodi inazidi kuongezeka kila mwaka, wakati pengine jengo ni lile lile na namna gani wanalinusuru Taifa kutokana na kuongezeka kwa kodi kila wakati kwenye jengo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa mahali ambapo Tume inafanyia kazi zake pako finyu sana, lakini pia kama mnavyofahamu tulipitisha Sheria ya Bunge, Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama, Sheria namba 4 ya mwaka 2011. Tume itajipanua katika majukumu yake. Kwa hiyo, tunatarajia Tume hii iweze kuhamia katika ofisi nyingine, lakini pia tutaajiri watumishi wengi zaidi, kwa hiyo basi, mahitaji yatakuwa yameongezeka na gharama za kodi zitapanda.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts ... ... ...* sh. 108,362,400/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Procurement Management Unit ... ... ... ... ... ... ... ... ... ..*sh. 55,155,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

Kif. 1004 - *Internal Audit Unit ... ... ... ... ...* sh. 46,935,500/=
Kif. 1005 – *Recruitment, Appointment and Confirmation... ... ... ... ..*sh. 318,038,400/=

*(vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. *1006 – Ethics and Discipline Section… … … … … … … …* sh. *837,146,500/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 16- Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kif. 1001 - *Administration and Human Resource Management… …* ..sh. 2,209,907,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit… …*sh. 715,142,000/=
Kif. 1003 - *Planning Division… … … … …*sh. 609,010,000/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit… … … … …*sh. 430,806,000/=
Kif. 1005 – *Government Communication Unit… … … … … … … …* ... sh. 237,152,000/=
Kif. *1006 – Legal Registry Unit… … … … …*sh. 302,968,000/=
Kif. 1007 – *Procurement Management Unit… … … … … … … … …* sh. 355,777,000/=
Kif. 1008 – *Research and Library Service Unit… … … … … … …*sh. 262,363,000/=
Kif. 1009 – *Information and Comm. Technology Unit… … … … …* sh. 478,873,000/=
Kif. 2003 – *Legislative Drafting… … … …* sh. 1,321,096,000/=
Kif. 3001 – *Civil Litigation and Arbitration Division… … … … … … … …*sh. 1,210,649,000/=
Kif. 3002 – Treaties and *Contracts Division… … … … … … … …*sh. 1,341,946,000/=
Kif. 4001 – *Constitutional Affairs and Human Rights… … … … …* sh. 1, 031,362,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 35 – Mkurugenzi wa Mashtaka**

Kif. 2002 - *Public Prosecution Division… …* sh. 9,195,519,000/=
Kif. 2004 – *Zonal Office Arusha… … ... …* ...sh. *912, 430,000/=*

Kif. 2005 – *Zonal Office Dodoma... ... ...* ..sh. 593,390,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

Kif. 2006 – *Zonal Office* Dar es Salaam*...* .sh. 1,492,614,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA***:* Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru. Kifungu hiki kinahusu Ofisi ya Mwendesha Mashtaka kwa upande wa Kanda ya Dar es Salaam, sasa ningeomba kupata ufafanuzi kuhusina na kasma 220100 kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawa kwa ajili ya ufuatiliaji wa matumizi ya hizi fedha. Hakuna maelezo yoyote kuhusiana na matumizi ya hizo fedha kwenye kitabu ambacho ninacho ukurasa 191, Fedha zimeongezeka kutoka shilingi milioni 34 mpaka shilingi milioni 40, lakini hakuna maelezo yoyote hizi pesa ni kwa ajili gani. Kwa ajili ya kuweka *record* sawa, naomba ufafanuzi hapa.

**MWENYEKITI:** Mmeona hakuna maandiko!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni kwa ajili ya kuhudumia mahitaji mbalimbali ya ofisi na imeongezeka kwa sababu mwaka jana Ofisi hizi katika Wilaya ya Kinondoni, Ilala na Temeke hazikuwepo, ni ofisi mpya.

**MWENYEKITI:** Shida yake ni hiyo kuongezeka, ila maneno gani yanayofuatia hapo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Wapi?

**MWENYEKITI:** Ukiangalia lile fungu litakuwa ni *office and general supplies and services*. Kwa sababu 220100 katika maeneo haya ndiyo sehemu yenyewe. Kwa hiyo, iandikwe ni *office and general supplies and services*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2007 -*Zonal Office Iringa... ... ... ... ...* sh. 440,193,000/=
Kif. 2008- *Zonal Office Moshi... ... ... ... ...* sh. 567,038,000/=
Kif. 2009 -*Zonal Office Kagera... ... ... ... ...*sh. 478,585,000/=
Kif. 2010- *Zonal Office Mbeya... ... ... ... ...*sh. 577,608,000/=
Kif. 2011-*Zonal Office* Mtwara... ... ... ... ...sh. 479,894,000/=
Kif. 2012 -*Zonal Office Mwanza... ... ... ...* sh. 885,305,000/=
Kif. 2013 -*Zonal Office Ruvuma... ... ... ...* sh. 460, 213,000/=
Kif. 2014 -*Zonal Office Sumbawanga... ...* sh. 354,705,000/=
Kif. 2015-*Zonal Office Tabora... ... ... ...* sh. 667,033,000/=
Kif. 2016-*Zonal Office Tanga... ... ... ... ...*sh. 618,598,000/=
Kif. 2017-*Zonal Office Shinyanga... ... ... ..*sh. 470,787,000/=
Kif. 2018 - *Zonal Office Singida... ... ... ...* sh. 347,589,000/=
Kif. 2019- *Zonal Office Lindi... ... ... ... ...* sh. 284,233,000/=
Kif. 2020 -*Zonal Office Mara... ... ... ... ...* sh. 383,532,000/=
Kif. 2021 -*Zonal Office Manyara... ... ... ...*sh. 313,904,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

Kif. 2022 - *Zonal Office Kigoma... ... ... ...* sh. 313,096,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura!

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi kwenye kifungu kidogo cha 221100, *Travel out of Country* katika Mkoa wa Kigoma kuna shilingi 250,000/=, nataka kujua kiwango hiki...

**MWENYEKITI:** Tuko Pwani sasa!

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Hapana ni Kigoma!

**MWENYEKITI:** Tuko Pwani sasa!

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Hapana ni Kigoma, kifungu 2022!

**MWENYEKITI:** Tumeshapita! Haya turudi, hebu simama Sabreena, endelea!

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko sahihi. Nataka kuuliza kwa sababu hapa kuna *travel out of country* Kigoma *Zone* ni shilingi 250,000/=, nataka kujua ni nchi gani ambayo watu watasafiri kwa sh. 250,000/=

**MWENYEKITI:** Umeiona hiyo! Ni 221100, ni *travel out of country.*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa Bajeti, hii ilikuwa ni kushikilia kifungu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

Kif. 2023- *Zonal Office* Pwani... ... ... ... ... sh. 350,737,000/=
Kif. 2024- *Zonal Office* Njombe... ... ... ... ...sh. 294,825,000/=
Kif. 2025- *Zonal Office* Morogoro... ... ... ...sh. 362,209,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 40- Mahakama**

Kif. 1001 - *Administration and Human Resouces Management* ... ... ... ... ... ... ..sh. 0
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit* ... ... ... ... ... ...sh. 0
Kif. 1003 – *Internal Audit Unit* ... ... ... ... ... ... ... ... ... sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Court of Appeal* Dar es Salaam ... ... ... ... sh. 117,580,157,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 41- Wizara ya Katiba na Sheria**

Kif. 1001- *Administration and Human Resources Management ... ...* sh. 7,677,431,000/=

**MWENYEKITI:** Haya mshahara wa Waziri. Mheshimiwa Sara Msafiri atafutiwa na Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Kange Lugola na Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Haya tuanze na Sara!

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kumekuwa na migogoro ya ardhi kati ya wakulima, wafugaji na wawekezaji, migogoro ambayo inapelekea uvunjifu wa haki za binadamu. Kwa vile Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ina mamlaka kikatiba kushughulikia masuala yote ya uvunjifu wa haki za binadamu na wana kitengo maalum kwa ajili ya elimu kwa umma.

Je, kwa nini sasa Serikali isitoe fedha ya kutosha kwenye kitengo cha elimu kwa umma kwenye Tume ya Haki za Binadamu ili kushughulikia migogoro hiyo na kuepusha gharama zinazoendelea kutokea. Inapotokea migogoro, kunaundwa Tume zingine ndogo za kushughulika migogoro hiyo?

**MWENYEKITI:** Naomba muwe mnaandika vizuri. Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye utaratibu mzima wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya. Kama ambavyo tulisema katika maoni ya Kambi, kumekuwa na utaratibu wa kibaguzi katika uteuzi, uchaguzi wa Baraza la Kikatiba, kati ya Tanzania Bara na Zanzibar. Huku Bara, Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba wamechujwa na Kamati za Maendeleo za Kata, wakati Zanzibar Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba wamechaguliwa moja kwa moja na wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bara Wenyeviti wa Vijiji na Watendaji wa Vijiji na Mitaa ndiyo waliokuwa Wenyeviti wa

mikutano ya uchaguzi wakati Zanzibar, Wenyeviti na Makatibu wa mikutano ya uchaguzi walichaguliwa na wale waliokuwa wanachagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja imeletwa kwamba, haya Mabaraza ya Kata yaliyofanya mchujo kwa Tanzania Bara, ni vyombo vya kisheria vinatumika kwenye mambo mengi, lakini ni muhimu nieleze hapa, Mabaraza ya Kata siyo vyombo vya kisheria, *these are not statutory bodies,* hazina kazi zilizoandikwa kwenye sheria zetu za Halmashauri za Mitaa. Hizi ni Kamati tu na hazina Mamlaka yoyote ya kisheria kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, hakukuwa na sababu yoyote ya kuzifanya kuwa Mamlaka za uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwenye suala hilo hilo, hata Zanzibar kuna Madiwani na kuna kwenye *Ward*, lakini Madiwani wa Zanzibar kwenye ngazi ya *Ward* hakukuwa na mchujo wa Wajumbe wa Mabaraza ya Kata, Mabaraza ya Wilaya, wamechagua moja kwa moja. Sasa Waziri amesema kwamba ngazi ya Kata kwa Tanzania Bara siyo ngazi ya kiuchaguzi, vilevile hapa amekosea, ngazi ya Kata ni ngazi ya uchaguzi, Madiwani wanachaguliwa kwenye ngazi ya Kata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama suala ni ngazi ya kiuchaguzi, hata kwenye Kata zetu kulikuwa na uwezekano wa kuwachagua moja kwa moja Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya badala ya kuweka watu wanne au watano wao ndiyo waamue nani anayekwenda kwenye Mabaraza ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba ufafanuzi wa jambo hili na nitoe hoja kwamba, kama sitaridhika na ufafanuzi wa Waziri, nitatoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri, ili jambo hili lijadiliwe kwa kirefu zaidi na Kamati hii ya Matumizi ya Bunge lako. Nashukuru.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Suala langu liko kwenye ujenzi wa Mahakama za Wilaya na za Mwanzo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Waziri kwenye ukurasa wa 52 amezungumzia kuwepo kwa *program* maalum kwa ajili ya ujenzi wa hizi Mahakama, lakini katika maelezo yake, ameelezea kijuu juu tu, hakuliambia Bunge hili kwamba *program* hii wanatarajia ianze lini na itakwisha lini ili Watanzania wajue kwamba kero zinazotokana na Mahakama zitakuwa zimekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitembelea Mahakama nyingi za Wilaya, nitolee mfano Mahakama ya Wilaya ya Bunda. Bunda ni Wilaya ambayo ni kongwe, ya siku nyingi, lakini mpaka leo wako kwenye jengo dogo la kukodi liko kwenye barabara kuu, vumbi kila siku, makelele kila siku. Kwa hiyo hata katika mazingira ambayo Mheshimiwa Waziri alikuwa anajaribu kulishawishi Bunge kwamba, huenda kukawa na upimaji na wameanza na Majaji kupima utendaji wao, kesi ngapi wamehukumu, watakapokuwa wamekwenda kwenye kupima Mahakimu kwenye Wilaya, nina uhakika Hakimu wa Wilaya ya Bunda ataonekana hafanyi kazi, kwa sababu mazingira ya kazi ni sehemu ya ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua, Mahakama hizi za Tanzania na hususan Mahakama ya Wilaya ya Bunda, kuiweka kwenye mpango huu ambao maandishi yanasema uko kwenye hatua za awali, hatua za awali miaka nenda rudi. Naomba kuwe na juhudi za makusudi kwenye hii Mahakama ya Wilaya ya Bunda kwa sababu ni Mahakama ya Wilaya kongwe, sasa kuniambia kwamba ipo katika *program* maalum kwa kweli sijaridhishwa na maelezo hayo.

Kwa hiyo, naomba nipate maelezo ya kina juu ya Mahakama hii ya Wilaya ya Bunda. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilifikiri umesema *programs* za kujenga Mahakama zikoje, hiyo ndiyo sera, hiyo nyingine ni ya kwako binafsi, uliza inavyostahili.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hotuba ya Waziri, ameelezea namna ya

Bunge la Katiba litakavyokuwa, lakini naona kuna jambo amesahau. Hakutuelezea Bunge hili la Katiba litafanyika Zanzibar au litakuwa Dar es Salaam ama litakuwa Dodoma. Naomba sana atuelezee na kama hajapanga basi napendekeza safari hii lifanyikie Zanzibar, hivyo katika maelezo yake naomba sana aeleze.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu alishajibu Naibu Waziri, sina tatizo naye tena.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Wakati nachangia nilipenda Serikali itoe ufafanuzi kuhusiana na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu unaofanywa na Watendaji wa Kata na wa Kijiji katika maeneo mbalimbali hapa Tanzania kwenye nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watendaji wa Vijiji na Kata wametumia ofisi za vijiji kuvifanya kama ni mahabusu ya kuweka wananchi. Nilitoa *specific* mifano ya Kata na Vijiji Wilayani Urambo na Kaliua ambapo Watendaji wa Kata wanafungia wananchi ndani ya ofisi za Vijiji siku tatu mpaka saba, wale ambao wameshindwa kutoa michango kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamerundikwa kule wanawake kwa wanaume bila kujali hata utu, saa nyingine hawaletewi hata chakula ni tatizo kubwa. Naomba Serikali iseme ni sheria gani inayoruhusu Mtendaji wa Kata au wa Kijiji kutumia Ofisi ya Kijiji kama Mahabusu kwa ajili ya kuwatesa wananchi. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ningependa nipate kauli ya Serikali kuhusiana na Mahakama za Wilaya zote nchini ambazo zimekuwa zinaendesha mashauri kule ndani. Kwa maana kwamba, wananchi hawana fursa ya kuweza kusikiliza na nitoe tu *case study* mfano, ni Mahakama ya Wilaya ya Kasulu, ambayo ina muda mrefu sana mashauri yake yanafanyikia ndani, kiasi kwamba wananchi hawajui ni kitu gani ambacho

kinaendelea. Nini kauli ya Serikali katika kuja kutatua matatizo kama haya kutokana na majengo ambayo mengine ni mabovu, hayatumiki, ambayo yalikuwa yakitumika na kesi zikifanyika waziwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa *commitment* ya Serikali katika hili na hasa nitoe mfano wa Mahakama ya Wilaya ya Kasulu. Kama hakuna mkakati wowote basi naomba nitangaze kwamba, nitatoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri, kama majibu yatakuwa hayajaridhisha.

**MWENYEKITI:** Ukiitolea Sera shilingi inakuwa shughuli, naomba mjibu moja moja.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lililoulizwa na Mheshimiwa Sara Msafiri kuhusiana na migogoro ya ardhi na kwamba ni kwa nini sasa Serikali isitenge fedha za kutosha kwa ajili ya kuiwezezesha Tume ya Haki za Binadamu kutoa elimu kwa umma ili waweze kushughulikia migogoro ya ardhi.

Mheshimwa Mwenyekiti, tumetenga fedha hizo kutokana na ufinyu wa Bajeti. Tungekuwa tuna fedha za kutosha, tungeweza kuongezea, lakini tunatambua umuhimu walio nao na ndiyo maana tumekuwa tukijitahidi kira mara kwa kadiri Bajeti inavyoruhusu kuongezea fedha za Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la Mheshimiwa Tundu Lissu, kuhusiana na utaratibu wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya na alituhumu kwamba katika uteuzi wa Wajumbe wa Mabaraza haya ya Katiba kulikuwa na ubaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukijibu mara kwa mara, lakini pia siku mbili zilizopita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Tume hii, Mheshimiwa Jaji Warioba, alilielezea hili kwa kina na endapo ana uthibitisho wa hayo, anaweza akaiwasilishia Tume ili waweze kuchukuliwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ameelezea pia wasiwasi wake ambao suala hili lilijitokeza katika Bajeti ya

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, kwamba kumekuwa na *double standard* katika Tanzania Bara, hatua ya uchaguzi wa Wajumbe ilikuwa ni hatua mbili wakati Tanzania Zanzibar walikuwa na hatua moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mwongozo wa Tume, katika aya ya pili, unaeleza kabisa bayana kwamba, utaratibu wa kuwapata Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya hautafanana kwa pande zote za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na sababu kwamba tuna tofauti ya mfumo wa utawala. Pia katika mwongozo huu kwa Tanzania Bara, katika ngazi ya Kitongoji au Mtaa, walieleza kwamba, hatua ile ni ngazi ya mapendekezo, ngazi ya kuchaguliwa au kuteuliwa ni ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la tatu, aliulizia pia ni kwa nini Wenyeviti kwa Tanzania Bara walikuwa ni Wenyeviti wa Mtaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo hata Mheshimiwa Mwenyekiti wa Tume alivyoeleza, ilionekana ili kuwapa wananchi ushiriki mzuri, ili waweze kushiriki katika suala hili, ngazi ya Mtaa kupitia Mamlaka ya Serikali ya Mtaa, ni vyema wao ndiyo washiriki katika kuchagua na hususan katika mikutano hii ya wananchi wote. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mtaa, Sheria namba 287 na 288. Hii si mara ya kwanza kwa mikutano hii ya wananchi kutumika katika kuamua masuala mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ilionekana kwamba, ni vyema suala hili likaamuliwa katika ngazi ya Mtaa na Vitongoji, lakini pia si mara ya kwanza katika masuala mbalimbali ya kuteua Wajumbe wa Kamati za Kata za Maji, Kamati za Shule, Kamati za Afya, wamekuwa wakitumika na wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, si vyema alivyokuwa akituhumu kwamba si sahihi, lakini pia kwa

upande wa Zanzibar alisema kwamba, kwa nini Wenyeviti walichaguliwa na Wajumbe wa mkutano. Kama ambavyo nimeeleza awali, hili limetokana na tofauti ya kimfumo wa kiutawala, kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la Mheshimiwa Lugola, ambapo ameuliza kwamba, ni kwa nini hatujaelezea *program* hii ya ujenzi wa Mahakama za Mwanzo na Wilaya utaanza lini na utakwisha lini. Suala hili ni *program* endelevu na kama ambavyo Wabunge wanafahamu, tuna mahitaji makubwa ya Mahakama zetu, kwa hiyo, suala hili tutaendelea nalo kwa muda mrefu kwa kadri Bajeti ikavyokuwa ikituruhusu. Tutakapomaliza basi tutaachana nalo, lakini tunaamini kwamba tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Mahakama ya Wilaya ya Bunda, kama akiangalia vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Mahakama hii imewekwa kwenye mpango, itajengwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Kuna maswali mengine hayo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijaribu kujibu swali lililoletwa na Mheshimwa Zubeir, alitaka kujua Mkutano huu wa Bunge Maalum wa Katiba utafanyika wapi, kama ni Dar es Salaam, Dodoma ama Zanzibar na alikuwa anapendekeza kwamba kama ikiwezekana basi ufanyike Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahali ambapo Bunge hili la Katiba litakutana ni mahali pale ambapo atapatamka atakayeliitisha Bunge hili. Bunge hili kisheria katika ile sheria tuliipitsha hapa sura ya 83, ni Rais ndiye atakayeliitisha Bunge hili na atakapoliitisha basi atatamka likutanie wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo lake ni zuri, nina hakika Mheshimiwa Rais atashauriwa ipasavyo, ni mahali gani patafaa kufanyia mkutano huu kwa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nisahihishe moja tu la Mheshimiwa Tundu Lissu hapa, aliposema kwamba Kamati za Maendeleo za Kata ni Kamati tu. Kamati hizi zimetungwa kisheria kwa mujibu wa sheria namba saba (7) na namba nane (8) za mwaka 1982 na Kamati hizi zinafanya maamuzi yake na maamuzi yake ni ya kisheria. Ni Kamati za kisheria, huwezi ukasema ni Kamati tu, ni Kamati tu zinafanya nini, zina kazi gani, Mheshimiwa Lissu, soma vizuri sheria. (*Makofi*)

Nafikiri yote sasa tayari.

**MWENYEKIT:** Bado Mheshimiwa Magdalena na Mheshimiwa Machali.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimwa Sakaya na Machali *yes*. Mheshimiwa Machali alikuwa anataka kwamba Mahakama zote zifanyike wazi na ndivyo inavyotakiwa kwamba, kesi zisikilizwe kwenye *open court*. Sasa kama hilo halifanyiki, nitawaomba wenzangu wa Mahakama na bahati nzuri wako hapa wakubwa wao, watatoa maelekezo kwa hawa wa chini ambao hawataki kusikiliza kesi kwenye *open court*, ni wajibu wao, wanatakiwa kufanya hivyo ili wananchi wote waone haki ikitendeka, siyo wasikie tu.

**MWENYEKITI:** Bado la Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kuungana na Mheshimiwa Magdalena Sakaya kukemea vitendo hivi vya uvunjaji wa sheria. Ni marufuku mtu yeyote, Mamlaka yoyote ya kijiji kufungia watu kwenye ma-*godown*. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge nafikiri tuungane pamoja kukemea mambo haya na watu hao kama tukishawajua tuwachukulie hatua za kisheria. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii, kumwomba Mheshimiwa Sakaya, baada ya kutoka hapa anipe majina, nitayashughulikia. (*Makofi*)

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na maelezo ya Mheshimwa Waziri na kwa hiyo, naomba nitoe hoja ya kutoa shilingi kwenye mshahara wake na naomba niielezee.

**MWENYEKITI:** Iwe *specific*.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni *very specific,* Mabaraza ya Katiba ya Wilaya yalivyochaguliwa. Hoja ya Waziri ni kwamba, kuna taratibu tofauti za kiutawala kati ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja si sahihi, kwani Tanzania Bara ngazi ya msingi ni kijiji, lakini Zanzibar hakuna vijiji bali wanaita Shehia. Baada ya kijiji kwa Tanzania Bara, ngazi inayofuata ni Kata na kwa upande wa Zanzibar inaitwa Wadi. Ni majina tofauti tu lakini ngazi ni zile zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye uchaguzi wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya upande wa Tanzania Bara ngazi ya kwanza ya kijiji imependekeza tu, wamepiga kura wote, wanakijiji wamehudhuria wote, lakini kura zao zote hazina maana, ni mapendekezo tu! Wanaochagua ni wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kata. Kamati ya Maendeleo ya Kata, nina Wajumbe wake ni Wenyeviti wa Vijiji na Diwani wa Kata, Kata nyingi zina vijiji vinne au vitano. Kwa hiyo, ni watu watano au sita ndiyo waliochagua wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Kata za Tanzania Bara wakati Zanzibar wamechaguliwa na wananchi wote. Kuna *direct democracy* Zanzibar, lakini kuna mchujo Bara na ndiyo ubaguzi ninaouzungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingekuwa na shida kabisa kama ngazi ya msingi ya Tanzania Bara, vijiji vingechagua moja kwa moja bila mchujo sawa na Tanzania Bara kwa sababu ni ngazi za msingi yaani Shehia Zanzibar na kijiji au mtaa Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja ni hiyo kwamba, kwa nini wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya

Tanzania Bara wamechujwa na Kamati ya watu wanne au watano wakati wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ya Zanzibar wamechaguliwa na wananchi wote. Hiyo ndiyo hoja na naomba hoja hii ijadiliwe kwa sababu tunatengeza Katiba, hatuwezi tukatengeneza Katiba ambayo wajumbe wake watakaokwenda kuizungumzia kwenye Wilaya ni watu waliopitishwa kwenye mchujo. Kama nilivyosema ni kwamba *Ward C* za Tanzania Bara over 80% ni za CCM, ndiyo hali halisi! Sasa kama ukitumia utaratibu huo maana yake ni kwamba walipitishwa wote ni wana CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, kuhusiana na hoja hii ni kwamba, Sheria imesema wazi, katika kifungu cha 17(8) kilisema Tume itabuni utaratibu unaofanana utakaotumika katika kila upande wa Jamhuri ya Muungano katika ukusanyaji na uchambuzi wa maoni, uendeshaji wa Mabaraza na uandaaji wa *report*. Hii ndiyo *mandate* ya Tume, Tume haikuambiwa itutengenezee utaratibu ambao watu wanakwenda kuchujwa na kikundi cha watu wanne au watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja hii naomba ijadiliwe kwa mapana na marefu yake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ukishatoa shilingi maana yake ijadiliwe, sasa tena unataka kujadili mara ngapi?

Mheshimiwa Simbachawene! Kuna wengine wameongea sana na wengine sijawasikia wakiongea.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme tu kwamba, kwa kweli hoja ya mtoa hoja hata kwa *formula* yoyote ile utakayoifanya, kama msingi wake ni uwiano wa vyama, matokeo yatakuwa yale yale. Lakini siamini kama msingi wa Mabaraza haya ni uwiano wa Vyama na ukijaribu kui- *transmute,* ukaipekela kwa *aspect* hiyo, kwa *direction* hiyo ya Vyama utapata matokeo yale yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtoa hoja anasema kwamba 80% ya Mabaraza haya ya Kata kwa maana ya *Ward C* ni ya CCM, maana yake nini? Viongozi waliochaguliwa na wananchi kule chini anakosema kwenye kijiji, kwa maana ya vitongoji na vijiji hivyo, ndiyo waliamua iwe hivyo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa vyovyote utakavyofanya hata ukienda kwenye kijiwe, uwiano huo kama ni *ratio* kwa maana yake kwa 80 na 20 maana yake ni nane kwa mbili, popote utakapokwenda nchi hii ukawakusanya hivi utapata uwiano huo huo hata ukienda kijiweni. Sasa sina hakika kama mtoa hoja anataka ku-*achieve* nini, lakini kama anataka ku-*achieve* uwiano wa uwakilishi katika Taifa hili huwezi ukaiweka pembeni CCM, huwezi, kwa namna yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu Mheshimiwa Mjumbe pamoja na mawazo mazuri na dhamira nzuri na mimi namheshimu sana, kwamba jambo hili alione katika mtazamo huo mpana. Anaweza akawa ana-*drive* kitu anachotaka kukifikia, lakini si rahisi akakifikia hata kwa *formula* anayokuja nayo. Naomba sana aunge mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ah! yeye ndiye mwenye hoja, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tuna *deal* na Katiba...

**MWENYEKITI:** Dakika tatu hizi, mnasikia ninyi nyote mnaosimama.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mawili yanayojitokeza ambayo ni vema kama Wabunge tuondoe ushindani wa kisiasa ku-*address logic.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokizungumza Mheshimiwa Tundu Lissu, Mnadhimu wetu, anazungumzia

kuchagua Wajumbe wa Mabaraza kutokana na uchaguzi wa wananchi na siyo uchaguzi wa Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua hapa ndani kwamba Vyama vyetu vyote vikichanganywa *members* wa Vyama vyote hatufiki milioni kumi, lakini nchi hii wapiga kura wapo zaidi ya milioni 20. Kwa nini tunaogopa na tunashindwa kuwapa wananchi fursa ya kuwachagua wawakilishi wao, wakiwa wa CCM hewala, wakiwa wa CHADEMA hewala na wakiwa hawana Chama pia hewala! *Where is the problem?* Hilo ni moja!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, pamejitokeza mazingira ya kujaribu kuchonganisha na kumchonganisha Mheshimiwa Warioba, tunaacha ku-*address issue,* watu wanajaribu kujenga hoja kwamba, pengine sisi tukijenga hoja dhidi ya Tume tunajenga hoja dhidi ya Mheshimiwa Warioba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jambo moja la msingi kwamba, tunamheshimu Warioba, tunawaheshimu Makashna wote na tunawaheshimu Watanzania wote katika hii *process* ya Katiba. Ila tunapokuwa tuna-*address issue* ambayo ni ya msingi, tusiondoe ile *issue* ya msingi, tukarudisha kwenye *personality*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake tumeona watu wengine wanasema, ooh tuna-*question* uwezo wa Warioba, hiyo siyo hoja! Mheshimiwa Warioba tukimtaja hapa ambaye tunamheshimu sana ni kwamba, tunamtaja Mwenyekiti wa Tume na hatuwezi tukamtaja Mwenyekiti mwingine kwa sababu Mheshimiwa Warioba ndiye ambaye ana-*communicate* na *public*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapokuja kuzungumzia mambo ya Katiba tusitafute ushindi wa kisiasa hapa. Hii *process* inahitaji *tolerance*, hii *process* inahitaji kuwa *inclusive* na inahitaji kuheshimiana. Tukitafuta wingi kwa sababu tupo ndani ya Bunge, Watanzania wanatusikiliza kwa pande zote mbili. Tunatafuta Katiba ya kutu-*unite*, kama ninyi mnataka kuleta Katiba ya kutu-*divide, try and do it!* *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimsikilize ambaye hajazungumza, Mheshimiwa Deo Sanga!

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Wajumbe ambao anawazungumzia Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba wamechaguliwa kutoka kwenye Kata, wajumbe wale waliochaguliwa kutoka kwenye Kata ni wale waliochaguliwa kutoka kila kijiji katika Kata hiyo. Kwa mfano, Kata ina Vijiji sita au saba, wametoka kila kijiji wajumbe wanne wane. Wakaenda sasa kwenye Kata ambapo sasa wakachaguliwa wanne na Baraza la Kata ambalo sasa kwenye Kata pale wapo Wenyeviti wa Vijiji na wa Vitongoji na ndiyo waliowachagua wale wale waliochaguliwa na wananchi kule. (*Makofi*)

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kwamba Tume imefanya ubaguzi kwa kutumia mfumo tofauti Bara na Zanzibar, Waziri ameeleza vizuri kwamba, mifumo yetu ni tofauti. Kwa hiyo, utaratibu usingefanana katika hiyo mifumo tofauti na tofauti yenyewe iko hivi, huku Bara tuna kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata yaani *Ward C,* wajumbe wake wanatoka kwenye vijiji ndiyo wanakwenda kwenye Kata, kwenye *Ward C* na ndicho kikao ambacho kilichotumika cha uwakilishi wa vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Zanzibar kikao kama hicho hakipo, Kamati ya Maendeleo ya Kata Zanzibar haipo. Kwa hiyo, usingetegemea kitu ambacho hakipo Zanzibar kifanye kazi hiyo. Hiyo ndiyo tofauti ambayo Mheshimiwa Waziri ameieleza. Namwomba Mheshimiwa Lissu aikubali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niseme hivi, suala la Katiba ni la Taifa na si la vyama. Kuna ushahidi unaonesha kwamba wajumbe waliochaguliwa kwenye vijiji ama mitaa, wamepata kura nyingi na wamechaguliwa na wananchi wengi, wamekwenda kuchujwa na wamepewa uwakilishi watu waliopata kura chache, hiyo ni moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, kuna ushahidi wa dhahiri, sheria inakataza Vyama kuingilia kabla hatujafika hatua ya *referendum* baada ya Bunge la Katiba. Kuna ushahidi wa barua ya Asha-Rose Migiro, wameingilia mchakato kuelekeza viongozi wa Wilaya na Vijiji kwenda kuingilia mchakato na kuchagua machaguo ambayo siyo sahihi kisheria. Lakini Waziri amekiri kwamba, Diwani amejichagua yeye na familia yake, huo ni mfano mmoja ambayo unaelezea mifano mipana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Tume amekiri kuna tatizo, anasema watu ambao hawajaridhika wakate rufaa. Ukipitia mwongozo ambao wametoa, watueleze kuna *mechanism* ya kukata rufaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niungane na hoja ya Mheshimiwa Lissu kwamba, kuna tatizo, Waziri amekubali, Mwenyekiti wa Tume amekubali, turekebishe kwa manufaa ya nchi. Hii Katiba ni zaidi ya CCM, ni zaidi ya CHADEMA, ni zaidi ya *NCCR* Mageuzi na hali kadhalika ni zaidi ya *CUF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa maslahi ya nchi kwamba, hili suala siyo jepesi na tukisema tujigawe hapa twende kwa wananchi tumwage sumu huko hamtatosha kwa sababu kabla ya mwaka...

**MBUNGE FULANI:** Kamwage sumu wewe, usimtishe mtu!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kabla ya uchaguzi wa mwaka 2010 na CCM ya sasa siyo....

**WABUNGE FULANI:** Kamwage! Kamwage sumu!

**MWENYEKITI:** Dakika tatu zimekwisha, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia hii hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Naibu Waziri kwamba, mifumo ya utawala ya Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara inatofautiana, wenzetu wametumia Shehia na sisi tumetumia Kata kwa sababu sisi Kata zetu nyingine zina vijiji mpaka nane na kila Kata inahitaji watu wanne. Ndiyo maana waliamua kila kijiji kifanye uchaguzi wa watu wanne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ngazi ya kijiji wananchi wote walishirikishwa na walivyokuja katika ngazi ya Kata, wajumbe wa Baraza la Kata ni Wenyeviti wa Vijiji ambavyo vinaunda Kata au mitaa kwa mijini. Hao Wenyeviti aidha wa mitaa kwa mijini au wa vijiji kwa maeneo ya Halmashauri wanatokana na vyama vyao. Sasa kama Wilaya ambayo CHADEMA haina kijiji hata kimoja wala haina Diwani hata mmoja nikichukulia Halmashauri ya Mtwara Vijijini, CHADEMA haina Diwani, Mwenyekiti hata mmoja wala Mwenyekiti wa Kitongoji hata mmoja. Hivi unategemea kwenye Baraza la Kata huyo wa CHADEMA ataingiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa maana ya wananchi wameshirikishwa katika ngazi ya Kata na Vijiji, lakini wanaotakiwa ni wanne na Kata zetu za Bara ni kubwa, huwezi kuwakutanisha wananchi zaidi ya 20,000 katika eneo moja, tofauti na Zanzibar ambapo Shehia zao zina watu kati ya 3,000 na 4,000. Kwa hiyo, hatuwezi kuwa na mfumo mmoja wa uteuzi kwanza wao wapo pamoja...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri na kwa mamlaka niliyonayo naongeza dakika 30 baada ya saa ya kuahirisha Bunge.

Mwanasheria Mkuu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishasema na narudia tena kusema kwamba, sina Chama. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mbona ninyi mna midomo jamani, kha!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Sijasema kuwa sijawahi kuwa mwanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi, hoja ni nini? Kwa sababu lazima kuna mtu aseme na mtu mwingine aamue na nawaomba sana Wanasheria waliomo Bungeni kama mmesoma vizuri sheria, ni lazima mheshimu maamuzi na mjenge hoja kwa kuangalia hoja, hoja ni nini? Je, Tume ya Mabadiliko ya Katiba katika kuamua hili imekosea?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Na kama ni ndiyo, imekosea wapi?

**WABUNGE FULANI:** Hapa! *(Kicheko)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Samahani kidogo, siwezi kujua, lakini najua kwamba watu wastaarabu kama ni wanaume, wakiona mwanaume mwingine amesimama wananyamaza. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Kama ni wanawake?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kama ni mwanamke mstaarabu yaani katika *English if is a lady not a woman*, kama ni *lady* anatakiwa kufumba tu mdomo. Sasa ukimwangalia mwanamke au *lady,* wakati unazungumza anakuonyesha midomo, basi unashindwa kujua kama umwa-*dress* kama ni *lady* au *gentleman*. (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Twende kwenye hoja!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Naomba kwa sababu kila mtu ana nyongo juu ya hilo.

Mheshimiwa Halima nashindwa kuku-*address* kama ni *gentleman* au ni *lady*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu ambacho Mheshimiwa Tundu Lissu amekielekeza kinachoipa mamlaka Tume kufanya haya, ni kile kifungu kidogo cha nane cha kifungu kikubwa cha kumi na saba na naomba nikisome kwa urefu kwa sababu Mheshimiwa Tundu Lissu amekisoma kuanzia katikati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema hivi: "Isipokuwa kama mazingira yatahitaji vinginevyo katika utekelezaji wa majukumu yake, Tume itabuni utaratibu unaofanana ambao utatumika katika kila upande wa Jamhuri ya Muungano katika ukusanyaji na uchambuzi wa maoni ya wananchi, uendeshaji wa Mabaraza na uandaaji wa ripoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, usianze kusoma katikati, mazingira yanayozungumzwa hapa ni yapi? Kwa upande wa Zanzibar ngazi za mitaa kuanzia Shehia na siyo sheria bali ni Shehia ambapo ndipo Sheha ana mamlaka ya kuitisha mikutano. Ngazi ya Wodi au *Ward* ambayo ni sawa na Kata kwa Tanzania Bara haina mikutano ya kisheria kwa mujibu wa sheria namba moja ya Mamlaka ya Tawala za Mikoa ya Zanzibar ya mwaka 1998. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania Bara, kwa busara za Tume, kuna utaratibu wa Kiserikali na huo ndiyo uliotumika. Sasa hapa hoja ni hii kwamba, je, katika kufanya hivi Tume ilifanya makosa? Jibu lenu ni kwamba ni ndiyo na ni kweli kwa sababu kila mtu ana kichwa na hapa tupo wengi. Kama ungekuwa wewe ungefanya hivyo, lakini Tume siyo wewe, bali Tume imefanya vile ilivyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia tena kwamba, kila mtu mwenye macho na naona wenzangu mnayo, anajua wakati gani Tume ilitoa mwongozo huu na watu wakatakiwa kutoa maoni yao.

**MBUNGE FULANI:** Na si lazima yakubaliwe!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Sasa akitoa maoni, kama Mheshimiwa Tundu Lissu anapokwenda kwenye Mahakama ana-*submit* mbele ya Jaji tofauti na anavyofanya kwa Mheshimiwa Spika...

**MBUNGE FULANI:** Anajibu kama nani?

**MWENYEKITI:** Anajibu kwa niaba ya Serikali kama utakavyopewa wewe. Someni kanuni!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona kwamba, Tume haijafanya kosa lolote na imefanya kazi hizi kwa mujibu wa sheria. Nafikiri tuache kutumia Bunge hili kama kituo cha malalamiko, kwa sababu nimeona tunaanza kutumia Bunge hili kama kituo cha Polisi, malalamiko yanayohusu mambo ya hujuma yanaletwa hapa. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Hakuna cha utaratibu. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Naomba uendelee kusema.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Naendelea, hakuna cha utaratibu hapa! Hakuna cha utaratibu kwa sababu Tume imefanya kazi yake. Nasema kwa mujibu wa sheria hii, Tume haijafanya kosa lolote na sheria hii tumetunga sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu, mtoa hoja.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba nijibu hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Wajumbe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa siyo uwiano wa Vyama katika Mabaraza ya Katiba ya Wilaya. Hoja ni je, Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba wanachaguliwa moja kwa moja na wananchi au wanapita kwenye chekecheke fulani? (*Makofi*)

Kwa upande wa Zanzibar, Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya za Zanzibar, wamechaguliwa moja kwa moja na wananchi bila kujali itikadi za Vyama vyao na bila kujali uchama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania Bara, Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya wamechaguliwa moja kwa moja na wananchi kwenye vijiji na mitaa, halafu wakapelekwa kwenye chekecheke fulani linaitwa *Ward C*. Hiki ni chombo cha wanasiasa, Mwenyekiti wake ni Diwani, Katibu wake ni Afisa Mtendaji wa Kata, Wajumbe wake ni Wenyeviti wa Vijiji au Mitaa. Wote hawa ni wanachama wa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili chekecheke kwa Tanzania Bara siyo chombo kilichoundwa na Sheria ya Halmashauri za Mitaa, si chombo chenye mamlaka yaliyowekwa kwenye sheria, ni Kamati na ndiyo maana inaitwa Kamati. Lakini utaratibu wa kupata Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba kwa kuwapitisha kwenye Kamati hii ya watu wanne au watano, wao ndiyo wanaoamua nani aende kwenye Baraza la Katiba, nani asiende. Hiyo ndiyo hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine imetolewa kwamba mifumo iko tofauti. Kama nilivyosema Zanzibar hawaiti Vijiji, wanaita Shehia. Ndiyo ngazi ya msingi kama ilivyo kijiji kwa Tanzania Bara. Huku Bara ukitoka kwenye kijiji unakwenda kwenye Kata, ukiwa Zanzibar unakwenda kwenye Wadi. Wadi kuna Diwani na Kata kuna Diwani. Diwani wa Wadi wa Zanzibar anachaguliwa, Diwani wa Kata wa Tanzania Bara anachaguliwa. Kwa hiyo, zinafanana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja ni kwamba, kwa nini hizi ngazi ambazo zinafanana ziwe na utaratibu tofauti? Kwenye mkutano wa Shehia Zanzibar, wale wote waliokusanyika kufanya uchaguzi jambo la kwanza wanachagua Mwenyekiti na Katibu wao. Kwa hiyo, Mwenyekiti wa Mkutano wa Katiba, Zanzibar anachaguliwa na wananchi, anasimamia uchaguzi wa watu watakaokwenda moja kwa moja kwenye Baraza la Katiba la Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Bara, Mwenyekiti wa Kijiji au Mtaa hachaguliwi na ule mkutano pale, ni Mwenyekiti *by virtue of* sheria ya Serikali za Mitaa. Kwa nini utaratibu uko tofauti kwenye ngazi zinazofanana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ni moja, ukija Bara *Ward C* nyingi kama ambavyo tumesema mara nyingi, ni za CCM na kwa hiyo Tume imetumia utaratibu wa *Ward C* ili kuhakikisha kwamba, wajumbe watakaokwenda kwenye Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ni wana-CCM. Ndivyo ambavyo imetokea na ndiyo maana ya hizo barua za Mwalimu wangu Dkt. Migiro na akina Nape Nauye na wengine humu ndani. Utaratibu huu wa kibaguzi, ndiyo tunaoupigia kelele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Tume imetumia busara zake. Nasita kusema busara za Tume hazikuwa sahihi. Busara za Tume kwenye jambo hili si sahihi, kwa sababu Tume haiwezi ikatengeneza utaratibu wa kibaguzi unaokiuka makatazo ya ubaguzi kwenye Katiba yetu, halafu ikasema ina busara. Hizi si busara sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walipoleta rasimu ya mwongozo, tulipeleka maoni, haya tunayoyazungumza tumeyapigia kelele tangu mwezi wa Pili. Tume imeziba masikio na imefumba macho. Inatengeneza utaratibu ambao kama ambavyo imetokea Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ni Mabaraza ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja ni kwamba, Bunge lako Tukufu siyo kituo cha malalamiko na sitaki kumbishia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Bunge si mahali pa malalamiko, Bunge ni mahali pa kuisimamia Serikali na kuiwajibisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili ni mahali pa kuisimamia Tume ya Katiba, ikikosea inatakiwa isemwe hapa kama ambavyo tumeisema. Kwa hiyo, hatujageuza Bunge kuwa mahali pa kulalamika, hili Bunge ni mahali pa kuisimamia Serikali na hii ni vema na haki kwa mujibu wa Katiba yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume yenyewe imekubali kwamba, utaratibu ulikuwa mbovu, imekiri kulikuwa na rushwa, kulikuwa na misukumo ya kisiasa, siasa ambazo haizisemi, lakini misukumo ni siasa za CCM. Barua zile za akina Asha Migiro, Mwalimu wangu, maelekezo ya akina Msome, Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Katibu wa CCM wa Wilaya ya Arusha, Ndugu Kingazi. CCM imehujumu mchakato wa Mabaraza ya Katiba, ndicho tunachokilalamikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Katiba itakayoongoza nchi hii kwa miaka 200 ijayo, mimi na wewe tutakuwa tumekufa. Tunataka watoto wetu siku moja waseme, *we are proud of our parents. They did us proud.* Kwa utaratibu huu, tunaelekea njia ya Zimbabwe ambayo ni njia mbaya. Kwa utaratibu huu, tunaelekea njia ya Kenya kabla ya mwaka 2010 na utaratibu huu unatupeleka kwenye maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tafadhali, tafadhali, tuokoe Taifa letu, tutengeneze Katiba itakayokuwa *worthy our while here*. Nashukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya sasa tutafanya maamuzi, naomba tusikilizane.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 1002 - Finance and Accounts... ... ... Sh. 399,255,000/=*
*Kif. 1003 - Policy and Information Services... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 642,746,000/=*
*Kif. 1004 - Internal Audit Unit... ... ... ... ... Sh. 215,657,000/=*
*Kif. 1005 - Government Communication Unit... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 288,905,000/=*
*Kif. 1006 - Procurement Management Unit... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 283,013,000/=*
*Kif. 1007 - Management Information System Unit... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 265,587,000/=*
*Kif. 2004 - Public Legal Services Unit... ... ...Sh. 511,780,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 4001 - Constitutional Affairs ... ... ... ... Sh. 191,389,000/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid ulisimama?

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndiyo. Niko kwenye kasma ya 221200, *Communication and information*. Mwaka jana ilikuwa sh. 6,480,000/= lakini mara hii sijui hamna fedha. Je, mwaka huu hamna *information* yoyote au ni vipi?

**MWENYEKITI:** Mmeipata *sub-vote* 4001, *communication and information*.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli hizo zimehamishiwa katika *sub-vote* 1005 ya *Government Communication Unit*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

*Kif. 1001 - Administration and Human Resources Management... ... Sh. 2,232,686,000/=*
*Kif. 1002 - Finance and Accounts... ... ... Sh. 234,343,000/=*
*Kif. 1003 - Internal Audit Unit... ... ... ... ...Sh. 124,790,000/=*
*Kif. 1004 - Legal Service Unit... ... ... ... ...Sh. 355,704,000/=*
*Kif. 1005 - Procurement Unit... ... ... ... ... Sh. 177,280,000/=*
*Kif. 1006 - Management Information System Unit... ... ... ... ... ... ...Sh. 213,307,000/=*
*Kif. 2001 - Administrative Justice... ... ... ...Sh. 850,337,000/=*
*Kif. 2002 - Human Rights... ... ... ... ... ... Sh. 595,448,000/=*
*Kif. 2003 - Research and Documentation... Sh. 309,975,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 2004 – Public Education and Training... ... ... ... ... ... ... ..Sh. 273,933,000/=*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho 2004 cha Elimu kwa Umma pamoja na mafunzo, kasma 221200 Communication & Information. Kasma hii mwaka wa fedha uliopita ilitengewa shilingi milioni 19.6, mwaka huu kiwango cha fedha kimeshuka mpaka milioni 1.2 peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati wa kupitishwa kwa kifungu hiki nilieleza kwamba, niliwasilisha malalamiko rasmi ya kimaandishi kwa niaba ya wananchi wa Kata ya Goba, kuhusiana na matatizo ya maji ya *DAWASA* na Manispaa ya Kinondoni, ambayo naamini Tume ya Haki za Binadamu inaelewa vizuri jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kulikuwa kuna tatizo la namna gani Tume inatoa elimu kwa umma na inawasiliana na umma pale ambapo malalamiko yanatokea. Maelezo niliyokuwa nimepewa ni kwamba, kiwango cha fedha ambacho Tume inacho kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma

ni kidogo sana, kwa wakati huo ikiwa shilingi milioni 19.6. Sasa kile kiwango cha milioni 19.4 ambacho kilikuwa kinaonekana ni kidogo, safari hii kimeshuka zaidi na kuwa shilingi milioni 1.2 peke yake katika wakati ambapo Tume ina malalamiko mengi, inahitaji kufanya mawasiliano na umma, ina mambo mengi ambayo inayafanyia uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kupata ufafanuzi kutoka kwenye Wizara, ni kwa nini kiwango hiki cha fedha kimeshuka na hakikisho la kwamba, kiwango hiki hakitaathiri uchunguzi wa tuhuma za ufisadi wa maji katika Kata ya Goba ambayo nilikuwa nimeishawasilisha kwenye Tume? Naomba maelezo.

**MWENYEKITI:** Maelezo mengine hayo hayahusiani na hapa. Kuuliza kwamba kwa nini fedha zimepungua, hiyo safi. Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba maelezo, umekiona lakini?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fungu la utawala, tumetenga shilingi milioni 58 kwa ajili ya shughuli hiyo. Pia ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, haiwezi kuathiri utatuzi wa migogoro; elimu kwa umma ni elimu kwa umma, lakini pia utatuzi wa migogoro na ushughulikiaji wa malalamiko ni kitu kingine tofauti. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba, tutafuatilia na Tume itaweza kufanya kazi zake kwa umakini. Fungu la elimu kwa umma limewekwa katika *Government and Communication Unit*, Idara ya Utawala.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 3001 - Zanzibar Office ... ... ... ... ... Sh. 242,992,000/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria**

*Kif. 1001 - Administration and Human Resources Management... ... Sh. 3,431,560,000/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

*Kif. 3001 - Civil Litigation and Arbitration Division... ... sh. 0*
*Kif. 3002 - Treaties and Contracts Division... ... ... ... ... ... ... ... sh. 826,000,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 35 – Mkurugenzi wa Mashtaka**

Kif. 2002 Public Prosecution Division*... ... sh.* 2,167,759,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 40 – Mahakama**

Kif. 1001 - *Administration and Human Resources Management... ... sh.* 42,716,668,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbowe na Mheshimiwa Halima nimekuona. Mheshimiwa Mbowe!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimi Mwenyekiti, *sub-vote 1001, kifungu 6312 Construction and Rehabilitation of Primary Court buildings***.**

Napenda tu kumuuliza Mheshimiwa Waziri kama ile Mahakama ya Mwanzo ya Machame iko katika fungu hili.

**MWENYEKITI:** Sawa! Sijui kama mnaweza kujibu.

**NAIBU WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya haipo na hii inatokana na ukomo wa bajeti. Kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alieleza asubuhi, alitaja kabisa ni Mahakama zipi ambazo zitajengwa kupitia fedha hizi, zikiwemo Mahakama za Mwanzo za Gairo, Ludewa, Lukuledi, Mangaka, Bunda, Bariadi, Nyamikoma na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo hicho hicho cha *6312, Construction and Rehabilitation of Primary Court buildings,* nilitaka nipate kauli ya mwisho ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima tukiishakijibu kile huwezi kuuliza tena.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana, inahusu Mahakama nyingine.

**MWENYEKITI:** Aah, sasa ndiyo kimejibiwa hapa. Mheshimiwa Waziri amejibu *extensively*.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa... aah!

**MWENYEKITI:** Hapana!

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

*Kif. 1001 Administration and Human Resources Management... ... sh. 3,017,560,000/=*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye kifungu kidogo 6210, kuhusiana na utekelezaji wa Mradi wa Kupambana na Rushwa...

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, tuko ukurasa wa 53, kifungu cha 1001, mbona hicho cha kwako sisi hatukioni?

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Kuna marekebisho.

**MWENYEKITI:** Angalia vizuri labda ni kingine.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif . 1003 – Policy and Information Services... ... ... ... ... ... ... sh. 4,881,280,00/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kif. 1001- *Administration and Human Resources Management... ... ... sh.* 206,414,000/=
Kif. 1004 - Legal Services*... ... ... ... ... ... ... ... ... ..sh.* 0
Kif. 2001- Administration Justice*... ... ... ... sh.* 52,000,000/=
Kif. 2002 - Human Rights*... ... ... ... ... ... sh.* 597,575,000/=
Kif. 2003 - Research and Documentation*... sh.* 52,180,000/=
Kif. 2004- Public Education and Training*... ... ... ... ... ... ... ...sh.* 126,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria**

**MWENYEKITI:** Hapa mtaona mmegawiwa karatasi inasema, Tume ya Kurekebisha Sheria Fungu 59, idadi ya pesa

pale mwanzo zilikuwa hazipo zimerudishwa milioni 616,350,000. Mmeona hiyo karatasi.

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management… … …sh.* 616,350,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

(Bunge lilirudia)

**TAARIFA**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa Fedha 2013/2014, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha pamoja na mabadiliko yake. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwe na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 yalipitishwa na Bunge )*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja chini ya Kanuni 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo 2013 kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge wa kushughulikia Bajeti ya Serikali pamoja na Shughuli nyingine za Bunge zilizopangwa umepangwa kumalizika tarehe 28 Juni, 2013;

NA KWA KUWA ratiba ya Shughuli ya zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano huu wa Kumi na Moja zimepangwa kwa kuzingatia Kanuni 99(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo 2013;

NA KWA KUWA tarehe 25 Aprili, 2013 Mheshimiwa Spika, baada ya kuzingatia michango ya Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji, alisitisha shughuli zilizokuwa zikiendelea na kuagiza Serikali kukaa na Kamati ya Bunge ya Bajeti ili kuona uwezekano wa kuongeza fedha kwa Bajeti ya Wizara ya Maji, jambo lililohitaji siku nyingine ya kuhitimisha hotuba ya bajeti ya Wizara hiyo;

NA KWA KUWA majadiliano ya Bajeti ya Wizara hiyo yaliendelea siku ya Jumatatu tarehe 29 Aprili, 2013 ambayo awali ilipangwa kujadili hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasilil na Utalii.

NA KWA KUWA katika Kikao cha Kamati ya Uongozi ya Bunge kilichofanyika katika Ukumbi wa Spika, tarehe 2 Mei, 2013, Wajumbe wote wa Kamati hiyo waliohudhuria waliazimia kuliomba Bunge likubali kufanya kazi siku ya tarehe 4 Mei, 2013 ili kujadili hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2013/2014;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa Kanuni ya 28(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo 2013 Bunge haliwezi kukutana na kufanya kazi siku ya Jumamosi, Jumapili au siku ya Mapumziko.

NA KWA KUWA ili kuliwezesha Bunge kuweza kukutana siku ya Jumamosi tarehe 4 Mei, 2013 ni lazima Bunge litengue kanuni 28(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo 2013 kwa mujibu wa Kanuni ya 153(1);

HIVYO BASI Bunge linaazimia kwamba, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa Shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Kumi na Moja Kanuni 28(15) kitenguliwa kama ifuatavyo:-

Kanuni 28(15) ambayo kwa ujumla wake kinaelekeza kwamba Bunge halitakutana siku ya Jumamosi, Jumapili na siku za Mapumziko itenguliwe na badala yake Bunge likutane siku Jumamosi yaani kesho tarehe 4 Mei, 2013 kuanzia Saa Tatu Asubuhi hadi Saa Nane Mchana isipokuwa kwamba siku hiyo hakutakuwa na kipindi cha Maswali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, kesho Waheshimiwa Wabunge, tutakuwa na kikao cha Bunge na ni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na ni Wizara ambayo katika hali ya kawaida ni ya siku moja. Kwa sababu sisi wenyewe tulipanga na kuchagua kuizungumza Wizara ya Maji kwa kirefu na kwa undani na kukawa na mafanikio, basi tukubali gharama yake nyingine ambayo ni kufanya kikao kesho.

La pili, Waheshimiwa Wabunge, naona kuna tabia ambayo siyo nzuri. Tukisoma Kanuni yetu ya 66(1)na(2) inasema hivi: “Wakati wa Vikao vya Bunge Spika anapokuwa anaingia au kutoka katika Ukumbi wa Bunge, Wabunge na wageni wote waliopo kwenye Ukumbi huo watasimama kwa utulivu mahali pao na kubaki kimya hadi Spika atakapokuwa ameketi katika kiti chake au atakapokuwa ametoka kwenye Ukumbi wa Bunge.” Yaani ninapoingia mnatakiwa msimame kimya na ninapotoka.

Waheshimiwa Wabunge, lakini ya pili, inasema: “Wakati Bunge linaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima au

katika Kamati ya Matumizi, Wabunge na wageni wote waliopo kwenye Ukumbi wa Bunge watasimama kwa utulivu mahali pao na kubaki kimya ili kutoa heshima kwa mchakato wa Bunge kuingia kwenye Kamati ya Bunge Zima au kwenye Kamati ya Matumizi na baadaye Bunge Kurejea."

Sasa naona wakati tunakwenda kubadilisha nguo kule wengine wanaanza kuzungumza, huyu anaweka Siwa hapo, Waheshimiwa wanaendelea kuzungumza sivyo kinachozungumzwa. Waheshimiwa Wabunge hii ndiyo kazi yetu na ni mahali petu, tusiposhika adabu za humu ndani, tutakuwa kama mahali pengine popote pale pasipokuwa hata na busara zozote. Tuelewane tujadiliane kwa hoja na siyo kufanya vitu ambavyo vinakuwa ni sehemu ya fujo ya kazi zetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nadhani siku ya Jumapili kuna Kamati zingine zitakuwa na Semina, kwa hiyo, nadhani wanaohusika watawaambieni. Lakini kesho tutakuwa na Kikao cha Bunge Saa Tatu Asubuhi. Kwa hiyo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka Kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa. 2.08 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumamosi, Tarehe 4 Mei, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*